# *TANZANIA OSAKA ALUMNI*

# Kitabu cha

# Mbinu Bora 2

**Ofisi ya Waziri Mkuu**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**S.L.P 1923**
**Dodoma**

**Mei, 2015**

# KITABU CHA MBINU BORA 2 (2015)

**Kimeandaliwa kwa ajili ya Tanzania Osaka Alumni (TOA) na:-**
**Paulo F. Faty,**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe;**
**Judicate N. Mwanga,**
**Mhadhiri, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo;**
**na**
**Michiyuki Shimoda,**
**Mshauri Mwandamizi – OWM-TAMISEMI**

**na kuhaririwa na:-**

**Eustard A. Ngatale,**
**Kaimu Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Huduma za Sheria – OWM - TAMISEMI;**
**Stella M. Paschal,**
**Afisa Serikali za Mitaa Mkuu, Kitengo cha Uboreshaji Huduma za Menejimenti – OWM -TAMISEMI;**
**Paulo F. Faty,**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe;**
**Judicate N. Mwanga,**
**Mhadhiri, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo;**
**Honorina L. Ng'omba,**
**Mshauri wa Serikali za Mitaa, JICA-TANZANIA;**
**Elias Magere,**
**Katibu wa Mikutano, Manispaa ya Dodoma.**

# Yaliyomo


| *Yaliyomo* | *Ukurasa* |
|---|---|
| *Dibaji* | *4* |
| *Utangulizi (TOA)* | *5* |
| *Utangulizi (JICA)* | *6* |
| *Vifupisho* | *7* |
| *Sura ya Kwanza:Utangulizi:Mafunzo Kutokana na Uzoefu wa Japani* | *9* |
| *Sura ya Pili: Upangaji Mipango Shirikishi Jamii na Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo* | *28* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa: Utawala Ngazi ya Msingi na Ushiriki wa Jamii katika Jitihada za Maendeleo* | *32* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo: Uwezeshaji Jamii kwa Maendeleo Ngazi ya Msingi* | *41* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero: Uwezeshaji Jamii kwa Maendeleo Ngazi ya Msingi* | *50* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro: Uwezeshaji Jamii kwa Maendeleo Ngazi ya Msingi* | *60* |
| *Sura ya Tatu:Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato* | *71* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba: Uboreshaji wa Mapato ya Ndani* | *73* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu: Mikakati ya Uboreshaji wa Mapato ya Ndani* | *85* |
| *Sura ya Nne:Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma* | *97* |
| *Halmashauri ya Jiji la Mwanza: Udhibiti wa Msongamano wa Magari Mjini* | *100* |
| *Halmashauri ya Manispaa ya Moshi: Ugatuaji wa Udhibiti wa Taka Ngumu* | *115* |
| *Halmashauri ya Jiji la Tanga: Udhibiti Endelevu wa Taka Ngumu* | *129* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga: Utoaji Endelevu wa Chakula cha Mchana Katika Shule za Msingi* | *142* |
| *Sura ya Tano: Maendeleo ya Jamii Kiuchumi* | *152* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda: Uanzishwaji wa Mnyororo wa Thamani wa Zao la Mpunga* | *155* |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga: Uzalishaji na Uongezaji wa Thamani zao la Mhogo* | *164* |
| *Marejeo* | *174* |

# Dibaji

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yamelenga katika utoaji bora wa huduma wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa za Serikali Kuu. Maboresho yamekaribisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, washirika wa maendeleo na wadau wengine tangu awamu ya kwanza hadi sasa. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) iliwekwa dhahiri mwaka 1998 na utekelezaji wake wa maboresho ya Serikali za Mitaa ulianza mwaka 2000. Kupitia ushirikiano huu maboresho ya Serikali za Mitaa hapa Tanzania yamefanikiwa kuleta Serikali za Mitaa za kidemokrasia, matumizi bora ya raslimali watu, kuongozeka kwa ruzuku toka hazina, kuimarika kwa utawala bora katika Serikali za Mitaa, kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi, na kwa ujumla kuongezeka kwa uhuru wa serikali za mitaa katika utoaji huduma.

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yametekelezwa kwa mkakati wa jumla ambao umejumuisha kujifunza jitihada za maboresho na utekelezaji wake katika nchi nyingine, Afrika na nje, na kuunda mkakati sahihi wa utekelezaji wake na mbinu mbadala kwa Tanzania. Tangu mwaka 2002 Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI) na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) kwa pamoja wameendesha mafunzo kuhusu Ugatuaji nchini Japani kupitia mafunzo ya Osaka. Mafunzo haya yamehudhuriwa na Wakurugenzi na Watumishi wengine toka OWM – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na wadau wengine wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Mafunzo haya pia yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na wakuu wa idara kupita mafunzo ya mikoa baada ya mafunzo ya Osaka (Reginal Post Osaka Training).

Mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa yametoa fursa kwa watumishi wa serikali kuu na serikali za mitaa kujifunza uzoefu wa ugatuaji madaraka wa kijapani, kuchagua mbinu bora za ugatuaji wa kijapani na kutekeleza mbinu hizo katika Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hili limeibua umuhimu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mbinu hizi bora kupitia kitabu, ili kuzifanya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kuona na kujifunza utekelezaji na siri zake humuhumu nchini.

Kitabu hiki cha pili ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kati ya OWM – TAMISEMI na JICA kuimarisha sera ya ugatuaji wa madaraka Tanzania. Kitabu hiki kinaanza kwa kuonyesha historia ya mafunzo ya Osaka na mbinu bora kama ifuatavyo: Sura ya Kwanza inaonyesha kwa ufupi Mafunzo kutokana na uzoefu wa Japani, Sura ya Pili inahusu Upangaji Mipango Shirikishi Jamiii na Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ikiwasilisha mbinu bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Kondoa, Bagamoyo, Kilombero na Morogoro; Sura ya Tatu inahusu Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na uboreshaji wa mapato ikiwasilisha mbinu bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Bukoba na Ushetu; Sura ya Nne inahusu Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji Huduma ambayo inawasilisha mbinu bora kutoka Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa ya Moshi, Jiji la Tanga na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Sura ya Tano inayohusu Maendeleo ya Jamii Kiuchumi ikiwasilisha mbinu bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Mpanda na Bagamoyo.

OWM – TAMISEMI inashauri watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na wa Halmashauri na wadau wote wa maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania kusoma kitabu hiki, kutambua jitihada mahsusi za ndani, kujifunza siri za mafanikio na kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kuleta utendaji mzuri katika muktadha wa ugatuaji wa madaraka.

**Jumanne Sagini**

**KATIBU MKUU - OWM-TAMISEMI**

# Utangulizi (TOA)

Kitabu cha pili cha Mbinu Bora cha *Tanzania Osaka Alumni* ni matokeo ya jitihada za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OWM – TAMISEMI na Serikali ya Japani kupitia JICA tangu mwaka 2002 kwa kuendesha mafunzo huko Osaka na mafunzo baada ya Osaka katika kila mkoa juu ya uzoefu wa Ugatuaji Madaraka huko Japani. Mafunzo haya yalitoa fursa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na wadau mbalimbali wa maboresho hapa Tanzania kujifunza uzoefu wa kijapani kuhusu Ugatuaji katika maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Raslimali Watu, Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato, Upangaji na Utoaji Huduma Shirikishi na Maendeleo ya Kiuchumi katika Halmashauri hasa kupitia dhana ya *"One Village One Product" Movement*. Mambo mazuri yaliyotokana na mafunzo haya yamekuwa yakitekelezwa katika Sekretariati za Mikoa na Halmashauri mbalimbali kwa lengo la kutaka kuboresha utoaji huduma kwa jamii kwa kuzingatia sera ya ugatuaji madaraka, yaani "D by D". Utekelezaji wa hizi Mbinu Bora umeonyesha mafanikio na matokeo chanya kwa jamii. Hata hivyo kwa maana ya uenezaji wa taarifa na Usomaji rahisi kuhusu Mbinu Bora zilizotekelezwa, Kamati Tendaji ya TOA imechapisha Toleo la Pili la Kitabu lenye Mbinu Bora 12. TOA inatarajia kuendelea kuchapisha matoleo mengine zaidi ya kitabu hiki sambamba na utekelezaji unaondelea wa masuala mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa.

Kukamilika kwa kitabu hiki cha Pili cha Mbinu Bora kumetokana na misaada kutoka taasisi na watu binafsi mbalimbali. TOA inapenda kutambua na kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufikia makubaliano na Serikali ya Japani, kufadhili na kuruhusu watumishi wa Tanzania kuhudhuria mafunzo ya Ugatuaji nchini Japani toka mwaka 2002 mpaka sasa. Pili TOA inaelekeza shukrani za dhati kwa serikali ya Japani na JICA kwa kuandaa, kusaidia na kufadhili mafunzo ya Osaka na Mafunzo ya Mkoa na uzalishaji wa kitabu hiki. TOA pia inapenda kutambua na kuthamini juhudi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu utekelezaji wa yale yaliyojifunzwa na utayari wao wa kuandika kwa ufasaha Mbinu Bora kama zinavyoonekana katika kitabu hiki.

Uchambuzi na uunganishi wa Mbinu Bora zilizopo kwenye kitabu hiki ulifanywa na Bwana Paulo F. Faty (Mhadhiri - Chuo Kikuu Mzumbe) na Bwana Judicate Mwanga (Mhadhiri - Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo), pia Masuala yaliyoigwa Japani yamechambuliwa na Bwana Michiyuki Shimoda (Mshauri Mwandamizi, OWM – TAMISEMI). TOA kwa dhati kabisa inapongeza mchango wao na inawashukuru sana. Mwisho TOA inapenda kuwashukuru watumishi wote wa OWM – TAMISEMI, JICA na TOA kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali iliyoboresha na kuunda kitabu hiki. Siyo rahisi kutaja wote waliochangia katika kazi hii, hata hivyo TOA inaheshimu michango yote iliyotolewa na Taasisi na Watu mbalimabali. Mwisho kabisa, ingawa Watu na Taasisi nyingi zimechangia katika kitabu hiki, TOA na timu ya uchambuaji wanawajibika kwa makosa na mapungufu yanayoweza kuhisiwa na wasomaji wa kitabu hiki.

**Jane Mutagurwa**

**MWENYEKITI - TOA**

# Utangulizi (JICA)

Wasomaji Wapendwa!

Utekelezaji wa sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) umechukua zaidi ya miaka 10 sasa ukiwa na lengo la kuboresha huduma kwa kugatua shughuli, majukumu na raslimali toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Kutokana na ukweli huu hapo juu Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) limejikita katika kusaidia utekelezaji wa sera hii hasa katika kuimarisha utoaji huduma katika ngazi za msingi kwa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sekta za afya, kilimo, maji na barabara.

Kuanzia mwaka 2002, JICA kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI) imekuwa ikiendesha mafunzo kuhusu maboresho katika Serikali za Mitaa yanayoitwa "Osaka Training". Mafunzo haya yalilenga Maofisa wa juu wa Menejimenti katika maboresho ya Serikali za Mitaa, yaani Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Maofisa wa OWM – TAMISEMI na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa malengo ya kujifunza uzoefu wa Kijapani katika maboresho ya Serikali za Mitaa. Baada ya mafunzo ya Osaka, washiriki wamekuwa wakiwasilisha na kujadiliana uelewa na uzoefu walioupata kwenye warsha za mafunzo za mikoa (2003 – 2007). Kutokana na mafunzo haya, Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (TOA) ulianzishwa ili kuwa na jukwaa ambalo wajumbe wa TOA wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu, mbinu bora na changamoto zilizopo. JICA imekuwa ikisaidia uimarishaji wa taasisi ya TOA.

Kutokana na utekelezaji wa mambo mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka, mbinu bora nyingi ziliwasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika warsha za Mikoa zilizofanyika katika kanda sita mwaka 2011/12. Baada ya uhakiki na uchambuzi toleo la pili la "Kitabu cha Mbinu Bora" hatimaye limechapishwa. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa ***"tunapaswa kujifunza siyo tu kutoka nchi nyingine bali kutoka katika jitihada mbalimbali zilizopo ndani ya nchi".***

Nitafurahi kama mtajifunza vidokezo muhimu kutoka kitabu hiki na kuchukua hatua chache lakini za uhakika ili kuboresha utendaji katika eneo husika.

JICA ina mpango wa kuifadhili TOA ili kuendesha warsha za mafunzo za mikoa zitakazoshirikisha watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Wakuu wa Idara za Halmashauri kwa kutumia kitabu hiki. Tungependa kuona kuibuliwa kwa Mbinu Bora zinazotokana na chachu ya kitabu hiki na mafunzo yake. Kwa siku sijazo, tunatarajia kuona jukwaa la kujifunza wenyewe kwa wenyewe *(Horizontal Learning)* linaanzishwa katika ngazi za msingi.

**Toshio NAGASE**
***Mwakilishi Mkuu – Ofisi ya JICA Tanzania***

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| AMCOs | Agricultural Marketing Cooperatives |
| ALAT | Association of Local Authorities In Tanzania |
| ASDP | Agriculture Sector Development Programme |
| AMSDP | Agricultural Marketing Systems Development Programme |
| CAG | Controller and Auditor General |
| CAMA | Computer Assisted Mass Appraisal |
| CMD | Cassava Mosaic Disease |
| CBD | Central Business District |
| CBSD | Cassava Brown Streak Disease |
| CFO | Commercial Farmers Organisation |
| CMT | Council Management Team |
| CRB | Contractors Registration Board |
| CRDB | Cooperative and Rural Development Bank |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DADPs | District Agricultural Development Plans |
| DALDO | District Agricultural and Livestock Development Officer |
| DCDO | District Community Development Officer |
| DED | District Executive Director |
| DRC | Democratic Republic of Congo |
| FAO | Food and Agriculture Organisation |
| FBO | Faith Based Organization |
| FFS | Farmers Field School |
| HQ | Headquarters |
| ICT | Information Communication Technology |
| KCMC | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| LGA | Local Government Authority |
| LAs | Local Authorities |
| LGCBG | Local Government Capacity Building Grant |
| LGLB | Local Government Loans Board |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (A Network of Farmer Groups in Tanzania) |
| MEOs | Mtaa Executive Officers |
| MoUs | Memorandum of Understanding |
| OVOP | One Village One Product Movement |
| POT | Post Osaka Trainings |
| PPP | Public –Private- Partnership |
| PRA | Participatory Rural Appraisal |
| RCC | Regional Consultative Committee |
| RUBADA | Rufiji Basin Development Authority |
| SACCOs | Savings and Credit Cooperative Societies |

| | |
|---|---|
| SEDP | Secondary Education Development Programme |
| SGR | Strategic Grain Reserve |
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| SMEs | Small and medium Enterprises |
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| TANZAM | Tanzania Zambia Highway |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs regulatory Agency |
| TFNC | Tanzania Food and Nutrition Centre |
| TANROAD | Tanzania Road Agency |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railways |
| TOA | Tanzania Osaka Local Government Reform Alumni |
| TOSCI | Tanzani Official Seed certification Institute |
| TSCP | Tanzania Strategic Cities Project |
| TZS | Tanzanian Shillings |
| VAEOs | Village Agricultural Extension officer |
| VETA | Vocational Education Training Authority |
| WAEO | Ward Agricultural Extension Officer |
| WEO | Ward Executive Officer |
| WDC | Ward Development Committee |
| WPs | Ward Patrons |

# Sura ya Kwanza: Utangulizi: Mafunzo Kutokana na Uzoefu wa Japani

## 1.0 MAFUNZO YA OSAKA

Kitabu hiki kimeandaliwa na Umoja wa Washiriki wa Mafunzo ya Osaka kuhusu Serikali za Mitaa wanatoka Tanzania (TOA). TOA ni Umoja wa washiriki wa kozi inayotolewa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA). Mafunzo haya yanajulikana kama "Mafunzo maalumu ya Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania", kwa jina maarufu "Mafunzo ya Osaka". Umoja una wanachama ambao ni Makatibu Tawala wote wa Sekretarieti za Mikoa na Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Mafunzo ya Osaka yalianza mwaka 2002. Kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Makatibu Tawala wote kutoka Mikoa 21 (kipindi hicho) pamoja na Wakurugenzi wa Halmahauri wawili kutoka kila mkoa walihudhuria. Pia maofisa wa juu toka OWM – TAMISEMI (wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi)[1], Katibu Mkuu wa ALAT na baadhi ya wanataaluma mashuhuri walihudhuria kozi hii.

Kutokana na mafanikio na matokeo dhahiri, JICA iliamua kuendelea na mpango huu, kwa kupanua wigo wake kwa kuongeza nchi nyingine tatu za kiafrika ambazo zilikuwa zikipanga na kuendeleza maboresho ya ugatuaji, yaani Kenya, Uganda na Zambia. Hadi leo zaidi ya viongozi 100 wa maboresho wanaojumuisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wamefaidika moja kwa moja na mafunzo ya Osaka. Pia washiriki hawa waliporudi katika mikoa yao waliendesha warsha za ndani zijulikanazo kama "mafunzo ya Post Osaka" ili kubadilishana uzoefu na uelewa walioupata Osaka kwa kuwaalika Wakurugenzi waliobaki pamoja na wakuu wa idara. Hivyo wafaidika wa mafunzo haya waliongezeka mpaka kufikia zaidi ya 1,500, ingawa uanachama wa TOA ulibakia kuwa wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kutokana na mambo mazuri mbalimbali yaliyoigwa Osaka na mafunzo ya Post Osaka, Halmashauri zilizohudhuria ziliandaa mipango kazi ya kuboresha utendaji wao. Kukiwa na zaidi ya miaka 10 ya utendaji, imethibitishwa kuwa kuna idadi kubwa ya mbinu bora zinazojitokeza katika Halmashauri nyingi kupitia utekelezaji wa mipango kazi ambayo itakuwa ni vyema kuwashirikisha wengine. Kwa hiyo TOA iliamua kuhakiki na kuchambua mbinu bora na kutengeneza kitabu hiki, ili viongozi wa Halmashauri waweze kufanyia rejea mbinu hizo na kuzitumia kwa kadri watakavyoona zinafaa na zinastahili kwa lengo la kuboresha utendaji wao.

Kabla ya kuelezea mbinu bora za Halmashauri mbalimbali katika kitabu hiki, ni vyema katika sura hii tukaangalia kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya kwa viongozi wa maboresho wa

[1] Pamoja na Mh. A. Mwanri, Naibu Waziri (MB), Makatibu Wakuu wawili wa Zamani wa OWM-TAMISEMI, yaani, Bi. Tarishi M.K. na Bw. H.A. Katanga.

kitanzania, mafunzo ya Osaka yalikuwa na maana gani kwa Tanzania na masuala gani yalijadiliwa kwenye mafunzo haya.

## 2.0 HISTORIA YA MAFUNZO YA OSAKA

Kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya na yalikuwa na maana gani kwa Tanzania?

### 2.1 Maoni ya JICA Kuhusu kufadhili Ugatuaji

JICA ina maoni ya kipekee kuhusu ufadhili wa masuala ya utawala ambayo yanaweza kutofautiana na maoni ya washirika wengine wa maendeleo. JICA imekuwa ikishuhudia juhudi kubwa za washirika wa maendeleo za kuingilia kati programu za maboresho katika nchi zinazoendelea na kama vile Programu ya kurekebisha Miundo ya Uchumi (SAPs) na kufadhili maboresho ya utawala ikiwa ni pamoja na Ugatuaji wa madaraka. Hata hivyo, twaweza kusema kwamba programu hizi na maboresho haya yaliyofanywa katika nchi zinazoendelea yako sawa kabisa na yale yanayojaribiwa sasa katika nchi zilizoendelea bila kujali tofauti iliyopo ya kihistoria na mazingira kati ya nchi hizi. Pia mara kwa mara inajidhihirisha kuwa maboresho haya yanatekelezwa kwa msukumo mkubwa toka kwa wafadhili, bila kuzingatia asili ya mchakato wa maendeleo na umiliki wa nchi husika.

Kutokana na machungu ya uzoefu wa kushindwa kufikia malengo katika ushirikiano wa kimataifa wa aina hii, JICA imekuwa na misingi ifuatayo katika kufadhili ugatuaji:

(i) Hakuna modeli moja inayoweza kutumika katika nchi zote.

(ii) Ugatuaji pekee siyo lengo bali ni njia ya kufikia lengo fulani.

(iii) Majadiliano ya kitaifa ni muhimu katika kuasilisha na kukuza maendeleo ya ndani ya nchi.

(iv) Jinsi gani ya kuhakikisha viwango vya chini vya kitaifa vya huduma[2] vinafikiwa ni muhimu katika kuandaa maboresho ya Ugatuaji.

(v) Maboresho ya Ugatuaji ni mchakato mrefu, ambao hautakiwi kuchukuliwa kama mradi.

(vi) Maboresho ya Ugatuaji ya haraka haraka yanaweza kuleta vurugu. Katika kila maboresho ya Ugatuaji (D by D), ni muhimu kuhakikisha kuna mazingira stahiki kwa upande wa Halmashauri na wanajamii kuwezesha kupokea majukumu makubwa yanayogatuliwa.

## 2.0 Changamoto Kubwa Iliyogunduliwa katika Programu ya Tanzania ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na Timu ya Maandalizi ya Mafunzo ya Mwaka 2002

Baada ya maombi ya Serikali ya Tanzania kuhusu kuwepo kwa Mpango wa mafunzo wa maboresho katika Serikali za Mitaa mwaka 2001, JICA iliamua kutuma Timu Maalumu kuchambua hali ilivyo na kuandaa kozi ya mafunzo yenye maudhui thabiti kuweza kutatua masuala muhimu. Timu hiyo ilipofika Tanzania, Novemba mwaka 2002, ilibaini Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania ilikuwa na changamoto zifuatazo:

[2] Viwango vya chini vya kitaifa vya huduma ni nadharia inayoeleza kuwa kiwango fulani cha huduma lazima kifikiwe na wote hata kama ni katika jamii maskini vijijini kama ilivyo mijini.

(i) Bao-mantiki kubwa la programu ya maboresho lenye hatua nyingi za utekelezaji (Zaidi ya kurasa 80)

(ii) Programu ya maboresho ilikuwa ikitekelezwa kwa bao-mantiki zuri sana lenye maelezo ya kina kwa kila hatua bila kuruhusu maboresho/mabadiliko zaidi. Timu iliona kulikuwa na fursa ndogo sana iliyoachwa ya kuweza kufanya mabadiliko ili kuruhusu majaribio ya masuala muhimu. Timu iliona kuwa kila kitu kimeshadhamiriwa, na Serikali ya Tanzania ililazimika kufuata reli hiyo bila kwenda pembeni au kurudi nyuma.

(iii) Programu iliandaliwa kwa msaada mkubwa kutoka kundi la wafadhili.

(iv) Wafadhili wa Mfuko wa Pamoja *“the Common Basket Funding Donors”* pamoja na serikali waliunda kamati ya usimamizi. Kazi ya kuandaa andiko la programu na utekelezaji wake ilifanywa na wataalamu washauri wa nje. Timu ilipata hofu kuwa Programu ya maboresho iliandaliwa bila kupitia mchakato stahiki wa kujenga uelewa ndani ya nchi na kupata makubaliano ya pamoja kulingana na mahitaji yao halisi.

(v) Hatari ya utekelezaji wa haraka haraka wa Ugatuaji wa Madaraka (D by D).

Timu iliona wazi kuwa sera ya ugatuaji wa madaraka (D by D) iliyokuwa ikihamasishwa na Serikali ya Tanzania ni kama vile Tanzania ilikuwa inatafuta modeli ya ugatuaji wa madaraka sawa na ya nchi zilizoendelea. Swali lilijitokeza kama Halmashauri na Wizara zote za Serikali zilikuwa na uwezo na mtazamo wa pamoja kwa mabadiliko haya ya haraka. Timu iliona changamoto zifuatazo katika hili:

- Wizara za kisekta kutokuwa tayari na kuonyesha ukinzani.
- Ukosefu wa majadiliano ya kina kuhusu ugatuaji katika jamii.
- Halmashauri hazikujengewa uwezo wa kutosha kuchukua majukumu yote yaliyogatuliwa.

## 2.3 Uwezekano wa kutumika kwa Uzoefu wa Japani katika Ujenzi wa Taifa na Maboresho ya Ugatuaji - Ujumbe wa Japani uliotolewa kwa Tanzania kupitia Mafunzo ya Osaka.

Baada ya kuona hali halisi ya Tanzania iliyoelezewa hapo juu, JICA iliona kuwa uzoefu wa Japani kwenye ujenzi wa Taifa na Maboresho yaliyokuwa na mchakato wa muda mrefu ya Ugatuaji ungeweza kuwa wa manufaa na muhimu kwa viongozi wa maboresho wa Tanzania kujifunza na kufanyia mapitio maboresho yao.

Japani ni nchi ndogo huko Bara la Asia isiyo na ustaarabu wa Magharibi, ambayo ilianza ujenzi wa taifa kama nchi iliyo nyuma kabisa lakini ikafikia maendeleo ya ajabu. Japani ina uzoefu mwingi wa aina yake wa kutumia mifano (models) ya nje (mfano wa Magharibi) ambayo wafadhili wengine hawana. (Mataifa ya Ulaya yamekuwa mara zote mstari wa mbele na katikati ya dunia na hujiona hayana sababu ya kujifunza toka nje). Kwa kweli, Japani ilianza Ujenzi wa taifa na maendeleo, kwa kujaribu kuiga mifano ya Magharibi lakini ikashindikana mwanzoni kabisa. Tokea hapo ikawa ni mchakato mrefu wa kujaribu na kushindwa mpaka hatimaye ilipofikia Japani ikaunda modeli yake wa kipekee unaoitwa “Nusu Kijapani nusu Kimagharibi”. Nchi ya Japani inaamini kuwa aina hii ya uanzishaji wa mfumo, pamoja na umiliki wake thabiti kwa kufanya mara nyingi marudio ya “kujaribu na kushindwa” ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Mchakato huu ambao Japani ilitumia ili kuanzisha mfumo wake wa Serikali za Mitaa na maboresho ya ugatuaji ni tofauti kabisa na modeli za Ulaya ambazo nchi zinazoendelea zinajaribu kuanzisha kwa sasa. JICA ilifikiri kuwa kuwasilisha "mfumo huu tofauti" unaweza kuwa muhimu, kwani kuwa na modeli moja tu, inaonekana kama vile "ndio njia pekee" hakuna nyingine. Lakini kukiwa na modeli zaidi ya mbili, Watanzania wanaweza wakaanza kulinganisha na kuona ni modeli ipi inafaa zaidi katika mazingira yao, na ni hatua ipi iwe ya kwanza katika kuandaa modeli yao wenyewe.

Ifuatayo ni mifano ya vigezo vya kuvutia vinavyoweza kuigwa toka modeli ya Kijapani kati ya mingi iliyopo:-

**(1) Mchakato wa Maboresho wa taratibu lakini wa uhakika**

Japani ilitumia miaka 110 toka ilipoanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa na Ugatuaji. Kumekuwa na miaka 55 ya Maboresho Makuu baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia kabla ya ugatuaji halisi (D by D) uliofikiwa mwaka 2000. Serikali ilijaribu kuhakikisha kuwa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha kabla ya kugatua majukumu, na siyo kukimbilia kurekebisha taasisi za Ugatuaji (D by D). Uzoefu huu wa Japani unaipa Tanzania fursa ya kufikiria mara mbili kama kasi ya maboresho yake siyo ya haraka sana, na kama nchi inataka kuendelea na mwendo kasi uliopo, basi haina budi kuhakikisha kuwa kunakuwa na mchakato stahiki wa kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa.

**(2) Ukasimishaji wa Shughuli/Majukumu kwa Wakala (Agency Delegated Functions)**

Katika kipindi tajwa cha miaka 55, Serikali ya Japani ilichagua mfumo wa "kukasimu" madaraka kwa Serikali za Mitaa unaojulikana kama "Ukasimishaji wa Shughuli/Majukumu kwa Wakala (Agency Delegated Functions-ADF" kama hatua ya mpito, badala ya kwenda moja kwa moja kwenye Ugatuaji. Kwa sababu ya utaratibu huu Japani ilipingwa sana na nchi za Magharibi kwa kipindi kirefu kuwa haijafanya Ugatuaji sahihi, na mwishoni kabisa Serikali ikaamua kuingia katika Ugatuaji halisi mwaka 2000 na kuondokana na mfumo wa kukasimu (ADF). Hata hivyo sasa hivi imethibitika kuwa ADF ilichangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mfumo mzuri wa Serikali za Mitaa na hatimaye kufikiwa kwa ugatuaji halisi (D by D) nchini Japani hususan katika vipengele vifuatavyo:

- Kutokana na kuwepo na kutumika kwa mfumo wa ADF, Halmashauri zilifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara husika, na zikaweza kujenga uwezo wao kupitia mafunzo kazini (on the job training) kukiwa na usaidizi wa kitaalamu wa karibu toka Wizarani. Kila walipopata changamoto, maofisa wa Serikali za Mitaa waliweza kuwasiliana na maofisa wa Wizara husika kwa simu na maofisa wa Wizara waliweza kusaidia kwa wema na kumaliza changamoto hizo pamoja. Haya yote yaliwezekana kwa sababu kimsingi shughuli zote zilikuwa ni wajibu wa Wizara na zilikasimishwa tu kwa Halmashauri. Hivyo ilipofikia Ugatuaji wa shughuli hapakuwa na ukinzani wowote toka Wizarani, zaidi ya ushirikiano, kinyume kabisa na yanayotokea katika nchi zinazoendelea zinapotekeleza ugatuaji.

- Wazo kuu lilikuwa ni kuhakikisha kuwa raslimali ambazo ni chache zilizopo ndani ya nchi zingeweza kutumika vizuri zaidi kwenye mwelekeo mmoja, yaani maendeleo ya nchi, badala ya kuzigawa na kutengeneza tofauti kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.
- Ilikuwa ni muhimu sana katika hatua za mwanzo ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na uwezo dhaifu. Bila mfumo wa kukasimu (ADF) kipindi hicho Halmashauri zisingeweza ama kufanya vizuri shughuli zao za kuhudumia watu au kujenga uwezo wao.
- Sababu nyingine muhimu ilikuwa mafunzo kazini (OJT). Kuwepo kwa mchakato wa mafunzo kazini (OJT) kwa miaka 55 kuliwezesha watumishi wote wa Serikali za Mitaa pamoja na muundo wao kwa ujumla kujenga uwezo thabiti, kwa kupata ujuzi na utaalamu kutoka Wizarani na kuwa tayari kupokea madaraka pale Serikali Kuu ilipoamua kuyagatua.

Uzoefu huu wa Japani unibua swali la msingi kwa Tanzania juu ya namna gani nchi inaweza kujithibitishia uhakika na ubora wa mchakato wa kuzijengea uwezo Halmashauri ilihali Ugatuaji (D by D) ukiendelea, kuhakikisha matumizi mazuri ya raslimali chache zilizopo nchini na kukwepa kabisa ukinzani toka Wizara za kisekta.

**(3) Utaratibu wa Kubadilishana Watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**

Nchini Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za maboresho, utaratibu wa kubadilishana watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ulitumika sana kama mbinu bora kabisa ya (a) kujaza upungufu wa watumishi hasa wenye sifa katika Halmashauri za pembezoni na (b) kuhakikisha uhamishaji wa ujuzi na utaalamu kutoka kwa wasomi wa Wizara kwenda kwa watumishi wa Halmashauri waliokuwa na ujuzi na uzoefu mdogo ili kujenga uwezo wa Halmshauri hizo.

Serikali iliunda jopo kubwa la maofisa wataalamu katika Wizara ya Serikali za Mitaa na kuwapeleka kwenda kwenye Halmashauri zilizokuwa na uwezo mdogo huko pembezoni ili kuzisaidia. Hatua hii ya uhamisho wa muda ilidumu kwa muda wa miaka 4 - 5 na baadaye watumishi hawa walirudishwa kwenye nafasi zao za kawaida kwenye Wizara zao mama. Kadri walivyokuwa na uwezo wa kitaalamu kuwezesha wengine ndivyo walivyopelekwa kwenye Halmashauri za mbali na zenye udhaifu mkubwa. Pale walipofaulu na kutenda vizuri katika vituo hivi vipya, waliahidiwa kupanda vyeo zaidi wanaporudi, ambayo iliwapa motisha wataalamu hawa waliobobea kwenda kwenye sehemu zisizovutia kwa hamasa ya juu kabisa. Pia Halmashauri nyingi zilipeleka watumishi wao kwenye Wizara mbalimbali kufanya kazi, katika misingi ya mafunzo kazini kwenye maeneo ambayo Halmashauri husika ilihitaji.

Baada ya kurudia mizunguko kadhaa ya kubadilishana watumishi, ujuzi na utaalamu wa kutosha ulihamishwa kikamilifu toka Wizara kwenda Halmashauri, kitu ambacho kilisaidia sana kujenga uwezo wa Halmshauri nchini Japani. Kwa sasa Halmashauri zinajitegemea katika raslimali watu bila kuitegemea Serikali Kuu tena.

Ni dhahiri kuwa ugatuaji wa raslimali watu ukifanyika bila umakini na mbinu za kutatua matatizo, hupelekea upungufu mkubwa wa watumishi kwenye Halmashauri ambazo zipo katika maeneo maskini na pembezoni. Ni kwa sababu hii Tanzania iliamua kurudisha baadhi ya Masuala ya raslimali watu kwa Serikali Kuu. Hata hivyo haina mantiki kuendeleza Ugatuaji

wa madaraka (D by D) bila Ugatuaji halisi wa raslimali watu. Badala ya “0 au 100”, serikali inatakiwa kutafuta mkakati wa namna ya kugatua raslimali watu na wakati huohuo kukwepa kutengeneza upungufu katika maeneo ya vijijini, na kujiridhisha kuwa kuna mchakato wa kujenga uwezo wa baadaye wa Halmashauri.

## 3.0 MASUALA YALIYOJITOKEZA NA KUJADILIWA WAKATI WA MAFUNZO YA OSAKA

Kutokana na upungufu wa nafasi masuala machache tu ya msingi yameweza kuwasilishwa kwenye sehemu hiyo hapo juu, kati ya mambo mbalimbali ya Japani yaliyowasilishwa kwa Tanzania kulingana na Uzoefu wake. Masuala machache yametajwa na kuelezwa kwa kifupi hapa chini.

### 3.1 Masuala ya Jumla

Masuala na maswali yafuatayo yalijitokeza na kujadiliwa wakati wa mafunzo ya Osaka:

**(1) Umuhimu wa kukuza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama kigezo cha mafanikio ya Ugatuaji**

- Je hakuna hatari ya kudidimiza utoaji huduma, kugatua wajibu mkubwa kiasi hiki ndani ya muda mfupi?
- Ni namna gani ya kukabiliana na hali halisi kuwa Halmashauri zinahitaji uwezo zaidi ili kutekeleza shughuli zilizogatuliwa?
    - Vipi kuhusu ajira? Namna gani itawezekana kupata watumishi wenye sifa katika Halmashauri zilizopo kwenye maeneo maskini na pembezoni?
    - Ni jinsi gani ya kuziba pengo kati ya ujuzi na uzoefu katika Serikali za Mitaa na kuziendeleza? Je siyo muhimu kwanza kuweka mbinu za kuhamisha ujuzi na utaalamu, pamoja na usaidizi wa kitaalamu kutoka Serikali Kuu kwenda Halmashauri? Siyo muhimu kwanza kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Halmashauri badala ya kutegemea misaada toka nje mara kwa mara?

**(2) Ugatuaji na Maendeleo**

- Ili kuweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi na kwa raslimali chache zilizopo, ni muhimu kutafuta mbinu mkakati ya kuzitumia raslimali hizi (hivi ndivyo ambavyo Japani imekuwa ikifanya kujiletea maendeleo yake).
- Jinsi gani ya kusimamia maendeleo ya nchi na ugatuaji kwa pamoja ambapo mara kadhaa hupingana. Jinsi gani ya kuhakikisha kuwa hakutakuwa na utengano wa raslimali na kutofautiana/kutokuelewana kati ya Serikali Kuu na Halmashauri au kati ya Halmashauri zenyewe?

**(3) Ugatuaji na Viwango vya chini vya kitaifa**

- Jinsi gani ya kusimamia ugatuaji na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa? Ni jinsi gani itahakikishwa kuwa Halmashauri zilizopo vijijini zitakuwa na uwezo wa kutosha wa raslimali watu na fedha kama zilivyo Halmashauri zenye uwezo katika kigezo cha utoaji huduma kwa watu?

**(4) Ukweli Kuhusu Uwezo wa Halmashauri kuweza Kutoa Huduma**

- Swali liliulizwa; Ni Maofisa Ugani wangapi waliopo katika Halmashauri ukijumuisha na wale ambao wanatumikia katika Kata na Vijiji, swali hili liliulizwa kwa washiriki ili kuwafanya waelewe hali ilivyo mbaya ambayo Halmashauri za Tanzania zinatakiwa kukabiliana nayo. Ukichukua Mkoa mmoja kama mfano, Mkoa wa Nagano nchini Japani, ni mkoa mdogo kabisa ulioko maeneo ya vijijini lakini una maofisa ugani wa kilimo wapatao 1500. Pia kuna Halmshauri 77 za ngazi za chini katika Mkoa huu ambazo kila moja inaajiri maofisa ugani kati ya 20 – 30. Maana yake ni kuwa wakulima katika Mkoa (prefecture)[3] wa Nagano wanafurahia huduma zinazotolewa na zaidi ya maofisa ugani 3,000 wa Halmshauri ikilinganishwa na wakulima wa Tanzania ambao wana maofisa ugani wasiozidi 100[4]. Pia nchini Japani kuna mashirika mengi ya binafsi yanayouza mashine za kilimo, mbolea, madawa, mbegu n.k pamoja na taasisi za ushirika zilizo imara; zote hizi hutoa huduma mbalimbali za ugani na ushauri wa kitaalamu.
- Ni vyema kutambua ukweli kuhusu hali ngumu iliyoelezwa hapo juu na kuanzisha mkakati mpya. Hatutakiwi kuota ndoto kwamba Tanzania inaweza kufikia kutoa huduma nzuri kama za nchi za viwanda kwa idadi ndogo hivi ya watumishi kwenye eneo lote hata kama Serikali Kuu itaamuwa kufanya kila kitu peke yake.

**(5) Umuhimu wa Juhudi za Wananchi na Ushirikiano kati ya Halmashauri na Jamii**

- Kwa sababu ya hali ngumu iliyotajwa hapo juu, haikwepeki kutumia kwa kiasi kikubwa Uwezo wa watu na Juhudi za kujitegemea ili kutoa huduma zilizo bora.
- Ni imani ya JICA kuwa kama watu wataongozwa na kuwezeshwa vizuri, wana uwezo wa kufanya mambo mengi wenyewe, kama kujenga shule za msingi, zahanati, barabara zao na kuzitunza.
- Kwa Japani pia, kipindi cha hatua za mwanzo za Maendeleo, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga shule za msingi. Kwa mfano, watu katika jamii zao walichangia kutoka mifukoni mwao na wakafanya kazi pamoja kujenga shule, na hatimaye wakatafuta watu wanaoweza kufundisha na wakawalipa mishahara yao. Ndiyo maana shule nyingi za kipindi hicho hazikuwa za “umma” bali “binafsi”, kwa maana ya “shule zinazomilikiwa na

[3] Mkoa (prefecture) huko Japani ni karibu sawa na Wilaya za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. (Ingawa Wilaya nyingine za Tanzania ni kubwa sana kuliko Mikoa ya Japani).

[4] Pamoja na hayo Japani siyo nchi ya kipekee kuhusu suala hili. Cha kushangaza Japani ni nchi yenye idadi ndogo kabisa ya watumishi wa umma kwa idadi ya watu waliopo ikilinganishwa na nchi zilizoendelea kiviwanda. Hii ina maana kwamba Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia n.k zina idadi kubwa ya watumishi wa Serikali.

jamii; ilikuwa ni baada ya miongo kadhaa, Serikali ilipotajirika na kuanza kuzimiliki na hatimaye kuwa shule za umma.

- Inahitaji mabadiliko ya fikra na mtazamo wa Serikali na Watu, kutoka fikra kuwa ni jukumu la Serikali kutoa huduma zote kwa watu kuelekea mtazamo kuwa watu wanaweza kufanya mambo mengi kwa juhudi zao wenyewe na Serikali ikawezesha mchakato huo badala ya kuachwa itekeleze peke yake.

**(6) Umuhimu wa Kuainisha vigezo Sahihi vya Ukubwa wa Serikali za Mitaa, na Kuweka Utaratibu Bunifu wa kutoka ngazi ya Halmashauri hadi kuifikia Jamii**

- Kutokana na hitaji lililotajwa hapo juu ni muhimu kuweka utaratibu bunifu na imara sana wa Halmashauri kuifikia jamii. Hapa Tanzania, Halmashauri za Wilaya ni kubwa mno, hivyo ni muhimu kufikiria jinsi ya kujenga daraja kati ya Halmashauri na jamii.
- Kutokana na wazo la kuimarisha madaraka kwa umma, eneo la Halmashauri linatakiwa kuwa dogo kiasi cha kuwezesha wananchi kuona kuwa sehemu hiyo kweli ni yao. Kwa upande mwingine sehemu hii ndogo ya Serikali za Mitaa inatakiwa iwe na uwezo wa kutosha kutoa huduma zinazokidhi mahitaji na hii inahitaji kiwango cha raslimali fedha na watu cha kutosha. Haya ni mahitaji mawili muhimu yanayokinzana.
- Ili kuwa na majibu mazuri ya kutosheleza kuhusu suala hili la ukinzani, suluhisho pekee ni kuwa na mfumo wenye ngazi nyingi kutoka Halmashauri hadi kwenye jamii. Kwa Japani mfumo huu wa ngazi nyingi unafanya kazi vizuri. Lakini Tanzania pia ina mfumo mzuri wenye wilaya – kata – kijiji – kitongoji. Mfumo huu una faida katika kuimarisha madaraka kwa umma na jitihada shirikishi za maendeleo kati ya Halmashauri na jamii. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii (O&OD) unaweza kuwa jukwaa zuri zaidi la kuboresha mfumo huu na kuuwezesha kufanya kazi vizuri zaidi.

### 3.2 Usimamizi na Ugatuaji wa Raslimali Watu

Kama ilivyo kwenye sehemu iliyotangulia, mafunzo ya Osaka yalitoa tahadhari kwa Viongozi wa Tanzania katika miaka michache ya mwanzo kuwa waangalifu kuhusu kutoharakisha kugatua na kupeleka madaraka kwa umma maarufu kama *D-by-D*. Hata hivyo, kuhusu ugatuaji wa masuala ya rasilimali watu, ujumbe ulikuwa tofauti kidogo kwa vile ilionekana kwamba mamlaka ya uteuzi wa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa Halmashauri yalikwisha anza kurudishwa Serikali Kuu, pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuendesha mchakato wa ajira kwa kada nyingine za watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nchi ya Japani haikugatua madaraka na kuyapeleka Halmashauri kwa haraka, bali Serikali Kuu ilendelea kuhodhi baadhi ya shughuli. Kwa mantiki hii, ugatuaji nchini Japani haukuwa umekamilika kwa miaka mingi mpaka ilipofika mwaka 2000. Hata hivyo, kuhusiana na kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu, Japani ilihakikisha kwamba madaraka haya yamegatuliwa na kupelekwa Halmashauri kikamilifu tangu mwanzo kabisa wa maboresho.

Hii ni kwa sababu kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu ndiyo jambo la muhimu sana na msingi wa ugatuaji. Kulingana na mfumo wa Serikali za Mitaa Japani, masuala yote huamuliwa na kutekelezwa ndani ya Mamlaka za Serikali Mitaa husika bila kuingiliwa na Serikali Kuu, yaani kuajiri na kufukuza, kuendesha mafunzo, kupanga ngazi za mishahara, kufanya uhamisho, kupandisha vyeo , mpaka kustaafu. Mamlaka za Serikali za Mitaa Japani huajiri wahitimu wapya kutoka vyuo vikuu kila inapofika mwezi Aprili (mwanzo wa mwaka wa fedha nchini Japani) kulingana na mahitaji yao. Wahitimu walioajiriwa na Mamlaka fulani ya Serikali za Mitaa, wataitumikia Mamlaka husika kwa maisha yao yote mpaka watakapostaafu. Hakuna Kanuni ya uhamisho kutoka Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa kwenda mamlaka nyingine.

Zaidi ya hayo, Mameya ni wanasiasa na huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kura, na ndio wakuu wa eneo la Utawala/Utendaji na huwajibika kwa Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Watendaji wa Halmashauri wanawajibika kwa Meya na siyo kwa Madiwani, kwa hiyo masuala ya watendaji hulindwa na huwakilishwa na Meya katika Baraza la Madiwani na kwa Madiwani.

Kwenye mafunzo ya Osaka, mambo matatu yafuatayo yalitiliwa mkazo kama ndivyo vipengele muhimu katika kufikia kiwango cha juu cha rasilimali watu katika Halmashauri:

1) <u>Kuajiri</u>
   Kuajiri watumishi <u>bora na wanaofaa</u> katika kufikia dhima/malengo ya mamlaka husika,
2) <u>Mafunzo</u>
   Baada ya kuajiri, <u>kuwapa mafunzo</u> yanayolenga na kuwezesha kufikiwa kwa <u>dhima/malengo</u> ya mamlaka husika (siyo malengo ya mtu binafsi),
3) <u>Kutumia Rasilimali watu Ipasavyo</u>
   Kuhakikisha kuwa <u>uwezo wote wa Raslimali watu katika Halmashauri unatumika kikamilifu</u> ili kutimiza malengo ya mamlaka husika.

Kwa minajili hiyo, Japani iliona kuwa ni jambo lisilokwepeka kutangulia kugatua madaraka yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu ili kila Halmashauri iweze kuchambua hali yake halisi, kupanga mipango, kuajiri, kutoa mafunzo, kutumia rasilimali watu ipasavyo. Mtumishi wa Halmashauri lazima awe mtu anayelipenda eneo husika na watu waliopo, anayefanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu, anayeelewa vizuri kuhusu hali ya eneo husika, anayewafahamu watu vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na wakazi wa eneo husika; hii ndiyo mantiki ya ugatuaji. Ni uzoefu wa nchi ya Japani kwamba, kwenye Halmashauri zenye mafanikio ya kuridhisha, kuna maofisa na watendaji wanaofanya kazi kwa kujituma hasa katika kuwahudumia watu, na kushirikiana na wakazi; na walio wengi wao ni wale watendaji waliozaliwa na kukulia katika maeneo hayo na wanayapenda makazi hayo, pamoja na uongozi thabiti wa Meya ambaye naye ni mzawa.

Jambo jingine muhimu linalozifanya Halmashauri za Japani ziwe na nguvu ni juhudi waliyonayo katika kuwapa watumishi wao mafunzo. Halmashauri za Japani zinawekeza sana kwa watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo pamoja na mpango wa mafunzo kazini ambao uko kimkakati kulingana na mahitaji ya kitaasisi (siyo mahitaji binafsi) na kwa mtazamo wa mbali.

Hili linawezekana kule Japani kwa sababu hakuna uhamisho wa watumishi toka Halmashauri moja kwenda nyingine na kiwango cha kufanya watumishi waendelee kubakia kwenye Halmashauri iliyomwajiri ni kikubwa sana, hivyo Halmashauri huwekeza bila hofu ya kuwapoteza baada ya kuwasomesha watumishi wake. Tofauti na Tanzania ni vigumu sana watumishi kubakia kwenye Halmashauri moja kwa muda mrefu kutokana na uhamisho wa mara kwa mara wa watumishi muhimu kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine. Katika hali kama hii, changamoto kubwa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba matokeo yatokanayo na mafunzo ya watumishi yanaendelezwa ili kuboresha utendaji kazi wa Halmashauri husika, na kuzifanya Halmashauri ziwe makini katika kujenga uwezo wa watumishi licha ya uwezekano mkubwa wa kuwapoteza baada ya kuwasomesha. Swali liliibuka kwenye mafunzo ya Osaka endapo Tanzania inaweza kuandaa na kutekeleza mpango mkakati na thabiti wa muda mrefu wa mafunzo ya kuwajengea watumishi wake uwezo katika mazingira haya.


Kwa upande mwingine, mafunzo ya Osaka yaliibua suala la “kufanya kazi kama timu” ili kuweza kutumia asilimia 120 ya uwezo wa nguvu kazi iliyopo na kuyafikia malengo ya kitaasisi. Katika Nchi ya Japani, yapo mambo kadhaa kuhusu mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu ambayo yamefafanuliwa kwa uangalifu mkubwa kama vile:

1) Ngazi za mishahara zimepangwa kwa lengo la kuondokana na rushwa na kuchochea watumishi wafanye kazi kwa bidii hadi watakapostaafu,
2) Mfumo wa kipekee wa Japani wa “kucheleweshа upandishaji vyeo” humfanya kila mtumishi afanye kazi kwa bidii kwa miaka mingi kabla ya kupandishwa cheo (kutumia asilimia 120 ya uwezo wa kila mmoja),
3) Watumishi kufanya kazi kwa kuzunguka kila idara ya Halmashauri husika na mtindo wa kuweka kumbukumbu za kila mwaka za utendaji wa kila mtumishi ili kufanya tathimini kwa haki na kwa malengo na kuchagua wale wenye uwezo mkubwa na wanaostahili kupandishwa vyeo kuwa Wakurugenzi,
4) Shughuli zote zinazohusu rasilimali watu ziko chini ya Idara ya Uendelezaji Rasilimali Watu ili iwezeshe namba 3 hapo juu,
5) Mazingira ya kipekee ya Japani yanawezesha “utendaji kazi kama timu”, usimamizi unaofanywa na wakuu/viongozi, na mafunzo kazini yanayoendeshwa na wasimamizi kwa kutumia chumba kikubwa (ofisi ya wazi inayotumika na watumishi wote wa idara au kitengo husika).

Yote yaliyoelezwa kwenye kifungu hapo juu yanatekelezwa na Mamlaka za SM za Japani ili kuhakikisha mambo matatu yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu yanazingatiwa yaani 1) Kuajiri; 2) Mafunzo; na 3) Kutumia rasilimali watu ipasavyo.  Swali liliibuliwa ni kwa jinsi gani katika mazingira ya sasa ya Halmashauri za Tanzania zinaweza kutekeleza mambo haya matatu.

**3.3 Fedha za Serikali za Mitaa na Ugatuaji wa Masuala ya Fedha**

**a) <u>Misingi ya kifedha katika Halmashauri</u>**





Michoro (1) na (2) inaonyesha picha halisi ya masula ya fedha katika Halmashauri za Japani.


Mchoro (1) unaonyesha majukumu makubwa yanayotekelezwa na Halmashauri za Japani ikionyesha matumizi ya kila sekta. Kwa mfano sekta ya afya, Halmashauri hutumia 94% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya afya ya taifa na Serikali Kuu hutumia 6% tu. Sekta ya elimu uwiano kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ni 85% kwa 15%. Ukizingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uzito wa majukumu na matumizi, Halmashauri za Japani zinafanya sehemu kubwa zaidi ya majukumu ya Serikali ya kutoa Huduma. Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba kiasi kikubwa cha bajeti <u>hutengwa</u> kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu mazito yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao.

Hali ikoje kwa Tanzania? Ukweli ni huu, ukiangalia majukumu yote yaliyogatuliwa na kupelekwa kwenye ngazi za msingi katika Halmashauri Tanzania, ukubwa wa majukumu ni sawa tu na yale ya Halmashauri za Japani. Lakini, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri za Tanzania, ilikuwa pungufu ya shilingi trilioni 3 ya bajeti ya taifa ambayo ni zaidi ya shilingi trilioni 11 kwa mwaka wa fedha 2011/12.

Ulinganisho mwingine wa kuvutia, ni ule unaohusu Halmashauri kuwa na uhuru kwenye bajeti zao. Mchoro (2) unaonyesha viwango na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri za Japani. Kama ilivyothibitishwa na takwimu hizi, 53% ya mapato hutokana na vyanzo vya ndani (kodi, ushuru na ada). Pia kuna <u>ruzuku ambazo hazina masharti yoyote ya matumizi</u> zinazoitwa “ruzuku toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa ” (ruzuku za Local Allocation Tax, LAT). Ruzuku ya LAT ni <u>fedha nyingi inayotoka Serikali Kuu kwa mara moja</u> kwenda Serikali za Mitaa na Serikali za Mikoa. Fedha hii inahamishwa toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti kuu ya kila Halmashauri <u>siku ya kwanza ya kila robo mwaka</u>. Ukijumlisha mapato ya ndani na ruzuku za LAT toka Serikali Kuu, Halmashauri za Japani zina aslimia 75% ya bajeti yao isiyo na masharti na wanaweza kutumia kama wanavyoamua wenyewe. Mchanganuo huu ni wa muhimu sana kwa Halmashauri za Japani katika kufikia malengo ya mipango yao ya maendeleo, kwani wana bajeti ya kutosha na ya uhakika kila mwaka. Washiriki toka Tanzania walipochunguza hali za Halmashauri za kwao, walithibitisha kwamba zina hali mbaya kifedha na kiasi kikubwa cha fedha wanayopokea ina masharti ya matumizi kama ilivyo kwenye Mchoro (3).




Mchoro(2): Vyanzo na viwango vya mapato ya SM za Japani
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010
(Ministry of Home Affairs of Government of Japan)




Mchoro (3): Muundo wa vyanzo mapato ya SM za Tanzania
Chanzo: Ni hesabu zilizofanywa na mwandishi toka tovuti ya serikali ya Tanzania


Kwa hakika, ingelikuwa jambo la maana endapo 94% ya ruzuku inayopokelewa na Halmashauri isingelikuwa na masharti. Hata hivyo zipo aina nyingi za ruzuku na baadhi yake zina masharti katika matumizi. Hivyo basi, hata kama Halmashauri itaandaa mipango mizuri ya maendeleo, ni vigumu sana kutekeleza miradi yao ya vipaumbele kwa sababu ya ruzuku zenye masharti, ambazo husababisha mipango ya maendeleo isitekelezeke kirahisi.

Zaidi ya hayo kiasi cha fedha inayotengwa kwenye bajeti za Halmashauri ni kidogo mno (Shilingi trilioni 3 kati ya trilioni 11 za bajeti ya taifa, 2011/12). Hizi Shilingi trillioni 3 ni sawa na 94% ya bajeti nzima ya Halmashauri, na hii inathibitisha jinsi ambavyo hazina vyanzo vya ndani vya kutosha.

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Serikali ya Tanzania kutenga kiasi cha kutosha cha bajeti kutekeleza wingi wa majukumu ya Halmashauri yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao kama kweli wameazimia kufikia ugatuaji wa madaraka. Fedha hizi zinaweza kuwa zile za kutoka vyanzo vya ndani au katika ruzuku isiyo na masharti[5]. Kama hakuna bajeti ya kutosha inayotengwa, basi hakuna sababu ya kugatua majukumu kwenda ngazi za Halmashauri. Vinginevyo, shughuli hizo

[5] Kwa hakika, bado haishauriwi kugatua madaraka ya kifedha na kuwapa Serikali za Mitaa mamlaka makubwa ya kutoza kodi kwa sasa. Hali hii itaziumiza Serikali za Mitaa zilizo kwenye maeneo yenye ufukara, kwa vile hazina vyanzo vya uhakika vya kodi, huku Serikali za Mitaa tajiri zitakuwa na mapato mengi kutoka vyanzo vyao vya ndani. Kwa hiyo ni busara zaidi kuendelea kutoa ruzuku kutoka chanzo kimoja, lakini Serikali za Mitaa ziwe na uhuru na maamuzi ya kuzitumia kulingana na vipaumbele vyao kwa sasa.

hazitatekelezwa na hatimaye jamii zitaathirika kwa kukosa huduma. Kama tulivyoona kwa Halmashauri za Japani, ikitokea kwamba 85% ya majukumu ya kutoa huduma za elimu yamegatuliwa na kupelekwa ngazi za Halmashauri, basi kiasi cha bajeti kulingana na majukumu hayo hugatuliwa na kupelekwa Halmashauri ili kufikia malengo. Vinginevyo si haki hata kidogo kwa Halmashauri na hasa kwa watu wanaotegemea huduma.



Mchoro (4): Aina za Kodi kwenye Majiji/Miji
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010 (Ministry of Home Affairs of Government of Japan)

**b) <u>Kodi za Ndani kwa Ustawi Endelevu wa Serikali za Mitaa</u>**

Katika Nchi ya Japani kuna falsafa ya wazi kuhusu mgawanyo wa kodi za ndani zinazotengwa katika ngazi zote mbili za Serikali za Mitaa. Wilaya (Prefecture) ikiwa ngazi ya juu za Serikali za Mitaa na Vijiji, Miji na Majiji (municipalities) zikiwa ngazi za chini za Serikali za Mitaa[6]. Pamoja na kwamba Wilaya (Prefecture) ndiyo ngazi ya juu ya Serikali za Mitaa nchini Japani, bado zinaweza kulinganishwa na Halmashauri za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. Kuhusu majukumu, ngazi za chini za Serikali za Mitaa Japani (Municipalities) ndizo zinalinganishwa na ngazi za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa Tanzania. Hata hivyo nchini Japani, huduma zote za muhimu kwa jamii hutolewa na Majiji/Miji (Municipalities) kwa sababu ndizo ngazi za msingi zilizo karibu na watu, wakati Wilaya (Prefecture) zinahusika zaidi na maendeleo ya kiuchumi kwa vile majukumu haya yanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya mipango na kuyatekeleza kimkakati.

Kwa kuzingatia aina ya majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa na Majiji/Miji, zifuatazo ni aina halisi ya kodi ambazo zimeruhusiwa kutozwa.

Kama inavyoonekana katika mchoro (4), kodi za majengo na mali zisizo hamishika ni sawa na 45.3% ya mapato yatokanayo na kodi, ambayo ni karibu na nusu ya mapato yote yatokanayo na kodi. Pamoja na "Kodi ya mkazi"(kodi ya Kichwa) na "kodi ya mipango miji" inakuwa ni zaidi ya 80% ya mapato yatokanayo na kodi. Kodi za Majengo na kodi ya mipango miji hutozwa kwenye ardhi na majengo na hizi ni kodi ambazo hazikwepeki. Kwa kuwa ardhi yote na majengo yote yamesajiliwa na kuthaminiwa vizuri, vyanzo hivi viwili ni vya uhakika kwa Serikali za Mitaa.

"Kodi ya mkazi wa Halmashauri za Japani" ni sawa na "kodi ya kichwa" iliyofutwa hapa Tanzania iliyojulikana kama "kodi ya maendeleo"[7]. Chanzo hiki cha kodi pia huwa ni chanzo cha kuaminika kwa sababu wakazi wote wameandikishwa na Halmashauri inajua wanapoishi. Tukiangalia hali ya Tanzania, vyanzo vingi vya mapato ni vile vinavyohusiana na shughuli za kiuchumi, mfano ushuru wa mazao (23%), ushuru wa huduma (18%), ushuru wa nyumba za kulala wageni(3%), leseni

[6] Kuna Prefecture/Wilaya 47 na (Munispaa) 1,742 hadi kufikia Octoba 2012. Manispaa za Japani zinajumuisha **<u>Majiji, Miji na Vijiji</u>**, na tofauti na mgawanyiko wa ngazi za SM za Tanzania.

[7] Tofauti pekee ni kwamba kodi ya kichwa Tanzania ilitozwa kwa kiwango sawa kwa kila mtu, kwa Japani kodi ya mkazi hutozwa kulingana na viwango vya kipato cha kaya. Kama hakuna kipato au kipato hakifikii kiasi kinachokubalika kutozwa, wanakaya hawana sababu ya kulipa kodi ya mkazi.

(10%), ada na malipo mbalimbali (17%), ambazo hubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa eneo husika, na wakati kodi ya majengo ni 8% tu ya mapato yatokanayo na kodi.

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kubaini kuwa ili Halmashauri ziweze kutoa huduma endelevu zinazohitajika kwa wakati na viwango vinavyotegemewa, ni lazima kujenga wigo mpana na mfumo wa uhakika wa kukusanya kodi ndani ya Halmashauri zenyewe. Kutokana na uzoefu wake Japani inaamini kwamba bila kuweka msisitizo kwenye vyanzo vyenye uhakika vya kodi/ushuru kama vile kodi za majengo, kodi ya kichwa/kodi ya maendeleo, siyo rahisi hata kidogo kutarajia Halmashauri zifanye vizuri. Kwa misingi hii, ni muhimu kuwa na mfumo wa daftari la kuandikisha ardhi na mali zisizo hamishika pamoja na daftari la wakazi wote kwa kila Halmashauri, hii itasaidia nchi nzima siyo tu kwenye masuala ya kukusanya mapato, bali kwa makusudio mengine zaidi.

Kwa mantiki hii, inafaa kusema kwamba tayari Tanzania kuna mifano mizuri inayofaa kuigwa kutoka Halmashauri zinazotekeleza kile kinachopendekezwa hapa. Rejea mbinu bora za Halmashauri za Wilaya ya Ushetu na Bukoba katika sura ya tatu ya kitabu hiki.

### 3.4 Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa – Uzoefu wa Kuvutia wa dhana ya Japani ya "Kijiji kimoja zao moja" au (OVOP Movement)"

Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa limekuwa suala la kipaumbele kwa Wakurugenzi wa Halmashauri Tanzania. Kuhusiana na hili, kuna uzoefu maarufu nchini Japani wa dhana ijulikanayo kama "kijiji kimoja zao moja" maarufu kama OVOP movement, iliyoanzia kwenye Wilaya (Prefecture) ya Oita ambayo hapo awali ilikuwa moja ya Wilaya fukara kuliko zote nchini humo. Uzoefu unaotokana na dhana hii unaweza kuwa muafaka kwa Tanzania kama utatafsiriwa na kutumika inavyostahili kulingana na mazingira ya Tanzania.

#### (a)Nini Dhana ya Kijiji Kimoja Zao Moja (OVOP Movement)?

Dhana hii ya "kijiji kimoja zao moja" au OVOP ni mkusanyiko wa ubunifu wa shughuli za maendeleo ya jamii zilizobuniwa na kupata msukumo wa viongozi kutoka jamii husika katika Wilaya (Prefecture) ya Oita, ambao waliipenda jamii yao na kuhofia hali ya ufukara iliyokuwepo. Ingawa juhudi kama hizo za mtu mmoja mmoja zilikuwepo hapa na pale kwenye Wilaya (Prefecture) ya Oita tangu miaka ya 1960, dhana ya "kijiji kimoja zao moja" au *OVOP movement* ilianzishwa rasmi mwaka 1979 na Dkt. Morihiko HIRAMATSU, aliyekuwa Gavana[8] wa Wilaya hiyo kwa kuanza kuzitambua baadhi ya juhudi za jamii zilizokwisha anza na kuziendeleza.

Katika kumwelezea Dkt. HIRAMATSU, alikuwa ni msomi mwenye mafanikio makubwa akiwa mtumishi wa cheo cha juu kwenye Wizara ya Biashara za kimataifa na Viwanda yaani "Ministry of International Trade and Industry (MITI)". Hii ilikuwa Wizara yenye nguvu sana, lakini aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi kwenye Wilaya ya Oita yaani nyumbani kwao. Kilichomsukuma ni kwa

[8] Cheo cha Gavana wa Prefecture ni cheo cha juu zaidi kwenye SM za juu Japani ikilinganishwa na Meya wa kwenye SM za Tanzania (Ona "3.2. Usimamizi wa Rasilimali Watu na Ugatuzi wa madaraka" kwa Meya.)

sababu alihofia sana kuwa Wilaya ya nyumbani kwake iliendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuwa miongoni mwa Wilaya fukara kuliko zote nchini Japani kwa wakati huo.

Baada ya kurudi kwao, aligombea na kushinda cheo cha Ugavana wa Wilaya ya Oita. Alipoanza kazi hii jambo la kwanza alilolifanya ni kutembelea vijiji vyote kwenye Wilaya hiyo. Wakati akifanya matembezi haya, alikuta miradi ya maendeleo na jitihada mbalimbali za watu wenyewe kujaribu kujinasua huko vijijini. Aliguswa sana na jitihada hizo za wananchi wakiongozwa na viongozi wao wenye mapenzi mema na juhudi hizi zilikuwa hazijulikani kwa serikali. Alithamini sana juhudi za jamii, na akawatia moyo waendelee na jitihada za kujikwamua. Kwa wanavijiji, wengi wao walikuwa hawajawahi kutoka nje ya vijiji vyao, kwa hiyo kwao ilikuwa ni faraja kubwa kutembelewa na mtu mkubwa kama Gavana na kusifiwa kwa kile walichokuwa wanakifanya!. Hawakuwahi kuwaza kwamba kile walichokuwa wanakifanya kilikuwa ni kitu cha kipekee na cha thamani machoni pa wengine. Tangu Gavana wao Dkt. HIRAMATSU alipofanya matembezi haya, juhudi hizo za jamii zilipewa msukumo mkubwa na watu wakahamasika zaidi na kujisikia fahari wenyewe.

Kwa upande wake, Dkt. HIRAMATSU alifikiri ni jukumu muhimu kwa Serikali ngazi ya Wilaya kuunga mkono na kuendeleza juhudi za thamani kubwa kama hizi zilizoanzishwa na wananchi kutaka kuboresha maisha yao wenyewe, kuzieneza zaidi na kubadilishana uzoefu huu mzuri baina ya viongozi wa vijiji ndani ya Wilaya yao.

Vuguvugu la “kijiji kimoja zao moja” lina mambo muhimu yanayolitofautisha na dhana nyingine kwani vuguvugu hili hupelekea kuzalisha bidhaa za kipekee (ikijumuisha utalii), ili kupata maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii husika. Hata hivyo, jambo jingine la tofauti kwenye vuguvugu la “kijiji kimoja zao moja” ni kwamba: kuna uzoefu thabiti wa jamii unaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi midogo ya maendeleo ya shughuli za kiuchumi ngazi za msingi. Wananchi husika huunganisha uwezo wao wa kujipanga na kutekeleza mustakabali wa maisha yao; jamii zimejijengea uwezo, zimeamka na zina ujasiri; Jamii zimeimarika na zimefikia uwezo wa kujitawala na kujiendesha zenyewe kama kijiji. Ukweli uliopo hapa ni kwamba wananchi wana uzoefu wa kufanikiwa na wakati mwingine kushindwa (lakini wamejijengea uwezo na tabia ya kujikwamua katika kushindwa huko), siyo tu kwamba jamii inategemea kupata mafanikio ya kiuchumi pekee, bali pia jamii inatarajia kujijengea uwezo, uzoefu na ujasiri na kupata nguvu zaidi katika mchakato huo. Ni jambo la msingi kuelewa ukweli huu ili kufahamu vizuri vuguvugu la “kijiji kimoja zao moja”. Ikumbukwe kwamba ni rahisi sana kupata mafanikio au faida ya mara moja katika biashara au mradi fulani kutokana na ufadhili mkubwa kutoka nje ya jamii, lakini kama jamii hiyo itakumbana na vikwazo fulani fulani baadaye, hawataweza kuvishinda kama watakuwa hawajajijengea uwezo kupitia michakato iliyotangulia ya kutatua matatizo yao kwa nguvu na jitihada zao wenyewe.

Kwa mantiki hii, inavutia kutambua kwamba nyingi kati ya juhudi zilizojitokeza kwenye vuguvugu la “kijiji kimoja zao moja” kule Oita, zilipitia mchakato ufuatao:

- Kabla ya vuguvugu la “kijiji kimoja zao moja” au OVOP, wanavijiji wa Oita walikuwa fukara sana, walikuwa wamekata tamaa kuhusu mabadiliko, wenye kijicho na kuoneana wivu wao kwa wao, kutokana na hali hii haikuwezekana kushirikiana baina yao ili kuboresha maisha kwa pamoja. Hata hivyo, kupitia Vuguvugu la “kijiji kimoja zao moja” walianza

kujitambua kwamba "Ndiyo, tunaweza kama tunataka!" Haya ni mafanikio makubwa katika mchakato wa kubadili fikra.

- Katika badiliko la fikra hapo juu, wanavijiji walianza kujijengea uzoefu wa kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali ndani ya jamii, wakizikabili changamoto wanazokutana nazo na kuzishinda kwa pamoja. Mchakato huu uliwafanya waweze kujipanga vizuri na vizuri zaidi.
- Kupitia mchakato huo huo, waliimarisha mahusiano na taasisi za nje zenye usaidizi ikijumuisha Halmashauri na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Pamoja na ujenzi wa uwezo wa jamii ulioelezwa hapo juu, jamii husika zilifanikiwa kupata matokeo dhahiri ya maendeleo ya kiuchumi.

**(b) Dkt. HIRAMATSU alifanya nini akiwa Gavana wa Wilaya?**

Kwanza kabisa, ieleweke vizuri kwamba vuguvugu la "kijiji kimoja zao moja" halikuwa ni programu ya maelekezo ya kutoka juu kwenda ngazi za msingi iliyoandaliwa na Dkt. HIRAMATSU na kuwaambia watu cha kufanya. Kwa bahati mbaya, baadhi ya nchi zinazoendelea ambazo zilivutiwa na vuguvugu la "kijiji kimoja zao moja", waliuelewa vibaya ukweli huu. Walizingatia tuu zile faida za kiuchumi zinazotokana na vuguvugu la OVOP na kulifanya kama sera ya taifa wakitumia utaratibu wa kutoa maelekezo kutoka ngazi za juu kwamba kila kijiji kizalishe kitu ambacho kinaweza kuuzwa ndani na nje ya nchi. Kinyume na haya, alichokifanya Dkt. HIRAMATSU kwenye Wilaya ya Oita ilikuwa ni, kwanza, kutembelea vijiji vyote, kuzitambua juhudi za wananchi za thamani ambazo zilikwishaanza, akiwasifia na kuwatia moyo.

Pili, alivitaarifu vijiji vingine na viongozi wao kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa ili habari hii iwe kichocheo, waanze na wao kufikiri kuhusu maendeleo yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo husika, badala ya kulalamika kuwa hawana chochote kwenye vijiji vyao na kukata tamaa.

Tatu, alipotambua bidhaa fulani za kipekee kwenye baadhi ya vijiji, alivisaidia kutafuta soko la ndani na nje ya Wilaya ya Oita. Alitumia maarifa yake, uzoefu na mitandao ambayo alikwisha jijengea alipokuwa afisa wa ngazi za juu Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda. Alizitangaza bidhaa hizi nchi nzima.

Nne, aliwezesha suala zima la kubadilishana uzoefu baina ya viongozi wa vijiji husika ili wajifunze na kuhamasika kutokana na kujifunza kwa watu walio kwenye ngazi moja na siyo kujifunza kwa waliopo kwenye ngazi tofauti ya maendeleo. Alianzisha shule ya kuendeleza rasilimali watu[9]" iliyoitwa "*Toyonokuni*[10]. Juhudi hizi za Gavana, zilisaidia kuchochea ari ya viongozi na hii ikapelekea kuibuka kwa miradi mingi yenye sura ya "kijiji kimoja zao moja".

Kama inavyoonekana hapo juu, "kijiji kimoja zao moja" ni vuguvugu lililoambatana na jitihada mbalimbali za jamii zilizotambuliwa, kuzisifiwa, kutiwa moyo na Halmashauri. Jukumu la Halmashauri lilikuwa ni "uwezeshaji" na siyo "mtekelezaji" au "mtoa maelekezo". Ambacho Dkt.

[9] Inaitwa "shule" lakini haina majengo. Ni aina ya programu ya mafunzo kwa njia ya warsha ili kuwakutanisha Viongozi

[10] "Toyonokuni" jina la asili la eneo hili la Wilaya ya Oita

HIRAMATSU alichokifanya si kuwaambia wanavijiji jambo la kufanya wala kuongoza vuguvugu, isipokuwa aliheshimu juhudi zao na umiliki wao, pamoja na nguvu zao. Mafunzo ya Osaka yanasisitiza jambo hili la vuguvugu la "kijiji kimoja zao moja" na umuhimu wake kwa mazingira ya Tanzania, kwa imani kwamba tayari zipo juhudi za namna hiyo kwenye Vijiji na wapo viongozi wazuri wanaojali maendelo ya nyumbani kwao. Ingelikuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa Tanzania kuunga mkono vuguvugu hili na kutoa fursa ya wazalishaji kujifunza kwa wenzao walio ngazi moja. Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kutofikiria kwamba hakuna chochote cha maana kwenye vijiji vyao. Kuna mambo mengi mazuri lakini hayafahamiki kwao. Wanapaswa kuanza kutambua juhudi za jamii zilizopo, kuwatia moyo, na kubadilishana uzoefu baina yao. Ingekuwa ni njia yenye tija zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi au kupitia kwenye vitabu.

Ni kutokana na mtizamo huu ndipo kitabu hiki kikaandaliwa.

### 3.5 Masuala Mengine

Kwa bahati mbaya yapo mambo mengi ambayo hatukugusia hapo juu kutokana na ufinyu wa nafasi bali yapo mambo mengi muhimu na mazuri yanayofaa kwa Tanzania kama vile uzoefu unaotokana na Minamata (Ugonjwa wa Minamata - Minamata Disease) na jinsi walivyoweza kuhuisha jamii kutokana na janga hilo, Upangaji mipango shirikishi jamii, mipango miji, mipango ya matumizi bora ya ardhi na maboresho ya matumizi ya ardhi, uzoefu wa Japani kuhusu maendeleo ya kiuchumi na nafasi ya Halmashauri katika maendeleo, n.k. Kuhusu uzoefu wa Minamata, mafunzo ya Osaka yanaweka msistizo kwenye umuhimu wake, na inaaminika kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zina mengi ya kujifunza kutokana na janga hili. Masuala ya janga hili yatagusiwa kwa undani kwenye kitabu kinachofuata.

## 4.0 MAENDELEO BAADA YA MAFUNZO YA OSAKA YALIYOSABABISHA KUCHAPWA KWA KITABU HIKI

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 1 hapo juu, mafunzo ya Osaka yalikuwa yameandaliwa mahsusi kwa nchi ya Tanzania kwenye miaka mitano ya mwanzo(2002 – 2007), yaliendelea kwa miaka mingine sita lakini wigo wake ukapanuliwa na kuingiza nchi nyingine tatu (2008 – 2012). Mafanikio makubwa katika miaka hii 11 hapa Tanzania ni kuanzishwa kwa umoja wa waliosoma Osaka (Tanzania Osaka Alumni, kwa kifupi TOA). Huu ni mfano wa pekee duniani kuwa na umoja wa wahitimu wa kozi ya aina moja ukijumuisha Wadau Maarufu ambao ni viongozi wa maboresho kama vile Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na wakuu wengine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM - TAMISEMI). Lilikuwa ni jambo la kupendeza hata kwa JICA ambao wanaendesha maelfu ya kozi za mafunzo nchini kote.

Kwa nyongeza, TOA imeendesha semina mbalimbali na warsha za mafunzo kama vile mafunzo baada ya Osaka na Warsha za Mafunzo za Kanda kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Halmaushauri wanachama. Fursa hizi, siyo tu kwamba zina saidia kubadilishana maoni baina ya Halmashauri wanachama, bali yametoa uwanja ambao ni nadra kuupata wa majadiliano na

kuhusu uhalisia wa Ugatuaji wa Madaraka, hususan changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza maboresho ya Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa, hakuna asasi ya namna hii hapa Tanzania, inayowahusisha Watendaji wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mikoa. Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT) ipo, lakini wahusika wake wakuu ni Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Wabunge. Vikao vya Jumuiya hii haviwapi fursa Wakurugenzi wa Halmashauri kushiriki kikamilifu na kutoa ushauri wa kitaalamu ingawa wao pia ni wajumbe. Kwa mantiki hii, TOA ina uwezekano mkubwa wa kukua hadi kuwa Umoja wa Watendaji Wakuu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa yaani Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa ambao ni wataalamu na watekelezaji wa ugatuaji wa madaraka na maboresho nchini. Hawa ndio wanaoshughulika kila siku kwenye mstari wa mbele wa maboresho. Maoni na mapendekezo yao ya pamoja yanaweza kuwa ni ya maana sana na ya kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza maboresho.

Kuhusu mambo mazuri na muhimu yanayofaa kuigwa, tayari Tanzania imejikusanyia uzoefu kwa zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji Ugatuaji wa Madaraka kwenda ngazi za msingi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mtaa. Lazima kutakuwepo na idadi kubwa ya mambo ya kufurahisha na uzoefu mzuri kwenye Halmashauri nyingi kote nchini ambao unafaa kushirikisha Halmashauri nyingine. Japani inaamini kwamba aina hii ya kujifunza kwa taasisi zilizo kwenye ngazi zinazofanana inaweza kuwa muafaka zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi yaani kutoka kwenye ngazi tofauti au ya juu sana na hasa kupitia uzoefu wake wa vuguvugu la OVOP kama zilivyoelezwa kwenye 3.4. hapo juu. Kitabu hiki cha rejea kiliandaliwa kwa kuzingatia maelezo na msingi huo ulioelezwa hapo juu. Ni matumaini ya TOA na mafunzo ya Osaka kwamba yatachangia kuboresha utendaji ndani ya Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa, kila moja ikimchochea mwenzie, na kuendeleza mambo mazuri yanayojitokeza, ambayo yatapelekea kwenye ufanisi na mafanikio ya ugatuaji wa madaraka katika nchi hii.

Mwisho, inastahili kusema kwamba kutokana na matokeo dhahiri yaliyotokana na mafunzo ya Osaka kwa nchi ya Tanzania, ambayo yameelezwa kwenye sura hii, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani (JICA) limeaamua kuendelea kutoa mafunzo ya Osaka kwa miaka mingine mitano, yakilenga Tanzania kwa mara nyingine tena na litatoa msisitizo maalumu katika kuwezesha shughuli za wanaumoja wa TOA na uimarishaji wa kitaasisi. Hii ina maana kwamba, viongozi wengine wengi wa maboresho Tanzania watafaidika kutokana na mafunzo ya Osaka ili waweze kuchangia utekelezaji mzuri zaidi wa maboresho ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi nchini.

# Sura ya Pili: Upangaji Mipango Shirikishi Jamii na Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo

Mipango shirikishi jamii ni mbinu inayotilia mkazo kushirikisha Jamii yote na wadau muhimu katika mikakati ya usimamizi na upangaji wa mipango ya maendeleo ya jamii au mchakato wa mipango katika ngazi ya jamii, katika mazingira yote ya vijijini na mijini. Mbinu Shirikishi hutoa fursa kwa kila mdau kuwa na sauti katika utoaji maamuzi ama yeye binafsi au kwa njia ya uwakilishi, na ni sehemu muhimu katika maendeleo ya jamii. Ushirikishwaji huambatana na hisia ya umiliki na hujenga msingi imara wa ushiriki wa jamii. Ushirikishwaji wa jamii hujenga Imani thabiti kwa miradi iliyopangwa kwa kuwa makundi yote katika jamii yamewakilishwa vyema. Kuwaweka pamoja wadau hupanua wigo wa mawazo na mitazamo mipana katika upangaji mipango. Mchakato wa upangaji mipango shirikishi hupunguza uwezekano wa kufanya makosa yatokanayo na uelewa mdogo wa jamii kuhusu hali halisi iliyoko katika jamii husika.

Inadaiwa kuwa, maendeleo enedelevu ni mchakato unaoendeshwa na wanufaika wenyewe badala ya ufadhili wa mara moja unaofanywa na wafadhili toka nje. Katika mchakato wa kujipangia mipango ya maendeleo, uwezo wa jamii wa kujipanga wenyewe na ule moyo wa kujitegemea wenyewe bila kuegemea mno misaada toka nje ni mambo ya muhimu na ya msingi sana, kwani mambo haya yakiwepo katika jamii, huifanya iweze kusonga mbele katika hatua ya juu zaidi ya maendeleo (Ohama 2002).

Kwa mujibu wa Kandie (2001), akitumia uzoefu kutoka Ghana Kaskazini alibaini kwamba utaratibu wa jamii wa kujipanga wenyewe ni kigezo muhimu katika mchakato wa upangaji wa miradi. Utaratibu huu wa jamii kujipanga yenyewe lazima usimamiwe na katiba, sheria ndogo, Dira ya Taifa ya maendeleo ili kuhakikisha miradi inayobuniwa inakuwa endelevu. Aina, muundo na uimara wa vyombo hivi ni vigezo muhimu kuliko vyombo vyenyewe (Chibehe, 2004; Sharma na Ohama, 2007; Kusago, 2008; Mwanga, 2011). Matokeo ya utafiti uliofanywa na Shikuku (2012) unathibitisha kwamba uimara wa vyombo vya jamii huthibitika kutokana na ushirikishwaji wa wanawake kama wadau muhimu katika miradi ya maendeleo ya jamii.

**Ushiriki katika Upangaji Mipango ya Maendeleo ya Jamii**

Tangu miaka ya 1990, ushiriki wa jamii katika juhudi za kujiletea maendeleo umepata msukumo mkubwa kimataifa, kitaifa na katika sera za ngazi za msingi za jamii (Scoones na Thompson, 1994; Sharma na Ohama 2007; URT, 2011; Howllet na Nagu 1997). Katika andiko la Abiona na Bello (2013), ushiriki wa jamii katika mipango yao wenyewe umetafsiriwa kama nyenzo muhimu katika kufanya mchakato wa kufanya maamuzi, kuweka ajenda za maendeleo, kuandaa kanuni zinazoongoza mchakato wa maendeleo. Ushiriki wa moja kwa moja wa jamii katika kupanga na kutekeleza mipango huhakikisha kuwa mikakati iliyowekwa ni sahiii na inakubalika na jamii. Ushiriki wa jamii huchochea uwajibikaji wa pamoja na mara nyingi huwa tayari kuchangia rasilimali zao ambazo zisingepatikana bila ushiriki wao (Helene *na wenzake,* 2013).

Jambo linalobishaniwa na kupigiwa kelele mara nyingi na wataalamu ni aina ya ushiriki na kiwango cha ushiriki katika mchakato wa maendeleo ya jamii (Makonda, 2003; Sharma na Ohama, 2007; Mwanga, 2011). Katika kushughulikia aina za ushiriki Tanzania ilitunga sheria ya Ubia (PPP act of 2010) ambayo inaruhusu ushirikiano wa jamii na sekta binafsi. Kabla ya hapo Pretty (1995) aliwasilisha hatua saba za

ngazi za ushiriki wa jamii ambazo ni: (i) Ushiriki wa kimyakimya wa Jamii (ii) ushiriki wa jamiii kwa kutoa taarifa(iii) Ushiriki wa jamii kwa njia ya maoni (iv) ushiriki wa jamii kwa kupewa motisha ya vitu (v) Ushiriki wa jamii katika utekelezaji (vi) ushiriki wa Jamii kuhusishwa (vii) ushiriki wa jamii kwa hiari. Wanazuoni wengine wakiwemo Sharma na Ohama (2007) wamejihusisha zaidi na ubora wa ushiriki kuliko aina ya ushiriki. Wao wanahoji kuwepo au kutokuwepo kwa ushiriki thabiti. Hivyo Sharma na Ohama (2007) waliainisha ngazi tatu za ushiriki zinazotekelezeka ambazo ni kutoshiriki kabisa, au kushiriki kwa maneno tu, au kushiriki kikamilifu kwa njia ya ubia au madaraka kwa umma.

Ili kurahisisha mchakato wa kugatua madaraka, Serikali za Mitaa zilirejeshwa kwa Sheria za Serikali za Mitaa Na.7 – 10 za mwaka 1982. Hii ni kwa mujibu wa ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ambayo inaruhusu uanzishwaji Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwezesha upelekaji wa madaraka kwa umma. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina haki na mamlaka ya kushiriki na kushirikisha watu katika kupanga na kutekeleza programu za maendeleo katika maeneo yao ya kiutawala na taifa kwa ujumla.

Kwa mantiki hiyo mfumo wa upangaji mipango shirikishi jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD), ulianzishwa mwaka 2001, ulifanyiwa majaribio katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na kufanyikwa uhakiki mwaka 2002 katika Halmashauri ya Hai na baadaye kuenezwa nchi nzima katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa 95%. Mfumo huu wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni mchakato wa upangaji mipango shirikishi wenye sifa zifuatazo:

- Una mtazamo chanya kwa jamii. Jamii huainisha rasilimali zilizopo katik kuondoa vikwazo hivyo kujenga moyo wa kujitolea na kujitegemea
- Zana shirikishi jamii hutumika nazo ni; Ramani ya kijiji, Matembezi mkato au kataa ya njia, Historia ya matukio muhimu, Kalenda ya msimu, Uchambuzi wa kitaasisi, Ratiba ya shughuli za kutwa kijinsia, Uchambuzi wa makundi ya uwezo kiuchumi, Majadilano mahsusi ya vikundi, Kutambua vyanzo mbalimbali vya mapato na matumizi.
- Modeli ya upangaji mipango inayowezesha jamii kuainisha Bao-mantiki. Kwa kutumia zana hii jamii itaweza kuchanganua malengo mahsusi, fursa zilizopo, visababishi vya vikwazo, miradi inayofaa, hatua muafaka za utekelezaji miradi, vyanzo vya mitaji na matumizi yake ambavyo ni vitu muhimu vivyoonesha jamii inaweza kufanya nini na haiwezi kufanya nini. Husaidia sana jamii kuweka vipaombele na kutengeneza mipango ya miaka mitatu.
- Husaidia jamii kutambua rasilimali walizo nazo na namna nzuri ya kuzitumia. Husisitiza juu ya kujitegemea zaidi kuliko kutegemea misaada.
- Mchakato huu unatumia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 kama mwongozo wa kisera katika utekelezaji mipango.
- Matokeo ya mchakato wa O&OD ni mpango kabambe unaojumuisha masuala yote muhimu ya maendeleo ya jamii na siyo mipango kazi.

Baada ya miaka mitano ya utekelezaji, changamoto zifuatazo zilijitokeza. Changamoto hizi ni pamoja na ubora usioridhisha wa mipango ya vijiji, baadhi ya idara za kisekta za Halmashauri hazikuzingatia mipango ya O&OD ya vijiji sawasawa na bajeti zilizotengwa kwa kutumia mfumo wa ruzuku ya maendeleo (ruzuku isiyo na masharti) hazikutosheleza kuteleza miradi ya vipaumbele vya jamii na hivyo miradi iliyopangwa na vijiji haikutekelezwa kikamilifu hali ambayo ilisabisha jamii kuvunjika moyo na kuchoka kushiriki. Kutokana na hali hiyo hapo juu mfumo huu wa O&OD haukuiwezesha jamii, ulijenga hali ya utegemezi na hivyo kusababisha jamii kutokuwa na umiliki.

Kutokana na hali hiyo hapo juu Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na Serikali ya Japani ilibuni mradi wa majaribio unaojulikana kama mradi wa “Kuimarisha Mpango Shirikishi na Mzunguko wa Maendeleo ya Kijamii kwa Utawala Bora wa Serikali za Mitaa ” yaani O&OD iliyoboreshwa.

Katika sura hii kuna mbinu bora nne zilizowasilishwa. Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ni mfano halisi wa mchakato wa O&OD na namna itakavyobadilisha mchakato wa upangaji miradi endapo jamii itapatiwa uwezeshwaji na usimamizi elekezi. Awali wanajamii walipanga mipango na kusubiri Halmashauri itekeleze. Matokeo yake miradi mingi haikukamilika. Uwezeshwaji thabiti wa Jamii kutoka kwa watumishi wa Halmashauri ulibadili na kufufua ari ya ushiriki wa jamii katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo. Mbinu bora za Kijiji cha Chamakweza katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Kijiji cha Maseyu katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na Kijiji cha Mangula-B katika Halmashauri ya Kilombero ni matokeo ya mradi wa O&OD iliyoboreshwa. Kutokana na mbinu bora hizi tunajifunza mambo makuu yafuatayo: umuhimu wa mfumo thabiti wa uwezeshaji jamii, uwezeshaji kwa kutumia wawezeshaji mahiri na imara, maandalizi ya jamii kwa muda mrefu wa kutosha na ujengaji uwezo wa jamii wa kutekeleza miradi yao. Mbinu bora hizi zinadhihirisha kwamba Halmashuri hazitaweza kabisa kutekeleza miradi yote inayoibuliwa, badala yake ni lazima jamii ijengewe uwezo ili itekeleze miradi yao kwa kutumia rasilimali zilizopo kijijini kabla ya kuomba usaidizi kutoka nje. Kutokana na mchakato wa O&OD iliyoboreshwa, kuna matokeo chanya mengi yanayo onekana na yasiyo onekana, haya yote yamefafanuliwa kwa ufasaha katika sura hii.

# HALMASHAURI YA WILAYA KONDOA

**UTAWALA NGAZI MSINGI NA USHIRIKI WA JAMII KATIKA JITIHADA ZA MAENDELEO**




***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ni moja kati ya wilaya saba za mkoa wa Dodoma. Halmashauri hii ipo umbali wa kilometa 160 kaskazini mwa makao makuu ya mkoa wa Dodoma. Halmashauri inapakana na wilaya za Kiteto, Kongwa na Chamwino kwa upande wa Mashariki, Manyoni, Chemba na Hanang kwa upande wa Magharibi, Babati na Simanjiro kwa upande wa Kaskazini na Chemba na Bahi kwa upande wa Kusini. Halmashauri ina idadi ya watu wapatao 269,704 kati yao 133,186 ni wanawake na 136,518 ni wanaume, ongezeko la watu ni wastani wa 1.7% na ukubwa wa kaya ni wastani wa watu 4.8.

Ukubwa eneo la wilaya ya Kondoa ni kilometa za mraba 5,557. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 4 ambazo ni tarafa za Bereko, Kolo, Pahi na Kondoa mjini; Kata 28, Vijiji 97, Vitongoji 388 na Mitaa 11. Madiwani wa kuchaguliwa wapo 28 kutoka kata 28 na Madiwani wa viti maalum CCM -7 na CUF -2; Jumla ya Madiwani ni 37. Halmashauri ina wabunge 2, Mbunge mmoja wa kuchaguliwa kutoka CCM na Mbunge mmoja viti maalum kutoka CUF.

Jukumu kuu la Halmashauri ni kutoa huduma bora za kiuchumi, kijamii na kimazingira kwa wananchi wote wa Kondoa ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kutumia mfumo wa upangaji mipango shirikishi Jamii wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) ambao ni mchakato wa kitaifa wa mipango na bajeti il kubainisha fursa na vikwazo kwa maendeleo kwa kufanya uchambuzi wa vipaumbele vyao, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia na kufanya tathmini ya ubora wa miradi ya maendeleo ili kupunguza hali ya umaskini.

Uchumi wa kaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa unategemea kilimo na ufugaji kwa asilimia 90%. Kwa tafsiri ya haraka ni kwamba kilimo ndiyo shughuli kuu inayoweza kupunguza ama kuondoa umasikini katika wilaya ya Kondoa. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 681,324, ingawa ni 30% ya eneo lote linalofaa kwa kilimo linatumika kwa uzalishaji. Hivyo kuna fursa kubwa ya kuendeleza kilimo hadi kufikia 90% ya eneo lote la kilimo. Mazao yanayolimwa katika wilaya ya Kondoa ni pamoja na mahindi, mtama aina ya tegemeo na okoa, uwele, viazi vitamu, mhogo, mpunga na viazi mviringo kama mazao ya chakula. Pia mazao ya biashara ni mbaazi, maharage, dengu, kunde, karanga, ulezi na ufuta.

Halmashauri ya Kondoa ina fursa zifuatazo:- Eneo kubwa la kilimo hekta 681,324, misitu ya hifadhi hekta 49,046.7, msitu wa Halmashauri hekta 4,249, misitu ya mradi wa Hifadhi Ardhi Dodoma (HADO) hekta 125,600 na misitu ya asili hekta 2,200 na vyanzo hadhaa vya uhakika vya maji. Fursa nyingine ni mtandao wa barabara uliojengwa kutokana na kushindiliwa kwa changarawe na udongo kilometa 854 na kilometa 5.62 zilizojengwa kwa lami eneo la Kondoa Mjini. Fursa nyingine ni kuwepo kwa miongozo ya kisheria na sera za kisekta ikiwa pamoja na Ilani ya uchaguzi 2010, MKUKUTA-II, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara Tanzania (MKURABITA, Mpango wa kuendeleza ujasiriamali Tanzania yaani (*Business Entrepreneurship Support Tanzania* - BEST), Ubia kati ya sekta ya Umma na Sekta binafsi (PPP), taasisi na asasi za kifedha mfano NMB, CRDB, SACCOs, Pride, Brac, Finca, SEDA, FAIDIKA, Bay pot n.k.

## 1.2 UPANGAJI MIPANGO SHIRIKISHI JAMII KATIKA WILAYA YA KONDOA

Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imekuwa ikijitahidi kushirikisha jamii katika upangaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Mchakato huu huanzia kwenye kutambua vikwazo, kuweka vipaumbele, kupanga shughuli na bajeti, utekelezaji , usimamizi, ufuatiliaji pamoja na tathmini ya utekelezaji/matokeo. Katika mchakato huu mambo makuu yafuatayo huzingatiwa; Kutambua tatizo, kuchambua tatizo, kupanga utekelezaji, kutekeleza, kufuatilia utekelezaji na kufanya tathmini. Halmashauri ya Kondoa ni moja ya Halmashauri za Tanzania ambayo imekuwa ikifanya ubunifu wakati wa kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo. Zaidi ya hapo Hamashasuri hii imekuwa ni moja

kati ya Halmashauri chache ambazo zimeanzisha utaratibu bunifu unaowezesha ufuatiliaji wa namnamaswala ya utawala bora yanavyoshughulikiwa katika katika ngazi za msingi kwa kutumia mratibu wa Utawala Bora. Kwa njia hii Halmashauri imefanikiwa kuwezesha jamii kushiriki katika upangaji wa mipango ya maendeleo na utekelezaji kwa jitihada zao kupitia uchangiaji wa gharama na kujitolea.

**1.3 MAELEZO YA TATIZO**

Kabla ya kuingilia kati kwa maana ya kuanzisha utaratibu wa jamii kuchangia gharama au kujitolea kikamilifu katika utekelezaji wa miraji mpaka kuikamilisha, hali ilikuwa kama ifuatavyo:- awali ya yote miradi mingi haikukamilika, mingi ya hiyo ni majengo yaliyofikia ngazi ya lenta. Hadi mwaka 2007 kulikuwa na maboma 246 yaliyojengwa kwa ajili ya vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabweni na ofisi za vijiji ambayo hayakukamilika. Hapakuwa na takwimu sahihi za watu wenye uwezo wa kufanya kazi ili kukadiria nguvu kazi halisi iliyopo katika jamii. Hapakuwa na uthaminishaji bayana wa uchangiaji wa nguvu kazi za wananchi ili kujua kiwango halisi cha uchangiaji wa jamii. Jamii katika Halmashauri ya Wilaya Kondoa haikuwa na utamaduni wa kuchangia fedha taslimu isipokuwa ilizoea kuchangia kwa hali na mali, kwa mfano ukusanyaji wa vifaa vya ujenzi kama mawe, mchanga, kokoto na matofali ya kuchoma. Kwa namna hiyo,jamii haikuweza kuhisi maumivu ya uchangiaji hali ambayo hulileta hisia za umiliki wa miradi ya maendeleo. Kulikuwa na uenguaji usio wa makusudi wa baadhi ya wadau katika mchakato wa upangaji wa maendeleo. Awali, Halmashauri ilizoea kuhamasisha jamii kujenga maboma hadi kwenye hatua ya lenta ambayo ilipelekea kuwepo kwa maboma 246 yasiyokamilika yaliyotelekezwa na jamii. Hii iliweka msingi na Imani kwa jamii kuwa maboma hayo ni mali ya serikali na Halmashauri itatoa fedha ili kuyakamilisha.



Boma la ofisi ya Kijiji cha Bubutole jengo ambalo halijakamilika



Wanajamii wa Bubutole wakijadili ukamilishaji wa ofisi

**1.4 MALENGO**

Juhudi za kuimarisha masuala ya utawala katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa zililenga kufikia malengo yaliyo orodheshwa hapa chini;

(i) Kuhakikisha kunakuwa na uchangiaji wa kutosha wa fedha kutoka ngazi ya jamii na wadau wengine kwa ajili utoaji wa huduma zilizopo na kukamilisha miradi ambayo haijakamilika katika halmashauri.

(ii) Kuhakikisha kumejengwa msingi wa uadilifu na ari kubwa kwa jamii juu ya umiliki na usimamizi wa miradi yao kwa maendeleo endelevu.

(iii) Kuiwezesha jamii hadi kufikia hatua ya kuwa na uwezo wa kupanga, kutekeleza miradi, kuwa na umiliki wa mipango yao ya maendeleo ili utegemezikatika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## 1.5 MIKAKAKTI YA UTEKELEZAJI

Hali ya utegemezi wa jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ya Halmashauri ya Wilaya ya kondoa ilisababisha halmashauri kuanzisha mpango maalum wa mafunzo ya upangaji mipango shirikishi jamii (O&OD) na hivyo kupelekea kuwepo kwa upangaji na utelezaji madhubuti wa miradi. Lengo la mpango huu wa mafunzo lilikuwa kuleta uelewa wa pamoja wa namna ya kupanga, kutekeleza na kujenga umiliki wa jamii wa miradi.

Katika mpango huu wa mafunzo shughuli zifuatazo zilitekelezwa; kwa mwaka 2008/2009 Halmashauri ilitoa mafunzo kwa wawezeshaji kutoka kwenye kata 35 ikilenga timu za menejimenti za kata kuhusu mchakato wa O&OD. Aidha, mafunzo rejea yaliendelea kutolewa kwa muda wa miaka mitatu mfululizo yakilenga watendaji wa kata (WEO) 35. Katika mafunzo hayo, maafisa watendaji wa kata pia walifundishwa kuhusu namna ya kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mwaka 2008/2009 wajumbe wa kamati za maendeleo za kata (WDC) pia walifundishwa kuhusu nfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo juu ya utambuzi thabiti wa tatizo, upangaji mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za maendeleo katika kata zao kila mwezi, robo na nusu mwaka.

Katika kipindi cha mwaka 2008/2009 timu za menejimenti za kata ziliendesha mafunzo kama haya kwa watendaji wa vijiji 168 katika kata zao, kila timu ikifanya mafunzo katika yake, yakilienga upangaji mipango shirikishi, uandaaji wa bajeti, taarifa za miradi ya maendeleo, taarifa za mapato na matumizi na namna ya kuwasilisha taarifa hizo kwenye mikutano mikuu ya kijiji. Kuanzia mwaka 2009 Halmashauri iliimarisha uwezo wa kamati za ukaguzi wa miradi katika ngazi ya kumi. Maafisa watendaji wa kata 10 walipewa kompyuta zinazotumia nguvu ya umeme wa jua kwa ajili ya uboreshaji wa utunzaji wa takwimu na utoaji taarifa.

Mwaka 2009/2010 wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango walipatiwa mafunzo kuhusu wajibu na majukumu yao. Wawezeshaji wa mafunzo hayo walikuwa wataalam kutoka makao makuu ya Jumuiya ya Serikali za Mitaa (ALAT) – Taifa. Tangu 2007/2008 Halmashauri ilieanzisha utaratibu wa vikao na wadau wa maendeleo kujadili na kuchambua changamoto mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mchakato wa O&OD. Kila kata ina mlezi ambaye ni mkuu wa idara akiwa na jukumu la kutembelea kata yake na kushauri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Halmashauri ya wilaya imeanzisha mfuko wa elimu wa wilaya ambapo kila kata hukusanya shilingi 5,000/= kwa mwaka kwa kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa kutumia vitabu maalum vya halmashauri namba HW5. Halmashauri pia imeanzisha mfuko wa maendeleo wa Wilaya (Kondoa Development Fund - KDF) kwa lengo la kufadhili utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Halmashauri iliendesha mafunzo ya kina kwa madiwani, watendaji wa kata, watendaji wa vijiji, timu za menejimenti toka kata zote kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Mikutano ya uhamasishaji iliendeshwa kwa kutumia watu mashuhuri na viongozi wa taasisi za dini. Mipango ya maendeleo ya vijiji iliandaliwa kupitia mchakato wa O&OD. Mfuko wa maendeleo wa halmashauri ulilenga kufadhili na kuchchea jitihada za jamii katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mwaka 2009, Halmashauri ilitunga sharia ndogo za kuongoza usimamizi wa Mfuko wa Elimu. Kuanzia 11/10/2013 Halmashuri ilianzisha mtandao wa vijana ambapo vijana 112 kutoka kata 28 (4 kila kata) walipatiwa mafunzo ya mchakato wa O&OD. Lengo lilikuwa kuwajengea uwezo wa kujihusisha na

ujasiriamali. Serikali za vijiji maeneo ya kilimo na ufugaji ambayo yangetumiwa na vjina katika vijiji vyao. Kwenye mwaka 2007/2008, Mkurugenzi wa Halmashauri kwa ubunifu alianzisha kitengo maalumu cha uratibu wa vijiji, mitaa na kata kuhusu utawala bora na miradi ya maendeleo. Mratibu aliteuliwa kutoka miongoni mwa maafisa watendaji wa kata wanaofanya vizuri kuongoza kitengo hicho (rejea kisanduku namba 1). Kadhaika aliteuliwa mratibu wa utawala bora anayehusika na ufuatiliaji wa siku kwa siku masuala ya utawala bora katika vijiji (rejea kisanduku 2). Kuteuliwa kwa waratibu hawa ni ubunifu pekee unaopatikana halmashauri ya wilaya Kondoa ambao umeharakisha kumeongeza tija katika ufuatilliaji wa miradi ya maendeleo na masuala ya utawala bora.

**Kisanduku 1:Wajibu na Majukumu ya Mratibu wa Kata, Vijiji na Mitaa**

- Kufuatilia Uzingatiaji wa ratiba ya vikao shirikishi vya kisheria katika ngazi ya kata (WDC), Vijiji na Mitaa.
- Kuhakikisha kuwa vikao vinafanyika kwa mujibu wa ratiba, sheria na kanuni zinazoongoza mikutano hiyo.
- Kupokea na kupitia mihutasari ya mikutano hiyo, kutoa taarifa ya mambo yaliyojitokeza kwa Mkurugenzi, kushauri njia bora za kuboresha utoaji wa huduma kwa uongozi wa kata, vijiji na mitaa
- Kuhakikisha jamii inapata taarifa za mapato na matumizi za robo mwaka kupitia mikutano ya kijiji na kwamba mikutano ya mwezi ya serikali ya kijiji ianafanyika mara kwa mara
- Kutoa mafunzo kwa viongozi wa serikali za vijiji, wajumbe wa kamati za maendeleo za kata na jamii kwa ujumla kuhusu majukumu na uwajibikaji
- Kushauri uongozi wa kuhusu njia bora ya kuandaa mipango shirikishi ya maendeleo kupitia mchakato wa O&OD

Kisanduku 2. Kazi na Majukumu ya Mratibu wa Utawala Bora

- Kushughulikia migogoro na kupokea maoni ya jamii kuhusu utendaji wa watendaji wa kata, vijiji na mitaa
- Kushughulikia mambo yote yanahusu utoaji huduma dhaifu, rushwa na ukiakwaji wa maadili kwa maofisa wa halmashauri katika ngazi zote
- Kuhakikisha kuwa kila Idara na kitengo zina rejesta za malalamiko na ufunmbuzi wa malalamiko hayo kulingana na katiba na sharia za nchi
- Kufuatilia utendaji kazi wa watendaji wa kata, vijiji na wataalamu wengine ngazi ya kata na kutoa taarifa kwa Mkurugenzi kuchukua hatua stahiki za kinidhamu.
- Kuhakikisha dhana ya utawala bora inazingatiwa katika ngazi zote za menejimenti za halmashauri wilaya.
- Kuandaa taarifa ya utawala bora na kuiwasilisha kwenye vikao vya kisheria vya Halmashauri kilarobo mwaka.
- Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara juu ya usimamizi na utendaji kazi wa maafisa watendaji wa kata, vijiji, mitaa na wakuu wa idara idarakuhusu uongozi wao na utoaji wa huduma.
- Kuratibu ratiba ya vikao vya kisheria katika ngazi ya kata vijiji, mitaa na idara za halmashuri.
- Kusimamia mchakato wa O&OD katika kutambua miradi, kupanga, kutekeleza, kufuatiliaji na kutathmini miradi yote kwa maendeleo endelevu ya wananchi

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ilinunua gari aina ya Toyota double cabin SM 10326 kwa gharama ya Tsh 75,000,000/= kwa lengo la kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya jamii inayotekelzwa. Tafadhali rejea picha hapo chini.




*Gari SM 10326 aina ya toyota double cabin kwa ajili ya shughuli za O&OD*
*Bwana Makha ni Mratibu wa Utawala Bora na miradi ya Maendeleo*

Katika mwaka wa fedha wa2012/2013, Halmashauri ilinunua pikipiki 2 aina ya honda XL 125 kwa shilingi 16,000,000/=. Vitendea kazi hivi vimetengwa mahususi kwa matumizi ya O&OD iliyoboreshwa inayotekelezwa kayika Halmshauri ya kondo kwa ushirikiano wa OWM-TAMISEMI na JICA. Mwaka 2013/2014 kiasi cha shilingi 18,500,000 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mraddi wa O&OD iliyoboreshwa. Tafadhali rejea picha hapa chini.




***Honda XL 125, SM 9720 na SM 9719, zilinunuliwa 2012/2013 kwa ajili ya mradi wa O&OD iliyoboreshwa***

### 1.6 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Rasilimali fedha, kiasi cha fedha za kitanzania jumla Tsh 232,500,000/= zilitumika kwa ajili ya programu ya mafunzo kuhusu mchakato wa O&OD katika kipindi cha mwaka 2011/2012. Serikali kuu ilichangia Tsh 209,250,000/=na Halmashauri ya wilaya ilitoa Tshs 23,250,000/= kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Kuhusu rasilimali watu zoezi lote hili lilipelekea wataalam wa halmashauri, wawezeshaji wa halmashauri, kata, wanufaika na wadau mbalimbali kaika halmashauri ya wilaya ya kondoa kutumika ipasavyo. Baadhi ya raslimali pia zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ili kurahisisha utekelezaji wa mchakato wa O&OD iliyoboreshwa.

### 1.7 MATOKEO

Viongozi wa kisiasa na wananchi kwa pamoja walielimishwa kuhusu mchakato wa O&OD wakati wa kutambua, kupanga, kutekeleza (kupitia utaratibu wa kujitolea) bila utegemezi wa katika kukamilisha miradi yao ya maendeleo. Idadi ya miradi isiyokamilika (vyumba vya madarasa na nyumba za walimu) imepungua 246 hadi kufikia 40.

Kumekuwa na ongezeko la uwezo wa jamii katika kutambua fursa na vikwazo kwa maendeleo yao. Kumekuwepo na kukomaa kwa umiliki wa jamii wa miradiya maaendeleo kwa maendeleo endelevu. Zaidi ya lipo ongezeko la utayari katika kuchangia mfuko wa elimu wa halmashauri kwa kiasi cha shilingi 290,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kufikia mwishoni mwa mwaka 2013 uchangiaji umefikia shilingi 343,207,870/=.

Hii inaonesha kwamba jamii in raslimali na ipo tayari kushughulikia maendeleo yake isipokuwa tatizo lipo kwenye uwezeshaji. Kupitia mchakato wa O&OD tazamo na ushiriki wa wanasiasa umekuwa wa kuridhisha tofauti na hapo awali kabla ya Mpango Shirikishi jamii kutekelezwa. Ubora na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo vimedhihirika kuongezeka.  Kumekuwa na mabadiliko chanya katika kiwango cha Ushiriki wa wanawake katika shughuli za maendeleo. Ikumbukwe Kondoa ni Wilaya yenye Waislaam wengi na kwa mujibu wa kanuni za dini wanawake hawategemewi kushiriki kwa uwazi katika shughuli za maendeleo pamoja na wanaume. (rejea picha hapo chini).



*Shule ya Sekondari Makorongo (Kamati ya ukaguzi miradi, inajumuisha wanawake)*



*Madarasa matatu yamejengwa na jamii ya  Gubali*



*Shule ya sekondari Bicha, wanafunzi wakiwa nje ya jingo la utawala*

**1.8 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Mabadiliko ya tabia nchi yanayoambatana na ukame wa mara kwa mara hupelekea uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo hivyo kuathiri kipato cha kaya na hatimaye kushindwa kuchangia miradi ya maendeleo. Miundombinu mibovu ya barabara na mifumo ya maji na mfumko mkubwa wa bei za chakula na bidhaa nyingine kwa pamoja vinapeleka kupanda kwa bei za bidhaa has vifaa vya ujenzi na mafuta.

Kwa sababu hizo hapo juu halmashauri imejiandaa kwa ukarabati wa mara kwa mara miundombinu ya barabara. Halmashauri ina mtandao wa barabara wa kilometa 854 kati ya hizo 450 zimekarabatiwa na zinapitika mwaka mzima. Lengo ni kukarabati kilometa zote 854 kwa kiwango cha changarawe kufikia 2014/2014. Halmashauri iliwekeza katika kilimo cha umwagiliaji ili kuinua kipato cha wananchi kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji. (angalia picha hapa chini).




***Mradi wa umwagiliaji, skimu ya Kikore kwa kilimo cha mpunga na mboga***

Halmashauri imerahisisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa kuwavutia wafanyabiashara wa pembejeo kufungua maduka vijijini na mjini Kondoa. Viongozi wa kisiasa (Madiwani) wameanza kutambua na kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kuhamasisha maendeleo. Kwa kuwa Madiwani ni wenyeviti wa WDC, wanalazimika kutia saini "**mikataba ya utekelezaji**" wa miradi kwa niaba ya jamii wanazoziongoza. Kwa njia hii madiwani wanalazimika kushirikiana na wawezeshaji.

## 1.9 SIRI ZA MAFANIKIO

**Uanzishaji wa kitengo cha Uratibu.** Moja ya siri za mafanikio kwa Halmashauri ya kondoa ilikuwa kuanzishwa kwa Kitengo cha Uratibu wa Kata vijiji na mitaa na uteuzi wa Mratibu Mahiri. Kitengo hiki hakipo katika muundo wa Halmashauri za Wlaya bali ni ubunifu wa Mkurugenzi. Somo tunalojifunza hapa ni kwamba shughuli za O&OD zinahitaji uratibu na ufuatiliaji wa karibu. Hili lilifanikiwa kwa kuwa na mratibu mahiri wa utawala bora. Mwaka 2008/2009, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa aliteua Mratibu mahiri wa Utawala Bora ili kusimamia na kuona kuwa haki inapatikana kwa jamii na kusuluhisha migogoro ya masuala ya uongozi, mipaka ya vijiji, wilaya na migogoro ya ardhi inayojitokeza. Kwa kiasi ubunifu huu uliboresha ushiriki wa jamii katika miradi ya maendeleo kwa kuwa waliondokana na migogoro.

**Kikao cha kazi kinachojumuisha madiwani, watendaji wa kata na timu ya menejiment ya halmashauri**. Ubunifu huu ulipelekea halmashuri kujadili kwa pamoja masuala yanayojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoibuliwa kwa mchakato wa O&OD katika Halmashauri. Katika kikao hiki kila Diwani sharti awasilishe taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopo kwenye kata yake, ikionyesha mafanikio na changamoto na pia sharti aeleze mpango mahsusi na mikakati ya kutatua ama kuondoa kabisa changomoto zilizopo katika kata yake, na atawajibika kujibu maswali ya wajumbe wa kikao cha kazi.

**Uteuzi wa walezi wa Kata miongoni mwa Wakuu wa Idara.** Kila Kata ina mlezi ambaye ni mjumbe wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri mwenye jukumu la kufuatilia na kutoa taarifa kwa haraka kwa Mkurugenzi Mtendaji kuhusu masuala yanajitokeza na kwenye vikao vya kisheria vya Halmashauri. Mlezi wa kata anatakiwa kutoa mapendekezo ya hatua stahiki katika kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji wa miradi. Walezi wa kata, wote huteuliwa na Mkurugenzi na kupitishwa

kwenye vikao vya kisheria vya Halmashauri. Jitihada hii imeleta uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa watendaji wa Halmashauri.

**Kikao cha wadau wa Halmashauri.** Halmashauri ilibuni utaratibu wa kukutana na wadau wa maendeleo (mashirika yasiyo ya kiserikali - NGOs, Asasi za kiraia – CBOs, Taasisi za Kiimani – FBOs na Wanaharakati wengine) ili kujadili kwa pamoja mapendekezo ya Mipango wa Maendeleo na Bajeti ya Halmashauri kwa miradi yote ya maendeleo. Majadiliano na ushauri ni muhimu katika kufanya mapitio ya mipango na bajeti za kila mwaka. Halmashauri kupitia timu ya menejimenti imekuwa ikifanyia kazi mapendekezo ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (CAG) katika kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matokeo yake hesabu za Halmashauri ni safi.

**Kuwekeana mikataba ya kazi na Watendaji wa Kata na Vijiji**. Mikataba hii ni hati za kisheria zinazofunga uongozi wa kata na vijiji kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa wakati na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa. Katika mikataba hii majukumu na stahili ya kila upande (mhusika) yameainishwa kwa ajili ya uwajibikaji. Katika mazingira magumu ya migogoro inayopelekea miradi kutokukamilika, viongozi wa kisiasa na watu mashuhuri hushirikishwa katika kuhamasisha wananchi kutatua migogoro kwa amani. Utaratibu huu ulianzishwa mwaka 2012. Halmashauri ina kamati za ukaguzi wa miradi inayohusisha watendaji toka idara za Halmashauri. Mikataba hii ya kazi imepunguza utendaji kazi wa mazoea miongoni mwa watendaji wa Kata na Vijiji.

**Kamati ya Ukaguzi Shirikishi wa Miradi ngazi ya Kata.** Katika kipindi cha 2007/2008, Halmashauri ilianzisha kamati ya usimamizi na ukaguzi wa miradi ngazi ya kata ili kutambua changamoto na kuzishughulikia kwa wakati. Lengo lilikuwa kuhakikisha vijiji vinatekeleza miradi yao bila misuguano. Kamati ya usimamizi na ukaguzi wa miradi inawajibika kutoa taarifa kwenye kikao cha WDC kila baada ya miezi mitatu au wakati wowote mwenyekiti wa WDC atakapoona inafaa au pakitokea jambo la dharura. Kamati hii imeimarisha moyo wa kujitolea na kujifunza kutokana na uzoefu wakati wa utekelezaji wa miradi.

**Kamati na taasisi za nje za kutathmini miradi**. Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Halmashauri ilijitahidi kualika na kupokea kamati za ukaguzi wa miradi kutoka taasisi za nje, wahandisi na wataalam washauri wa kujitegemea ikiwemo taasisi ya SIKIKA. Kwa mfano, Wajumbe wa ALAT Mkoa, walikagua miradi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Maoni na ushauri wao vilizingatiwa katika kutatua changamoto zilizotambuliwa.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO

## UWEZESHAJI JAMII KWA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI



*Uzoefu wa Kijiji cha Chamakweza*

**1.0 Utangulizi**

Kijiji cha Chamakweza ni miongoni mwa vijiji 97 vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambayo ni moja kati ya Halmashauri 5 zinazotekeleza mradi wa O&OD iliyoboreshwa. Kijiji cha Chamakweza chenye idadi kubwa ya jamii ya Wamasai kipo katika kata ya Pera yenye vijiji vinne ambavyo ni Malivundo, Pingo, Pera na Chamakweza. Kijiji hiki kina jumla ya wakazi 2,566 kati yao wanaume ni 1,077 na wanawake 1,489. Kijiji cha Chamakweza kinapakana na Kijiji cha Magulumata kwa upande wa Kaskazini, Kijiji cha Gwata kwa upande wa Kusini, Ranchi ya Ruvu upande wa Mashariki na Kijiji cha Pingo upande wa Magharibi. Chamakweza ni moja kati ya vijiji kumi vinavyotekeleza mradi wa O&OD iliyoboreshwa.

Mradi wa O&OD iliyoboreshwa ulianza katika kijiji cha Chamakweza mwaka 2010. Utekelezaji wa mradi ulianza kwa kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa Kata kwa muda wa miezi mitatu. Baada ya mafunzo wawezeshaji wa Kata walianza shughuli ya utafiti wa awali kwa kufanya uchambuzi ili kujua hali halisi ya kijiji. Utafiti huu ulianza kwa wawezeshaji kushauriana na Halmashauri ya Kijiji kwa lengo la kutambulisha mradi. Kamati za kudumu za vijiji zilihojiwa ili kukusanya taarifa muhimu kwa ajili ya upangaji mipango. Utafiti huu wa awali ulijikita katika Vitongoji kwa kuendesha mikutano isiyo rasmi na Wenyeviti pamoja na kamati za vitongoji. Mikutano isiyo rasmi iliendeshwa kwa makundi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ili kupata taarifa za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, kimila na kimazingira. Wawezeshaji wa Kata walishiriki shughuli mbali mbali za kijamii kama vile ngoma za kimila ili kujenga mahusiano mazuri na Imani kati ya jamii na wawezeshaji. Hatimaye wanajamii wakawa huru kujieleza bila hofu na wawezeshaji wakaweza kuelewa hali halisi ya jamii kuliko hapo awali. Taarifa zote zilizopatikana ziliandikwa kwenye taarifa ambayo ilitumika kama msingi wa jamii wa upangaji. Taarifa hii ilitoa picha halisi na hali halisi iliyopo kwenye jamii. Taarifa pia iliibua majadiliano kwa wanakijiji kuhusu namna ya kutatua vikwazo vilivyotambuliwa kwa kutumia fursa zilizopo kwa kuzingatia kanuni mila na taratibu imara za Wamasai zilizopo kwenye kijiji.

**1.2 MATATIZO YALIYOBAINIKA KATIKA ZOEZI LA UCHAMBUZI WA HALI HALISI YA JAMII**

Orodha ndefu ya matatizo ilitambuliwa ikiwa ni pamoja na: Uhaba wa maji kwa mifugo na binadamu na eneo dogo la malisho ukilinganisha na idadi ya mifugo iliyopo kijijini. Matatizo mengine yalikuwa upatikanaji duni wa huduma za afya, umbali mrefu kuzifikia huduma za elimu ya msingi kwani ni vitongoji vichache vilivyokuwa na shule za msingi, Mahudhurio hafifu ya wananchi katika mikutano ya kisheria ya utoaji wa maamuzi na uzalishaji duni wa mazao ya mifugo (maziwa na nyama). Mengine ni ongezeko la matukio ya wizi wa mifugo kijijini kila mwaka, Kipato cha chini kwa wafanyabiashara ndogo ndogo kinachosababishwa na ukosefu wa mitaji ya biashara, miundombinu mibovu (barabara za vitongoji) iliyokwamisha usafirishaji wa watu na mazao kutoka kwenye vitongoji hadi barabara kuu. Kutokana na hali ya umaskini kijiji kilikumbwa na wimbi la Vijana (Morani) kukimbilia mijini kutafuta fursa mbadala za maisha na shughuli za kujipatia kipato kama vile ususi wa nywele au kazi za ulinzi. Migogoro ya ardhi kati ya jamii za wafugaji na wakulima ilitajwa lakini tatizo kuu lilikuwa uongozi wa kijiji usiowajibika vyema kwa jamii.

Licha ya changamoto hizo hapo juu, jamii na wawezeshaji kupitia utafiti wa awali waliweza kutambua fursa zilizopo ambazo zingweza kutumika kuondoa vikwazo vilivyotambuliwa kama ifuatavyo: uwepo wa ardhi inayofaa kwa kulisha mifugo na makazi, uwepo wa gulio la mifugo, idadi kubwa ya mifugo (ng'ombe wapatao 27,000), shule mbili za msingi za Chamakweza na Mbala, Mabwawa saba (manne yanayomilikiwa na serikali ya kijiji, moja la kikundi cha wafugaji na mawili ya watu binafsi) na uwepo wa vikundi imara vya jamii (NARETISAHO, NALEPO na Chamakweza Women Group).

Baada ya zoezi la utafiti wa awali hatua za maandalizi ya mchakato wa upangaji mpango wa kijiji zilifanyika. Kwanza, taarifa ya utafiti iliwasilishwa katika mkutano mkuu wa kijiji. Katika mkutano huu wawakilishi wa jamii 50 waliteuliwa kwa ajili ya kushirikiana na wawezeshaji wa Kata kuandaa rasimu ya mpango wa maendeleo wa kijiji. Timu ya wawakilishi wa jamii (50) pamoja na wezeshaji wa Kata walitembelea vitongoji vyote vinne kupata maoni ya jamii ili kuboresha rasimu. Lengo la kutembelea vitongoji lilikuwa kuhakisha ushiriki wa jamii yote katika mchakato wa upangaji. Timu hii pia ilipata ushauri wa kitaalam kutoka kwa kamati ya maendeleo ya kata (WDC) na hatimaye mkutano mkuu wa kijiji uliitishwa kujadili na kufanya maamuzi juu ya rasimu iliyopendekezwa ya mpango wa maendeleo wa kijiji cha Chamakweza kwa mwaka 2012 ambayo ilikuwa na vipaumbele vifuatavyo;

(i) Matumizi bora ya ardhi na kutafuta eneo mbadala la malisho nje ya kijiji
(ii) Ujenzi wa zahanati ya kijiji ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya
(iii) Ujenzi wa malambo ili kupunguza tatizo la maji
(iv) Ujenzi wa shule moja ya msingi katika moja ya vitongoji vilivyo mbali na shule zilizopo
(v) Kuongeza idadi ya wanakijiji kushiriki kwa hiari katika vikao na mikutano ya maamuzi.
(vi) Kuongeza pato la mfugaji kwa kuongeza uzalishaji wa maziwa na uzito wa ng'ombe.
(vii) Kupunguza matukio ya wizi wa mifugo kwa kuanzisha mafunzo ya mgambo kwa vijana na kuimarisha ulinzi wa jadi kupitia Morani.
(viii) Kuongeza kipato cha wanakijiji kwa Kuunda vikundi vya ujasiriamali, kutafuta mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha, kupata elimu ya biashara na
(ix) Kuboresha utawala bora.

## 1.3 MALENGO

Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo na Kijiji cha Chamakweza waliazimia kushughulikia orodha ndefu ya changamoto zilizoainishwa hapo juu. Halmashauri na jamii waliweka malengo bayana kupitia jitihada za uwezeshaji wa jamii ambayo ni pamoja na:

(i) Kuapata hati miliki kwa ajili ya ardhi ya ufugaji kwa kaya 652 zilizoko kijijini Chamakweza.
(ii) Kupunguza umbali wa upatikanaji wa huduma za afya kutoka kilometa 20 hadi 3 toka kwenye kaya.
(iii) Kupunguza umbali wa upatikanaji maji kwa mifugo na binadamu.
(iv) Kupunguza umbali wa upatikanaji wa huduma za shule ya msingi kwa baadhi ya vitongoji kutoka kilometa 5 had 2.
(v) Kuongeza ushiriki wa jamii katika vikao vya kisheria kutoka watu 150 hadi kufikia watu 500 kwa kikao kimoja.
(vi) Kuongeza uzalishaji wa maziwa toka lita 1.5 hadi kufikia lita 4 kwa ngombe kwa siku na uzito wa ng'ombe toka kilo 80 hadi 200 kwa ngombe mmoja.
(vii) Kupunguza matukio ya wizi wa mifug toka matukio 40 hadi 10 kwa mwaka.
(viii) Kuongeza kipato cha kaya toka shilingi 3000 hadi 5000 kwa siku na
(ix) Kurahisisha kufikika baina ya vitongoji vinne vya kijiji kwa kuboresha barabara nne zinazounganisha vitongoji na barabara kuu.

## 1.4 MIKAKATI WA UTEKELEZAJI

Mikakati ya utekelezaji ilifikiwa kupitia majadiliano na makubaliano katika mkutano mkuu wa kijiji. Mpango wa maendeleo wa kijiji cha Chamakweza uliainisha hatua zitakazofuatwa wakati wa utekelezaji ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Kuzingatiwa kwa kanuni, taratibu na sheria.** Katika mpango wa maendeleo iliainishwa waziwazi kuwa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo, kanuni, taratibu na sheria lazima zifuatwe. Kwa mfano jamii ilikubaliana kuwa kila mwanakijiji atachangia shilingi 1,000/= kwa kila ng'ombe kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kwa hiyo kila mwanajamii atachangia kulingana na idadi ya ng'ombe alionao. Kutokana na hilo kamati maalum iliundwa kufanya sensa ya ng'ombe kwa kila boma kijijini.

**Utekelezaji.** Katika kupunguza umbali wa upatikanaji wa maji kwa mifugo na binadamu wanajamii walianza kwa kuondoa uongozi usiowajibika. Mradi wa O&OD ulifadhili ziara ya mafunzo ya wanajamii kubadilishana uzoefu na wenzao wa kijiji cha Tulo kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro mwaka 2011. Waliporudi, na kwa kutumia uzoefu walioupata kwenye ziara ya mafunzo wanajamii walianzisha mchakato wa maboresho uliondoa Uongozi usiowajibika na kuweka Timu imara ya Uongozi kidemokrasia. Uchaguzi mdogo uliendeshwa Machi 2012. Mabadiliko haya yalimotisha jamii kupenda mabadiliko na utayari wa kuchangia shughuli za maendeleo.

<u>Kisanduku namba 1: Kikundi cha LORPARAKO</u>
Kikundi hiki kina wanachama 52 kutoka katika vitongoji vya Idara ya maji na Mji mwema. Wanakikundi walichanga jumla yaTsh. 11,600,000 kwa ajili ya kujenga lambo na jina la lambo likawa ni LORPARAKO lenye maana ya "ng'ombe". Viongozi wa kikundi waliwezeshwa kuandaa katiba ya kikundi. Ili kuwe na uendelevu wa mradi wa lambo, kamati ya usimamizi iliundwa. Majukumu yao ni kuhakikisha matumizi ya lambo ni kwa ajili ya wanachama na mifugo yao. Asiye mwanachama akitaka kutumia atalipia shilingi 100 kwa kichwa cha ngombe. Mapato yote yanahifadhiwa kwenye akaunti ya kikundi.

**Ujenzi wa malambo**: Katika kuweka kwa vitendo uzoefu walioupata kwenye ziara ya mafunzo vikundi viwili vya kiuchumi, LORPARAKO (kisanduku namba 1) na NALEPO (kisanduku namba 2) vilichangisha fedha kwa ajili ya kujenga malambo. Hii ni kulingana na sera ya serikali ya kuwezesha wananchi kupitia vikundi. Ikumbukwe kwamba kwa jamiii za wafugaji kama Wamasai, maji ya mifugo ni jambo la muhimu sana.

**Kisanduku Namba 2: Kikundi cha NALEPO**
Kikundi hiki kiliundwa mwaka 2010 na wanakitongoji cha Njiapanda kwa lengo la kutatua tatizo la upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na binadamu. Kwa njia ya kujitolea wanakikundi walichangia jumla ya shilingi 8,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa lambo. Kufuatia mabadiliko ya tabia ya nchi na kwa kutumia uzoefu wa ujenzi wa lambo, mwaka 2012 wanakikundi walichangisha fedha nyingine kiasi cha shilingi 6,430,000/= kwa ajili ya kuondoa tope kwenye lambo, kuongeza kina na hivyo kuongeza ujazo wa lambo. Jitihada hizi siyo tu zilitatua tatizo la maji bali ziliwapa uzoefu wa ziada, kwa mara ya kwanza katika jamii ya wamasai ilianzisha ufugaji wa samaki kwenye lambo ili kupata chanzo cha ziada cha protini. Ikumbukwe kwamba Wamasai hawana asili ya kufuga samaki wala kula samaki, haya ni mabadiliko makubwa! Sifa ziwaendee wawezeshaji mahiri wa kata kwa uwezeshaji thabiti ulioibua miradi mingine miwili ya kikundi hiki. Mradi mmoja ulikuwa wa ununuzi wa ng'ombe kwenye mnada kw aajili ya kuwanenepesha na kuwauza kwa faida. Walianza na ng'ombe wawili mwaka 2012 hadi kufikia ng'ombe saba mwaka 2013. Waliendelea zaidi na kuanzisha ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOs) ili kutoa mikopo kwa wanakikundi waweze kuanzisha biashara binafsi. Walianza kwa kuchangia fedha za mbegu (mtaji) toka mifukoni kiasi cha shilingi 1,026,000/=.

**Ushawishi ili kupata Eeneo Mbadala la Malisho katika Wilaya ya Kisarawe:** Kama ilivyoelezwa awali eneo la malisho lilikuwa dogo ikilinganishwa na idadi ya mifugo iliyokuwepo kijijini (ng'ombe wapatao 27,000). Katika kutatua tatizo hili vikundi saba yaani Ning'ori, Ladoe , Citycorner, Osonyai , Ngotaana, Morani na Kitunda viliungana ili kuunganisha nguvu na kuunda ushirika wa ILARAMATAK kwa lengo la kwenda Wilaya ya Kisarawe kuomba maeneo ya malisho Januari 2012. Vilikundi hivi viliteua kamati teule kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kuomba eneo la malisho. Kutokana na mikakati mizuri ya ushawishi pamoja na mbinu za uwezeshaji walizozipata toka kwa wawezeshaji wa Kata walifanikiwa kupata eneo la malisho la hekta 15,728.94. Wakati kitabu hiki kinachapwa, wafugaji walikuwa wanajiandaa kuhamia kwenye maeneo mapya huko Kisarawe.

**Kuongeza Mahudhurio ya wananchi katika Mikutano kisheria ya Maamuzi:** Mahudhurio hafifu yalisababishwa na wananchi wa kijiji cha Chamakweza kukata tamaa ya kushiriki. Hapakuwa na Uwazi kuhusu matumizi ya raslimali za kijiji ikiwa ni pamoja na ukosefu wa taarifa za mapato na matumizi. Hata pale taarifa hizi zilipotolewa kwa uongozi kulazimishwa wanajamii walikwishapoteza imani kwa takwimu zilizokuwa zikitolewa. Kufuatia ziara za mafunzo katika kijiji cha Tulo jamii iliondoa Uongozi uliokuwepo wa Serikali ya Kijiji na kuweka Timu mpya ya Uongozi inayowajibika. Tangua hapo ushiriki wa jamii katika utoaji maamuzi uliongezeka kutoka 10% hadi 60% mwaka 2013.

**Kudhibiti ongezeko la matukio ya wizi wa mifugo kijijini:** Hili lilitekelezwa kwa kuimarisha Jeshi la Jadi la Morani. Wanamgambo 5 walipatiwa mafunzo ya kijeshi ili kushughulikia matukio ya uhalifu katika kijiji katika misingi ya polisi jamii. Matokeo yake matukio ya uhalifu yamepungua kutoka wastani wa matukio 40 kwa mwaka hadi mawili kwa mwaka**.**

**Kuboresha Barabara Nne za Vitongoji kwa kutumia Mafundi wa Ngazi ya Jamii**. Mafundi 3 vijana kutoka kijiji cha Chamakweza walipelekwa kwenye mafunzo ya tecknoljia mbadala inayotumia nguvu kazi ya utengenezaji wa barabara za vitongoji mwaka 2013/14. Baada ya kurudi toka mafunzoni wamekuwa wakitumiwa kuongoza utengenezaji wa barabra za vitongoji kila inapohitajika.

**Kupunguza umbali wa upatikanaji wa huduma za afya:** Utekelezaji wa kipaumbele hiki ulianza kwa kutenga eneo la ujenzi wa zahanati. Eneo lililotengwa lina ukubwa wa hekta na wakati wa uaandaji wa kitabu hiki vifaa vya unjezi kama vile mawe (lori 2), mchanga (lori 1) vilikuwa katika eneo la Ujenzi.

**Ujenzi wa ofisi ya kisasa ya kijiji**: Shughili hii ilipangwa kutekelezwa katika bajeti ya 2013/14. Hata hivyo kwa kutumia misingi ya kujitolea serikali ya kijiji ilianza kutekeleza mradi kwa kutumia mapato yake. Jamii ilichangia jumla ya shilingi 17,000 na kwa wakati wa uchapishaji wa kitabu hiki ujenzi wa boma ulikuwa umefikia hatua ya lenta. Jengo hili limezingatia viwango vyote vya majengo ya umma, yaani mchanganyiko wa saruji na mchanga kwa ajili ya matofali ni mfuko kwa matofali 25 (1:25). Jengo lina nafasi ya kutosha kwa shughuli za kijiji pamoja na chumba cha mahabusu.

## 1.5 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Kufuatia mchakato wa O&OD iliyoboreshwa rasilimali zilizotumika zimeoneshwa kwenye Jedwali namba 1.

**Jedwali Namba 1: Fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo Kijiji cha Chamakweza**

| MRADI WA MAENDELEO | RASILIMALI ZILIZOTUMIKA (shilingi) |
|---|---|
| Ujenzi wa lambo la kikundi cha LORPARAKO | 11,600,000/= |
| Upanuzi wa lambo la kikundi cha NALEPO | 6,430,000/= |
| Jumla | 18,030,000/= |

## 1.6 MATOKEO YA MCHAKATO WA O&OD ILIYOBORESHWA

Kuna mafanikio kadhaa yaliyopatikana kupitia mchakato wa O&OD iliyoboreshwa yaani kupitia ushirika wa kuweka na kukopa wa vikundi sita vya kiuchumi (ILARAMATAK) jamii ya chamakweza imeweza kumiliki eneo jipya la malisho lenye ukubwa wa hekta 15,728.94 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe; Ardhi hii bado halijafanyiwa uthamini. Viongozi wenye mrengo wa maendeleo na uwajibikaji walichaguliwa katika maboresho yaliyopelekea uchaguzi mdogo uliofanyika Machi 2013. Mipango ya maendeleo inatekelezwa kjwa ushiriki mkubwa wa walengwa wenyewe ikiwemo ujenzi wa ofisi ya kijiji uliofikia hatua nzuri. Ofisi ya kijiji ni muhimu kwa uwepo wa utawala bora katika utoaji wa huduma, ushiriki wa jamii katika mikutano umeongezeka kutoa watu 30 -60 mwaka 2010 hadi kufikia 172 mwaka 2013. Malambo mawili mapya yamejengwa kwa mafanikio na yanatumika. Kwa kiasi kikubwa malambo yamepunguza tatizo la upungufu wa maji kwa mifugo na binadamu. Kwa ujumla jamii ya Chamakweza ina malambo 9. Rejea picha hapo chini.



***Lambo na Timu ya wawezeshaji ikiwa pembeni mwa lambo***

Wizi wa mifugo umedhibitiwa kwa kuimarisha ulinzi wa jadi wa mgambo na Morani.Vikundi vya uzalishaji vimeongezeka kutoka 2 hadi 17. Kwa kutumia juhudi za pamoja jamii imeweza kutatua baadhi ya changamoto na kukusanya mitaji ya kuanzisha biashara binafsi na kazi za jumuia za kijiji.



***Kikundi cha NALEPO wakiwa na Wawezeshaji***



Mradi wa kunenepesha ngombe, Kikundi cha ***NALEPO***

Ukusanyaji wa mapato umeboreshwa na matumizi ya fedha za kijiji na utoaji taarifa umekuwa wa wazi zaidi kwa wanajamii walio wengi hasa wanaohudhuria katika mikutano na taarifa hizi huwekwa katika mbao za matangazo. Fedha zote za Kijiji zinahifadhiwa katika akaunti ya benki na fedha zote za matumizi zinatolewa benki (hakuna matumizi ya fedha mbichi). Utekelezaji wa shughuli za maendeleo unafuata taratibu, kanuni na maamuzi ya vikao. Ushiriki wa wanawake katika shughuli za maendeleo umeongezeka sana. Hili ni badiliko kubwa jema katika utamaduni wa kimasai.

Kijiji cha Chamakweza kimepokea wageni mbalimbali kutoka nje ya Halmashauri na vijiji jirani. Wanajamii kutoka kijiji cha Pingo walifika kujifunza masuala mbalimbali yaliyotekelezwa katika jamiii ya Chamakweza. Kijiji cha Pingo kiliiga toka Chamakweza na kufanya maboresho kwa kuwaondoa viongozi wa Serikali ya Kijiji wasiowajibika. Wafugaji wa kijiji cha Malivundo waliiga jitihada za kujitolea, walichangisha jumla ya shilingi 22,000,000 na kujenga lambo kwa ajili ya huduma ya maji ya mifugo na binadamu. Wanajamii wamehamasika na kwa sasa wanahamasisha "elimu ya mtoto wa kike".

Wanajamii wamehamasishwa kuhusu umuhimu wa ardhi na hati miliki. Kupitia utekelezaji wa maendeleo kwa kutumia njia ya kujitolea kujiamini kwa wanajamii kumeongezeka kwa kiasi kikubwa. Hii inadhihirika kwa namna mradi mmoja unavyopeleka uanzishwaji wa mradi mwingine kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika miradi iliyotangulia.

**1.7 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika mchakato wa utekelezaji, jamiii ilishuhudia migogoro ya mara kwa mara ya mipaka baina ya vijiji viwili vya Chamakweza na Pingo. Zaidi ya hapo kulikuwa na udhaifu katika usimamizi saidizi katika sekta ya mifugo ya Halmashauri ya Wilaya na kasi ndogo na udhaifu katika kutatua migogoro ya ardhi kati ya vijiji. Hali hii ilizidi kuwa mbaya kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mradi wa maji ya bomba kutoka Kijiji cha Pingo kwenda Vigwaza ambapo Kijiji cha Chamakweza kingeunganishwa kwenye mtandao wa mabomba. Maji ya bomba ni safi na salama zaidi ikilingwanishwa na maji ya lambo. Kwa kuwa hii ni jamii ya wafugaji, ipo haja ya kupata madume bora ya ngo'ombe ili kuongeza viinitete/vinasaba vyenye tija kwa ng'ombe wa asili na hivyo kuongeza uzalishaji wa maziwa na nyama. Katika miongo miwili iliyopita jamii imeshuhudia wimbi kubwa la uporaji ardhi kwa mbinu mbalimbali na hivyo kupunguza maeneo ya malisho.

Ili kupambana na changamoto hizi viongozi wa mkoa wa Pwani na Wilaya ya Bagamoyo walipelekewa malamiko ya migogoro ya ardhi na usuluhishi wa mipaka kati ya vijiji viwili ulifanyika mwaka 2013 kwa makubaliano ya pande zote mbili. Kuhusu mtandao wa maji y abomba Uongozi wa mamlaka ya maji ya Chalinze (CHALIWASA) waliitwa na uongozi wa kijiji kwa mashauriano. Kwa kujibu uongozi wa CHALIWASA

uliahidi kutekeleza mradi utakaosambaza maji ya bomba kwenda Kijiji cha Chamakweza. Jitihada zote hizi zilifanywa na Uongozi mpya wa Kijiji cha Chamakweza wenye mrengo wa maendeleo pamoja na jitihada za uwezeshaji mahiri wa wawezeshaji wa Kata.

**1.8 SIRI ZA MAFANIKIO**

Kabla ya mradi wa O&OD iliyoboreshwa jamii ya cha Chamakweza iliamini kwamba ni jukumu la Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kufadhili utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo. Hali hii ilijenga utegemezi , miradi mingi haikukamilika na wajaamii walibakia kuilaumu serikali kwa kushindwa, licha ya kwamba kulikuwa fursa na uwezo wa kushughulikia matatizo yao. Hivyo siri za mafanikio yaliyoelezwa hapo juu zimetokana na vipengele vifuatavyo:

Mfumo thabiti wa Mafunzo kupitia O&OD iliyoboreshwa umefungua macho na mitazamo ya watu kutambua fursa zilizopo katika maeneo yao na kwamba mfadhili mkuu wa maendeleo ya wanannchi ni wananchi wenyewe, huu ndio msingi wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Kupitia mafunzo ya O&OD jamii imewezeshwa kuchambua vikwazo vya maendeleo yao, kupanga, kutekeleza na kujenga umiliki wa miradi yao ya maendeleo. Mtazamo wa jamii umebadilika, kuna ongezeko la uchangiji wa jamii kwenye jitihada za maendeleo, mahudhurio katika mikutano yameongezeka, na ujasiri wa kuhoji viongozi umeboresha maazimio yao.

Wanajamii wamepata ujuzi mpya na uzoefu wa kupanga ma kuweka vipaumbele vya jitihada za maendeleo angalau kwa mwaka mmoja. Ujuzi huu ulikuwa muhimu katika awamu nyingine ya upangaji mipango. Ziaza ya mafunzo katika kijiji cha Tulo ilikuwa muhimu kwa utatuzi wa matatizo yao. Kupitia ziara hii jamii imetambua kuwa ni wajibu wao kutambua matatizo yao na kuwa kwa kiasi kikubwa matatizo yanaweza kutatuliwa na jamii yenyewe. Kwa mfano, waliweza kuchangia fedha kulingana na idadi ya mifugo kiasi cha shilingi 1,000 kwa kichwa cha ng'ombe kwa sababu ufugaji ni fursa katika jamii. Uwezeshaji mahiri wa wawezeshaji wa Kata, ushirikiano wao na jamii usiokoma, ushiriki kwa vitendo katika shughuli za maendeleo na majadiliano ya muda mrefu na kubadilishana mawazo na vikundi mbalimbali katika kijiji kulijenga Imani ya jamii kwa wawezeshaji, watu wakahiari kuchangamana nao.


Wadau wanazingatia kalenda za vikao hasa kwa vikao vya kisheria. Ikiwa vikao havifanyiki mara kwa mara hakuna maamuzi yanyoweza kufikiwa na hivyo kuchelewesha maendeleo. Kuna ufuatiliaji wa karibu na endelevu wa shughuli za maendeleo na jamii. Kwa kuwa jamii ilikuwa inafuatilia utekelezaji ulifanyika kama ulivypangwa na rasilimali kutumika kwa ufanisi. Kuna usimamizi thabiti na matumizi ya rasilimali kwa kutumia sheria ndogo. Usimamizi imara wa sheria ndogo na adhabu kali zilitolewa kwa wakiukaji. Kiwango cha adhabu kilikuwa kikubwa chenye maumivu makali ili kutisha watu kutofanya makosa. Zaidi ya hayo ni marufuku kwa Serikali ya Kijiji kutumia fedha mbichi ambayo haikuhifadhiwa kwenye akaunti ya benki. Kwa njia hii raslimali fedha ipo salama.

Mwisho jamii ya Wamasai ni wachapa kazi, siyo wazembe, na wapo makini kuhusu fursa za kuishi. Wamasai ni wawazi na wakweli. Haiwezekani Masai kwamba kitu hiki ni cheupe ilihali ni cheusi, hatakubali kabisa (maoni ya kiongozi wa kike wa kikundi). Kama jamii imewezeshwa inaweza kufanya mambo mengi. Mafunzo ya darasani na ziara za mafunzo katika jamii za ngazi moja vina thamani kubwa katika mchakato wa maendeleo. Yote haya yaliwezekana kupitia ufadhili wa mradi wa O&OD, wawezeshaji wa Kata na wa wilaya.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO

HALMASHAURI YA WILAYA KILOMBERO

## UWEZESHAJI JAMII KWA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI




*Ramani ya Wilaya ya Kilombero*

***Uzoefu wa Kijiji cha Mangula-B***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ni mojawapo kati ya Halmashauri 7 za mkoa wa Morogoro, nyingine ni Morogoro, Manispaa ya Morogoro, Mvomero, Kilosa, Gairo na Ulanga. Kiutawala halmashauri ya Kilombero ina Tarafa 5, Kata 23 na Vijiji 98. Wilaya ina ukubwa wa kilometa za mraba 14,918 sawa na hekta 1,491,800 ambazo zimegawanyika katika matumizi yafuatayo ( angalia jedwali namba 1).

**Jedwali Namba1: Matumizi ya Ardhi Halmashauir ya Wilaya ya Kilombero**

| Matumizi | Ukubwa (Ha) | Ukubwa kilometa za mraba |
|---|---|---|
| Eneo linalofaa kwa kilimo | 445,896 | 4,458.96 |
| Eneo linalofaa kwa mifugo | 120,000 | 1,200 |
| Eneo la maji na ardhi oevu | 107,626 | 1,076.26 |
| Eneo la misitu ya asili | 125,000 | 1,250 |
| Eneo la hifadhi | 107,915 | 1,079.15 |
| Eneo la misitu iliyopandwa | 6,698 | 66.98 |
| Eneo linalofaa kwa makazi | 578,665 | 5,786.65 |
| JUMLA | 1,491,800 | 14,918 |

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ina wakazi 407,880 wanaume wakiwa 202,789 na wanawake 205,091. Zaidi ya 80% ya wakazi wa Wilaya ya Kilombero wanajishughlisha na kilimo. Mazao yanayolimwa kwa ajili ya chakula ni pamoja na mpunga, mahindi, mihogo, migomba, jamii ya kunde, viazi vitamu na karanga. Mazao ya biashara ni miwa, kokoa na ufuta. Eneo hili linafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji wakati wa kiangazi kwani linapata maji toka vijito na mito mingi. Shughuli nyingine za kiuchumi ni ufugaji, uvuvi, ufugaji wa nyuki na biashara ndogondogo.

**2.0 HISTORIA YA MRADI WA O&OD**

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ni moja kati ya halmashauri 5 zinazotekeleza mradi wa "Kuimarisha Upangaji Mipango shirikishi jamii kwa ajili ya mchakato wa maendeleo ili kuhakikisha upatikanaji wa utawala bora" (O&OD iliyoboreshwa). Mradi ulianza mwaka 2009, kwa kutekeleza shughuli mbali mbali katika vijiji 2 vinavyotekeleza mradi. Vijiji hivyo ni Mang'ula-B kilichopo Kata ya Mang'ula na Matema kilichopo Kata ya Kamwene. Kazi ya awali ilikuwa ni mafunzo ya kina kwa timu za Wawezeshaji wa Kata yaliyolenga kuwajengea uwezo na stadi za kuwezesha na kuratibu mchakato wa upangaji mipango katika vijiji husika.

**3.0 TATIZO**

Kabla ya mradi huu kulikuwa na mfumo wa upangaji mipango wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) ya zamani ambao ulioanza kutekelezwa nchini mwaka 2002. Lengo la mchakato huu lilikuwa kuziwezesha jamii kupanga, kutekeleza, kusimamia, kutathmini na kumiliki mipango yao ya maendeleo kwa utaratibu wa kutoka chini kwenda juu. Mchakato huu ulienezwa kwa kasi kubwa kwa zaidi ya 90% ya Halmashauri zote Tanzania bara. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero mchakato huu ulianza kutekelezwa mwaka 2005 ingawa kwa mafanikio hafifu. Changamoto zilizojitokeza katika mchakato huu zilikuwa:

Ushiriki mdogo wa jamii katika juhudi za pamoja za maendeleo, uwajibikaji na uwazi duni katika masuala ya utawala, ushiriki mdogo katika upangaji halisi na utekelezaji wa miradi, matumizi duni ya rasilimali za jamii, kukosekana kwa uwiano kati ya raslimali, asasi za kusimamia rasilimali na kanuni zinazosimamia raslimali hizo na viongozi wa jamii hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu wajibu na majukumu yao.

Ukosefu wa mfumo thabiti wa kufadhili vipaumbele vya jamii, ushirikiano hafifu wa kisekta na ukosefu wa mfumo wa mrejesho kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii.

**4.0 MALENGO YA MRADI**

Lengo kuu la Mradi lilikuwa ni kuhakikisha kuwa mchakato wa O&OD unaboreshwa ili uweze kufanya kazi kama mfumo thabiti ili kufikia madaraka halisi kwa jamii kupitia mchakato wa ushirikishwaji wa jamii. Mradi ulidhamiria kufikia malengo yake kwa kupata matokeo yafuatayo: (i) Uanzishaji wa mfumo unaotekelezeka wa mafunzo ya wawezehsaji wa Kata. (ii) Modeli ya utekelezaji wa O&OD kwa ajili ya kuimarisha umiliki wa Jamii wa mchakato wa maendeleo yao inafafanuliwa kwa njia ya uhakiki. (iii) Modeli ya matumizi thabiti ya mipango ya maendeleo ya jamii kwa idara za kisekta za hamlashauri inafafanuliwa na kuhakikiwa. (iv) Vigezo muhimu (ujengaji uwezo, uundaji wa taasisi, nk) vinaandaliwa kwa ajili ya hatua za uenezaji.

## 5.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Upekee wa mbinu bora hiii unatokana na mikakati ya utekelezaji iliyotumika. Ili kutekeleza mradi huu, kulikuwa na mambo ya msingi ambayo yalitakiwa kuzingatiwa kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi. Baadhi ya mambo hayo ni kuchagua wawezeshaji wa Kata na Wilaya miongoni mwa watumishi wa ngazi hizo. Katika kila kijiji cha mradi wawezeshaji watatu walichaguliwa na wawezeshaji 4 kutoka ngazi ya Halmashauri ili washiriki kikamilifu katika mchakato.

Mafunzo ya kina ya Wawezeshaji wa Kata na Wilaya; moduli maalumu ilitumika kutoa mafunzo ambapo mawazo, stadi na mbinu za kiubunifu zilifundishwa. Wajibu wa wawezesha ulielezwa bayana. Jukumu kuu la wawezeshaji lilikuwa ni kuiwezesha jamii ili kuinua uwezo wa kutambua na kuelewa masuala yanayohusu jitihada zao na kuboresha uwezo wao wa kujipanga katika kuandaa mipango inayokidhi mahitaji yao. Kufanya tafsiri ya sera, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali ili kuihabarisha jamii kuhusu mapendekezo ya maendeleo. Mengine yalikuwa ni kuheshimu, kutia moyo jamii juu jitihada zao na kushirikiana nao katika utekelezaji wa jitihada zao za maendeleo. Mada kuu katika mafunzo ya wawezeshaji wa kata na Wilaya yalihusisha mbinu shirikishi za kuwezesha jamii, mchakato wa ugatuaji wa madaraka, uimarishaji wa taasisi, upangaji mipango shirikishi, utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

Wawezeshaji wa Kata na Wilaya walihusishwa kikamilifu katika kutoa ushauri wa kitaalamu kulingana na taaluma zao na kujenga daraja kati ya jamii na Halmashauri. Majukumu ya wawezeshaji ngazi ya Wilaya katika mchakato wa O&OD iliyoboreshwa yalikuwa ni kutoa usimamizi elekezi, ufuatiliaji wa mchakato na kutoa mrejesho kwa jamii. Kabla ya O&OD iliyoboreshwa majukumu haya ya wawezeshaji wa Wilaya na kata hayakufikiwa na kila mtumishi wa Ugani alijikita katika sekta kulingana na taaluma yake. Watumishi wengine wa Ugani katika Kata na Vijiji waliwezeshwa kikamilifu na wawezeshaji wa Kata na Wilaya.

Mafunzo ya darasani yalikuwa mafupi na baadaye wawezeshaji walijikita kwenye zoezi la muda mrefu la maandalizi ya jamii kwa muda wa siku 72 kwenye vijiji vyao kwa kutembelea na kuendesha majadiliano yasiyo rasmi katika kila Kitongoji. Na hii ndiyo tofauti kubwa ambayo inaonekana kati ya mfumo wa awali na huu unaoboreshwa. Katika kipindi hiki wawezeshaji waliendesha utafiti shirikishi wa jamii ili kuelewa hali halisi na fursa za jamii na mahitaji ya watu, kutambua fursa zilizopo na namna fursa hizo zinavyoweza kutumika. Pia walitambua shughuli zinazofanywa na vikundi mbalimbali na kuwatia moyo na kuwaimarisha. Hatimaye walitoa mrejesho kwa jamii kuhusu matokeo ya utafiti jamii. Baada ya maandalizi ya jamii, jamii ilihamasika kikamilifu na kuelewa hali halisi. Ni baada ya kipindi hiki upangaji wa mipango ya jamii ulianza kwa kutumia mchakato wa O&OD iliyoboreshwa unaotumia hatua zita muhimu:

(i) Maandalizi: Katika hatua hii kuna mambo makuu mawili yanayofanyika, la kwanza ni uzinduzi wa mchakato wa upangaji na kuchagua wawakilishi wa jamii watakaoandaa mpango wa maendeleo. Na la pili ni kutoa mafunzo ya upangaji mipango kwa wawakilishi wa jamii.

(ii) Kufanya mapitio ya taarifa na nyaraka: katika hatua hii jamii inapitia taarifa mbalimbali zilizopo ili kufahamu hali halisi ya jamii kwa kipindi cha upangaji. Pia inahusisha kupitia mipango ya miaka iliyopita, mipango ya TASAF, PADEP na miradi mingine iliyopo kijijini. Hii inasaidia kujikumbusha vipaumbele vilivyopita na kwa kiasi gani vilitekelezwa.

(iii) Upangaji halisi wa mipango. Katika Hatua wawakilishi wa jamii kutoka kila kitongoji wanachambua hali halisi na hatua zilizofikiwa kwa kutumia uzoefu wa nyuma ili kupanga hatua za utekelezaji kulingana na vipaumbele vya jamii.

(iv) Mikutano ya Mashauriano: Katika hatua hii rasimu ya mpango wa jamii inajadiliwa katika ngazi ya Kitongoji ili kuweza kupata maoni ya watu kwenye ngazi ya msingi kwa ajili ya kuboresha mpango. Maoni kutoka vitongoji vyote yanajumuishwa kuboresha mpango ulio na maoni ya Kijiji chote. Baada ya hapo mpango wa jamii ulioboreshwa unajadiliwa katika kamati ya maendeleo ya kata, kupata ushauri wa kitaalamu na baadaye unarudishwa kwenye jamii kwa ajili ya makubaliano.

(v) Makubaliano na Kupitisha Mpango. Katika hatua hii, mkutano mkuu maalum wa Kijiji unaitishwa ili kupata makubaliano ya kijiji kizima, wanakijiji wanapata fursa ya kujadili rasimu na makubaliano yakifikiwa rasimu inapitishwa na kupelekwa ngazi ya Halmashauri ya Wilaya.

(vi) Kuwasilisha Mpango wa Jamii Katika Ngazi ya Halmashauri ya Wilaya: Mpango wa Kijiji unawasilishwa katika Halmashauri ya Wilaya na Afisa Mtendaji wa kijiji.

Baada ya hatua hizi sita kwa kiasi kikubwa ushiriki wa jamii umeweza kuonekana katika kila hatua. Katika mpango huu jamii imetambua fursa, muda wa utekelezaji na ina miliki mpango wa kijiji utaotekelezwa na jamii yenyewe na endapo kuna usaidizi kutoka nje hiyo ni fursa ya ziada kwa sababu jamii inaweza kufanya yenyewe.

**Utekelezaji wa Mckato wa O&OD iliyoboreshwa kijiji cha Mang'ula-B**

Mafunzo ya nadharia na vitendo ya Wawezeshaji wa Wilaya na Kata yalifuatiwa na zoezi la uchambuzi shirikishi wa hali halisi ya jamii kwa kutembebelea Vitongoji vyote. Mikutano isiyo rasmi ilifanyika ili kuhamasisha jamii. Wawezeshaji wa Kata waliendelea kuwa karibu na jamii kwa kushiriki shughuli za kila siku za jamii. Wawezeshaji wa Kata walihakikisha, uundwaji na uimarishaji wa vikundi na asasi za kijamii. Baadaye jamii ilianza kupanga mipango ya maendeleo inayozingatia mahitaji halisi ya jamii.



Wawezeshaji wa Kata ya Mangula, Timu ya O&OD toka TAMISEMI, Wawezeshaji wa Wilaya na Kata ku toka H/W Ulanga wakikagua ujenzi wa madarsa 2 na ofisi ya Waalimu



Jamii ya Mangula-B wakikakarabati na kutengeneza barabara za vitongoji

Hatua muhimu katika mradi huu ilikuwa ni utekelezaji wa mpango wa jamii ya Mang'ula-B, huku jamii yenyewe ikiwa imeshikilia usukani wa mchakato huo. Ili kufaidi matunda yatokanayo na kujifunza kwa wengine walio kwenye ngazi moja, yaani vijiji vilivyofanikiwa, jamii ya Mang'ula-B iliandaa safari ya mafunzo kwenda kijiji cha Kaole-Halmashauri ya Bagamoyo; na Mang'ula-B nao kwa kupokezana wakapokea wageni waliokuja kujifunza kutoka vijiji vya Homboza- Kisarawe, Libenanga na Nakafuru-Ulanga na Matema -Kilombero.

Wawezeshaji wa Kata waliendesha mafunzo ya utawala bora kwa wajumbe wa serikali ya kijiji na viongozi wa vikundi vilivyoko hapo kijijini. Pia waliendesha mafunzo ya ujasiariamali kwa ajili ya vikundi vinavyohusika na shughuli za uzalishaji-mali ili kuvijengea uwezo. Wawezeshaji wa Kata waliwezesha zoezi la kuchagua na kufundisha Wawezeshaji kumi (10) wa ngazi Jamii yaani (WJ) juu ya stadi mahiri za uwezeshaji , (hawa ni wanajamii wapenda maendeleo) wenye uwezo wa kuwezesha wanajamii wenzao.

Mafundi watatu wa kijijini waliteuliwa na kupelekwa kwenye mafunzo ya ujenzi wa barabara (ujenzi wa barabara mlisho). (yaani bila kutumia mashine). Mafunzo haya yalifanyika kijiji cha Matema, na kuendeshwa na Chuo cha Tekinolojia Rahisi (*Appropriate Technology Institute -ATI)* kwa ufadhili wa Mradi wa O&OD iliyoboreshwa. Siku ya Jumamosi ilitengwa maalum kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii. Kuna sheria ndogo inayotoa adhabu ya shilingi 2,000 kwa kaya ambazo hazitashiriki shughuli za maendeleo. Fedha iliyotokana na faini na adhabu hizi ilitumika kununulia vifaa vya kufanyia kazi kama vile majembe na koleo.

## 6.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

### Rasilimali-fedha

Mradi hautoi fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya jamii (inajenga moyo wa jamii wa kujitegemea) hata hivyo mradi una mchango mkubwa sana katika ujengaji wa uwezo wa jamii kwa Wawezeshaji wa Kata, Wawezeshaji wa Wilaya na Wawezeshaji ngazi ya Jamii. Kwa mantiki hiyo, washirika wanachangia moja kwa moja gharama na haikuwa rahisi kuonyesha viwango hivyo hapa. Hata hivyo wanufaika wameoneshwa kwenye Jedwali namba 3 hapo chini.

**Jedwali namba 3: Wanufaika wa Mafunzo ya Mradi wa O&OD Kijiji cha Mang'ula-B**

| Walengwa | Shughuli | Mwaka |
|---|---|---|
| **Jamii ya Mang'ula-B** | Maandalizi ya Jamii/Ujenzi na uimarishaji wa taasisi | 2009/2013 |
| **Wawezeshaji wa Kata Mang'ula-B** | Mafunzo ya O&OD | 2009/2013 |
| **Wawezeshaji wa Wilaya KIlombero** | Mafunzo ya O&OD | 2009/2013 |
| **Vikundi vya Jamii** | Mafunzo ya Ujasiriamali | |
| **Vikundi vya Jamii** | Ziara za mafunzo | |
| **Vikundi vya Jamii** | Kuwezesha Vikundi | |
| **Wawezeshaji wa Kata/Wilaya** | Usafiri kwa shughuli za O&OD /Pikipiki | |
| **Mafundi watatu wa jamii** | Mafunzo ya teknolojia rahisi ya ujenzi wa barabara kupitia chuo cha ATI | |

**Rasilimali watu**

Wakufunzi wawili kutoka chuo Cha Serikali za Mitaa Hombolo walihusika katika kuandaa moduli ya kufundishia na kuendesha mafunzo kwa Wawezeshaji wa Kata. Wataalam wanne toka Japan walihusika katika kuwezesha na kutoa usaidizi kwenye mchakato huu. Wataalamu wanne kutoka OWM-TAMISEMI walihusika kusimamia shughuli za mradi kutoka makao makuu. Waratibu watatu kutoka kila Halmashauri ya majaribio na Mratibu mmoja kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa walikuwa na jukumu la kuratibu mchakato na kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye ngazi za msingi. Utaratibu huu pia ulikosekana katika utekelezaji wa O&OD ya mwanzo. Mafundi mchundo watatu walihusishwa katika kutoa mafunzo kwa vitendo kwa mafundi mchondo kutoka vijiji vya majaribio ya mradi.

## 7.0 MATOKEO NA MAFANIKIO

Baada ya miaka mitatu (2010 - 2012) ya utekelezaji wa mradi wa majaribio kumekuwepo na mafanikio ya kuridhisha. Matokeo haya yamegawanyika katika makundi matatu nayo ni: Mafanikio katika usimamizi na matumizi yenye tija ya rasilimali na usimamizi wa sheria na kanuni. Mafanikio haya yanaweza kutazamwa katika mitazamo miwili, mafanikio yanaonekana dhahiri (vitu halisi) na mafanikio yasiyoonekana dhahiri (ambayo huwezi kuyaona kwa macho mfano mchakato). Baadhi ya matokeo yanayoonekana dhahiri yamefafanuliwa hapa chini.

**Usimamizi Imara na Matumizi Sahihi ya Rasilimali**

Vyanzo vipya vitano vya mapato viliibuliwa na Kijiji, hivyo kuongeza idadi ya vyanzo vya mapato kutoka vitatu mwaka 2010 hadi vinane mwaka 2012. Ubunifu huu wa vyanzo vya mapato ulihusu ujenzi wa vibanda kwa ajili ya kukodisha wafanya biashara kuzunguka uwanja wa mpira wa kijiji na vyumba vya biashara kuzunguka ofisi ya Kijiji na ofisi ya Kata. Shule mpya Msingi ilijengwa na jamii kwa njia ya kujitolea. Madarasa mawili, ofisi moja ya waalimu katika shule ya msingi vilijengwa na jamii mwaka 2010.
Madarasa matatu yalijengwa katika Shule ya Sekondari ya Kata kwa juhudi kubwa kutoka jamii ya Mang'ula B. ujenzi wa barabara za Vitongoji uliongezeka kutoka 1.25 mwaka 2010 hadi kilometa 15 mwaka 2012. Jamii ya Mang'ula B ilichangia kwa kiasi kikubwa gharama za ujenzi wa ofisi ya Kata na kutoa eneo la ujenzi. Kutokana na mchakato huu vikundi vya kijamii viliimarika kwa kasi. Hii inadhihirishwa na kupanuka kwa shughuli za vikundi na vikundi kuwa na zaidi ya mradi mmoja. Rejea jedwali namba 4 hapo chini.

**Jedwali namba 3: Mtawanyo wa miradi iliyoanzishwa na vikundi vya kijamii na kiuchumi Kijiji cha Mangu'la-B**

| Vikundi | Miradi |
|---|---|
| **AMANI** | Uzalishaji mpunga, kilimo cha bustani, ufugaji ng'ombe wa maziwa, Kuanzisha chama cha ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOs) |
| **UPENDO** | Uzalishaji mpunga, kilimo cha bustani, ufugaji ng'ombe wa maziwa, Kuanzisha chama cha ushirika kuweka na kukopa (SACCOs) |
| **UVUMILIVU** | Ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOs), kilimo cha bustani |
| **LENGO LETU** | Uzalishaji mpunga, Kuanzisha chama cha ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOs) |
| **JIINUE NIKUINUE** | Ufugaji ng'ombe wa maziwa, kilimo cha bustani, kilimo cha migomba, kupanda miti |
| **NJOKAMWONI** | Hifadhi ya mazingira kwa ushirikiano na TANAPA kwa mafunzo stahili, ufugaji wa nyuki, kupambana na wanyama waharibifu mfano kuzuia tembo wasiingie mashambani kwa kutumia elimu asilia ya kuzungusha kamba ya katani iliyolowekwa kwenye pilipili kuzunguka mashamba, mradi wa "benki ya matofali" kwa ajili ya amatumizi mbalimbali ya miradi ya maendeleo ya jamii . |



*Kikundi cha Upendo - ufugaji wa ng'ombe wa maziwa*



*Ujenzi wa barabara ya Kijiji cha Mang'ula B kwa tekinolojia rahisi*

### Uimarishaji wa Taasisi

Vikundi vya jamii vimeongezeka toka 3 mwaka (2010) hadi kufikia 15 mwaka (2013). Utaratibu wa kutumia vikundi ndio utaratibu wa kitaifa wa kuiwezesha jamii kiuchumi badala ya utaratibu wa kutumia mtu mmojammoja. Moyo wa jamii wa kujitolea katika shughuli za jamii umeongezeka kutoka watu 150 mwaka (2010) hadi watu 450 mwaka (2013). Mikutano ya hadhara ya kijiji imeongezeka toka mkutano mmoja mwaka (2010) hadi mikutano sita mwaka (2013). Vikao vya kisheria vya kijiji vimeongezeka toka viwili mwaka (2010) hadi vinne mwaka (2012). Mahusiano ya kikazi yameimarika kati ya jamii na taasisi zinazozunguka kijiji yaani Mamlaka ya Mbuga za Wanyama (TANAPA), *Mang'ula Engineering Company (MECO)* na hoteli ya kitalii ya Hondohondo; ambapo TANAPA imejenga madarasa mawili ya shule ya Sekondari, MECO walitoa mawe na mchanga kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Kijiji na Shirika la Misaada la Kikatoliki (CARITAS) waliendesha mafunzo kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa. Mafundi mchundo watatu waliopewa mafunzo na mradi kuhusu teknolojia rahisi ya ujenzi wa barabara za Vitongoji katika Kijiji tayari wameonyesha ujuzi wao kwa kujenga barabara na makaravati.

### Utungaji na Utekelezaji wa Sheria Ndogo na Kanuni

Vikundi vya kijamii tayari vina katiba ambazo hutumika kuongoza shughuli za vikundi. Vikundi vingi vina sheria ndogo na hutumika kuadhibu wanaokiuka taratibu za kikundi mfano kutoza faini kwa anayechelewa kwenye mikutano. Sheria ndogo hizi zilipitishwa na Mkutano Mkuuwa Kijiji Septemba 2012.

**Matokeo ambukizi**
Jamii ya kijiji cha jirani cha Mang'ula-A imeiga kutoka kijiji cha Mang'ula B na kujenga barabara ya kilometa moja inayounganisha vijiji hivi viwili na walichangia Tsh 1,000, 000 kwa ajili ya ujenzi wa makaravati. Jamii ya Kijiji cha jirani cha Msalise iliiga kutoka Mang'ula B na kujenga kilometa 5 za barabara ili kuunganisha vijiji hivyo viwili. Zaidi ya hayo vikundi vinne vya vimeanzishwa. Jamii ya Kijiji cha jirani cha Kanyenja, wameiga kutoka Mang'ula B kwa kusafisha pori, kungoa visiki na kujenga barabara ya Kilometa saba kuunganisha vijiji viwili. Hivyo, vijiji vitatu zaidi vimeunganishwa na kijiji cha Mang'ula-B kwa barabara zilizojengwa kwa njia ya kujitolea.



*"…….. Posho za vikao katika shughuli za maendeleo siyo muhimu, bali kilicho muhimu ni elimu na ujuzi utakaopatikana utakaoleta mabadiliko chanya yaliyokusudiwa……"*



*Mzee. Mohamedi Kawala mwenye umri zaidi ya miaka 70 anasema mwanzoni alitarajia mradi utagawa posho; hivyo alipinga utekelezaji wa mradi kwa njia ya kujitolea. Alipita nyumba hadi nyumba kushawishi watu wakatae mradi. Leo mtazamo wake umebadilika, ameomba radhi kwa wanajmii na kwa sasa yuko mstari wa mbele kutekeleza mradi (nimezaliwa upya! anasema)*

**Matokeo yasiyoonekana**
Wanajami wamejengewa uwezo wa kutosha wa kupigania maendeleo yao, kutambua rasilimali na wanaweza kuthubutu kudai uwajibikaji wa viongozi kwa jamii. Kuna mabadiliko chanya ya mtazamo wa jamii, kwa sasa kuna ongezeko kubwa la ushiriki katika shughuli za maendeleo na wamechana na tabia ya utegemezi. Kwa mfano mmoja wa wanajamii Bwana Habibu Ally alinukuliwa akisema "…posho za vikao vya maendeleo zinadumaza maendeleo..." Rejea kisanduku picha ya kwanza na kisanduku hapo juu.

Wanajamii wa Mangula-B wamefurahia sana na wanatoa shukrani kwa ajili ya stadi, ujuzi, mbinu na maarifa mapya waliyopata kupitia machakato wa mradi wa O&OD. Kuna ongezeko la ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za maendeleo mfano, ushiriki katika ujenzi wa madarasa, vyumba vya kupangisha na ofisi ya Kata. Kijiji kina akiba yamatofali ya kuchoma "benki matofali" ambayo hutumika kutekeleza miradi ya jamii. Vikundi vya jamii vimeongezeka kutoka vitano mwaka 2009 hadi 12 mwaka 2013.

Vikundi vya jamii vinanguvu na vimewezeshwa zaidi kuliko hapo awali. Wanavikundi wamepata mafunzo na matokeo yake wameweza kutengeneza katiba zao, wamepanua wigo wa shughuli zao mfano ufugaji nyuki, uhifadhi wa mazingira, ufugaji ngombe wa maziwa, ujenzi wa barabara. Mahudhurio kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji yameongezeka kutoka watu 50 hadi watu 450. Viongozi wa vikundi na wa vijiji huchaguliwa kidemokrasia na kwa uwazi zaidi, ni wawazi zaidi kuliko ilvyokuwa awali, kuna kuboreka kwa haraka kwa mahusiano kati ya viongozi wa kijiji na wanajamii.

Mahusiano na ushirikiano kati ya jamii na wadau wengine umeimarika na yana tija kuliko ilivyokuwa hapo awali. Kiwango cha uhalifu kimepungua kutoka matukio 12 mwaka 2009 na kufikia mawili tu mwaka 2013. Kwa ujumla, jamii imedhihirisha kiwango cha juu cha ukomavu katika kuimarisha misingi ya utawala bora, mfano upotevu wa fedha za kijiji kiasi cha Tsh 2,300,000 uliotokea huko nyuma ulishughulikiwa ambapo viongozi wa kijiji waliohusika wamefikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

**7.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA**

Maandalizi ya jamii huchukua muda mrefu na hili ni pungufu mojawapo la upangaji mipango shirikishi. Hivyo, wawezeshaji wanapaswa kuwa wavumilivu sana huku wakijua kwamba mipango endelevu huhitaji upembuzii wa kina na maandalizi ya kutosha.

Mafunzo yaliyotolewa kwa jamii hayakufikia makundi yote ya kiumri ya jamii; badala yake yaliekezwa kwa viongozi wa kijiji na vikundi vinavyojishughulisha na masuala ya ujasiriamali. Hata hivyo katika utekelezaji wa mradi wa O&OD iliyoboreshwa, mradi ulifungua milango kwa wageni na vikundi toka nje kuja kujifunza na hivyo kuwa na haja ya kuboresha ubora wa huduma zao. Bado kuna watu wachache katika jamii ambao hawajahamasika, kujitambua na kushiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo za jamii.

Usaidizi toka ngazi ya Mkoa na Halmashauri bado ni kidogo kuufanya mchakato kuwa endelevu. Mwingiliano wa kisiasa katika mipango ya jamii bado ni tatizo. Mmoja wa wanasiasa katika jimbo hili wakati fulani alijaribu alilazimisha kuanzisha mradi ambao haukuwa katika vipaumbele vya jamii. Kilichosaidia ni uelewa wa juu na jamii iliukataa mradi huo papo hapo.

**8.0 UENDELEVU NA MIPANGO YA BAADAYE**

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ina mikakati ifuatayo katika kutatua changamoto zilizopo: Kuendelea na uhamasishaji wa jamii ili ijitambue na kutekeleza mipango yao ya maendeleo kwa njia ya kujitegemea. Ipo mipango ya kuanzisha kundi kubwa la Wawezeshaji wa Jamii ili kuchochea mchakato wa maendeleo miongoni mwa wanajamii wenzao. Kwa sasa wapo 10 ikimaanisha wawezeshaji wa jamii wawili kwa kila kitongoji cha kijiji cha Mang'ula B.

Viongozi wa Halmashauri wamejizatiti kuainisha, kuzitambua na kuunga mkono pamoja na kutia moyo juhudi zote zinazoanzishwa na jamii kulingana na mahitaji yao kwa kutumia rasilimali fedha kutoka vyanzo mbalimbali. Kuna mafunzo yanayoendelea kwa watendaji wa Vijiji na Kata kuhusu uwajibikaji kwa jamii na uwazi ili kuchochea moyo wa kujitegemea. Halmashauri itaendelea kuitisha vikao vya pamoja na wadau wa maendeleo vya mara kwa mara ili kuendeleza shughuli za maendeleo.

**9.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Siri ya mafanikio ni pamoja na uwezeshaji mahiri wa Wawezeshaji wa Kata na Wilaya ambao walikuwa wamepata mafunzo ya kina ya nadharia na vitendo. Kuna ushiriki endelevu wa jamii na wawezeshaji wa Kata katika mambo yote yanayogusa jamii katika maisha yao. Ziara za mafunzo ni zana madhubuti katika kubadilishana uzoefu na kujifunza katika ngazi moja miongoni mwa vijiji vilivyoko katika mradi. Matokeo yake washiriki wa ziara za mafunzo wamedhamiria zaidi kufanya vizuri katika miradi yao ya maendeleo.

Mafunzo yaliyotolewa kwa jamii kupitia mradi huu yalikuwa ya muhimu katika kubadili fikra. Maandalizi ya jamii ya muda mrefu wa siku 72 yalikuwa ni chombo cha kufanya jamii ijitambue, kubadilika halitabia, kubadilika mwelekeo na huu ulikuwa msingi mkuu wa maendeleo asilia. Kuwepo kwa uzalishaji mkubwa

wa mazao ya miwa na mpunga kama mazao ya biashara ni fursa muhimu katika kusaidia uwezo wa kifedha. Mahusiano mazuri baina ya jamii na wadau wengine wa maendeleo waliozunguka kijiji mfano TANAPA, TANESCO na Hoteli ya Kitalii ya Hondohondo yalikuwa muhimu katika kuendeleza juhudi za jamii.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO

## UWEZESHAJI WA JAMII KWA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI



*Uzoefu wa Kijiji cha Maseyu*

## 1.0 UTANGULIZI

Wilaya ya Morogoro ni miongoni mwa Wilaya tano za Mkoa wa Morogoro. Wilaya hii ipo Kaskazini-Mashariki mwa mkoa, kati ya Latitudi 6º00’ na 8º00’ kusini mwa Ikweta na kati ya Longitudi 36º00’ na 38º’ Mashariki mwa Griniwichi. Inapakana na wilaya za Bagamoyo na Kisarawe (Mkoa wa Pwani) kwa upande wa Mashariki; Wilaya ya Kilombero kwa upande wa Kusini na Wilaya ya Mvomero Kaskazini-Magharibi. Eneo la wilaya hii ni kilometa za mraba 11,731, hii ni sawa na 16.06% ya eneo lote la mkoa wa Morogoro lenye kilometa za mraba 73,039. Kiutawala, Wilaya hii imegawanyika katika Tarafa sita, Kata 29, Vijiji 146 na Vitongoji 737, ona Jedwali namba 1.

**Jedwali 1: Ngazi za kiutawala Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro**

| Tarafa | Kata | Vijiji | Vitongoji |
|---|---|---|---|
| **Bwakira** | 5 | 21 | 124 |
| **Mvuha** | 5 | 26 | 160 |
| **Mikese** | 3 | 13 | 59 |
| **Mkuyuni** | 4 | 24 | 121 |
| **Matombo** | 7 | 39 | 173 |
| **Ngerengere** | 5 | 23 | 100 |
| **Jumla** | 29 | 146 | 737 |

*Chanzo: Idara ya Mipango, takwimu na ufuatiliaji, 2012*

Kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 , Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ina jumla ya watu 286,248, kati yao 140,824 ni wanaume na 145,424 ni wanawake. Wilaya hii ni miongoni mwa wilaya tano nchini zinazotekeleza mradi wa majaribio wa mchakato wa fursa na vikwazo kwa maendeleo almaarufu kama O&OD iliyoboreshwa na kijiji cha Maseyu ni miongoni mwa vijiji 10 nchini ambavyo vinatekeleza mradi huu. Kijiji cha Maseyu kipo kandokando ya barabara ya Morogoro-Chalinze, mara baada ya msitu wa hifadhi wa Kitulungalo na kina Jumla ya Vitongoji vitano.

Kabla ya ujio wa mradi wa O&OD iliyoboreshwa, Kijiji cha Maseyu kilikuwa miongoni mwa vijiji vyenye historia mbaya sana ya vitendo vya uhalifu, huduma duni za kijamii, utawala mmbovu, umaskini wa kipato, uharibifu wa mazingira na miundo mbinu mibovu. Hata hivyo, baada ya utekelezaji wa mradi wa O&OD iliyoboreshwa, mambo yamebadilika kiasi kwamba Maseyu iliyokuwa na historia mbaya sasa imegeuka kuwa kitovu cha kujifunzia kuhusu utawala bora. Hii ndiyo sababu inayofanya mbinu bora ya Maseyu ijadiliwe kwenye sehemu zinazofuata.

## 2.0 TATIZO

Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa msaada wa kitaalamu toka Shirika la Ushirikiano la Kimataifa la Serikali ya Japani, imekuwa inaendesha mradi wa “Kuimarisha Upangaji Mipango shirikishi jamii kwa ajili ya mchakato wa maendeleo ili kuhakikisha upatikanaji wa utawala bora” (O&OD iliyoboreshwa) kuanzia mwezi Oktoba 2009. Mradi huu ni matokeo ya mapendekezo yaliyofanywa na timu ya utafiti kuhusu uboreshaji wa mchakato upangaji mipango shirikishi jamii wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) ya zamani uliofanyika kati ya mwaka 2006 na 2008. Utafiti ulibaini mapungufu au changamoto kadhaa za mchakato wa O&OD kama inavyooneshwa kwenye kisanduku namba 1.

**Kisanduku 1: Mapungufu ya O&OD ya zamani**

- *Maandalizi duni ya jamii*
- *Mchakato wa O&OD ya zamani ulisisitiza zaidi upangaji mipango na uandaaji wa bajeti kuliko jamii kutekeleza na kufuatilia vipaombele vilivyoainishwa hivyo kudumaza jamii katika kujitolea na kujitawala.*
- *Uwezo mdogo wa Wawezeshaji wa Kata katika kuwezesha jamii kwa misingi endelevu*
- *Mahudhurio duni, ushiriki hafifu wa jamii katika mchakato mzima wa O&OD*
- *Vipaumbele vya jamii havikuwa vikijumuishwa vya kutosha katika mpango na bajeti ya Halmashauri na bajeti haikutengwa kulingana na vipaombele vya jamii hivyo miradi mingi haikukamilika.*
- *Idara za kisekta hazikuzingatia vipaumbele vya jamii wakati wa kuandaa mpango wa Halmashauri .*

Ili kuondoa mapungufu haya, Serikali ya Tanzania iliiomba Serikali ya Japani kutoa msaada wa kitaalamu kwa ajili ya kuimarisha mchakato wa upangaji mipango shirikishi na mchakato wa maendeleo ya jamii. Kufuatia maombi hayo, JICA ilianza maandalizi ya andiko la mradi kwa kufanya utafiti mwezi Febuari 2009. Kutokana na matokeo ya ufafiti huo, Serikali ya Japani ilikubali kufadhili mradi. Mradi wa O&OD ulilenga vijiji 10, katika Halmashauri 5 katika mikoa ya Morogoro na Pwani. Katika Mkoa wa Morogoro Wilaya tatu zilichaguliwa nazo ni Halmashauri za Wilaya za Morogoro, Kilombero na Ulanga. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Kata mbili za Gwata na Mvuha na Vijiji viwili vya Maseyu and Tulo vilichaguliwa kama Kata na Vijiji vya majaribio.

Katika sehemu hii, mbinu bora katika kijiji cha Maseyu imewasilishwa. Hii ni kwa sababu wakati wa utekelezaji wa mradi wa O&OD iliyoboreshwa, kijiji cha Maseyu kilionekana kuwa ni mbinu bora katika kuimarisha mchakato wa upangaji mipango shirikishi jamii kuleta utekelezaji mzuri wa O&OD iliyoboreshwa na hivyo kuleta mafanikio ya kweli ya madaraka kwa umma na utawala bora kwa maendeleo ya jamii.

## 3.0 MALENGO

Lengo kuu lilikuwa ni kuhakikisha kwamba mchakato wa upangaji mipango wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) unaboreshwa hadi kuwa mbinu bora yenye ufanisi kufikia mafanikio ya kweli ya madaraka kwa umma na utawala bora kupitia mchakato wa maendeleo shirikishi jamii asilia. Malengo mahsusi ya kuboresha mchakato wa O&OD kwa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro yalikuwa ni pamoja na:-

(i) Kuboresha mchakato wa upangaji mipango katika jamii

(ii) Kuimarisha umiliki wa jamii wa mchakato wa maendeleo yao

(iii) Kuhakikisha Idara za kisekta zinajumuisha vipaumbele vya jamii na kuwapa huduma kulingana na vipaumbele na mahitaji halisi

(iv) Kuboresha uratibu wa kisekta katika Halmashauri

(v) Kutoa usaidizi katika kuboresha mchakato wa upangaji mipango na maendeleo ya jamii.

(vi) Kuimarisha uwezo wa Wawezeshaji ngazi ya Kata katika jamii.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Watekelezaji wa mradi waliimarisha juhudi za wananchi kwa njia ya kuhakikisha kwamba kuna maandalizi ya jamii ya kutosha na ya kina. Katika ngazi za msingi, mradi ulisisitiza na kuweka mkazo sana katika suala zima la maandalizi ya jamii kama hatua ya muhimu na ya msingi katika mchakato wa maendeleo ya jamii. Maandalizi ya jamii hujumuisha wawezeshaji kutembelea jamii mara kwa mara, kushikamana na kushirikiana na jamii katika mambo yote. Wawezeshaji huenda kwa jamii kama timu ya uwezeshaji yenye taaluma na uzoefu wa fani mbalimbali ili kujibu hoja za jamii kwa ujumla. Katika maandalizi ya jamii kazi kubwa ni kuhamasisha jamii ijitambue, ielewe kwa undani mazingira yanayowazunguka na kisha kujipanga wenyewe kisha kupanga hatua za kuchukua ili kufikia mahitaji ya jamii nzima.

Maandalizi ya jamii ndiyo msingi na hatua ya kwanza katika shughuli zote za maendeleo ya wananchi ikiwa ni pamoja na upangaji wenyewe wa mipango. Lakini maandalizi ya jamii huimarishwa pale jamii yenyewe inapopata fursa ya kushiriki moja kwa moja kwa vitendo na kutekeleza yenyewe mipango yake. Maandalizi ya jamii yanalenga kuifanya jamii ifike mahali pa kubadili halitabia, kuzitambua na kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii na katika maisha ya siku kwa siku kwa maendeleo yao wenyewe. Katika zoezi la maandalizi ya jamii, Wawezeshaji ngazi ya Kata na Wawezeshaji ngazi ya Wilaya, wanapokuwa wanafanya kazi pamoja na jamii, hali hii hujenga kuaminiana na maelewano ya karibu baina yao, na mahusiano haya ni ya muhimu sana katika maendeleo endelevu ya jamii.

**Mchakato wa Upangaji Mipango ya Jamii.** Katika mchakato wa upangaji mipango shirikishi jamii kuna hatua sita muhimu:- (i)Kuiandaa Jamii ni pamoja na (Kuzindua mpango na mafunzo kuhusu mbinu za upangaji mipango), (ii) Utafiti au uchambuzi wa hali ya jamii na kufanya marejeo ya nyaraka mbali mbali ili kutambua hali halisi ya jamii ilivyo wakati wa kupanga na kama kuna mipango inyoendelea, (iii) kupanga mipango, (iv) kushauriana wataalam na wadau wengine wa maendeleo, (v) kupitisha mpango, (vi) kubadilishana mawazo kuhusu mpango wenyewe.

**Kuimarisha Mahusiano baina ya Jamii na Halmashauri.** Mahusiano haya yalijengwa kwa wale Wawezeshaji Kata kuwa karibu na jamii na wakati huo huo Wawezeshaji wa ngazi ya Wilaya wakijenga uwezo wa Wawezeshaji wa kata kwa njia ya usimamizi elekezi. Katika mazingira ya kupanga mipango ya jamii, Wawezeshaji wa Kata hufanyika kiungo katika kuwasilisha vipaombele vya Jamii kwa Halmashauri na kuchukua juhudi au mawazo ya Halmashuri kwenda kwa Jamii. Pia Wawezeshaji ngazi ya kata hufanyika kiungo cha kupeleka mrejesho kwa jamii kuhusu usaidizi toka Halmashauri, teknolojia toka taasisi za nje kama zile za utafiti na pia kama kuna fursa zimepatikana za mikopo toka vyombo vya fedha. Wawezeshaji ngazi ya Wilaya katika mradi huu walikuwa na majukumu makuu mawili. Kwanza kuwapatia maelekezo na usaidizi unaohitajika katika kazi zao Wawezeshaji wa kata na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa vipaombele vya jamii ili kuhakikisha kwamba juhudi za jamii zinapata usaidizi unaostahili wa kifedha na kiufundi toka Halmashauri.

**Kuimarisha Mahusiano ya Kirafiki kati ya Jamii na Halmashauri kupitia Uratibu wa Kisekta.** Itakumbukwa kwamba usaidizi, maelekezo na ushauri wa Halmashauri ulikuwa unapelekwa kwa jamii kupitia Wawezeshaji Ngazi ya Wilaya na Ngazi ya Kata (DTFs na WFs,) na watumishi wengine mfano Walezi wa Kata ambao wana jukumu la msingi la kuwezesha mchakato wa kupanga mipango shirikishi ya maendeleo. Katika mchato huo na mazingira hayo ya ushirikiano na usaidizi, maelewano yanayojengeka hapa yanaakisi vipaombele vya jamii kwa upande mmoja na kwa upande wa pili unaakisi jitihada za Halmashauri ndani ya upangaji mipango, kutenga bajeti ya miradi husika na kutoa usaidizi wa kiufundi kulingana na mahitaji ya jamii.

Katika kubadilishana habari na uzoefu ndani ya mikutano ya timu ya menejimenti ya Halmashauri yaani (CMT) husaidia sana wajumbe wa timu hii ambayo hujumuisha wakuu wa idara kuelewa vipaombele vya jamii na kuviingiza katika mipango na bajeti za idara zao za kisekta. Baada ya mipango na kupitisha bajeti katika ngazi ya Halmashauri, wawezeshaji ngazi ya kata, wakisaidiwa na wale wa wilaya hupeleka mrejesho kwa jamii kuhusu ni kwa kiasi gani vipaombele vyao vimezingatia katika mipango ya idara za kisekta na bajeti husika. Kulingana na usadizi halisi wanaoweza kupata kutoka ngazi ya Halmashauri, wawezeshaji ngazi ya kata wanawezesha jamii kurejea tena mpango wao na kuufanyia marekebisho stahiki, kisha kuweka mawazo mbadala wa namna ya ketekeleza mpango wao na viapaombele vyao bila kutegemea sana misaada ya Halmashauri. Inasisitizwa hapa kwamba kuhusu masuala haya ya jamii kujitegemea, mafunzo ya wawezeshaji katika mradi huu yalikuwa ya vitendo zaidi kuliko nadharia, ili waweze kuiwezesha jamii inavyostahili badala ya kuijengea utegemezi.

Utafiti shirikishi jamii uliolenga kuchambua halisi ya jamii ulifanywa na timu ya wawezeshaji ngazi ya kata wenye fani na utaalam mbalimbali, kwa kutembelea mara kwa mara na kuhojiana, kujadiliana na wanajamii katika kila kitongoji au mtu mmoja mmoja au katika vikundi vya kijamii kupitia mikutano isiyo rasmi. Kwa namna hii ilikuwa rahisi watu kuongea kwa uhuru na kuonesha hapa yale mambo ambayo yasingejulikana kwa njia nyingine. Hapa ikumbukwe kwamba kwenye kitongoji ndiko hasa shughuli za maendeleo zinakofanyika. Kwenye kisanduku namba 2 pameoredheshwa baadhi shughuli zilizofanywa na wawezeshsaji ngazi ya kata kwenye vitongoji katika mradi wa O&OD iliyoboreshwa ambavyo ni ubunifu ambao haukuweko katika O&OD iliyotangulia.

**Kisanduku namba 2 : Shughuli muafaka au za viwango katika mchakato wa O&OD iliyoboreshwa**

- Wawezeshaji ngazi ya Kata (WFs) kufanya mikutano isiyo rasmi ili kuhamasisha jamii.
- Wawezeshaji ngazi ya Kata (WFs) kushirikiana na jamii katika shughuli zote za kijamii.
- Wawezeshaji ngazi ya Kata (WFs) kuwezesha vikundi kujipanga na kivijengea uwezo wa kujisimamia vyeneywe.
- Kupanga mipango shirikishi jamii ya kina kwa kuzingatia mahitaji halisi ya jamii.
- Kutekeleza mipango shirikishi jamii, jamii yenyewe ukiwa mstari wa mbele katika utekelezaji .
- Kufanya ziara za mafunzo kwa kubadilishana na vijiji vingine.
- Wawezeshaji ngazi ya Wilaya (DFs)kuendesha mafunzo mafunzo ya utawala Bora kwa viongozi wa kijiji na vikundi.
- Wawezeshaji ngazi ya Wilaya (DFs)kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa wanavikundi vya ujasiriamali .
- Kufundisha na kuwaandaa Wawezeshaji 10 ngazi ya Jamii (CFs)ili kurahisisha zoezi la kuhamasisha na kuongeza mwamko wa jamii.

**Shughuli za Maendeleo za Jamii.** Katika kijiji cha Maseyu kuna makundi mawili ya mipango ya shughuli bunifu za jamii. (i) miradi midogo ya jamii ikihusisha kijiji chote na (ii) Shughuli za ujasiariamali za vikundi vya kijamii na kiuchumi.



*Ujenzi wa shule ya awali (chekechea) katika kitongoji cha Kitulung'alo na matumizi ya vipaza-sauti katika mfumo wa upashanaji habari katika kijiji cha Maseyu*

Shughuli zilizotekelezwa katika miradi ya kijiji kizima inajumuisha ujenzi wa zahanati ya kijiji, ujenzi ulishafika ngazi ya linta wakati wa uhakiki wa kisamkasa hiki. Ujenzi wa madarasa ya awali yaani chekechea na nyumba za walimu katika kila Kitongoji, ilikuwa ni hitaji la muhimu la jamii kujenga shule za awali katika kila kitongoji kwa sababu kuna barabara kuu kukatikaza kijiji, inayopitisha magari yaendayo kasi na hivyo kuhatarisha maisha ya watoto wa chekechea wanapovuka barabara kwenda kwenye madarasa ya awali upande wa pili wa barabara. Kiwango cha utekelezaji wa ujenzi hutofautiana toka kitongoji hadi kitongoji kingine, vitongoji vilivyo vingi walishafika kwenye linta. Wakishafika kwenye linta ni wajibu wa Halmashauri kutoa usaidizi hasa kwa kupaua na kupigilia mabati kwenye majengo ya kijiji.

**Shughuli za Maendeleo za Vikundi.** Hizi hutekelezwa na vikundi husika kama inavyooneshwa katika kisanduku namba 2.

**Jedwali namba 2: Shughuli za Maendeleo za Vikundi kijiji cha Maseyu**

| Jina la kikundi | Jina la mradi au shughuli |
|---|---|
| Amani | Ufugaji wa kuku (Kuku chotara kutokana wale wa kisasa na kienyeji)<br>Biashara ndogondogo za utengenezaji sabuni za maji, kutengenzeza nguo za mawingu au batiki, kuuza vitenge |
| KIUMAMA | Ufugaji wa kuku (Kuku chotara )<br>Kilimo cha wakulima wadogo kifamilia<br>Mradi wa ufyatuaji matofali ya kuchoma<br>Hifadhi ya mazingira<br>Kupambana na maambukizo mapya ya UKIMWI na unyanyapaa |

| | |
|---|---|
| MMEMA | Kilimo cha wakulima wadogo kifamilia<br>Hifadhi ya mazingira |
| Mshikamano | Kilimo cha wakulima wadogo kifamilia<br>Mradi wa ufyatuaji matofali ya kuchoma |
| Upendo | Kilimo cha wakulima wadogo kifamilia<br>Ufugaji nyuki, kilimo cha bustani |
| Tupendane VICOBA | Kuweka na kukopa (SACCOs), kupanda miti |
| Juhudi | Ufugaji wa kuku (Kuku chotara) |
| Chekanao | Ufugaji wa kuku (Kuku chotara ) |

**5.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA KATIKA UTEKELEZAJI**

Wanajamii wenyewe kwa njia ya kujitolea na kujisaidia wenyewe, mkakati ambao umekuwa ukienezwa kwa bidii na Wawezeshaji ngazi ya Kata wameweza kujenga shule za awali katika vitongoji vyote vitano na kila shule moja ya awali iligharimu siyo chini ya Tsh 2,500,000. Kwa hiyo, jumla ya Tsh 12,500,000 zimechangwa na wananchi, kati ya hizo thamani ya vitu (nguvu kazi, vifaa vya ujenzi mfano mchanga na mawe) vilikuwa na thamani ya Tshs 800,000. Kwa upande wake, Halmashauri ya Morogoro Vijijini ilitoa usaidizi wa Tsh 22,500,000/- kwa vitongoji hivyo vitano. Fedha hii ilitokana na mfuko wa ruzuku kujenga uwezo wa Halmashauri yaani (CDG Fund) iliyokuwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha wa 2013/2014).

Zahanati ya kijiji iligharimu Tsh 42,858,500/-, kati ya hizo mchango wa jamii (fedha taslim, nguvu-kazi na vifaa vya ujenzi) vilikuwa na thamani ya Tshs. 20,000,000/-. Mchango wa Halmashauri ilkuwa Tsh 22,858,500 kupitia ruzuku ya kujenga uwezo yaani CDG. Hadi wakati kuhakiki kisa mkasa hiki, akunti ya kijiji iliyoko Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini - CRDB ilikuwa na akiba kiasi cha Tsh 7,000,000.

**6.0 MAFANIKIO**

Baada ya kupitia mchakato wa O&OD iliyoboreshwa, wanajamii wa Maseyu wana mafanikio mengi ya kuelezea. Mafanikio yako katika makundi mawili, (i) yanaoonekana na yale (ii) yasioyonekana kwa macho. Mafanikio yanayonekana ni pamoja na ujenzi wa miundombinu, mfano ujenzi wa shule tano za awali au chekechea (5) na nyumba moja ya mwalimu kila kitongoji, jumla nyumba 5. Mengine ni ujenzi wa zahanati ya kijiji yenye vyumba 13, mfumo mzuri wa upashanaji habari na kueneza mambo mapya kupitia mbao za matangazo na vipaza sauti hadi kwenye ngazi ya kitongoji.

Mafanikio mengine ni kuwepo kwa akaunti ya kijiji iliyo hai kaunzia mwezi Februari 2012, uenezwaji wa mbegu za kisasa za mhogo kutoka kijiji cha Homboza-Kisarawe zinazojulikana kama *kiroba* na *rasta.* Mbegu hizi ni za muda mfupi, zinahimili ukame, na zinazaa sana. Kijiji kimeanzisha Baraza la Usuluhishi na kutatua Migogoro, Kimeunda kamati ya kuthibiti kuenea kwa UKIMWI na kimewezesha uchaguzi wa Bodi ya shule ya Msingi ya Maseyu kwa ajili ya utawala bora.

Kutokana na mafanikio yaliyo hapo juu, pameanzishwa vikundi vya uzalishaji-mali na jamii yenyewe bila ushawishi toka nje, kwa vile sasa hali ya uaminifu kwenye ngazi ya uongozi imerejea kijijini. Vikundi vimetengeneza katiba zao na zile zilizokuwepo zimeimarishwa (vikundi vitano kati ya 10 vina katiba zao) . wigo wa shughuli za vikundi umepanuka kama inavyooeneka katika picha hapa chini.




***Mizinga ya nyuki wa asali ni mingi sasa kijijini  Maseyu***




***Kikundi cha wanawake kawa ajili ya ufugaji mbuzi wa maziwa ,                Kilimo cha ufuta***

**Mfumo wa ulinzi na usalama umeboreshwa.** Kabla ya ujio wa mradi wa mradi wa O&OD iliyoboreshwa, eneo lote la kijiji cha Maseyu lilikuwa na sifa mbaya kabisa likijulikana kama eneo hatari katika barabara kuu ya Morogoro-Chalinze. Eneo hili lilikuwa na ajali nyingi za makusudi, mfano majambazi kuteka magari, kuweka vitu vyenye ncha kali barabarini ili magari yapate ajali na kisha kuwavamia wahanga wa ajali hizo na kuwaibia mali zao. Kwa sasa hali ya usalama imerejea kijijni na kuna mfumo mzuri wa kumtambua kila mgeni anayeingia katika kila kaya ya kijiji hicho.

Kuna mfumo wa doria kwa masaa 24 kuzunguka eneo la kijiji chote. Ikitokea kwa bahati mbaya gari ikapata ajali au matatizo ya kiufundi ndani ya eneo la kijiji, basi serikali ya kijiji hutoa walinzi wa kulinda wahanga wa ajali na mali zao. Wenye magari watalipa Tshs 5,000 kwa kila gari bila kujali itakaa muda gani wakati ikingoja kuondolewa. Hata hivyo, wenye magari wana hiyari ya kuwapa motisha walinzi kwa kadri watakayoona wao bila kushurutishwa.

Miaka mitatu nyuma ilkuwa vigumu sana kwa wanawake kwenda shambani wenyewe kwa hofu ya kubakwa. Matukio ya ubakaji yamepungua kutoka 5, miaka mitatu iliyopita na kufika sifuri mwaka 2013, kwa sasa hali ni salama kabisa. Hii inatokana na utekelezaji dhabiti wa sheria ndogo za kijiji dhidi ya uhalifu ndani ya kijiji cha Maseyu.

**Matokeo yasiyonekana**

Mahusiano baina ya vikundi vya kijamii na kiuchumi vyenyewe kwa vyenyewe na dhidi ya serikali ya kijiji yameboreshwa. Kwa sasa kuna ratiba ya vikao katika ngazi ya kitongoji na kijiji kwa mwaka mzima na wananchi wanazingatia ratiba hizo. Kuhusu sheria na kanuni za shughuli za miradi maisha ya kila siku hapo kijijini zinatekelezwa kwa nguvu zote. Kuna mwamko wa wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa hiyari kulingana na mpango kazi wao, na pia wanahamasishana wao kwao ili kutekeleza miradi yao.

Ule mfumo wa maamuzi ya pamoja kuhusu masuala ya maendeleo baina ya viongozi umeimarika. Viongozi wa kijiji wamebadilika na kuwa wawazi zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya mradi na hususan ni kwenye ripoti ya mapato ya matumizi ya fedha za kijiji na masuala mengine yenye maslahi kwa jamii nzima. Ushiriki wa jamii katika miradi ya maendleo na mahudhurio katika vikao vya kijiji na kitongoji yamoeongezeka. Hii inatokana na kutekeleza kwa dhati sheria ndogo inatoa adhabu ya faini ya Tsh 5,000 kwa kutoshiriki shughuli au vikao. Matokeo yake ni kwamba mahudhurio yameongezeka kutoka wastani wa 47% mwaka 2009 hadi wastani wa 83% mwaka 2012.

Viongozi wa kijiji na wanakijiji wamepata fursa ya kufungua macho na kupokea mawazo mapya kutokana na wingi wa wageni wa aina mbalimbali waliokuja kwenye ziara za mafunzo hapa kijijini. Wageni hao ni pamoja na watendaji wa serikali na wanasiasa toka Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilileta Madiwani kuja kujifunza kuhusu utawala bora. Pia kijiji kilipokea mgeni mmoja mfanyakazi wa kujitolea toka shirika la ushirikiano wa kimataifa (JICA toka Japan) aliyekuja kujifunza kwa mtindo wa mafunzo kazini. Kutokana na mawazo mbadala, hali-tabia ya wanakijiji imebadilika sana na kuachana na ile tabia ya kuomba posho kutoka kwa wawezeshaji, watafiti na wadau wa maendeleo na badala yake wamekuwa makini kudai na kupokea stadi na maarifa wakati wa vikao vya kujengeana uwezo wa kiutendaji na uongozi.

Uwezo wa jamii umeimarika kupitia mchakato wa O&OD iliyoboreshwa. Jamii iliweza kuwaondoa madarakani viongozi wa kijiji wasiowajibika na kuchagua timu ya viongozi mbadala wenye uwezo mkubwa zaidi wa uongozi. Haya yalikuwa ni matokeo na uzoefu kutokana na ziara ya mafunzo ambayo baadhi ya wanakijiji waliifanya kule kijiji cha Homboza-Kisarawe. Waliporudi tu walifanya mageuzi, na kijiji cha jirani nao walivyoona kilichotokea Maseyu nao waliiga nakuleta mageuzi kwenye kijiji chao. Utayari wa wazazi kuandikisha watoto na idadi ya watoto walioandkishwa darasa la kwanza siyo tatizo tena; wazazi wenyewe hupeleka na kuwaandikisha watoto wao kwa hiyari yao wenyewe tofauti na ilivyokuwa miaka mitatu ya nyuma ambapo ililazimu waalimu kutembelea kila kitongoji kuandikisha watoto kwa nguvu. Mahudhurio shuleni yameongezeka toka 75% hadi 85%. Mdondoko wa wanafunzi wanaoshindwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali umepungua toka 7% miaka mitatu nyuma hadi 0.5% mwaka 2013.

Jamii imeshatambua umuhimu wa kutekeleza mipango yao ya maendeleo wenyewe bila kutegemea misaada toka Halmashauri. Pia jamii imeshatambua umuhimu wa kujitegemea na kujitolea nguvu zao wenyewe. Matokea ya yale yanayotokea Maseyu ni kwamba vijiji vya jirani sasa vimeanza kuiga matokeo chanya yaliyopatikana Maseyu. Mfano kijiji cha Kinonko nao wameiga ujenzi wa madara ya shule ya chekechea, ujenzi wa zahanati na madarasa matatu kwenye Shule ya Msingi ya Gwata.




*Ongezeko la ushiriki wa jamii katika mipango shirikishi jamii*


Ujenzi wa zahanati kijiji cha Kinonko


Ujenzi wa madarasa ya chekechea kijiji cha Kinonko

## 7.0 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA UENDELVU

Kukosekana kwa chanzo cha maji ya uhakika kwa mwaka mzima ni changamoto kubwa ya kijiji hiki. Pia viongozi wa kijiji wanapwaya sana kuhusu maarifa na stadi rahisi za mahesabu ya fedha na kutunza vitabu vya mahesabu. Serikali ya kijiji ina uwezo mdogo wa kifedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya vipaombele vya jamii. Kuna uhaba wa vyombo vya usafiri kwa viongozi na watendaji wa kijiji ili kuweza kuzungukia vitongoji vyote. jamii na vikundi haina elimu ya ujasiriamali na baadhi ya vikundi vya kijamii na kiuchumi havijaandikishwa.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, Halmashauri imetoa msaada wa kiufundi kwa baadhi ya miradi. Serikali ya kijiji iliiomba Halmashauri iendeshe mafunzo kuhusu kutunza mahesabu na kumbukumbu za fedha kwa viongozi wa kijiji. Serikali ya kijiji imefanya jitihada za kuwasiliana na wadau wengie wa maendeleo kuona uwezekano wa usaidizi kwa baadhi ya changamoto. Kuna utekelezwaji wa dhati wa sheria ndogo kwa ajili ya uendelevu.

Kuna juhudi za kupanua wigo wa mradi na kufikia vijiji vingine ndani ya Halmashauri ili kuueneza mchakato wa O&OD iliyoboreshwa. Hili litaondoa tatizo la jamii kukosa fursa ya kujifunza kwa jamii zingine kwa kupitia ziara za mafunzo na kubadilishana uzoefu na jamii zingine.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

Mafanikio ya Maseyu yalitokana na: Mfumo imara wa mafunzo kwa ajili ya timu za wawezeshaji ngazi ya kata (WFs) na wawezeshaji ngazi ya wilaya (DFs). Timu ya WFs ilikuwa na mchanganyiko wa taaluma hivyo kuwezesha na kujibu hoja mbalimbali za jamii kulingana na taaluma zao. Timu ya WFs ilikuwa karibu na jamii wakati wote kwenye shughuli mbalimbali jambo lililoongeza kuaminiana na kukubalika kwao. Kule kuaminika na kukubalika vilikuwa vichocheo vikubwa kwa ajili ya kuleta mabadiliko tarajiwa katika jamii.

Uwezeshaji wa jamii haukua tukio la mara moja, bali ilikuwa shughuli endelevu ikitekelezwa na timu za wawezeshaji za Kata na Wilaya kwa miaka mitatu. Ushirikiano wa WFs, DTF, na Wagani wengine walioko kwenye kata katika shughuli za O&OD ilikuwa wa muhimu sana.

Jamii kujifunza kutoka wanajamii wenzao kupitia ziara za mafunzo katika vijiji vya Homboza na Gwata kwenye Halmashauri ya Kisarawe ilikuwa jambo la msingi sana “maana kuona ni kuamini”. Kuna mafundi wanakijiji watatu walichaguliwa kuhudhuria mafunzo ya teknolojia rahisi ya ujenzi wa miundombinu kwa mikono badala ya mashine yaliyoendeshwa na Chuo cha ATI kule kijiji cha Matema-Kilombero kwa ufadhili wa JICA. Hawa mafundi baada ya kurudi walisaidia sana kuchochea ujenzi wa miundo mbinu hasa barabara za vijijii kuunganisha vitongoji na barabara kuu.

Mafunzo ya utawala bora yaliyoendeshwa na timu ya O&OD mwezi Mei 2011 yalisaidia sana kufufua uongozi bora na kujenga uwezo wa viongozi wa jamii. Kupitia mafunzo haya halitabia ya watu binafsi na jamii kwa ujumla imebadilika. Timu ya menejimenti ya Halmashauiri ya Wilaya ya Morogoro (CMT) ilitembelea kijiji cha Maseyu, ziara hii iliwasaidia wao kutambua jitihada za jamii, kuwatia moyo na kuwahamasisha wanajamii katika huhudi zao za kujiletea maendeleo. Mwisho ni misaada ya fedha na kiufundi toka kwa mshirika wa maendeleo (JICA), kwa sababu pamoja na mambo yote, bado uhakika wa fedha ni muhimu katika kufanya shughuli za jamii kuwa endelevu. Suala la maandalizi ya kina ya jamii na usaidizi na ushauri toka Halmashauri vilikuwa vya muhimu sana katika kuwezesha juhudi za wananchi.

# Sura ya Tatu: Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato

Ugatuaji wa Masuala ya Fedha humaanisha mamlaka ya kukusanya kodi na kutumia yanahamishwa toka ofisi za juu (Serikali kuu) kwenda ofisi za chini (Serikali za mitaa) kwa lengo la kutoa huduma za umma sahihi ili kuboresha ustawi wa wananchi. Wapo wanaoamini kuwa kuna uwiano unaotakiwa kati ya fedha za Serikali Kuu na fedha za Serikali za Mitaa, au kuwa Serikali za Mitaa zina nguvu ya kufanya maamuzi kwa ajili ya kuboresha masuala ya fedha. Ingawa kuna maoni mbalimbali kuhusu ugatuaji wa masuala ya fedha, kwa ujumla kiasi cha maamuzi kuhusu fedha na mamlaka iliyonayo Halmashauri, huongezeka kadri ugatuaji wa masuala fedha unavyoongezeka katika ngazi za chini. Mambo ya lazima katika ugatuaji wa masuala ya fedha ni Baraza la Madiwani, maafisa wakuu walioteliwa katika eneo husika, uwezo thabiti wa mapato ya Halmashauri, jukumu thabiti la matumizi ya Halmashauri, uhuru wa bajeti, uzingatiaji wa bajeti na uwazi. Mazingira yanayostahili ni pamoja na uhuru wa kutokuingiliwa na udhibiti wa Serikali Kuu, haki ya matumizi, fedha kutolewa bila masharti na uwezo kukopa.

Andiko la maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania (1998) linaonyesha kuwa ugatuaji wa masuala ya fedha maana yake ni kuzifanya Halmashauri ziwe na vyanzo vyao vya uhakika vya mapato, kuanzisha uhamishaji fanisi wa fedha toka Serikali Kuu, kuwepo kwa upatikanaji fanisi wa fedha za kutolea huduma zilizokasimishwa, kuboresha ongezeko la mapato, kuhakikisha uwepo wa uwazi na usawa katika mgawanyo wa fedha na kuhakikisha usawa katika utoaji wa huduma. Ugatuaji wa masuala ya fedha kwa Tanzania kimsingi unajumuisha ukweli ufuatao;

(i) Halmashauri hazitakiwi kukasimishwa wajibu wa majukumu ambayo hayatengewi fedha.

(ii) Mfumo wa ruzuku unatakiwa kuruhusu sera za kitaifa kutekelezwa kupitia Halmshauri ambazo zingelipiwa kupitia ruzuku zenye masharti na zinazozingatia viwango vya chini vya kitaifa.

(iii) Mfumo wa ruzuku unatakiwa kuzihamasisha Halmashauri kuamua vipaumbele vyao kwa kuanzisha ruzuku ya kawaida na ya maendeleo bila masharti.

(iv) Ruzuku ambazo hazina masharti lazima zitolewe kwa mtindo wa usawa ili kusaidia Halmashauri ambazo zina vyanzo dhaifu vya mapato.

(v) Ukokotoaji wa ruzuku lazima ufanyike kwa kufuata fomula yenye viwango vya kutegemewa, vya haki na visivyo na upendeleo

(vi) Ruzuku toka bajeti za Wizara za sekta zinatakiwa kuachwa kadri iwezekanavyo.

Uongezaji wa Mapato ya Ndani humaanisha matumizi ya uhuru uliotolewa na Serikali Kuu kwa Halmashauri kukusanya mapato na kutumia kulingana na vipaumbele vyao. Uongezaji wa Mapato hujumuisha upanuaji wa wigo wa mapato, uhamasishaji shughuli za kiuchumi zinazoongeza vyanzo vya kodi na kutunga sheria ndogo za kuwezesha ukusanyaji na utumiaji wa mapato.

Katika sura hii Kesi mbili zimewasilishwa. Kesi ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani inahusu mfumo wa ukusanyaji mapato wa Digitali unaotumia kompyuta kuainisha Majengo, kupiga picha na kufanya tathmini ya haki na sawa ya thamani za majengo. Kesi ya Halmashauri ya

Jiji la Mbeya inahusu jitihada za kijasiriamali za kuongeza mapato kupitia uwekezaji wa ndani. Kesi hii inaonyesha ujasiri na umakini unaotakiwa na Halmashauri kukopa fedha toka taasisi za fedha na kuziwekeza kwenye miradi inayolipa haraka. Ikizingatiwa kuwa mgawo wa fedha toka serikali kuu unaendelea kupungua na una masharti magumu, Halmashauri zinalazimika kuchangamka kutafuta mapato kutoka vyanzo vingine kama miradi ya kuongeza mapato. Uchambuzi wa kesi kwenye sura hii unaonyesha kuwa;

(i) Kodi ya majengo ni chanzo muhimu kwenye vyanzo vya ndani vya Halmashauri nyingi ambacho kinatumiwa chini ya uwezo wake. Sababu za kutumika chini ya uhalisia inajumuisha kutokutambuliwa kwa majengo, kutosajiliwa majengo, utunzaji hovyo wa takwimu, tathmini za thamani zisizo na haki, na kumbukumbu za thamani zilizopitwa na wakati. Ili kukabiliana na changamoto hizi mfumo huu wa Digitali unaweza kuwa msaada siyo tu katika kuongeza mapato bali pia kwa kupata takwimu muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi mengine.

(ii) Halmshauri ni taasisi zinazojiendesha zenyewe kisheria. Kwa mantiki hii na kwa kuzingatia upungufu wa raslimali toka Serikali Kuu, Halmashauri zinatakiwa kujiingiza kwenye uwekezaji mkubwa na shughuli za kijasiriamali zenye mwelekeo wa kuzalisha mapato ya kutosha. Halmashauri zinatakiwa kuwa na maamuzi na ubunifu wa kuingia kwenye mambo ya ardhi, uchimbaji madini, kuendesha shughuli za mafunzo na utalii. Ili kuweza kufanya hivi zinahitaji kuchukua hatua na kudiriki kukopa kutoka kwenye taasisi za fedha zilizopo kama Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), benki ya uwekezaji, mfuko wa kijiji cha millennia, mfuko wa majiji wa millennia, Mpango wa mazingira wa Umoja wa Mataifa (UN Habitat) na nyingine nyingi.

(iii) Uendeshaji wa uwekezaji wa umma unahitaji umakini wa menejimenti, hivyo Halmashauri lazima zishirikiane na sekta binafsi kupitia mfumo wa ushirikiano kati ya taasisi za umma na binafsi yaani PPP.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA

## JITIHADA YA UBORESHAJI WA MAPATO



*Uzoefu wa Halmashauriya Wilaya ya Bukoba*

**1.0 UTANGULIZI**


Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba ni moja kati ya halmashauri nane zinazounda mkoa wa Kagera. Halmashauri ina eneo la mraba Hekta 2, 844. Kijiografia halmashauri ipo kati ya $30^{o}45$ na $32^{0}00$ Mashariki, na $1^{0}00$ hadi $3^{0}00$ kusini mwa Ikweta. Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba hupakana na Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi kwa upande wa kaskazini, Ziwa Victoria kwa upande wa mashariki, Manispaa ya Bukoba kwa upande wa Kaskazini Mashariki, Halmashauri ya wilaya ya Bukoba kwa upande wa kusini na Halmashauri ya wilaya ya Karagwe kwa upande wa Magharibi. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa nne ambazo ni BUGABO, KYAMTWARA, KATERERO, na RUBALE. Halmashauri ina kata 29, vijiji 92, vitongoji 508, kaya 54,803 zenye wastani wa watu watano. Kuna vyama hai vya siasa vine (4) vinavyounda Baraza la Madiwani ambavyo ni; CCM, CUF, CHADEMA na TLP.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, halmashauri ina watu 289,697 ambapo 148,555 ni wanawake na 141,142 ni wanaume. Ukuaji wa kiuchumi wa halmashauri ni 1.8% kwa mwaka, pato la mwananchi lilikuwa ni shilingi 186,780 mwaka 2005. Lakini mpaka kufikia Juni 2013 pato la mwananchi kwa mwaka limepanda na kufikia wastani wa shilingi 450,000. Kwa sasa halmashauri ipo katika mchakato wa kutathmini pato halisi la mwananchi kwa mwaka, kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali wa Takwimu (NBS) na ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Halmashauri imejaliwa kuwa na rasilimali mbalimbali za ardhi. Ardhi inayofaa kwa kilimo ina eneo lipatalo 1,045 $km^2$ (37%), ardhi ya malisho $km^2$ 620 (22%), msitu na miamba $km^2$ 879 (30.5%) na maji $km^2$ 300 (10.5%). Hali ya hewa ya Halmashauri ni ya Tropiki ya Savanna yenye misimu miwili ya mvua, yaani mvua ndefu za masika zitokanazo na mgandamizo wa kitropiki (ITCZ) hasa kipindi cha miezi ya Machi hadi Juni. Mvua fupi za vuli ambazo husababishwa na uhamaji wa mgandamizo wa kitropiki kuelekea kusini, hunyesha kipindi cha Septemba na Desemba. Hali ya joto hutegemea urefu kutoka usawa wa bahari. Halmashauri ipo kwenye ukanda wa 700m hadi 1200m juu ya usawa wa bahari. Mabadiliko katika viwango vya joto kwa mwezi ni kati ya $22^{0}C – 26^{0}C$. Msimu wa joto hudumu kuanzia Oktoba hadi Machi na huambatana na unyevu wa hewa wa juu unaopelekea joto kufikia $35^{0}C$. Msimu wa baridi huanza mwezi Juni mpaka Septemba na huwa na joto la wastani kwa mwezi, kati ya $18^{0}C$ hadi $20^{0}C$.

Halmashauri imegawanyika katika kanda kuu tatu za Ikolojia na Kilimo. Ukanda mvua nyingi upo kati ya m900 hadi m166 juu ya usawa wa bahari. Ukanda huu hupata mvua kati ya mm1400 hadi mm2000 kwa mwaka. Sehemu kubwa ya mazao ya biashara na chakula huzalishwa katika ukanda huu. Ukanda huu una mazingira mazuri ya ufugaji. Ukanda wa kati wa mvua upo kati ya mm 900 hadi mm1666 juu ya usawa wa bahari. Ukanda huu hupata mvua kati ya mm700 hadi mm1250 kwa mwaka. Ukanda huu pia unafaa kwa mazao ya biashara na chakula na unamazingira mazuri ya ufugaji. Ukanda wa chini wenye mvua kidogo upo chini ya mm900 kutoka usawa wa bahari na kupata mvua mm600 hadi mm1000 kwa mwaka.

Shughuli kuu ya kiuchumi ni kilimo na mazao makuu ni Mahindi, Mihogo, Maharagwe na Ndizi. Ufugaji mdogo unayofanyika katika eneo hili husaidiwa na mfumo wa ufugaji wa kiasili wa ng'ombe aina ya Zebu, Kondoo, Mbuzi na wanyama wengine wadogo.




*Mazao na bidhaa ambazo ndio chanzo cha mapato ya Halmashauri*

Kama ilivyotajwa hapo awali asilimia 85 ya wakazi hutegemea kilimo kwa kuishi. Mazao muhimu yanayozalishwa ni Mahindi, Maharagwe, Ndizi, Kahawa na Mihogo.

**Jedwali 1: Uzalishaji Kilimo Mwaka 2013/2014**

| ZAO | ENEO LILILOLIMWA (Ha) | UZALISHAJI TARAJIWA (tani) |
|---|---|---|
| **Mahindi** | 16461 | 18553 |
| **Maharage** | 24815 | 17498 |
| **Viazi Mviringo** | 10618 | 36781 |
| **Ndizi** | 29604 | 100891 |
| **Mihogo** | 10379 | 38791 |
| **Kahawa** | 9783 | 6577 |

**Jedwali 2: Idadi ya Wanyama Mwaka 2013/2014**

| AINA | JUMLA |
|---|---|
| **Ng'ombe wa Nyama** | 29,689 |
| **Ng'ombe wa maziwa** | 2,518 |
| **Mbuzi** | 5,412 |
| **Mbuzi wa Maziwa** | 681 |
| **Kondooo** | 5,412 |
| **Nguruwe** | 1,345 |
| **Kuku** | 736 |
| **Mbwa** | 4,795 |

**<u>Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba</u>**

Halmashauri ina mtandao wa Barabara unaofikia km 839. Barabara zote zinapitiaka mwaka mzima. Barabara zimegawanyika katika makundi manne, yani barabara za changarawe (TANROAD) km236, barabara za lami (TANROAD) km38, barabara za changarawe za halmashauri km 224, barabara za udongo za halmashauri km263, na barabara nyinginezo km 78. Jumla ya urefu wa barabara ni km839.

Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba ina meli moja ambayo husafiri kati ya Mwanza na Bukoba mara tatu kwa wiki. Meli hii ni moja ya usafiri unaopendelewa zaidi na wakazi wa kawaida wa Halmashauri kwa ajili ya urahisi wa kwenda mikoa ya mbali nchini hasa Mwanza na Dar-es-Salaam. Bukoba kuna uwanja wa ndege unaoruhusu ndege ndogo kutua na kufanya safari kati ya Mwanza na Dar-es-Salaam kila siku. Baadhi ya maeneo ya Halmashauri yana huduma za simu za mezani hasa katika makao makuu ya Tarafa. Kampuni za simu za mkononi zilizopo ni pamoja na VODACOM, TIGO, ZANTEL na AIRTEL ambazo hurahisisha sana mawasiliano. Halmashauri ina skimu (5) za maji za mvutano wa ardhi (gravity), visima vifupi 161, kisima kimoja kirefu, mabwawa manne na chemchem 137 ambazo kwa pamoja vinahudumia wastani wa wakazi 173,818 sawa na asilimia 60 ya wakazi wote wa halmashauri. Lengo la halmashauri ni kufikia mwaka 2015,

vijiji vyote 92 viwe na maji safi na salama ndani ya mita 400 kutoka kila kaya kama inavyoelezwa kwenye sera ya maji ya mwaka 2002. Takribani asilimia 15 ya kaya zote zimeunganishwa na umeme. Kwa sasa kuna mradi unaoendelea wa kusambaza umeme Bukoba Vijijini (REA) ambapo Halmashauri inategemea mradi utakapokamilika zaidi ya asilimia 45 ya eneo la halmashauri litakuwa na umeme.

**2.0 TATIZO**

Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, kama ilivyo kwa halmashauri nyingi Tanzania ina wigo mwembamba sana wa kodi ambao hupelekea makusanyo duni ya mapato. Wigo wa kodi hutegemea zaidi mazao ya kilomo ambayo nayo hutegemea idadi ya wakulima wadogo wenye motisha ya kufanya shughuli za kilimo, kiasi cha mvua halisi iliyonyesha katika msimu husika wa uzalishaji, bei ya mazao ya kilimo na soko la mazao ya kilimo kwa ujumla. Pia uwezo wa halmashauri kukusanya Kodi, Ushuru na Ada mbalimbali ulikuwa mdogo sana kutokana na motisha hafifu kwa upande wa wakusanya mapato, upungufu wa vifaa na huduma ya usafiri isiyotosheleza. Mitizamo ya walipa kodi yani wananchi haikuwa sahihi kuhusu ukusanyaji wa kodi. Pia hapakuwa na mawasiliano bora kuhusu kodi kati ya Halmashauri na walipa kodi. Haya yote yalipelekea ukusanyaji duni wa mapato kutoka vyanzo vya ndani na hivyo Halmashauri kuwa na uwezo mdogo sana wa kifedha katika kukamilisha matumizi katika shughuli za kawaida na hata zile za maendeleo. (Tazama kiambatanisho 1).

**3.0 MALENGO YA JITIHADA**

Hali hii ilipelekea halmashauri kujiingiza katika mkakati wa kuboresha mapato. Lengo kubwa la mkakati huu lilikuwa kuongeza uwezo wa Halmashauri kifedha katika kuendesha shughuli za kawaida na za Maendeleo kwa kupanua wigo wa kodi, kuwapa motisha wakusanya kodi na kuboresha vifaa vya kukusanyia kodi. La muhimu zaidi hapa, Halmashauri ililenga katika kuongeza vyanzo vipya vya mapato na kuhakikisha kuwa kodi zote katika vyanzo hivi zinakusanywa. Lengo la mwisho la mkakati huu wa kuboresha mapato lilikuwa ni kuunda na kuimarisha ufuatiliaji wa karibu sana wa ukusanyaji wa kodi katika vyanzo vilivyopo. Lengo la jumla lilikuwa kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka Shs 354 milioni mwaka 2010/2011 hadi Shs 1,372 milioni mwaka 2013/2014.

**4.0 MIKAKATI NA SHUGHULI**

Ili kuweza kufikia malengo yaliyotajwa hapo juu Halmashauri iliainisha na kupitisha mikakati na shughuli ambazo zimeelezewa hapo chini.

**(i) Uhamasishaji wa Jamii kuhusu kulipa Kodi**

- Halmashauri iliunda na kuendesha mikutano ya uhamasishaji jamii katika ngazi zote (Vijiji na Kata). Hili lilifanywa na kikosi kazi imara cha ukusanyaji wa mapato chenye wajumbe watano (5), yaani Mweka Hazina, Mwanasheria, Afisa Biashara, Mhasibu wa Mapato na Afisa Uvuvi. Timu nzima ya menejimenti ya Halmashauri ilishiriki kikamilifu kupitia kuweka mikakati na kupokea taarifa za uhamasishaji wa jamii kuhusu kulipa kodi. Zoezi hili lilifanywa kwa miezi mitano (Julai – Novemba, 2011) katika mwaka wa fedha 2011/2012.
- Halmashauri iliweka mabango katika vituo vyote vya kukusanyia mapato, masoko na katika ofisi za Vijiji na Kata yaliyoonyesha bidhaa zinazotozwa kodi na viwango vya kulipa. Baadhi ya masoko na vituo vya kukusanyia mapato ambapo mabango yaliwekwa ni pamoja na Soko la Izimbya, Rubaler, Ruhoma, Iberwa, Nyakibimbili, Katoro, Kyamulaire, Makonge, Nongo, na Kihumilo, bidhaa na mazao ya Mali Asili katika vituo vya ukaguzi vya Kyema, Kalyankolo, Nongo na Kihumilo, matoleo ya samaki ya Rushara, Igabilo, Marehe, Kyonge, Bilolo na Karwazi na katika minada yot eya

wanyama mabango yaliwekwa yanayoonesha taarifa za bidhaa za kodi na viwango vinavyotakiwa kulipwa.




***Siku ya soko la Rukoma - Alhamisi***

**(ii) Mapitio ya Sera, Sheria Ndogo na Viwango vya Kodi**

- Halmashauri ilifanya mapitio ya sera yake ya kodi kwa kuanzisha mfumo mpya wa ufuatiliaji na usimamizi katika ukusanyaji wa kodi kwa kutumia kikosi kazi cha wataalam mchanganyiko, kufanya ufuatiliaji wa moja kwa moja katika masoko na vituo vya kukusanyia mapato na kutoa fedha za kutosha kulipia usafiri kwa ajii ya shughuli za ukusanyaji wa kodi.
- Uamuzi wa Halmashauri kuongeza ukusanyaji wa mapato usingeweza bila mapitio Sera na Sheria Ndogo. Sheria ndogo zote zilizokuwa zimepitwa na wakati kuhusu vyanzo vya kodi, aina mbalimbali za ushuru na ada, adhabu na faini mbalimbali zilifanyiwa mapitio na kuanzisha viwango vipya vya kodi vyenye ushindani na ambavyo vinaonyesha hali halisi. Kwa mfano ushuru wa Samaki ulibadilishwa kutoka Shs 10/= hadi Shs 250/= kwa kurekebisha sheria ndogo ya mwaka 2011.

**(iii) Kuanzisha Ukusanyaji Mapato wa Gharama Nafuu Kupitia Timu ya Menejimenti**

- Halmashauri ilijiridhisha kuhusu viwango vya juu kabisa vya mapato kutokana na kila chanzo kwa kipindi cha miezi mitano (5), yaani kuanzia Julai hadi Novemba 2011 katika mwaka wa fedha 2010/2011. Wakati wa zoezi hili Ukusanyaji wa mapato ulifanywa na Timu ya menejiment na kikosi kazi cha mapato. Lengo kuu likiwa kujiridhisha kuhusu kiasi cha juu cha makusanyo kwa mwezi katika kila chanzo.
- Baada ya kutambua kiasi cha juu cha kila chanzo cha mapato, ukusanyaji wa mapato ulibinafsishwa kwa wazabuni kwa kuzingatia viwango vya juu vya kila chanzo.
- Wazabuni wote walioshinda walitakiwa kuilipa halmashauri fedha sawa na makusanyo ya miezi miwili siku ya kutia saini mkatba kama dhamana kwa halmashauri.
- Pia ilielezwa waziwazi katika mikataba kuwa wazabuni watakaochelewa kuilipa halmashauri makusanyo ya mwezi (yaani baada ya siku ya tano (5) ya mwezi unaofuata), watapata adhabu ya kuongeza 5% ya fedha zinazotakiwa kulipwa halmashauri kupitia Benki.

**(iv) Kuanzisha Vyanzo Vipya vya Mapato**

- Halmashauri ilianzisha vyanzo vipya vya mapato. Katika vifaa vya ujenzi ushuru ulianzishwa katika matofali, kokoto, mawe na moramu. Kila bidhaa ilipangiwa ushuru mahsusi kulingana na thamani, mahali na kiasi.





*Mchanga wa kujengea Katika eneo la Kyetema*




*Kokoto za kujengea katika eneo la Katoma*

- Mpango wa ujenzi wa stendi ya mabasi katika eneo la Kemondo utakaoanza kwenye mwaka wa fedha 2013/2014. Stendi hii itachangia katika vyanzo vya mapato kupitia ada za mabasi, ushuru wa biashara ndogo ndogo, ada za viingilio vya wageni, gharama za kuegesha magari na vyombo vingine vya usafiri na fedha za pango la vibanda vya biashara.
- Kutungwa kwa sheria ndogo ya minara ya mawasiliano. Kampuni za simu za mezani na mikononi hutumia minara kupokea na kurusha mtandao. Minara hii imetapakaa katika eneo lote la Halmashauri. Kampuni hizi ni mojawapo ya makapuni ambayo yanafanya vizuri sana kibiashara hapa Tanzania. Halmashauri inaona kuwa, ingawa kodi baada ya faida ya makampuni haya hukusanywa na TRA, kampuni hizi zinatakiwa kulipa ushuru wa minara iliyopo kwenye eneo la halmashauri. Halmashauri nyingine hapa Tanzania zimeshafaidika tayari kutokana na ushuru huu.
- Ujenzi wa Mnada wa wanyama katika kijiji cha Nshesha mwaka 2010. Mnada huu umechochea biashara mbalimbali zinazoendana na shughuli za mnadani. Kuna biashara za mazao ya shambani, bidhaa za viwandani, ubadilishanaji wa huduma na huduma za burudani. Haya yote sasa yametumiwa na halmashauri na yamechangia katika kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani. Mpaka itakapofika mwaka 2015, jitihada hizi zitapelekea mabadiliko makubwa katika mapato ya ndani ya halmashauri ya wilaya ya Bukoba.





***Mnada wa Wanyama Uliojengwa Kijiji cha Nsheshe***



*Mnada ukiendelea katika Kijiji cha Nsheshe*

**(v) Kuundwa kwa Kikosi Kazi cha Mapato**

- Kuundwa kwa Kikosi Kazi cha mapato. Mbinu Bora ziliiarifu Halmashauri kuwa bila ubunifu, ufanyaji kazi kwa mfumo wa Timu na Menejiment thabiti, jitihada za kuboresha ukusanyaji wa mapato zinakuwa changamoto na ngumu kuzitimiza. Kutimiza lengo hili, Kikosi Kazi cha mapato kilianzishwa ili kiwe mvumbuzi wa kupanua wigo wa kodi, na mshauri wa menejimenti kuhusu upatikanaji wa mapato na maendeleo ya kifedha. Muundo wake umejumuisha Mweka Hazina, Mwanasheria, Afisa biashara, Mhasibu wa Mapato na Afisa Uvuvi. Jukumu kubwa la Kikosi Kazi hiki ni kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyote na kuishauri Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kuhusu hatua za kuchukuliwa ili kuongeza mapato na kudhibiti masuala yote yanayoweza kupunguza makusanyo. Wajumbe wa Kikosi Kazi hiki hukutana mara mbili kwa wiki kupitia utekelezaji wa mipango ya makusanyo ya mapato ikilinganishwa na ukusanyaji halisi.

## 5.0 RASLIMALI ZILIZOTUMIKA KATIKA JITIHADA HII

Halmashauri ya wilaya ya Bukoba ilijikita katika kuboresha ukusanyaji wa mapato ikijua wazi kuwa bila kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya jitihada hii, lengo la kupanua wigo wa kodi na kuongeza mapato ya ndani lisingefikiwa. Halmashauri hii hupatwa na upungufu mkubwa wa fedha hivyo uamuzi ulifikiwa kuwa Kikosi Kazi na wengine wote watakaoshiriki katika jitihada za kuongeza mapato hawatalipwa posho kwani maeneo yote ya halmashauri hufikika ndani ya siku moja ya kazi. Kwa kutumia mkakati huu Halmashauri iliweza kufanya safari kuendesha mikutano ya kuhamasisha jamii na kusimamia shughuli za ukusanyaji wa mapato bila kutumia gharama kubwa za posho za kazi za ziada, posho za muda wa ziada, posho za nje ya kituo na posho za kujikimu. Rasilimali zilizotumika zimeelezewa hapa chini.

**(i) Raslimali Watu**

- Timu ya Menejiment ya Halmashauri (CMT). Chombo hiki hupanga na kusimamia utekelezaji wa mipango ya ukusanyaji wa mapato.
- Kikosi Kazi cha mapato. Timu hii hufanya utafiti, uainisha vyanzo vipya vya mapato na hushughulika na utekelezaji wa mipango ya ukusanyaji mapato, kupitia matokeo na huishauri timu ya menejimenti ya Halmashauri juu ya ukusanyaji wa mapato.
- Maafisa Watendaji wa Kata (WCOs) ambao husaidia utambuaji wa vyanzo vipya, hukusanya moja kwa moja mapato na hutoa taarifa kwa kikosi kazi kwa ajili ya ufuatiliaji.
- Maafisa watendaji wa vijiji (VEO) ambao huainisha vyanzo vipya vya mapato katika maeneo yao ya utawala, hushiriki moja kwa moja katika ukusanyaji wa mapto na hutoa taarifa kwa kikosi kazi kwa ajili ya ufuatiliaji.
- Madereva ambao hujitoa kuwezesha usafiri.

**(ii) Usafiri**

- Magari: Halmashauri ya wilaya ya Bukoba imetenga gari moja kwa matumizi endelevu ya idara ya fedha kuwezesha ukusanyaji wa mapato. Ni muhimu kufahamu hapa kuwa magari yote hutumika muda wote na mahali popote pale Timu ya Menejimenti ya Halmashauri inapoamua kufanya ufuatiliaji wa masuala ya mapato.
- Pikipiki: Idara ya fedha, idara nyingine, maafisa watendaji wa Kata na maafisa watendaji wa Vijiji hutumia pikipiki walizogawiwa kwa kufanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato katika masoko, stendi za mabati na vituo vyote vya ukusanyaji wa mapato.

**(iii) Fedha**

- Kama ilivyoelezwa hapo juu, Halmashauri ilitumia kiasi kadhaa cha fedha kwa ajili ya posho, mafuta, nauli na uandaaji na usambazaji wa mabango kwenye masoko. Fedha zilizotumika zilipatikana kutoka mapato ya ndani na fedha za matumizi mengine (OC). Posho hulipwa kwa wajumbe wa kikosi kazi kwa kiasi kidogo sana na kwa mazingira pekee. Mafuta hutumiwa na magari na pikipiki wakati wa utekelezaji tu. Nauli hutolewa mara zote panapokuwa na dharura na hakuna vyombo vya usafiri.

.

## 6.0 MATOKEO YA JITIHADA

Mikakati ya kuboresha mapato iliyoelezwa katika sehemu ya 4.0 imeonyesha wazi wazi matokeo chanya juu ya ukusanyaji wa mapato ya ndani. Jedwali lililopo hapa chini linaonesha ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kipindi cha miaka mitatu.

**Table 3: Ongezeko la Mapato mfululizo kwa miaka miatatu**

| MWAKA | MAKISIO | MAPATO HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **2010/2011** | 442,995,000.00 | 355,178,665.00 | 80.18 |
| **2011/2012** | 948,046,451.00 | 896,462,701.00 | 94.56 |
| **2012/2013** | 1,348,959,000.00 | 1,320,225,615.00 | 97.87 |

**Chanzo: Halamashauri ya Wilaya ya Bukoba**

Ongezeko hili la mapato limetokana na uhamasishaji mkubwa wa jamii uliofanywa na kikosi kazi, madiwani na maafisa watendaji wa kata na wa vijiji katika maeneo yao ya utawala hasa kipindi cha mikutano ya kisheria na mikutano maalumu. Kwa kutambua sababu za kulipa kodi, ada na ushuru, wafanyabiashara wamekuwa wakilipa kodi zao bila usumbufu. Pia uhamasishaji umeamsha ari ya wafanyabiashara kujituma zaidi katika biashara zao kwani ulipaji kodi umekuwa ukweli uliokubalika na kuonekana una lengo la maendeleo.

Lengo la kuongeza mapato limeenda sambamba na uboreshaji wa masoko, minada ya wanayama, machimbo ya madini, masoko ya samaki, masoko ya wazi, stendi za mabasi na vituo vingine vya huduma ambavyo vinapelekea uwepo wa tozo mbalimbali kama ada na ushuru. Miundombinu yenyewe kiuhalisia imeboresha utoaji wa huduma katika maeneo ilipo na kufanya ukusanyaji wa mapato kuwa fanisi na endelevu.



*Eneo la Matoleo ya Samaki, Rushara – mojawapo ya vituo ukusanyaji Mapato*

## 7.0 CHALLENGES ENCOUNTERED

Halmashauri ya Wilaya Bukoba imepata changamoto nyingi kipindi cha mchakato wa mabadiliko haya. Baadhi ya wanasiasa walipinga kabisa wazo la kulipisha kodi bidhaa na vitu kama matofali na moramu na kuzifanya jamii katika Kata kutoipenda Halmashauri hatimaye kujizuia kulipa kodi na tozo nyingine. Pia mwanzoni mwa jitihada hii na kutokana na mwingiliano huu wa kisiasa baadhi ya jamii katika Kata zilileta upinzani mkubwa uliopunguza ari ya watu kulipa kodi, ada na ushuru kwa hiari.

Jamii pia zilibuni mbinu zisizofaa kama ujazaji wa ziada katika magunia ya mazao ya shambani na bidhaa nyingine ili kukwepa kodi halali (mfano, maharage, mahindi, n.k) ujazaji wa ziada (Rumbesa) ni hali ambayo mkulima au mfanya biashara wa kati (dalali) anapozidisha kiasi au ujazo ulioelekezwa kwa ajili ya vipimo vinavyo tambulika kama gunia la mahindi. Lengo la ujazaji wa ziada (Rumbesa) ni kupunguza kiasi cha ushuru unaotakiwa kulipwa. Katika mazingira mengine ujazaji hufanywa katika vipimo vidogo vidogo ili kuwachanganya watoza ushuru waone kuwa vipimo hivyo havina hadhi ya kulipiwa kodi.

Kipengele kimoja kiovu cha Halmashauri za ziwani ni uvuvi haramu ambao umepelekea kupungua kwa samaki wanaovuliwa. Uvuvi huu hutumia mbinu haramu za kukamata samaki kama baruti na neti ambazo hazifai. Matokeo yamekuwa upungufu mkubwa wa samaki wanaovuliwa ziwani na kusababisha upungufu wa bidhaa za kutozwa kodi. Samaki waliovuliwa kwa mbinu haramu hawatozwi kodi. Haya yote hupunguza kasi ya halmashauri kuongeza makusanyo ya mapato.

Mwisho, Usafirishaji wa kahawa kwa magendo kwenda nchi za jirani, hasa Uganda umeongezeka sana. Tabia hii ya wafanyabiashara waovu hutumia mbinu za kukusanya mazao ya shambani na usafirishaji ambazo huinyima Halmashauri kufikia mazao hayo na kupata fursa ya kukusanya ushuru na ada. Kwa mfano Kahawa inayozalishwa katika Wilaya ya Bukoba haidhibitiwi yote na Halmashauri ili kutozwa ushuru kwa sababu za magendo. Mtindo huu huenda pamoja na usafirishaji wa mazao (ya shamba na ya misitu) usiku na (au) kwa masaa ambayo wakusanya kodi hawapo vituoni.

## 8.0 MIKAKATI YA KUPAMBANA NA CHANGAMOTO

Halmashauri ya wilaya ya Bukoba haikukata tamaa kukabiliana na changamoto zilizoelezwa kwenye sehemu ya saba. Halmashauri kupitia maafisa watendaji wa vijiji (VEO) na wa kata (WEO), madiwani na kile kikosi kazi wameendelea kuhamasisha jamii, wafanya biashara, na wanasiasa juu ya umuhimu wa kulipa kodi, ushuru na ada za halmashauri. Halmashauri pia inafanya kazi na taasisi za Serikali Kuu kama Wakala wa Mizani na Vipimo, Kamati ya Ulinzi na Usalama na Ofisi ya Mkuuwa Wilaya kudhibiti tabia za kifisadi zinazonyima Halmashauri ufanisi katika ukusanyaji wa kodi. Pia, Halmashauri imeweka wazi

kwenye sheria zake ndogo kuwa ni haramu kwa mfanyabiashara yeyote kusafirisha mazao ya shamba/misitu baada ya saa 12 jioni.

Halmashauri ya wilaya ya Bukoba imeweka mikakati ya kuhakikisha jitihada hii ya kuboresha mapato inakuwa endelevu. Mikakati hii ni pamoja na kuendelea kupitia sheria ndogo na viwango vya kodi mara kwa mara kulingana na thamani ya shilingi na uwezo wa jamii kulipa. Mkakati wa pili ni uainishaji wa uwezo wa juu wa makusanyo katika kila chanzo.

**9.0 SECRET OF SUCCESS**

Halmashauri ya wilaya ya Bukoba imefanikiwa kuongeza mkusanyaji wa mapato ya ndani kwa sababu ya sifa pekee zilizotajwa kwa muhtasari hapa chini.

- Masoko ambayo ni vituo vya ukusanyaji wa mapato yameanzishwa na jamii. Vituo vya huduma ambayo huanzishwa na jamii hutengeneza hisia za umiliki thabiti unaopelekea dhamira ya jamii ya kuendeleza kituo na hatimaye uendelevu.
- Hali nzuri ya hewa ambayo inaleta uhakika wa kudumu wa uwepo wa mazao na bidhaa zinazofika sokoni, na hivyo kuwepo kwa uhakika wa makusanyo endelevu ya ushuru.
- Kikosi Kazi imara chenye wataalamu mchanganyiko kinachofanya kazi kwa misingi ya timu, ushirikiana na ubunifu ili kuanzisha vyanzo vipya vya mapato, kuendesha uhamasishaji thabiti wa jamii juu ya ukusanyaji mapato, kufuatilia na kuhakikisha ukusanyaji thabiti wa kodi, ushuru na ada za halmashauri.
- Ukusanyaji wa mapato umeazimiwa kuwa ni jukumu la wajumbe wote Timu ya Menejimenti. Hii inawapa haki wajumbe wote hata wakiwa binafsi kufuatilia, kusimamia na kuongoza mchakato mzima wa uainishaji wa vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri, ukusanyaji na udhibiti wa mahesabu katika ngazi za vijiji, kata na halmashauri.

# Kiambatisho 1


**BUKOBA DISTRICT COUNCIL**
**OWN SOURCE REVENUE COLLECTION FROM 2008/09 - 2010/11**

| DEPARTMENT | CODE | DESCRIPTION | FINANCIAL YEAR 2008/2009 | | | FINANCIAL YEAR 2009/2010 | | | FINANCIAL YEAR 2010/2011 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | PROJECTION | ACTUAL | % | PROJECTION | ACTUAL | % | PROJECTION | ACTUAL | % |
| **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** | **9** | **10** | **11** | **12** |
| **FINANCE AND TRADE** | 051039 | Magulio fees | - | - | - | - | 12,605,900.00 | - | - | 24,955,300.00 | - |
| | 051069 | Tobbaco levy | 800,000.00 | 1,632,483.00 | 204 | 1,600,000.00 | 1,929,171.17 | 121 | 2,000,000.00 | 2,296,948.10 | 115 |
| | 051074 | Tender fee | 1,370,000.00 | 9,945,000.00 | 726 | 1,870,000.00 | 11,492,870.18 | 615 | 11,310,000.00 | 8,550,000.00 | 76 |
| | 090295 | Insurance commission | 1,500,000.00 | 485,743.00 | 32 | 1,500,000.00 | 1,010,900.24 | 67 | 1,000,000.00 | 439,561.41 | 44 |
| | 140113 | Sales of revenue books | 2,500,000.00 | 2,608,600.00 | 104 | 2,500,000.00 | 2,013,700.00 | 81 | 1,500,000.00 | 5,532,900.00 | 369 |
| | 051250 | Service Levy | 10,620,000.00 | 20,255,311.00 | 191 | 10,020,000.00 | 10,858,309.71 | 108 | 12,400,000.00 | 37,473,455.14 | 302 |
| | - | Intoxicating liquor license fee-local | 1,200,000.00 | 1,100,400.00 | 92 | 900,000.00 | 273,000.00 | 30 | - | 172,000.00 | - |
| | 050703 | Intoxicating liquor license fee-foreign | 650,000.00 | - | - | 1,920,000.00 | 70,000.00 | 4 | 2,000,000.00 | 1,754,100.00 | 88 |
| | 050802 | Other revenues | 3,500,000.00 | 10,852,793.00 | 310 | 2,000,000.00 | 2,744,571.08 | 137 | 7,000,000.00 | 8,444,747.96 | 121 |
| | 090296 | Revenue from renting of houses | 9,285,600.00 | 16,274,378.00 | 175 | 16,005,600.00 | 22,389,281.00 | 140 | 28,260,000.00 | 14,913,081.48 | 53 |
| | 140102 | Revenue from renting of assets | 253,000,000.00 | 168,857,075.00 | 67 | 306,881,950.00 | 238,338,753.00 | 78 | 228,560,000.00 | 120,406,800.00 | 53 |
| | **TOTAL FINANCE AND TRADE** | | **284,425,600.00** | **232,011,783.00** | 82 | **345,197,550.00** | **291,120,556.38** | **84** | **294,030,000.00** | **199,983,594.09** | **68** |
| **LAND AND NATURAL RESOURCES** | 051033 | Timber produce cess | 500,000.00 | 1,026,238.00 | 205 | 999,282.00 | 268,800.00 | 27 | 500,000.00 | 12,613,297.00 | 2523 |
| | 051006 | Gobole fee | 500,000.00 | 105,300.00 | 21 | 500,000.00 | 327,100.00 | 65 | 500,000.00 | - | - |
| | 090157 | Land rent | 800,000.00 | 144,900.00 | 18 | 2,700,000.00 | 431,783.90 | 16 | 1,500,000.00 | 2,142,016.00 | 143 |
| | 081150 | Land survey service fee | 2,700,000.00 | 3,270,590.00 | 121 | 7,340,000.00 | 1,934,000.00 | 26 | 4,640,000.00 | - | - |
| | 100106 | Fines imposed by magistrate | 1,000,000.00 | 76,550.00 | 8 | 900,000.00 | 367,000.00 | 41 | 300,000.00 | 225,500.00 | 75 |
| | 0540461 | Revenue from timber | 3,600,000.00 | 2,187,700.00 | 61 | 2,500,000.00 | 2,577,150.00 | 103 | ` | 2,148,300.00 | - |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 050462 | Revenue from charcoal | 3,600,000.00 | 2,200,000.00 | 61 | 4,800,000.00 | 5,000,000.00 | 104 | 2,400,000.00 | 2,300,000.00 | 96 |
| | **TOTAL LAND AND NATURAL RESOURCES** | | **12,700,000.00** | **9,011,278.00** | **71** | **19,739,282.00** | **10,905,833.90** | **55** | **9,840,000.00** | **19,429,113.00** | **197** |
| **LIVESTOCK** | 050951 | Fishing vessel license fees | 6,645,000.00 | 4,812,200.00 | 72 | 6,645,000.00 | 6,126,100.00 | 92 | 6,645,000.00 | 10,238,300.00 | 154 |
| **FISHERIES** | - | Livestock market fee | - | - | - | - | - | - | - | 8,956,000.00 | - |
| **DEVELOPMENT** | 051076 | Fish landing facilities fee | 31,140,000.00 | 23,846,500.00 | 77 | 31,080,000.00 | 13,393,000.00 | 43 | 38,280,000.00 | 26,883,395.00 | 70.2 |
| | | Commercial fishing license fees | - | - | - | - | - | - | - | 1,423,999.41 | - |
| | | **TOTAL LIVESTOCK & FISHERIES** | **37,785,000.00** | **28,658,700.00** | **75.8** | **37,725,000.00** | **19,519,100.00** | **51.7** | **44,925,000.00** | **47,501,694.41** | **106** |
| **AGRICULTURE** | 050713 | Coffee crop cess | 125,000,000.00 | 152,531,287.00 | 122 | 175,000,000.00 | 126,806,880.00 | 72 | 90,000,000.00 | 84,943,807.50 | 94 |
| **IRRIGATION** | 050713 | Tea crop cess | 5,000,000.00 | 4,253,112.00 | 85 | 3,200,000.00 | 3,780,723.40 | 118 | 3,000,000.00 | 2,940,456.00 | 98 |
| **COOPERATION** | 050713 | Other food crop cess | 2,760,000.00 | 610,000.00 | 22 | 1,800,000.00 | 1,400,000.00 | 78 | 1,200,000.00 | 380,000.00 | 32 |
| | **TOTAL AGRICULTURE, IRRIG. COOP** | | **132,760,000.00** | **157,394,399.00** | 119 | **180,000,000.00** | **131,987,603.40** | 73 | **94,200,000.00** | **88,264,263.50** | **94** |
| | **GRAND TOTAL** | | **467,670,600.00** | **427,076,160.00** | 91 | **582,661,832.00** | **453,533,093.68** | 78 | **442,995,000.00** | **355,178,665.00** | **80** |

# HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

## MIKAKATI YA UBORESHAJI NA UENDELEVU WA MAPATO YA NDANI





*Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama – Ushetu*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya wilaya ya Ushetu iliyopo Mkoa wa Shinyanga imetokana na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama iliyogawanywa kuwa Halmashauri tatu. Halmashauri nyingine mbili ni Halmashauri ya Mji wa Kahama na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala. Halmashauri nyingine Mkoani Shinyanga ni pamoja na Manispaa ya Shinyanga na Halmashauri za Wilaya za Shinyanga na Kishapu. Jitihada za kuboresha Mapato za Halamashuri ya Wilaya ya Ushetu zilianza enzi za Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na zikarithiwa na kuboreshwa na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.


Wilaya ya kahama ilianzishwa mwaka 1962 na mwaka 1982 kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa No.7 Wilaya ya Kahama ikawa Halmashauri ya Wilaya. Halmashauri ilikuwa na Tarafa 5, Kata 55, Vijiji 232 na Vitongoji 1137. Ramani iliyopo hapa chini inaonyesha jiografia ya mgawanyiko wa maeneo ya kisiasa na kiutawala.

**Mchoro 1: Halmashauri ya Wilaya ya Kahama (Kabla ya Mgawanyiko)**





Mwezi Julai mwaka 2012 Halmashauri ya Wilaya ya Kahama iligawanywa na kuwa halmashauri mbili; Halmashauri ya Mji wa Kahama iliyochukua Tarafa 2, Kata 20, Vijiji 45 na Vitongoji 315 na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama iliyobaki na Tarafa 3, Kata 35, Vijiji 187 na Vitongoji 822. Uamuzi wa serikali wa kugawa Halmashauri ni ili kupeleka huduma karibu na jamii na watu. Mgawanyiko huo unaonyeshwa kwenye ramani hapa chini.

**Mchoro 2: Ramani ya Halmashauri ya Mji wa Kahama**




Julai Moja (1) mwaka 2013 Halmashauri ya Wilaya ya Kahama iligawanywa tena na kuzaa Halmashauri mbili za Wilaya za Ushetu na Msalala. Msalala ilichukua Tarafa 1, Kata 16, Vijiji 82 na Vitongoji 322 kama inavyoonyeshwa kwenye ramani hapa chini.

**Mchoro 3: Halmashauri ya Wilaya ya Msalala**




Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ilirithi Tarafa 2, Kata 19, Vijiji 105 na Vitongoji 500 kutoka Halmashauri ya awali ya Kahama. Ramani iliyopo hapo chini inadhirisha ukweli huu. Kiutawala Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu in Km2 5,311 na jumla ya wakazi wapatao 273,075 kama sensa

watu na makazi ya mwaka 2012 inavyoonyesha. Halmashauri ya Ushetu inapakana na halmashauri za Wilaya za Nzega kwa upande wa Mashariki, Msalala kwa upande wa kaskazini, Mbogwe kwa upande wa Magharibi na Uyui kwa upande wa Kusini.

**Mcoro 4: Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu**




Kijiografia Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu imejaaliwa ardhi yenye rutuba wastani inayopanda polepole na kuwa milima na tambarare zilizofunikwa na misitu. Tambarare hizi huruhusu kilimo na jamii za ushetu hujishughulisha na uzalishaji wa mazao mbalimbali kama tumbaku, Pamba na Alizeti yakiwa mazao ya biashara. Karanga, mahindi, mpunga, mtama, viazi vitamu, mihogo, maharagwe na njugu hulimwa kama mazao ya chakula.

**2.0 TATIZO LILILOKUWEPO**

Tangu enzi za Halmashauri ya Wilaya ya Kahama makusanyo ya mapato yalikuwa duni sana miaka yote. Kwa mfano mwaka 2008/2009 mapato ya ndani yalikuwa ni 7.6% tu sawa na shs 2.5 bilioni ya bajenzi nzima ya Halmashauri. Ikilinganishwa na utajiri na shughuli za kiuchumi zilizokuwepo katika Wilaya ya Kahama kiasi hiki cha makusanyo ya mapato ya ndani ni cha chini sana. Sababu zilizopelekea usugu katika makusanyo ya chini ni pamoja na hizi zifuatazo.

(i) Vyanzo vingi vya mapato ambavyo ni vya kutegemewa havikuwa vinaingizwa kwenye mipango ya mapato kutokana na utafiti duni wa kuainisha na kuchambua vyanzo hivyo vizuri.

(ii) Vyanzo vya mapato ambavyo viliainishwa na kuchambuliwa viliweza kuchangia ushuru kidogo sana na usimamizi na ukusanyaji wake ulikuwa dhaifu sana.

(iii) Vifaa na mbinu ambazo zilitumiwa kukusanya ushuru wa mazao, ushuru wa huduma na ada mbalimbali kutoka vyanzo vilivyoainishwa zilikuwa za gharama, mbaya na za kinyama.

(iv) Ukosefu wa vyanzo vya mapato vilivyochambuliwa vizuri ilizidisha tatizo la kutambua uwezo halisi wa makusanyo kila chanzo kinaweza kuzalisha ili kufanya maamuzi sahihi kuhusu ubinafsishaji wa ukusanyaji wa mapato kwa wakala binafsi na wazabuni.

(v) Ukwepaji mkubwa wa kulipa ushuru uliofanywa na makampuni, wafanya biashara na washiriki katika sekta isiyo rasmi na kilimo.

(vi) Viwango vilivyopitwa na wakati vya ada, ushuru na tozo mbalimbali katika bidhaa za kilimo, misitu na hata migodi ya madini.

(vii) Sheria ndogo zilizopitwa na wakati na ambazo hazikuakisi mahitaji na uwezo halisi wa kila chanzo cha mapato ya ndani.

(viii) Mipango, ufuatiliaji na usimamizi mbaya na duni wa ukusanyaji wa mapato.

(ix) Ushiriki dhaifu wa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata katika kupanga, kukusanya na kuandaa taarifa za fedha.

## 3.0 MALENGO YA HALMASHAURI

Lengo la jumla la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu-Kahama kwenye mkakati huu lilikuwa kuboresha utendaji katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kujenga uwezo wa mapato ya ndani na kupunguza utegemezi kwenye ruzuku toka Serikali Kuu. Halmashauri ilidhamiria kuongeza mapato ya ndani kutoka 7.6% hadi 25% ya bajeti nzima ya Halmashauri na kukusanya mapato toka vyanzo vyote kwa 100%. Malengo mahsusi ya mkakati huu yalijumuisha yafuitayo;

(i) Kuainisha na kuchambua kwa kina vyanzo vyote vya mapato ya ndani katika maeneo yote ya Halmashauri.

(ii) Kuboresha mbinu na mikakati ili kuleta usimamizi imara wa ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyote.

(iii) Kuhakikisha ushiriki thabiti wa wadau wote, yaani jamii, biashara mbalimbali, makampuni na maafisa watendaji wa Kata na Vijiji katika ukusanyaji wa mapato.

(iv) Kupitia, kufuta na kutunga sheria ndogo zinazoelekeza viwango vya tozo vyenye uhalisia (ushuru wa mazao, kodi, ushuru wa huduma, ada, faini na adhabu) kwa aina mbalimbali za vyanzo vya mapato.

(v) Kuzuia na kuondoa kabisa vitendo na tabia zote zinazozuia ukusanyaji fanisi wa mapato ya ndani. Tabia hizi hujumuisha rushwa, ujazaji haramu wa bidhaa na matumizi ya njia za siri kusafirisha bidhaa kwa lengo la kukwepa/kupunguza kulipa kodi, ushuru na ada mbalimbali.

## 4.0 MIKAKATI NA SHUGHULI ZA KUONGEZA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI

Kama ilivyoonyeshwa kwenye malengo, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ilijikita katika kuongeza mapato ya ndani toka chini ya 8% mwaka 2008 hadi 25% mwaka 2013/14 ya bajeti nzima ya Halmashauri. Ili kuweza kufikia lengo hili Halmashauri iliafiki uamuzi mzito wa kufanya utafiti wa kina ili kutafuta, kuchambua na kutathmini vyanzo vyote vya mapato ya ndani viwezekanavyo na kuelezea uwezo halisi wa kila chanzo. Utafiti huu ulifanywa na Kikosi Kazi cha wataalam mchanganyiko kilichoteuliwa na Kamati Tendaji ya Baraza la Halmashauri. Utafiti ulifanyika kwa siku 14 katika vijiji na kata zilizoingizwa kwenye sampuli.

Wakati wa utafiti huu mbinu zifuatazo zilitumika;

(i) Kufanya mikutano na wadau muhimu katika vijiji. Hili lililenga kupata taarifa moja kwa moja toka kwa wanavijiji kuhusu uwezo na uthabiti wa vyanzo vya mapato vinavyopendekezwa.

(ii) Kuendesha majadiliano ya moja kwa moja na wafanya biashara na vikundi mbalimbali katika masoko, minada na vituo vyote vya biashara.

(iii) Kukutana na Mawakala wote na Wazabuni wa Ukusanyaji wa Mapato na kufanya uchimbuzi wa kina kuhusu changamoto zote zinazozunguka ukusanyaji wa mapato ya ndani katika maeneo na vyanzo walivyokabidhiwa.

(iv) Kutembelea maeneo yote ambayo yanaweza kuwa na vyanzo tarajiwa vya mapato kama vile masoko, minada ya wanyama na vituo vya biashara vya vijijini.

(v) Kupendekeza mabadiliko ya kufanyika katika sheria ndogo za vyanzo vya mapato na kuhakikisha rasimu za sheria ndogo zinakuwa tayari kwa kupitishwa na Baraza. Mabadiliko katika sheria ndogo yalizingatia moja kwa moja viwango mbalimbali vya kodi, ushuru, ada na faini zitakazotozwa kwa kila bidhaa iliyotambuliwa katika kila chanzo cha mapato.

(vi) Kupitia sampuli za miaka ya nyuma ya makadirio ya makusanyo ya mapato na makusanyo halisi ili kujua mtiririko ulivyokuwa ili kubaini sababu na ufafanuzi wa tofauti za miaka. Hili lingesaidia Kikosi Kazi kuunda mikakati ya ukusanyaji wa mapato ambao ni endelevu na hakika.

Baada ya Utafiti na uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa, Kikosi Kazi kiliainisha na kupendekeza vyanzo vipya vya mapato vilivyoorodheshwa kwenye mchoro hapa chini.

**Mchoro 5: Kodi, Ushuru na Ada**

- Ushuru kutoka Migodi inayomilikiwa na watu binafsi katika maeneo ya vijijini
- Ushuru kutoka mitambo na vifaa vya migodini
- Ushuru kutoka Mazao ya chakula na matunda
- Ada kutoka stendi za mabasi na maegesho vijijini
- Ushuru kutoka minara ya simu
- Kodi kutoka makazi yaliyopangwa na mipango miji
- Ushuru kutoka vifaa vya ujenzi kama mchanga, kokoto, mawe, udongo, nk
- Ushuru kutoka pikipiki na maegesho ya pikipiki
- Ushuru kutoka mashine za kukoboa na kusaga
- Ushuru kutoka mazao ya misitu kama mkaa na mbao

Mikakati na shughuli nyingine baada ya utafiti na uainishaji wa vyanzo vipya ilikuwa kama ifuatavyo;

(i) Kuimarisha utozwaji wa viwango vipya na zoezi la ukusanyaji katika maeneo na vyanzo vyote vya mapato ya ndani vya zamani ili kuzuia kurudi nyuma.

(ii) Kuwasilisha mapendekezo ya viwango vya tozo na vyanzo vipya vya mapato kwenye Baraza ili vijadiliwe, vikubaliwe na viidhinishwe.

(iii) Kuunda Kikosi Kazi cha wataalam sita watakao endelea kutafuta vyanzo vipya, kusimamia na kufuatilia mchakato mzima wa ukusanyaji wa mapato.

(iv) Kuunda kamati ndogo ya Madiwani na kuwapa jukumu la kuhamasisha, kumotisha na kuhimiza jamii, wachimbaji wa madini, wakulima na wafanya biashara kulipa kodi, ushuru na ada mbalimbali kutoka vyanzo vya zamani na vipya hasa ushuru wa mazao shamba, mkaa, mbao na vifaa vya ujenzi vitokavyo ardhini.

(v) Kutunga sheria ndogo mbalimbali kwa ajili ya kila chanzo cha mapato. Ilikuwa muhimu kufuta na kutunga sheria ndogo ambazo ni fanisi na halisia kwa vyanzo na viwango vyote vipya ili kuwa na ukusanyaji wa kodi na uboreshaji wa mapato ambao ni wa kisheria. Sheria hizi ndogo zinaeleza wazi wazi vyanzo gani, viwango gani vya tozo na mwenendo gani unatarajiwa kwa upande wa walipa kodi pamoja na faini na adhabu kwa wale wanaokosea.

(vi) Kutenga na kugawa maeneo muhimu kwa ajili ya uwekezaji, biashara ndogondogo, vituo vya biashara, masoko, minada na vituo vya mabasi. Hili hurahisisha ukusanyaji wa aina mbalimbali za mapato kwa sababu linapelekea uwepo wa maeneo na vituo rasmi vya ukusanyaji wa mapato.

(vii) Kutumia fursa ya Ushirikiano na Sekta Binafsi. Halmashuri ilibinafsisha vyanzo vyote vya mapato ambavyo ni vigumu na ni gharama kukusanywa na kusimamiwa moja kwa moja na Halmashauri. Hilli lilifanywa kulingana na sera ya serikali ya kubinafsisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuweza kujikita zaidi katika utoaji wa huduma.

## 5.0 RASLIMALI ZILIZOTUMIKA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

Uboreshaji wa mapato ya ndani hujumuisha uimarishaji wa miundombinu, usimamizi imara, ufuatiliaji wa karibu na ukusanyaji fanisi wa ada na ushuru wa papo kwa papo. Haya hayawezi kufanyika kirahisi tu bila kutenga raslimali za kutosha kuwezesha michakato. Raslimali zinazohusika hapa ni raslimali watu, fedha, muda na usafiri. Tangu mwaka 2008/09 hadi 2012/13 halmashauri ilitumia jumla shs 396,181,000/= kwa shughuli hii. Majedwali yaliyopo hapa chini yanachambua kila kipengele cha matumizi katika mkakati huu wa kuboresha mapato.

**Jedwali 1: Gharama za mikutano ya Baraza**

| Kikao | Mwaka | Gharama kila Kikao (Tshs | Gharama za Vikao kwa Mwaka (Tsh) |
|---|---|---|---|
| **Baraza** | 2008/2009 | 21,254,000 | 85,016,000 |
| **Baraza** | 2009/2010 | 21,254,000 | 85,016,000 |
| **Baraza** | 2010/2011 | 21,254,000 | 85,016,000 |
| **Baraza** | 2011/2012 | 16,090,000 | 64,360,000 |
| **Baraza** | 2012/2013 | 16,090,000 | 64,360,000 |
| | | **Jumla** | **383,768,000** |

**Jedwali 2: Raslimali Fedha**

| Raslimali | Mwaka | Gharama kwa kila moja(Tsh) | Gharama kwa mwaka (Tsh) |
|---|---|---|---|
| **Wataalam 7** | 2012/2013 | 3,430,000 | 3,430,000 |
| **Madereva 2** | 2012/2013 | 700,000 | 700,000 |
| **Mafuta (diesel)** | 2012/2013 | 1,500 x 2,202 | 3,303,000 |
| **Kamati ya fedha** | 2012/2013 | 2,490,000 | 4,980,000 |
| | | **jumla** | **12,413,000** |

## 6.0 MATOKEO NA HADITHI YA MAFANIKIO

Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu-Kahama imefanikiwa kwenda kwa kasi kuelekea kufikia lengo la 25% ya mapato ya ndani kuwa sehemu ya bajeti nzima ya Halmashauri. Mkakati huu kiukweli umeshafanikiwa kuonyesha matokeo yaliyoelezewa hapa chini.

Kumekuwa na ongezeko dhahiri la mapato kutoka vyanzo vya ndani na kufikia 21.5% kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali 3: Makusanyo ya Mapato**

| Mwaka | Kiasi kilichokusanywa |
|---|---:|
| **2008/2009** | 2,520,000,000 |
| **2009/2010** | 3,210,000,000 |
| **2010/2011** | 3,320,000,000 |
| **2011/2012** | 3,388,192,000 |
| **2012/2013*** | 3,069,493,600 |

**tafadhali zingatia kuwa mapato ya mwaka 2012 yalipungua kidogo kutokana na kugawanywa kwa halmashauri ya Wilaya ya kahama ili kuunda Halmashauri ya Mji wa Kahama.*

Halmashauri imekuwa fanisi katika kutoa michango yake kwa miradi ya maendeleo katika jamii kama inavyoelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi chini ya mfumo wa ruzuku ya maendeleo (LGDG). Utoaji wa 5% ya mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya jamii, mfuko wa mikopo wa wanawake na mfuko wa mikopo wa vijana limekuwa zoezi la kawaida la Halmashauri. Jedwali lililopo hapa chini linaonyesha kiasi cha fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maendeleo na mifuko mbalimbali ya jamii.

**Jedwali 4: 5% Michango**

| Mwaka | Kiasi kilichangwa (Tshs) |
|---|---:|
| **2008/2009** | 298.12 million |
| **2009/2010** | 514.29 million |
| **2010/2011** | 931.89 million |
| **2011/2012** | 982,.42 million |
| **2012/2013** | 350.0 million |

Badiliko hili dhahiri la ukusanyaji wa mapato linashuhudiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya wa sasa kwa kusema *"… nilikuta jitihada hizi tayari zikiwepo, nilichokifanya ni kukitia moyo Kikosi kazi kufanya kazi kwa bidii na nikaahidi kulipia zoezi zima mpaka tutakapofikia shabaha ya 25% mwakani…. Ninayo nia thabiti ya kuhakikisha kuwa tunajitegemea walau kwa 25% kabla hatujaweka shabaha nyingine….matokeo ya jitihada hii sasa yapo dhahiri….wananchi wameshaelewa umuhimu wa kulipa kodi, masoko yanafanya kazi sawasawa, mabanio yote tunapokusanyia ushuru wa mkaa na mazao mengine ya misitu yanachangia sana katika mapato yetu….ni kweli…tunafikia lengo letu la jumla…."* .

Mapato ya ndani yamejazia kwenye ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya jamii kama ujenzi wa madarasa na mabweni katika shule za sekondari, ukarabati wa barabara za Halmashauri na uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi kwa ujumla. Picha zilizopo hapo chini zinaonyesha mifano ya maboresho yaliyofanyika kutumia michango ya wananchi na mapato ya ndani.





*Maabara ya Sekondari ya Ntobo Segese* *Bweni la Wasichana sekondari ya Balohal* *Uboreshaji wa Barabara ya Jomu –*

## 7.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI

Jaribio la kuongeza mapato tangu enzi za Halmashauri ya Wilaya ya Kahama limekabiliana na changamoto nyingi zenye sura mbalimbali ambazo ni muhimu kuzitaja hapa kwa lengo la kujifunza has kwa zile halmashauri ambazo zina nia ya kutumia medeli hii kuongeza mapato ya ndani.

Kugawanywa kwa halmashauri ya wilaya ya Kahama. Pamoja na kuwa lengo la jumla la kugawa Halmashauri ni kugatua zaidi utoaji wa huduma kwenda kwa jamii na watu na kufanya vituo vya huduma kuwa karibu na watu zaidi, ugawaji wa Halmashauri ya Wilaya ya kahama kuwa sehemu mbili za ushetu na Msalala uliathiri sana jitihada za ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano, mgawanyiko huu umeleta mgogoro katika ukusanyaji wa ushuru wa mazao ya misitu na kilimo. Wafanya biashara wanaamini kuwa kodi na ushuru wa mazao haya vinatakiwa kulipwa Halmashauri ya Mji wa Kahama. Pia mipaka ya hizi Halmashauri bado haijaeleweka wazi kwa wananchi hivyo kuleta ugumu katika ukusanyaji wa mapato. Kutokana na mgawanyo huu wa Halmashauri makusanyo ya mapato yalipungua mwaka 2012/13.

Ukataaji wa makampuni makubwa ya ushimbaji madini kulipa ushuru wa huduma wa 0.3% kutoka kwenye mapato yao ya mwaka. Sheria ya fedha sura Na 190 kifungu cha 7(2) kinazitaka Halmashauri kukusanya ushuru wa huduma wa 0.3% kutoka katika faida za Makampuni makubwa. Pia Mashirika haya yanalazimika kulipa mrahaba kwa Halmashauri. Lakini Mwekezaji mkubwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu-Kahama ni Kampuni ya Barick ambayo hukataa kulipa Ushuru wa Huduma kwa kisingizio kuwa mkataba wake na serikali kuu unaonyesha kuwa Kampuni inatakiwa kulipa Mrahaba tu kwa Haalmashauri wenye thamani ya Dola za Kimarekani 200,000 kwa mwaka. Hii ni kinyume kabisa na sheria za Bunge kuhusu mapato ya ndani ya Halmashauri. Pia Kampuni ya Buzwagi mines iliyopo chini ya kampuni ya African Gold Mine, tangu kuanza kwake shughuli za uchimbaji madini mwaka 2009 hadi 2012, imelipa mrahaba wa dola za kimarekani 800,000 tu. Kama kampuni hizi zingekubali kulipa ushuru wa huduma wa 0.3%, Halmashauri ingepata jumla ya dola za kimarekani 3,143,065.49 za ushuru wa huduma katika kipindi cha miaka mine. Hii inabaki kuwa changamoto hadi sasa.

Kuingiliwa kwa ajabu na wanasiasa wa Halmashauri na wa Kitaifa. Kwa miaka mingi Halmashauri ya Wilaya ya kahama haikuwa na ushuru wa mazao ya misitu kama mkaa na mbao. Uanzishaji wa ushuru huu siku za karibuni umekumbana na pingamizi hata kutoka kwa wanasiasa walioridhia chanzo hiki. Kwa kuungana na wanasiasa wa kitaifa wamekuwa wakitoa hotuba katika mikutano ya hadhara kupinga chanzo hiki tajiri cha mapato ya ndani. Wananchi hupenda kuungana na wanasiasa kuliko watumishi wa Halmashauri katika masuala ya Kodi.

Sura ya Utumishi na Ikama ya Halmashauri. Ikama ya Halmashauri imebanwa na baadhi ya watumishi bado wameshikiliwa na wizara zao mama. Kwa mfano maafisa madini wameshikiliwa na wizara ilihali huduma za madini zinazohitajiwa na wananchi zinatolewa na Halmashauri. Vibali, mapendekezo ya vibali vya umiliki wa migodi na Leseni za uchimbaji wa madini hutolewa na maafisa wa wizara. Taarifa na takwimu za shughuli za uchimbaji wa madini pia hazijakasimishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Haya yote huzuia Halamashauri kupata taarifa za uzalishaji wa madini kwa mwaka na faida zake ili kuweza kukadiria kodi na ushuru.

Wachimbaji wadogo wa madini wa halmashauri ya Ushetu-Kahama. Katika miaka ya karibuni wachimba madini wadogo wameongezeka sana tena bila utaratibu kutokana na ongezeko kubwa la vijana wanaodai kutokuwa na ajira. Kila wanaposikia kuwa kuna sehemu ya ardhi inayotoa matarajio ya madini, hukimbilia katika eneo hilo kwa idadi kubwa bila hata kujali umiliki wa ardhi hiyo. Mbinu wanazotumia kuchimba na kupata madini ni mbaya na hatari kiafya. Shughuli hizi huharibu sana mazingira kutokana na ukataji miti kwa fujo, uharibifu wa vyanzo vya maji wanayoyatumia kuchanganya na zebaki ili kukusanya dhahabu na uchimbaji wa mashimo marefu na makubwa yanayofanya ardhi kutofaa tena kwa matumizi ya shughuli nyingine za kiuchumi kwa miaka mingi. Shughuli zote hizi siyo rasmi na haziwezi kuingizwa kwenye mipango ya uzalishaji endelevu wa mapato ya ndani. Pia kuna vibali vingi sana vya utafiti wa madini vinavyotolewa na serikali kuu. Haya yote huleta misuguano na migogoro ya ardhi katika Halmashauri ambayo ni lazima itatuliwe na kusimamiwa ilihali halmashauri haiwezi kukusanya mapato yenye thamani kutokana na matumizi haya ya ardhi kuongeza mapato ya ndani.

Minara ya simu imekingwa kutozwa kodi za Halmashauri. Minara ya simu imetapakaa katika maeneo mengi ya makazi ndani ya halmashauri. Minara hii ni vitengo vya uzalishaji ambapo kabla ya kusimikwa inatakiwa kulipiwa ada za vibali na baada ya kusimikwa inatakiwa kuendelea kulipiwa ushuru wa huduma. Hata hivyo kiuhalisia makampuni yanayomiliki minara hii hayalipi ushuru wa huduma. Badala yake kampuni hizi hulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri nyingine ambapo wanauza bidhaa na vifaa vya mawasiliano. Kwa mfano Halmashauri ya Ushetu ilikisia kukusanya shs milioni 62 mwaka 2011/12 kutokana na minara 31 ya simu iliyopo katika Kata na Vijiji lakini makusanyo kutoka chanzo hiki yaka wa sifuri kwa sababu ya kukataa kwa makampuni haya ya mawasiliano kulipa ushuru wa huduma kwa madai kuwa hawana maduka yanatouza bidhaa za mawasiliano na simu katika eneo la Halmashauri.

## 8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Changamoto zilizoelezwa hapo juu hazijafanya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kukata tama na kuachana na juhudi za kuongeza makusanyo ya mapato na kufanya ongezeko la mapato ya ndani kuwa endelevu. Halmashauri imejiwekea mbinu za kuhakikisha mapato ya ndani yanafikia shabaha ya 25% na zaidi kila mwaka. mbinu hizi ni pamoja na;

(i) Utafiti na ubunifu usiokoma kuhusu vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuhuisha viwango ushuru, ada, faini na adhabu mbalimbali.

(ii) Utekelezaji wa sheria ndogo za halmashauri usiokoma tena bila uzembe wa aina yoyote. Hili litajumiuisha ugawaji wa sheria ndogo na za Bunge kwa wadau wote, Maafisa watendaji wa Kata na vijiji, Mabaraza yote ya Kata, mahakama zote za mwanzo na maeneo yote ambapo sheria hizi ndogo zinaweza kufanya ukusanyaji wa mapato kuwa fanisi.

(iii) Kuendeleza uhamasishaji shirikishi wa madiwani, jamii na wadau wote kuhusu umuhimu na wajibu wa kulipa kodi, ushuru, n.k. hii itapunguza upinzani na migogoro wakati wa ukusanyaji wa mapato.

(iv) Kufuata kikamilifu misingi ya sera ya ushirikiano na Sekta Binafsi (PPP) kwa kubinafsisha vyanzo vyote vya mapato ambavyo ni vigumu na gharama sana kukusanywa na Halmashauri kwa ufanisi. Hili litafanyika tu kila baada ya utafiti wa msingi wa uwezo wa uzalishaji wa mapato wa vyanzo husika.

(v) Kuendelea kuhimiza makampuni makubwa yaliyomo ndani ya halmashauri ya Ushetu kulipa ushuru wa huduma na mirahaba kulingana na sheria za nchi na sheria ndogo. Hii itajumuisha kutafuta upatanishi kati ya Halamshauri ya Wilaya ya Ushetu, Serikali kuu na Kampuni za Uchimbaji madini ili kuzilazimisha kulipa Ushuru wa Huduma.

(vi) Kuendelea kushiurikiana na serikali kuu kuhusu namna ya kudhibiti ongezeko la wachimba madini wadogo. Hapa serikali kuu inahitajika kutenga maeneo ya migodi/machimbo kwa makundi haya.

(vii) Kuanzisha vitalu vya miche ambavyo Halmashauri itatumia kushawishi wakulima kupanda miti katika maeneno yaliyoathiriwa na kilimo cha tumbaku kwani ardhi imeharibika sana kuwa nusu jangwa. Huduma hii tayari inapatikana katika shule za msingi na sekondari. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu inategemea kilimo cha tumbaku kwa sababu 52% ya mapato ya ndani hutokana na uzalishaji wa tumbaku ambao hutumia sana miti katika uchakataji wake.

(viii) Halmashauri pia imedhamiria kujenga barabara, vyoo vya umma, masoko na maghala na kusambaza maji katika maeneo yenye vyanzo vya mapato vya uhakika. Hii itasaidia sana uhakika wa masoko na usafiri wa bidhaa; vyote hivi huongeza uzalishaji wa mapato.

**9.0 SECRETS FOR SUCCESS**

Mafanikio yaliyopatikana katika Halmashauri hii yamejengeka katika siri zifuatazo

(i) Halmashauri ya ushetu-Kahama imejikita muda wote katika utafiti na tathmini ili kujiridhisha kuhusu ubora, ufanisi na uwezo wa vyanzo vyake vya ndani vya mapato. Siri hii imesaidia halmashauri kukusanya takriban 61% ya mapato yake ya ndani kwa mwaka 2013/14.

(ii) Siri ya pili ambayo ina uhusiano na siri ya kwanza inahusu matumizi mazuri ya ushirikiano na sekta binafsi (PPP) kwa kubinafsisha kimkakati kabisa ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya vyanzo. Lakini hili linafanywa kwa umakini sana hasa baada ya uchambuzi wa kina wa uwezo wa juu wa mapato wa kila chanzo. Mawakala wanaopewa mkataba wanalazimika kulipa kiasi sawa na makusanyo ya robo nzima ya mwaka kabla ya kuanza kwa ukusanyaji wa mapato katika chanzo husika kwa mwaka wa fedha unaoanza.

(iii) Ushirikishwaji wa wadau wa mapato ni siri nyingine. Wafanya biashara wote kwa makundi yao mahsusi hualikwa katika mikutano ya kuanzisha ushuru na ada mpya katika maeneo mahsusi. Kwa mfano kwa kuanzisha ushuru wa mazao shamba, ushuru wa matumizi ya soko na ushuru wa mazao ya misitu wadau walishiriki katika majadiliano na maamuzi ya

viwango vya tozo vya Halmashauri. Jamii pia zinashiriki kupitia madiwani katika mikutano. Haya yote yamefanya ukusanyaji wa mapato kuwa rahisi na fanisi.

(iv) Kufanya kazi kama Timu na Kujitoa kwa dhati. Timu nzima ya menejimenti na watumishi wote wa halmashauri ya Ushetu wamejitoa kwa dhati kufanya kazi kwa kujituma sana katika kuongeza mapato ili kuboresha utendaji wa Halmashauri. Uhamasishaji na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato unafanywa na wajumbe wote wa Timu ya Menejiment ya Halmashauri. Na masuala yanayohusiana na ukusanyaji wa mapato ni dondoo ya kudumu ya mikutano ya kila siku asubuhi ya Timu ya menejimenti ya halmashauri.

(v) Watumishi wenye motisha na furaha. Halmashauri hurudisha 10% ya mapato yaliyokusanywa na watumishi katika ngazi za vijiji na kata kwa vyanzo vyote ambavyo havijabinafsishwa kwa mawakala binafsi. Hili hutia moyo watumishi kufanya kazi kwa kujituma katika kuhakikisha mapato yanakusanywa kikamilifu.

# Sura ya Nne: Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma

Kupanga mipango kwa njia shirikishi ni hatua ya mwanzo kabisa katika kutoa huduma kwa jamii. Kupanga mipango ni mchakato endelevu wa kuweka malengo, kutambua fursa au rasilimali na uwezo uliopo wa kutekeleza miradi hadi kufikia malengo, katika muda muafaka uliowekwa na Taasisi, Serikali, Idara au Kitengo cha Utawala. Kupanga mipango kunasaidia sana katika kutekeleza miradi kwa utaratibu wenye mantiki na kufikia malengo yaliyowekwa, kufuatilia matumizi ya rasilimali na kutatua vikwazo. Katika mazingira halisi ya Serikali za Mitaa, mipango husaidia kuanisha maeneo yanayohitaji kuwekewa mkazo na vipaumbele vya jamii vinavyohitaji kushughulikiwa kwa kutumia rasilimali zilizopo. Mipango husaidia katika kugawanya rasilimali na utekelezaji wa kila shughuli iliyopo kwenye mpango. Mpango shirikishi ni zana ya kuusadia uongozi wa taasisi ili uweze kusimamia shughuli za maendeleo na kutoa huduma kwenye Serikali za Mitaa.

Mipango shirikishi humaanisha kwamba wadau, walengwa, wataalamu, washitiri wa maendeleo, watunga sera hukaa kikao/vikao vya pamoja kuchambua, kujadiliana, kukubaliana na kuweka mkakati au mpango wa pamoja. Kwenye ngazi za msingi za Serikali za Mitaa kama vile Kijiji katika Tanzania, mipango shirikishi inahusisha Kamati ya Kijiji, Maafisa Ugani wote wa Kijiji, wanakijiji, na marafiki wa maendeleo. Wadau wote hawa, hujaribu kuchambua hali halisi iliyopo, kukubaliana juu ya hali njema tarajiwa, kukubaliana juu ya hatua muafaka za kuchukua ili kufikia hali njema tarajiwa, mikakati ya utekelezaji, kujadili na kukubaliana kuhusu mgawanyo wa majukumu, muda hadi mradi kukamilika, na vipindi vya utekelezaji.

Azma ya mpango shirikishi jamii ni kujenga uhusika halisi na wa haki wa kila mdau katika maamuzi ya rasilimali, matumizi mazuri ya raslimali za asili, kufikia muafaka na makubaliano juu ya mustakabali wa maisha ya jamii husika, kuhakikisha maoni na mahitaji ya makundi mbali mbali ya kijamii yamezingatiwa ndani ya mpango, jamii kumiliki mchakato, uwekezaji na uendelevu wa mradi hata baada ya muda wa utekelezaji kuisha.

Katika sura hii, visa mkasa vinne kuhusu ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa huduma vimewasilishwa. Halmashauri ya Ileje ina kisa mkasa kuhusu mipango shirikishi jamii, uwekaji vipaumbele, utekelezaji wa miradi shirikishi jamii inayogusa mahitaji halisi ya jamii, tena kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii, uzoefu na ujuzi wa jamii yenyewe. Ni mfano halisi wa maendeleo ya jamii asilia kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa daraja la mawe ili kutatua tatizo la vivuko.

Jiji la Mwanza ni kisa mkasa kuhusu uzoaji taka shirikishi, Jiji limetumia ushitiri wa sekta ya umma na sekta binafsi. Linahusisha ubunifu wa kufanya uskauti wa kukagua usafi kwa kutumia kampuni binafsi (Sherifu) kukamata wakiukaji na kwa kutumia kamera za siri. Halmashauri ya Nzega ina kisa mkasa kuhusu usafi wa mazingira kwenye Kata ya Mambali ambacho kilipelekea jamii kubadili fikra, hali, tabia , utamaduni na desturi potofu za kutotumia vyoo na kuanza kuchimba na kutumia vyoo kwenye Vijiji vinne. Mwisho, Halmashauri ya Igunga ina kisa mkasa kinacholenga usimamizi imara wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye huduma za afya kama njia mbadala ya kupata fedha za kutoa huduma za afya kwa jamii, kwani bajeti yake siku zote haitoshelezi mahitaji.

Masomo makuu tunayojifunza kutokana na visa mkasa vilivyopo kwenye sura hii yanaonesha kwamba:

- Maendeleo ya watu yataletwa na watu wenyewe. Kwa mantiki hiyo Tanzania haipaswi kuendelea kutegemea misaada na rasilimali za kutoka nje, bali kuna haja ya kutekeleza maendeleo asilia kwa njia shirikishi.
- Kama ikitumika njia muafaka katika kuwashirikisha watu, jamii ya Watanzania imekwishaamka ili kujiletea maendeleo yao.
- Tanzania bado hatujatumia rasilimali zetu za asili inavyopasa. Bado zipo rasilimali nyingi zinazohitaji ubunifu tu na kuanza kuzitumia. Tanzania haipaswi kuendelea kufikiri kwamba taka siku zote ni kitu kibaya na kisicho na faida, ni muhimu kuzichukulia taka kama rasilimali kwa kuanza kuzitenga taka kwenye makundi mbalimbali tangu zinakozalishwa, na kurudisha baadhi kwenye matumizi mbadala mfano plastiki, chupa, vyuma na kuzalisha gesi kutokana na taka.
- Ufanisi katika huduma za kuzoa na kutupa taka huenda sambamba na upangaji mzuri wa Mipango Miji; utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo, kanuni, makubaliano na maelewano ili kujenga utii wa sheria bila shuruti.
- Ushitiri kati ya sekta binafsi na sekta ya Umma maarufu kama PPP ni wa muhimu sana kwenye huduma shirikishi jamii. Sekta binafsi, vikundi vya kiraia lazima vihusike ipasavyo katika kuboresha utoaji wa huduma.

# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

## UDHIBITI WA FOLENI NA MSONGAMANO WA MAGARI MIJINI



*Uzoefu wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza*

## 1.0 UTANGULIZI

Jiji la Mwanza lipo kwenye fukwe za kusini za Ziwa Victoria Kaskazini Magharibi mwa Tanzania. Jiji lina eneo la $Km^2$ 1,325, kati ya hizo $Km^2$ 900 zimefunikwa na Maji sawa na 67% na $Km^2$ 425 ambazo ni 33% ni nchi kavu. Kati ya hizi $Km^2$ 425 za nchi kavu, takriban $Km^2$ 173 ni Mji na maeneo yaliyobaki ni misitu, mabonde, mashamba na milima yenye majani na miamba. Maeneo ya milima yana mawe na matuta ya miamba ya granites na granodiorite yanayopanda taratibu na kutengeneza milima mikubwa kiasi iliyotengana ikiambatana na mawe makubwa yaliyosimama. Maeneo mengine yana udongo wenye mchanga usiotuwamisha maji utokanao na kusagika kwa miamba. Uoto wa asili ni wa aina ya savanna wenye miti mirefu iliyotawanyika na majani marefu. Jiji la Mwanza lipo katika urefu wa meta 1,140 juu ya usawa wa bahari. Wastani wa hali ya joto ni kati ya 25.7oC na 30.2oC msimu wa joto na kati ya 15.4oC na 18.6oC msimu wa baridi.

Kiutawala Jiji la Mwanza lima Wilaya mbili ambazo ni Nyamagana na Ilemela. Kuna Kata 21 (kata 12 zipo Nyamagana na Kata 9 zipo Ilemela) zenye madiwani waliopo chini ya uongozi wa Bwana Meya. Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonyesha Jiji la Mwanza lina watu 363,452, kati yao 177,812 ni wanaume na 185,640 ni wanawake (hii inahusu wilaya ya Nyamagana tu). Ukuaji wa idadi ya watu kwa mwaka ni 3.0% (Sensa ya Watu na Makazi, 2012). Wastani wa wakazi wa kaya ni 4.7 ambao upo karibu sana na wastani wa kitaifa wa 4.8. Hii inaonyesha kuwa Jiji la Mwanza lina Msongamano mkubwa wa watu unaofanya kuwepo na umiliki mkubwa wa vyombo vya moto vya usafiri na msongamano mkubwa wa vyombo hivi jijini.

Halmashauri ya Jiji la Mwanza in jumla ya mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 866.2073 za aina mbali mbali kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali 1 hapa chini. Kwa wastani, mtandao huu wa barabara hubeba takriban vyombo vya usafiri 2,300 kwa siku (ilikuwa Januari 2014). Ongezeko hili la kasi la vyombo vya usafiri jijini ndio chanzo cha kukwama mara kwa mara kwa magari yanayotembea na kusababisha misongamano mikubwa ya magari kwenye barabara za jiji. Msongamano wa magari hutokea pale magari yanapotembea kwa mwendo mdogo ulio chini ya km 20 kwa saa kwa sababu ya uwepo wa magari mengi zaidi ya barabara zinavyoweza kubeba.

**Jedwali 1: Mtandao wa Barabara za Jiji la Mwanza**

| N | Aina ya Barabara | KM |
|---|---|---|
| 1 | Lami | 61.000 |
| 2. | Changarawel | 101.580 |
| 3. | Udongo | 699.693 |
| 4. | Zege | 1.270 |
| 5. | Mawe | 2.530 |
| **Jumla** | | **866.073** |

**Chanzo: taarifa ya Utambulisho wa Jiji la Mwanza**

## 2.0 TATIZO

Jiji la Mwanza lilianza kukumbwa na ongezeko la watu na makazi na hatimaye misongamano ya magari barabarani tangu miaka ya 1990 hasa kutokana na matatizo ya miundombino duni na bajeti ndogo ya barabara za Jiji. Msongamano wa magari uliongezeka zaidi kutokana na Magari makubwa ya biashara na mabasi kulazimika kupita katikati ya jiji kwenye watu na magari mengi hali

iliyopelekea Jiji kuwa na mazingira mabaya, foleni ndefu za magari, viwango vya juu vya ajali na kuongezeka kwa muda wa watu kusafiri jijini.

Katika miaka ya hivi karibuni msongamano wa vyombo vya usafiri umechochewa zaidi na ukuaji wa matumizi ya pikipiki zijulikanazo zaidi kama *Bodaboda*. Mwendo wa magari jijini pia uliathiriwa sana na makutano mengi ya magari yanayopishana, ukosefu wa taa za kuongoza magari barabarani, barabara nyembamba, nafasi chache za maegesho ya magari, uegeshaji hovyo wa daladala na ongezeko la watumiaji wa *Bodaboda*. Picha hii hapa chini inaonyesha hali halisi ya msongamano wa magari katika barabara za jiji.



***Daladala katika eneo la Buzuruga kuelekea Mjini***

Msongamano wa magari katika Jiji la Mwanza ulitokana na mafanikio katika ukuaji wa uchumi, upatikanaji wa ajira, ujenzi wa majengo na sera za kijamii zilizowavutia watu wengi kuishi na kufanya kazi jijini. Makampuni mengi ya kibiashara (ya ndani na ya kimataifa) pia yalijiunga katika hili ili kupata faida za uzalishaji na ukuaji wa jiji la Mwanza. Hivyo idadi ya magari iliongezeka sana kutoka magari 200 kwa siku mwaka 1990 hadi kufikia takriban magari 2300 yanayopita jijini kwa siku moja, Januari  mwaka 2014. Kwa sasa (2014) jiji la Mwanza lina Daladala 965, kila daladala ikifanya wasatani wa mizunguko minne kutoka mjini na kurudi. Hii inafanya jumla ya idadi ya daladala kufikia 3860 kwa siku na takriban magari makubwa 430 yanayoingia Jijini kwa siku.

Msongamano na kukwama kwa magari pia kumezidishwa na wembamba wa barabara zilizopo kwenye mtandao wa barabara wa takriban km 28 katikati ya jiji ambazo haziwezi kubeba idadi kubwa ya magari, yaani magari 2300 kwa siku. Hali ilitokea kuwa mbaya sana kutokana na barabara ambazo zilitakiwa kuwa na njia mbili au zaidi kila upande zina njia moja tu, na zimebanwa na majengo na maegesho ya kiholela katika pande zote za barabara hizo. Gharama za kupanua barabara hizi ni kubwa sana kwani itatakiwa kubomoa majengo yote yaliyo pembezoni mwa barabara na kuwafidia wamiliki. Kutokana na haya yote, pamoja na ukosefu wa fedha za kukabiliana na changamoto hizi, Jiji la mwanza lilizama katika katika tatizo kubwa la Msongamano Mkubwa na Kukwama kabisa kwa mwendo wa magari jijini.



*Barabara ianyoruhusu pande mbili za magariikiwa na njia moja kila upande*

## 3.0 LENGO

Baada ya kushuhudia tatizo la kuongezeka kwa kukwama kwa magari na msongamano mkubwa kwa miaka zaidi ya kumi, Jiji la Mwanza liliamua kupangua na kupanga upya mwenendo wa magari katika Jiji ili kupunguza muda wa wakazi wa Jiji wanaotumia kusafiri katika barabara za jiji ifikapo mwaka 2015. Malengo mahususi ya uamuzi huu wa gharama sana yalikuwa;

- Kuboresha miundombinu ya barabara kutoka barabara za udongo na changarawe na kuwa za lami.
- Kupanua barabara za jiji kwa kuondoa vibanda, vioski na maduka yaliyokuwa kwenye hifadhi za barabara pamoja na kuanzisha maegesho rasmi ya magari.
- Kupunguza au kuondoa kabisa msongamano wa magari jijini ili kuwapatia fursa wakazi wa jiji kusafiri kwa muda mfupi jijini.
- Kuzuia na kutokomeza kabisa uendeshaji holela wa magari Jijini

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO – MIKAKATI NA SHUGHULI

Hatua za kawaida zilizopo (kwa upande wa watoa huduma) za kudhibiti msomgamano wa magari zimegawanyika katika maeneo makuu mawili yaani kuongeza miundombinu mipya na kuboresha miundombino iliyopo. Miundombinu mipya ya usafirishaji inayoweza kuongezwa ni ujenzi wa barabara mpya, kuweka mitambo ya kuongoza magari, kuongeza idadi ya njia katika barabara zilizopo, kujenga madaraja ya juu na ya chini mwa barabara katika maungio ya barabara kuu na kwenye misongamano na kujenga barabara za mchepuko. Mfumo bora wa kudhibiti msongamano wa magari unaweza kupatikana kupitia uanzishaji wa barabara za mwelekeo mmoja tu, kupiga marufuku kugeuza magari, kuanzisha njia za kugeuzia magari, kuboresha matumizi ya alama za barabarani, utoaji wa taarifa za safari za magari, kuchukua hatua haraka za ajali zitokeazo barabarani na kushughulikia matukio maalum na kazi za barabarani zinazoleta msongamano na kukwama kwa magari. Kwa upande wa watumiaji msongamano wa magari unaweza kudhibitiwa kwa kuanzisha usafiri wa umma wa ubora wa hali ya juu ambao utapunguza magari ya watu binafsi barabarani. Jitihada hizi pia zinajumuisha kudhibiti uegeshaji holela wa magari, kusimamisha magari hovyo pembezoni mwa barabara au barabarani na kuanzisha na kuhamasisha matumizi ya njia panda, tozo za msongamano, matumizi ya pikipiki na baiskeli, utembeaji na uanzishaji wa muda mbadala wa masaa ya kazi.

Katika kuondoa changamoto za Msongamano wa magari mijini, Jiji la Mwanza lilitekeleza mikakati na shughuli nyingi. Mikakati hii ilibuniwa ili kuboresha miundombinu ya mjini, kudhibiti maegesho holela na kuongeza kasi ya mwendo wa magari katika jiji. Mikakati hiyo imeelezwa kwa muhutasari kama ifuatavyo;

(i) Hatua ya ubunifu na uundaji wa mfumo huu iliyofanywa na Mhandisi wa Zamani wa Jiji (Mhandisi Emmanuel Kalobelo ambaye ni mtaalam wa masuala ya msongamano wa magari mijini). Hatua hii ilijumuisha kuboreshwa kwa ramani za jiji za barabara, kutambua maeneo yenye msongamano na mwendo wa magari chini sana na kuainisha vibanda, vioski na majengo mengine yaliyopo kwenye hifadhi za barabara za jiji, n.k.

(ii) Kuanzisha mizunguko mipya ya Daladala na vituo vya mabasi na kuainisha maenesho ya kutengenezea magari, maeneo ya maegesho na vituo vya bishara



***Maegesho ya Daladala Jijini  Mwaka 2011***

(iii) Utumiaji na ufuatiliaji wa sheria ndogo kwa ajili ya utekelezaji fanisi wa kuondoa msongamano wa magari jijini. Sheria ndogo iliyotungwa mwaka 2002 ilijikita katika matumizi fanisi ya mtandao wa barabara za Jiji na aina zote za vyombo vinavyotembea, vyombo vinavyoegeshwa na watumiaji wengine wa barabara.



***Mikokoteni iliyoondolewa katikati ya jiji mwaka 2006/07***

(iv) Uanzishaji wa stendi kubwa za mabasi nje ya eneo la kati la kibishara la Jiji. Hizi ni stendi za Buzuruga na Nyegezi.

(v) Ujenzi wa barabara za mawe katika makazi ambayo hayajapangwa kurahisisha usafirishaji.

(vi) Kuimarisha skimu za ushirikiano na sekta binafsi kama Televisheni ya Barmeda na Benki ya CRDB, idara ya polisi wa barabarani na waendeshaji huduma za maegesho.

(vii) Kufungua na kuboresha barabara zote za michepuko ili kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara kuu.

(viii) Mipango isiyokoma ya kupanua mtandao wa barabara, kuanzisha stendi za mabasi mbili, kuongeza idadi ya njia katika barabara kuu, kuanzisha vituo vya mikutano vyenye maegesho ya magari, kuanzisha usafiri wa uma unaomilikiwa na halmashauri ya jiji, ujenzi

wa miji ya satelaiti, na utungaji wa sheria ndogo inayolazimisha ujenzi wa magorofa kuwa na maegesho ya magari.

(ix) Katika kuboresha miundombinu ya mjini, programu na shughuli zifuatazo zimetekelezwa. Programu ya Miji mkakati ya Tanzania (TSCP) imetekelezwa na kuleta maboresho katika barabara za mzunguko na mchepuko. Barabara hizi ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Pasiansi – Buzuruga yenye km 7.23, Sanga – Kiloleli yenye km 1.30, Liberty yenye km 0.20, Mzunguko wa Pepsi wenye km 1.40, Mkuyuni – Butimba yenye km 4.2. na Mzunguko wa Tunza – Uwanja wa Ndege yenye km 4.40; zilizojengwa mwaka 2013.




***Ujenzi wa barabara ya Pasiansi – Buzuruga yenye km 7.32 mwaka 2012 kwa kiwango cha lami***

(x) Kubuni na kujenga madaraja ya juu ya waenda kwa miguu. Ujenzi wa daraja la juu la waenda kwa miguu katika eneo la Mabatini na upanuzi wa barabara ya Mwanza – Musoma kutoka katikati ya Jiji hadi Buzuruga kwa kuifanya kuwa na njia tatu badal ya mbili unaofanywa na Wakala wa Barabara (TANROADS).



***Daraja la watembea kwa miguu na upanuzi wa barabara uliofanywa na TANROADS Mkoa, mwaka 2013***

(xi) Kuanzisha tozo za maegesho ya magari katika eneo lote la kati na la kibiashara jijini na kutumia mawakala wanaoshindanishwa katika kukusanya ada za maegesho.

(xii) Kuanzisha barabara za mwelekeo mmoja wa magari jijini. Hizi ni barabara za Rwagasore, Lumumba, Regional Drive na Sheikh Amin

## 5.0 AINA NA KIASI CHA RASLIMALI ZILIZOTUMIKA

Katika kutekeleza mikakati na shughuli hizi Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilitumia raslimali nyingi za fedha, watu na muda.

**Raslimali Fedha**
Katika mwaka wa fedha 2011/2012 – 2012/2013 Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilitumia shs bilioni 16.0 kwa kuboresha barabara za mjini. Fedha hizi ni mkopo toka Benki ya Dunia. Muda wa kutumia mkopo huu katika kujenga, ukaguzi na utambuzi wa kasoro za ujenzi ni miezi 40.

Kuhusu ujenzi unaoendelea wa daraja la juu la waenda kwa miguu katika eneo la Mabatini na upanuzi wa barabara ya Mwanza – Buzuruga, TANROADS walipata fedha toka Bodi ya mfuko wa barabara zenye jumla ya shs bilioni 1.2850.

Uanzishaji wa tozo za maegesho ili kupunguza msongamano wa magari na uegeshaji holela mjini unaendeshwa na wakala ambaye hukusanya ada kwa wamiliki wa magari. Tozo hizo ni shs 600 kwa gari moja saa moja kwa magari madogo na shs 1,000 kwa gari moja kubwa (malori) kwa saa moja. Jitihada hii huongeza mapato ya jiji kama inavonyeshwa kwenye jedwali Na.1 kwenye viambatisho. Jedwali linaonyesha tozo za maegesho na kiasi gani kilikusanywa mwaka 2012/2013 na makisio ya makusanyo kwa mwaka 2013/2014.

**Raslimali Watu, Vitu na Muda**
Aina nyingine ya raslimali zilizotumika katika kuboresha mwenendo wa magari mjini ukiacha fedha ni raslimali watu. Katika kutekeleza maboresho haya Halmashauri ya Jiji na TANROADS walitumia wakandarasi binafsi na katika kusimamia maegesho ya magari na ukusanyaji wa ada za maegesho Jiji linatumia wakala ambaye ana watumishi 32 wanaokuwepo katika eneo lote la kati la kibiashara la Jiji.

Halamshauri ya Jiji la Mawanza ina wahandisi saba waliobobea na Mfundi wane katika idara ya Ujenzi na Miundombinu. Kati ya hawa watumishi wahandisi wanne na mafundi wawili hushughulika na usimamizi na ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji ya jiji tu. Pia halmashauri ya Jiji ina maafisa watatu wa Mipango Miji ambao husaidia utaalam katika maendeleo ya Jiji, kudhibiti na kushiriki katika kuandaa ramani kuu mpya ya jiji.

## 6.0 MATOKEO YA JITIHADA

Kwa ujumla imekuwa ikijengwa hoja kuwa tatizo la Msongamano wa magari katika miji haliwezi kuondolewa kabisa ila linaweza kupunguzwa tu kufikia viwango vinavyokulbalika. Tena kiuhakika hakuna suluhisho moja katika kufikia hili. Ili kupunguza msongamano wa magari, jiji lilitumia mbinu kuu tatu. Hizi zilihusu kushughulika na upande wa watoa huduma yaani kuchukua hatua stahiki zinazoongeza na kuboresha uwezo na ufanisi wa miundombinu ya usafirishaji, kufanyia kazi upande wa watumiaji wa huduma yaani kuchukua hatua zinazopunguza matumizi ya magari mjini, kupunguza matumizi ya mikokoteni katikati ya jiji na mwisho kabisa kuimarisha mipango miji ili kuwepo na mgawanyo mzuri wa matumizi ya ardhi na miundombinu katika jiji la Mwanza. Kutokana na mikakati hii matokeo yafutayo yaliweza kupatikana.

- Mizunguko mipya ya magari arobaini (40) imeanzishwa katika jiji, na hasa mizunguko ya Daladala.

- Hifadhi zote za barabara na maeneo ya pembezoni mwa barabara ni wazi kabisa na masafi. Hakuna biashara wala vioski pembezoni mwa barabara au kwenye njia za waenda kwa miguu zilizo barabarani.




***Njia za waenda kwa miguu zikiwa wazi kabisa bila biashara wala vioski katikati ya jiji***

- Eneo lenye taa za usiku barabarani limeongezeka sana na kuboresha usalama wa kutumia barabara masaa ya usiku.



***Taa za usiku katika barabara ya Mkuyuni – Butimba mwaka 2013/2014***

- Karakana 22 na mauzio ya mbao 56 yamehamishwa kutoka katikati ya jiji na kupelekwa viwanja vya sabasaba vilivyopo barabara ya Makongoro/airport.
- Usafishaji wa barabara umekuwa rahisi sana ikilinganishwa na huko nyuma kwa sababu sababu pembezoni mwa barabara na njia za waenda kwa miguu ni wazi kabisa na safi.



***Usafishaji wa barabara ukiendelea***

- Uwezo wa miundombinu umeongezeka. Kwa mfano kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 km 18.33 za barabara za lami zilijengwa ndani ya jiji na km 23.0 zilikarabatiwa na kuboreshwa.



*Ukarabati wa barabara ukiendelea*

- Km 1.96 za barabara za udongo zimeboreshwa kwa kujengwa na mawe katika maeneo korofi yenye miinuko mikali na kurahisisha sit u usafirishaji bali pia kuleta mandhari nzuri katika viunga vya jiji.





*Ujenzi wa barabara kwa mawe*

- Jumla ya km 1.80 za barabara ya Mwanza – Musoma imepanuliwa na kuwa njia tatu na ambayo imepunguza msongamano wa magari kwa viwango vya kuridhisha.
- Msongamano wa Magari umepunguzwa sana kwa kuchepusha magari kutoka Nyakato na Igoma kwenda uwanja wa ndege bila kupitia katikati ya jiji kama ilivyokuwa hapo mwanzo.



*Barabara iliyowazi bila msongamano wa magari*

- Ujenzi wa barabara ya Buzuruga – Pasiansi kwa kiwango cha lami



Ujenzi wa barabara ya Buzuruga – Pasiansi



Uwekaji wa lami katika barabara ya Buzuruga – Pasiansi

Kupitia kwa mikakati ya upande wa watumiaji wa huduma na hasa katika utumiaji wa magari, watumiaji wa barabara wamepokea mfumo wa kufuata taratibu za maegesho ya mjini ili kuruhusu magari mengine kuendelea na safari na mizunguko. Tafadhali zingatia kuwa mabasi ya kubeba abiria Jijini Mwanza yaliongezeka toka 230 mwaka 2010 hadi kufikia 965 desemba mwaka 2013 (Chanzo: SUMATRA – MZA). Utekelezaji wa mikakati ya upande wa watumiaji wa huduma ulizaa matokeo dhahiri yafuatayo;

- Hakuna tena wapiga debe wa daladala kwenye vituo vipya na vya zamani vya mabasi vilivyopo katikati ya jiji.
- Matumizi ya Mikokoteni midogo midogo katikati ya Jiji imepungua sana. Matumizi ya mikokoteni midogo midogo hupunguza kasi ya magari barabarani na ni kero katika maeneo ya kati ya mijini yenye watu wengi hapa Tanzania. Kero hii imeondolewa kabisa katika Jiji la Mwanza.
- Uanzishaji wa barabara za mwelekeo mmoja wa magari umepunguza sana ajali za barabarani, umeimarisha uendeshaji salama wa magari na umechangia sana matumizi mazuri ya muda na wakazi wa Jiji; muda waliokuwa wakiupoteza katika msongamano.
- Halmashauri ya Jiji inaendelea kupata ongezeko la mapato ya kutikisa kutokana na ada za maegesho na faini wanazotozwa wale wanaoegesha magari kiholela ndani ya jiji. Kwa mwaka 2012/2013, jiji lilikusanya takriban shs 307,800,000.00 na mpaka Desemba katika mwaka wa fedha 2013/2014 tayari halmashauri ilikuwa imeshakusanya shs 117,600,000.00 kutoka kwenye ada na faini za maegesho. Halmashauri ya Jiji lilikisia kukusanya shs 506,400,000.00 mpaka Juni 2014. Hili ni tokeo kuu katika eneo la mapato ya Halmashauri.
- Ujenzi wa barabara za mawe umetengeneza na kuongeza fursa za ajira kwa wakazi wa jiji, hasa Vijana. Ujenzi wa barabara kwa mawe hutumia vifaa vya asili na hauzalishi taka hata kidogo. Matumizi ya vifaa na teknolojia asilia huongeza ajira katika jamii husika kupitia mafundi wenyeji na ziada ya nguvukazi iliyopo Jijini.



*Ajira – Vijana wakipasua mawe kwa ajili ya ujenzi wa barabara*

## 7.0 CHANGAMOTO WA UTEKELEZAJI

Jitihada za kuondoa msongamano wa magari siyo jukumu rahisi kwa hapa Tanzania. Majiji na Miji mingi imetumia mikakati mbalimbali na haikuweza kuwa fanisi. Katika mchakato wa kutekeleza mikakati ya pande zote mbili za utoaji huduma na upokeaji wa huduma jiji la Mwanza limekumbana na changamoto nyingi. Hizi ni pamoja na;

(i) Upungufu wa nafasi za maegesho katika eneo la kati la kibishara la Jiji. Barabara nyingi zinakosa nafasi za kutosha za maegesho na hakuna nafasi za hifadhi za barabara kwa ajili ya maegesho. Hili hufanya magari kuegesha pembezoni mwa barabara za jiji na hatimaye kuzibana.

(ii) Mipango miji iliyo duni hasa upande wa miundombinu kama vile upana wa barabara na makutano ya barabara ambayo hayana nafasi za kutosha kutoa njia za ziada ili kuruhusu mwendo mzuri wa magari.

(iii) Upungufu mkubwa wa fedha za kuwezesha kuweka mifumo mizuri ya kudhibiti magari yaliyopo barabarani hasa wakati wa asubuhi na jioni ambapo kuna msongamano zaidi.

(iv) Upungufu wa wataalam kama Maafisa Mipango wa Usafirishaji na Wahandisi wa Msongamano wa Magari katika Halmashauri. Kwa mfano, Halmashauri ya Jiji haina kabisa mhandisi wa msongamano wa magari ambaye ni muhimu sana kwa udhibiti wa mwenendo wa magari na watumiaji wengine wa barabara ili kuleta matumizi bora kabisa ya barabara na miundombinu mingine ya usafirishaji ya Jiji.

(v) Hakuna muunganiko dhahiri na unaofanya kazi ulioundwa kati ya Mipango ya Usafirishaji Jijini na Mipango Miji ili kujiridhisha kwamba ukuaji wa Jiji utakuwa wa pamoja kwa ujumla wake. Maendeleo mapya na makubwa katika majengo, viwanda na maduka katika Jiji la Mwanza yanahitaji kiungo (daraja) imara kati ya mipango ya usafirishaji na mipango miji ili kudhibiti matatizo zaidi ya msongamano wa magari siku zijazo.

(vi) Halmashauri ya jiji la Mwanza haina mtaalam wa mipango ya usafirishaji, ambaye ni muhimu sana katika kupima na kutambua mahitaji ya vyombo vya usafiri na kushauri mapema kuhusu michakato na namna mpya za usafirishaji wenye tija.

## 8.0 MIKAKATI ILIYOTUMIKA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Changamoto zilizoikumba Halmashauri ya Jiji la Mwanza katika kuboresha mwenendo wa vyombo vya usafiri mjini hazikufanya jitihada hii kukoma. Mikakati mbalimbali imetumika kukabili madhara ya changamoto hizi. Mikakati hii ni pamoja na;

(i) Kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuendelea kuboresha na kutunza miuondombinu ya mtandao wa barabara za Jiji.

(ii) Kutumia mapato ya ndani kukarabati na kuongeza ubora wa matandao wa barabara. Hii pia inajumuisha kujadiliana na Bodi ya Mfuko wa Barabara ili kulipia maboresho na uongezaji wa ubora wa barabara kuu zinazopita Jijini.



*Ukarabati wa barabara ya Pamba Ukiendelea mwaka 2012 kwa fedha za Halmashauri*

(iii) Kuimarisha Mkakati wa Ukusanyaji na Uendeshaji wa Tozo za Maegesho ya Magari hasa katika barabara zilizoboreshwa katika eneo la kati la kibiashara la jiji ili kuboresha mwenendo wa magari.

(iv) Kupeleka wahandisi wawili kwenye mafunzo ya Uhandisi Jamii katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT) na wabobee katika Uhandisi wa Usafirishaji. Hawa watasadia halmashauri katika mipango na usimamizi wa usafirishaji jijini.

## 8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Halmashauri ya Jiji la Mwanza imelenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuendelea kutoa huduma za usafirishaji Jijini kwa ufanisi na uendelevu. Kwa nia hii Halmashauri imeweka mkakati wenye vipengele vilivyotajwa hapa chini;

(i) Mpango halisi wa kuanzisha usafiri wake wa umma (yaani kumiliki mabasi ya kisasa na mitambo ya usafirishaji) Jijini na kuanzisha mabasi makubwa ambayo kubeba watu wengi mara moja badala ya daladala binafsi. Zinahitajika si chini ya Dola za Kimarekani 1,250,000 kwa kuanzia.

(ii) Halmashauri ina mpango wa kujenga Jengo la kisasa la ghorofa saba lenye maegesho katikati ya jiji litakalotumiwa na vyombo mbalimbali vya usafiri vya kibiashara kati ya 250 – 300 kwa siku. Michoro ya awali inaonyesha ;mradi huu utagharimu takriban shs 1,250,000.00 milioni.

(iii) Halmashauri pia imepanga kuanzisha Miji katika viunga vya Jiji (satelaiti) iantojitegemea kabisa kihuduma na sio Miji Mabweni (Domitory) katika Kata (maeneo) za Buhongwa, Nyamhongolo na Luchelele.

(iv) Halmashauri inaanzisha maegesho ya magari makubwa yenye eneo la hekari nane Buhongwa na hekari saba Nyamhongolo. Baada ya kukamilika kwa maegesho haya hakuna magari makubwa yanayozidi tani 10 yatakayoruhusiwa kuingia katika eneo la kati la kibiashara. Zoezi hili litagharimu takriban shs bilioni tatu (3.0).

(v) Halmashauri imedhamiria kujenga barabara nyingine kuu na za mzunguko. Kwa mfano ujenzi wa barabara ya Mkuyuni – Maina – Nyakato (Kiwanda cha Nilepich) yenye km 23.7 kwa kiwango cha lami, barabara ya Isamilo – Mji mwema inanyounganisha eneo la kati la jiji na Manispaa ya Ilemela katika sehemu ya barabara ya Sanga – Kiloleli, barabara ya

Bugando – Bugarika – Mwananchi, barabara zenye maegesho kama za Sukuma, Bomba, Pamba, Uzinza, Hekalu (Temple), Vijana, Regasore – Lumumba, Mchepuko wa Kamanga na Capripoint, Mabatini – Nyamunge – Nyasaka (kwenye makutano na barabara ya Pasiansi – Buzuruga). Ujenzi huu utagharimu takriban dola za kimarekani 27,000,000.00 chini ya program ya TSCP kwa mwaka 2014/2015.



***Barabara zilizoboreshwa na zitakazoboreshwa kwa mradi wa TSCP mwaka 2014/2015***

(vi) Halmashauri ipo katika hatua za mwisho za kutunga sheria ndogo ambazo zitasaidia kuhimiza na kulazimisha kila ghorofa refu Jijini liwe na maegesho yake kama siyo ndani ya Jengo basi nje kuwe na eneo la maegesho ya magari la kutosha.

(vii) Halmashauri imejizatiti kujenga madaraja na njia za juu katika makutano ya barabara ndogo na zile barabara kuu tatu zinazoingia eneo la kati la Jiji


***Daraja la juu la waenda kwa miguu lililopo Mabatini***

(viii) Halmashuri ya Jiji imeandaa mkakati wa kuendelea kuboresha bila kukoma usimamizi wa ubinafsishaji wa ukusanyaji wa ada na udhibiti wa magari katika maegesho.

## 9.0 SIRI ZA MAFANIKIO

Mafanikio katika mpango huu wa kudhibiti msongamano wa mgari mijini katika Jiji la Mwanza hayakutokana kwa urahisi na mipango ya kawaida ya Halmasahuri na utekeliezaji wake. Kuna siri kuu zilizojificha zinazoambatana na mafanikio haya. Baadhi ya siri hizi zimetajwa kwa muhtasari hapa chini kwa lengo la kujifunza na kuiga.

- Ushirikiano wenye ubora wa juu kati ya TANROADS na Halmashauri ya Jiji ambao umeleta upanuaji wa barabara ya Musoma ambayo imepunguza sana kukwama na msongamano wa magari kwenye barabara hiyo. Pia ujenzi wa daraja la juu la waenda kwa miguuu katika eneo la Mabatini limepunguza uwezekano wa ajali hasa kwa waenda kwa miguu wanaokatisha barabara hiyo.
- Ushirikiano thabiti na ofisi ya Mkoa ya Usalama Barabarani. Halmashauri imeweza kuanzisha kamati ya usafirishaji ya jiji ambayo hukutana mara kwa mara kujadili maswala ya usalama barabarani, usafiri na masuala yote ya usafirishaji ndani ya jiji (kimsingi hukutana mara moja kwa mwezi).
- Uwepo wa fedha na matumizi mazuri ya fedha za Benki ya Dunia na DANIDA vilirahisisha ujenzi thabiti na fanisi wa barabara za lami ndani na nje ya eneo la kati la kibiashara. Hii imepunguza muda wa safari uliokuwa ukitumiwa na watumiaji wa barabara na kuongezeka kwa muda wa uzalishaji na kuboreshwa kwa shughuli za kiuchumi.
- Matumizi ya redio ya Jiji 90.2 (City Radio FM 90.2) kutangaza masuala na matatizo ya mwenendo wa magari jijini hasa wakati wa msongamano na ajali na kuwaarifu watu kubadili barabara imechangia sana mafanikio ya mpango huu.
- Ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) hasa na Televisheni ya Barmedas. Stesheni hii ya televisheni ina kamera jijini na zinatumika kudhibiti mwenendo wa magari. Televisheni hii pia hutangaza matatizo mbalimbali ya msongamano wa vyombo vya usafiri na njia zilizo wazi pamoja na muda wa kutua na kuondoka kwa ndege mbalimbali katika uwanja wa ndege wa Mwanza. Pia taarifa za msongamano wa vyombo vya usafiri huonyeshwa katika vioo vya televisheni vilivyopo katika maeneo ya umma ya Jiji.

## Table No. 1 Parking Charges and revenues in the CBD for 2013/2014

| S/N | STREET NAME | OBSERVED PARKED VEHICLES PER PER DAY | PARKING FEES PER DAY | REVENUES PER DAY | REVENUES PER YEAR |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Liberty | 94 | 600 | 56,400.00 | 1,692,000.00 |
| **2** | Mkurumah | 44 | 600 | 26,400.00 | 792,000.00 |
| **3** | Nkomo | 27 | 600 | 16,200.00 | 486,000.00 |
| **4** | Bantu | 60 | 600 | 36,000.00 | 1,080,000.00 |
| **5** | Shinyanga road | 26 | 600 | 15,600.00 | 468,000.00 |
| **6** | Nyerere | 72 | 600 | 43,200.00 | 1,296,000.00 |
| **7** | Balewa | 25 | 600 | 15,000.00 | 450,000.00 |
| **8** | Rufiji | 41 | 600 | 24,600.00 | 738,000.00 |
| **9** | Uhuru | 130 | 600 | 78,000.00 | 2,340,000.00 |
| **10** | Mbita/Mission | 17 | 600 | 10,200.00 | 306,000.00 |
| **11** | Rwagasore | 139 | 600 | 83,400.00 | 2,502,000.00 |
| **12** | Lumumba | 47 | 600 | 28,200.00 | 846,000.00 |
| **13** | Karuta | 63 | 600 | 37,800.00 | 1,134,000.00 |
| **14** | Kenyatta | 108 | 600 | 64,800.00 | 1,944,000.00 |
| **15** | Musoma road | 15 | 600 | 9,000.00 | 270,000.00 |
| **16** | Posta | 105 | 600 | 63,000.00 | 1,890,000.00 |
| **17** | Mahakama | 28 | 600 | 16,800.00 | 504,000.00 |
| **18** | Station | 70 | 600 | 42,000.00 | 1,260,000.00 |
| **19** | Miti mirefu | 45 | 600 | 27,000.00 | 810,000.00 |
| **20** | Pamba | 112 | 600 | 67,200.00 | 2,016,000.00 |
| **21** | Market | 26 | 600 | 15,600.00 | 468,000.00 |
| **22** | Mlango Mmoja | 10 | 600 | 6,000.00 | 180,000.00 |
| **23** | Makoroboi | 24 | 600 | 14,400.00 | 432,000.00 |
| **24** | Voil | 25 | 600 | 15,000.00 | 450,000.00 |
| **25** | Dubai nyuma | 15 | 600 | 9,000.00 | 270,000.00 |
| **26** | Sheik Amin | 28 | 600 | 16,800.00 | 504,000.00 |
| Sub Total | | **1,396** | | **837,600** | **25,128,000.00** |
| **Vehicles paying per month** | | 25 | 20,000.00 | 500,000.00 | 15,000,000.00 |
| **Reserved parking** | | 25 PLACES | 100,000.00 | 250,000.00 | 7,500,000.00 |
| **Penalty** | | 3 (ASSUMPTION) | 50,000.00 | 150,000.00 | 4,500,000.00 |
| Sub Total | | | | **1,737,600.00** | **27,000,000.00** |
| **GRAND TOTAL** | | | | | 52,128,000.00 |

**Source: City Council Budget 2013/2014.**

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

**UDHIBITI WA TAKA NGUMU ULIOGATULIWA**



*Uzoefu wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi*


**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni moja kati ya Halmashauri saba zinazounda Mkoa wa Kilimanjaro. Mji wa Moshi ulianzishwa mwaka 1892 katika eneo la Kolila, Old Moshi (lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Moshi) na kuhamishiwa kwenye eneo la sasa kutokana na kushindwa kwa garimoshi kupanda mlima mpaka Kolila. Mwaka 1926 Moshi ikawa Mamlaka ya Mji mdogo ulioendelea na kuwa Halmashauri ya Mji mwaka 1956. Tangu mwaka 1988 Moshi imebaki kuwa Halmashauri ya Manispaa.

**Eneo la Ardhi**

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi (MMC) hupakana na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa upande wa Kusini, Mashariki na Kaskazini na Halmashauri ya wilaya ya Hai kwa upande wa magharibi. Halmashauri hii ina mpango wa kumiliki eneo zaidi ili kufikia $Km^2$ 142 na hatimaye kufaulu kuwa jiji ifikapo mwaka 2015, Jiji likalo zingatia misingi ya Utawala bora.

**Mchoro 1: Ramani ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi**




**Idadi ya watu**

Mji wa Moshi ulianza na wakazi 8,048 mwaka 1948 waliongezeka hadi 13,762 mwaka 1957, 26,969 mwaka 1969 na 96,838 mwaka 1988 ulipo pandishwa kuwa Halmashauri ya Manispaa. Mwaka 2002 wakazi wa Manispaa ya Moshi walikuwa 144,336. Kutokana na sensa ya watu ya mawaka 2012 Manispaa ya moshi ina jumla wa wakazi 184,292 ambao kati yao 95,118 ni wanawake na 89,174 ni wanaume. Kipindi cha mchana Manispaa ya Moshi hupokea watu kati 76,000 na 85,000 wanaoingia kila asubuhi kwa sababu ya kibiashara na kurudi vijijini wakati wa jioni. Hawa hutokea katika Halmashauri zote zinazo izunguka Manispaa ya Moshi.

**Dira ya Manispaa ya Moshi**

Halmsahauri ya Manisapaa ya Moshi inatarajia kuwa modeli bora katika utoaji wa huduma za jamii, utoaji wa ushauri wa kitaalam na ujenzi wa uwezo wa wadau wote ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini ifikapo mwaka 2025. Dira hii inajumuisha kufikia Malengo ya Maendeleo ya Millenia na kuboresha utoaji wa huduma kwa kuwashirikisha wananchi katika kupanga na kutekeleza mipango kwa uendelevu kwa kipindi cha miaka kumi ijayo tangu 2005.

**Mgawanyiko wa Kiutawala**
Kiutawala Manispaa ya Moshi ina Tarafa 2, yaani Moshi Mashariki na Moshi Magharibi, Kata 21, Mitaa 60 na Kaya 41,345 ambazo zina wastani wa wakazi 5 kila moja. Manispaa ya Moshi inaunda jimbo moja la uchanguzi kwa uwakilishi Bungeni. Halmashauri ina Madiwani 29.

## 2.0 MATATIZO KABLA YA UGATUAJI WA UDHIBITI WA TAKA NGUMU

Kati ya mwaka 1990 na 2000, idadi ya watu katika Manispaa ya Moshi iliongezeka sana. Idadi ya wageni wa kila siku (kutoka Halmashauri zote Mkoani Kilimanjaro) wanaokuja katika eneo la kati la kibiashara kwa shughuli za kibiashara na kiuchumi pia iliongezeka sana. Ongezeko la wakazi toka mwaka 1948 mpaka 2000 limekuwa la kasi sana na kupelekea msongamano wa watu katika eneo la kati la kibiashara (CBD), kuongezeka kwa makazi holela na kuzidi kwa shughuli za kiuchumi. Haya yote yakaleta uzalishaji mkubwa wa taka ngumu kutoka tani 100 mwaka 2000, tani 145 mwaka 2000 na tani 220 mwaka 2013.

Wakati msukumo wa taka ngumu ukiongezeka mjini vifaa vya kudhibiti taka vilibaki vilevile. Yaani, magari manne machakavu yaliyotolewa kama msaada na serikali ya Japani mwaka 1987. Magari haya yaliweza kukusanya tani 100 tu kwa siku tangu 1987 hadi 2000.

Uwezo wa idara iliyohusika na mazingira na ukusanyaji taka, kipindi hicho Idara ya Afya, ulikuwa dhaifu sana kutokana na kutegemea sana ruzuku toka serikali kuu. Michango ya jamii na michango ya fedha taslimu kwa ajili ya ukusanyaji taka haikuwepo kabisa kabla ya mwaka 2000. Sheria ndogo pia zilikuwa zimepitwa na wakati kwani Halmashauri ilikuwa Sura Na. 101 ya mwaka 1947, enzi za Tanganyika. Wakazi wa Manispaa ya Moshi pia hawakuwa wamejipanga kushiriki kwenye udhibiti wa taka ngumu tangu kuzalishwa, kukusanywa, kusafirishwa na kuharibiwa kwa taka hizo. Ilichukuliwa suala la ukusanyaji taka ni jukumu la Halmashauri au Serikali tu.

Matokeo ya matatizo haya yote yakawa milundikano ya kutisha ya taka ngumu katika eneo la kati la kibiashara la Manispaa (CBD) na viunga vyake, marundo ya uchafu yanatooza pembezoni mwa barabara za mjini, jamii isiyowajibika kuhusu uzalishaji na ukusanyaji taka na kwa ujumla mji mchafu, barabara zilizofungwa na taka, mitaro ya maji machafu isiyotunzwa na barabara kuwa nyembamba sana.


## 3.0 MALENGO YA KUGATUA UDHIBITI WA TAKA NGUMU

Tangu mwaka 2006 Halmashauri ya Manispaa ya Moshi iljiwekea lengo kuu la kuboresha usafi na unadhifu wa mazingira ya Mji wa Moshi na kupunguza kusambaa kwa magonjwa yanayotokana na mazingira machafu na yaliyoathirika. Malengo mahususi katika jitihada hii yakawa ugatuaji wa shughuli za udhibiti wa taka ngumu kwenda kwenye Kata, uejengaji wa uelewa wa kina kuhusu jukumu la jamii katika uzalishaji, uchambuaji na usafirishaji wa taka ngumu, uanzishaji wa tozo za huduma, uhamasishaji wa usindikaji wa taka na utupaji taka ulio bora.

## 4.0 SHUGHULI ZA UTEKELEZAJI

Tangu mwaka 1996 Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilianza usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ulio bora kwa kutumia sheria ndogo. Hii ilijumuisha tozo za ukusanyaji taka, ukaguzi na upuliziaji dawa wa maeneo ya biashara kabla ya kutoa leseni za biashara. Mwaka 2006 sheria

ndogo ilitungwa iliyoanzisha tozo, ada na faini mpya. Ada ya ukusanyaji wa taka za kaya ikawa shs 12,000/= na kwa maeneo ya biashara shs 36,000/=. Sheria hii ndogo pia ilianzisha faini inayoanzia shs 10,000 – 50,000 kwa wasiolipa ada, au kifungo cha miezi sita au vyote kwa wale ambao kesi zao zitafika mahakamani.




*Kitabu cha sheria ndogo cha Manispaa ya Moshi*

Sheria ndogo kama zinavyoonekana kwenye kitabu huonyesha tozo zilizoorodheshwa kwenye jedwali hapa chini. Funzo moja kuu kuhusu ugatuaji (d-by-d) katika sheria hizi ndogo ni kuwa usimamiaji wa sheria hizi umegatuliwa kwenye katika Kata na utekelezaji upo katika ngazi ya Mtaa.

**Mchoro 2: Tozo chache za ukusanyaji wa taka ngumu**

*Kwa wastani gharama za udhibiti wa taka zinakadiriwa kuwa shs milioni 250. Sheria ndogo ya mwaka 2006 inaonyesha viwango vifuatazo vya tozo ikitegemea na aina ya makazi na biashara kwa shilingi za kitanzania.*

| | |
|---|---|
| *Mahoteli* | *260,000/=* |
| *Migahawa* | *80,000/=* |
| *Maduka ya Jumla* | *60,000/=* |
| *Viwanda vikubwa naTaasisi* | *780,000/=* |
| *Viwanda Vidogo* | *260,000/=* |
| *Biashara nyingine* | *36,000/=* |
| *Kaya* | *12,000/=* |
| *Soko/stendi/magari kwa tripu* | *15,000/=* |
| *Ushuru wa Dampo* | *5,000/=* |

*Kama makusanyo yakifikia 90% kwa mwaka halmashauri inaweza kukusanya shs 180,000,000 kwa mwaka, hivyo shughuli za udhibiti wa taka zinasaidiwa na mapato toka vyanzo vingine.*

Halmashauri ilianzisha mpango mkubwa wa kujenga uelewa katika jamii kuhusu kuenea, kuugua na kufa kwa magonjwa yanayoenezwa na mazingira machafu kama kuhara na kipindupindu. Wananchi wameeleweshwa kuhusu kuzuia na kudhibiti magonjwa haya ambayo awali yalitawala katika mji. Shughuli hii pia ilihusisha kuelezea umuhimu wa usafi wa mazingira kwenye afya njema ya mtu katika kaya na jamii mji wa Moshi kwa Ujumla.

Shughuli nyingine muhimu iliyo karibu na ugatuaji ni uhamasishaji na utekelezaji wa ushiriki wa jamii kwenye shughuli za udhibiti wa taka ngumu. Kata na jamii zilipewa madaraka zaidi kwenye masuala yote yanayohusu taka ngumu, usafi wa mitaa na ukusanyaji wa ada na faini. Mwaka 2009 shughuli zote za ukusanyaji wa taka ngumu ziligatuliwa kwenda kwenye ngazi ya Kata. Viriba vya kulundika taka viliondolewa na kuanzishwa maghuba na ving'ora. Kamati za maendeleo za Kata zilipewa madaraka ya kusimamia na kufuatilia shughuli zote za ukusanyaji wa taka ngumu. Shughuli hizi zinajumuisha ukusanyaji wa ada za mtumiaji, maamuzi kuhusu namna na wakati wa kutumia magari ya taka, manunuzi ya vifaa vya ukusanyaji taka na kulipa ujira na posho kwa madereva na vibarua.

Kwa ajili ya usimamizi bora wa taka ngumu Halmashauri ilianzisha Kamati za Afya za Kata na za Mtaa zilizopewa jukumu la la kuhakikisha usafi na utunzaji wa mazingira. Kamati hizi zinafanya kazi kwa ukaribu na Jamii ili kuhakikisha kuwa mji ni msafi, nadhifu na umepangwa. Ukiacha kamati hizi, Jamii pia ziliunda vikundi vya viwili kijamii, yaani RAKAS na BORESHA ambavyo vilipewa jukumu la kutekeleza sheria za usafi moja kwa moja kupitia faini za papo kwa papo kwa wachafuzi wa mazingira katika eneo la kari la kibiashara ikiwa ni pamoja na stendi kuu na kwenye masoko.

Ili kuwezesha ufanyaji kazi bora wa ukusanyaji wa taka katika ngazi ya Kata Halmashauri ilikarabati magari yote ya taka na kuyakabidhi katika Kata. Kata zina uhuru kamili wa kutumia magari hayo lakini zinawajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Manispaa kuhusu usafi na unadhifu wa Mji kila siku.



***Mtambo maalumu wa kusukuma na kusambaza taka (wheel Loader) katika Dampo la kisasa***

Ujenzi wa vyoo vya umma katika maeneo yote ya watu wengi kama stendi ya mabasi, masoko na ofisi za Kata ulikuwa ubunifu mwingine mkubwa. Vyoo hivi vilijengwa kwa kutumia mapato ya ndani na vinaendeshwa kibiashara kwani watumiaji wanalazimika kulipia huduma. Vyoo vingine vya umma vilijengwa na wawekezaji binafsi kwenye ardhi ya Halmashauri kwa mikataba maalumu ambapo Halmashauri itavimiliki jumla baada ya miaka iliyoainishwa kwisha. Vyoo hivi vya umma vimejengwa ili kuondoa uharibifu wa mazingira kupitia haja ndogo na kubwa za binadamu. Vyoo vinaendeshwa na mawakala waliopatikana kwa michakato halali ya manunuzi na mikataba. Vyoo huunda chanzo kimojawapo cha mapato ya ndani ambapo mwaka 2011/2012 Halmashauri ilikusanya shs milioni 19.6, mwaka 2012/2013 shs milioni 25.4 na ilitarajia kukusanya shs milioni 29.6 mwaka 2013/2014.

Halmashauri ilianzisha mashindano ya Usafi ya Kata ambayo hufanyika kila mwaka na washindi hupatiwa kikombe na cheti cha usafi. Picha iliyopo hapa chini inaonyesha Kata ya Mawenzi imekuwa ikishinda Tuzo kwa miaka mingi. Vigezo vinavyotumika kuamua kata iliyoshinda ni vile vilivyoainishwa kwenye mashindano ya usafi ya kitaifa ya halmashauri za manispaa. Kuna timu ya majaji watano kutoka idara za afya na usafi wa mazingira pamoja wataalamu wa mazingingira kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Majaji hawa huziandaa kata 21 kwa mashindano na hutoa uamuzi wa Kata zilizoshinda na nafasi zao. Mshindi hupata shs 300,000/=, mshindi wa pili shs 200,000/= na mshindi wa tatu shs 100,000/=. Vyeti hutolewa siku ya serikali za mitaa au kwenye tukio la Mbio za Mwenge wa uhuru.



*Vyeti vya Usafi vya kata ya Mawenzi*

Shughuli hizi pia zilijumuisha (i) kuhakikisha na kuimarisha uwajibikaji kati ya watumishi wa ngazi mbalimbali, na hasa maafisa watendaji wa kata na Mitaa (ii) Kuimarisha utekelezaji wa sheria ndogo ya usafi wa mazingira ya mwaka 2006 kama ilivyorekebishwa Aprili mwaka 2012 na utumiaji thabiti wa sheria ndogo ya ushuru na ada ya mwaka 2006. Sheria hizi zimeleta utii wa hali ya juu kwa shughuli za udhibiti wa taka katika Manispaa ya Moshi hasa kutokana na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa sheria hizi na Halmashauri na (iii) Usimamizi na Uratibu thabiti unafanywa na idara ya Usafi wa mazingira. Idara hii imejitoa kiujumla kuhakikisha kuwa Manispaa ya Moshi ni safi, nadhifu na ina mazingira mazuri.

**Mchoro 3: Idara ya Usafi wa mazingira (shughuli chache)**

- *Ukusanyaji wa taka ngumu kwa kutumia magari na maghuba*
- *Utakatishaji bora wa taka ngumu kwenye dampo*
- *Uendeshaji vitalu vya miche kwa ajili ya upandaji miti ndani ya eneo la Manispaa*
- *Uhamasishaji wa uzalishaji wa miche na upandaji miti katika Kata za Manispaa*
- *Uratibu na Usimamizi wa usafishaji wa barabara, stendi na masoko*
- *Utatibu na Usimamizi wa ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, uokotaji wa taka na usafishaji wa mitaro mjini*

Ufanyaji kazi wa Mfumo wa udhibiti taka uliogatuliwa ndani ya Manispaa ya Moshi uliboreshwa na kufanywa wa kisasa na una sifa za pekee zifuatazo;

(i) Jukumu la udhibiti wa taka ndani a ya Manispaa ya Moshi ni jukumu la kila mwananchi.

(ii) Menejimenti ya Halmashauri imeweka vipaumbele katika udhibiti wa taka na katika hili inafanya kazi kama timu.

(iii) Usafi wa mazingira katika mji wa Moshi ni moja ya vipaumbele vya siku ambapo mkurugenzi wa Halmashauri huhakikisha kuwa mfumo mzima wa uondoaji taka katika maeneo yote muhimu unafanya kazi kila siku. Hii ni pamoja na ugawaji wa mafuta kwa siku, ukarabari wa mitambo ya taka na uwepo wa watumishi. Pia kuhakikisha kuwa barabara zinafagiliwa, takataka zinasafirishwa mpaka kwenye dampo na wakiukaji wa sheria wanashughulikiwa. Hii inahitaji uangalizi wa kila siku tena kwa kuzungukia maeneo. Kwa kutumia mbinu hizi halmashauri ya manispaa ya Moshi huweza kukusanya 80% ya taka zinazozalishwa kwa siku.

(iv) Maeneo yanayozalisha taka ngumu kwa wingi yanapewa kipaombele cha usafishaji kila siku, kwa sababu haya ndiyo maeneo yanayoudhi wageni na watalii.



*Kibarua akifagia pembezoni mwa barabara mjini*

(v) Watu wanahabarishwa kupitia vipeperushi, mikutano ya mitaa, matangazo ya redio na matumizi mazuri ya maofisa wa Halmashauri. Pia vikundi vya kijamii vilivyo pewa mikataba na Halmashauri hufanya kazi kwa bidii kukusanya taka za kwenye kaya na kuziweka katika maghuba.

(vi) Kata, Maofisa wa mitaa na Vikundi vya kijamii kwa pamoja wamepewa mamlaka ya kutembelea kaya na kuchukua shs 1000/= kwa mwezi. Hii hufanyika baada ya vikundi vya kijamii kukusanya taka mwezi mzima. Siyo kaya pekee zinazotembelewa lakini pia Taasisi mbalimbali kama mahoteli, viwanda vikubwa, viwanda vidogo, n.k

(vii) Ada hukusanywa na walipaji hupewa stakabadhi za halmashauri. Fedha zinazokusanywa hutumiwa na Halmashauri kununua mafuta, kulipa posho na kukarabati vifaa vya ukusanyaji taka ngumu.

Shughuli zote hizi hufanyika katika ngazi ya kata. Hii inazipa Kata na Mitaa fursa ya kupanga na kusimamia ukusanyaji wa taka pamoja na kuzalisha nafasi za ajira, kuwaunganisha vijana katika vikundi vya kijamii na kuwashirikisha wananchi katika mchakazo mzima.




***Ghuba mojawapo lilipatikana kupitia urafiki na mji Delray Beach, Marekani***

Mfumo huu uliogatuliwa umesaidia Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kuhakikisha usafi wa kila siku wa mji, kushirikisha ngazi zote za kiutawala za Halmashauri mpaka chini na kujenga utamaduni wa usafi kwa wakazi wa Moshi. Kwa sasa jukumu la makao makuu ya Halmashauri limepungua na kubakia la kuhakikisha ufanisi katika uendeshaji wa mfumo wa ukusanyaji wa taka ngumu.

Sifa nyingine muhimu ya mfumo huu wa ukusanyaji taka ni ushiriki wa hiari wa taasisi za biashara, taaluma na viwanda katika ukusanyaji taka na utunzaji wa mazingira safi na nadhifu katika bustani za umma na mizunguko ya barabara. Utunzaji huu huhusisha kupanda majani, kumwagilia majani, kupanda miti na maua na kusafisha. Taasisi zinazoshiriki katika jukumu hili ni Kampuni ya Bia Tanzania, kampuni ya Bia ya Serengeti, Mamlaka ya Maji safi na Taka ya Moshi, Kampuni ya Bonite Botllers, Klabu cha Laliga, Kampuni ya Tanzania Discovery Heritage na Klabu ya Michezo ya Mawenzi.

Halmashauri hutangaza zabuni kila mwaka kuwavutia wawekezaji kuyachukua maeneo ya umma na ya wazi ili kuyaendeleza na kuwa safi na nadhifu kwa mikataba ambayo haipelekei umiliki wa ardhi. Maboresho katika bustani na maeneo ya wazi hufanywa kulingana na mipango na faida kwa kampuni husika na kwa miaka kadhaa iliyokubalika tu.



***Mzunguko wa barabara ya Moshi – Arusha unaotunzwa na Kampuni ya Bia Tanzania***




*Mzunguko wa barabara ya Taifa karibu na YMCA unaotunzwa na Mamlaka ya Maji Safi Na taka ya Moshi*

**5.0 RASLIMALI ZILIZOTUMIKA MIAKA MITATU YA MWISHO**

Ukusanyaji wa taka ngumu ni moja ya vipaumbele vya vya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. Lengo kuu ni kuhakikisha mazingira safi na salama kwa afya njema za wakazi wa mji. Halmashauri inaamini kuwa afya njema ya wakazi ni mtaji muhimu katika maendeleo. Pia huamini kuwa mazingira masafi huondoa maradhi na kupunguza gharama za kutibu watu wasio na afya njema. Kwa nia hii, halmashauri ilitumia zaidi ya shs bilioni 1.2 kutoka vyanzo mbalimbali kama inavyonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali 1: Gharama zilizotumika kwa miaka mitatu**

| Chanzo cha fedha | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|
| **Mapato ya ndani** | 256,000,000.00 | 200,500,000.00 | 374, 513,000.00 |
| **Ruzuku** | 25,500,000.00 | 12,000,000.00 | 5,000,000.00 |
| **Wafadhili** | 95,487,000.00 | 185,000,000.00 | 51,000,000.00 |
| Jumla ya Shs | **376,987,000.00** | **397,500,000.00** | **430,513,000.00** |

Licha ya raslimali fedha, Halmashauri imetumia raslimali watu kama wajumbe wa timu ya menejimenti, watumishi wa Kata na Mitaa, watumishi wa vikundi vya kijamii, wafagiaji wa barabara, migambo, madereva, mapolisi na watumishi wa mahakama kuhakikisha Manispaa ya Moshi ni safi na nadhifu.

Halmashauri hii ina uwezo wa kudhibiti taka ngumu kwa mafanikio ikilinganishwa na manispaa nyingine nchini Tanzania kwa sababu inamiliki dampo la kisasa, magari, mtambo wa kuharibu taka katika dampo, maghuba, mapipa, vifaa vya ufagizi, vifaa vya kulinda afya na ofisi za kutosha.

**6.0 MATOKEO NA HADITHI YA MAFANIKIO**

Tangu miaka ya mwanzo ya ugatuaji wa ukusanyaji wa taka ngumu katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, mji wa Moshi umeshuhudia matokeo mengi chanya. Halmashauri imekuwa ikishinda mara saba mfululizo katika mashindano ya kitaifa ya usafi na utunzaji wa mazingira katika Manispaa yanayofanyika Juni 5 kila mwaka, yaani siku ya kimataifa ya mazingira. Kati ya Halmashauri za

Manispaa 17 hapa Tanzania, halmashauri hii ina tuzo na na vikombe saba kwa kuongoza katika mashindano ya usafi na utunzaji wa mazingira. Halmashauri ya Manispaa ya Moshi pia inatambuliwa na kuthibitishwa na Shirika la Makazi Duniani (UN – Habitat) kama moja ya miji misafi na yenye kudhibiti vyema taka ngumu katika Afrika kwa kuchapishwa kwenye jarida la UN-Habitat pamoja na mji wa Lusaka (Zambia), Salaga (Ghana) na Bamako (Mali). Uzinduzi wa jarida hili ulifanyika Aprili Mwaka 2010 huko Rio de Jeneiro (Brazili) na uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi Ulishiriki.



*Vikombe na Vyeti vya Tuzo za usafi*

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imekuwa kituo cha kujifunzia. Halmashauri hupokea wataalam na madiwani toka ndani na nje ya nchi. Kwa mfano halmashauri 13 toka Kenya zimeshatembelea Manispaa ya Moshi kujifunza sheria ndogo za udhibiti wa taka ngumu na kubadilishana uzoefu kuhusu utekelezaji wa sheria ndogo. Pia Halmashauri 43 za Tanzania zimeshatembelea Manispaa ya Moshi kwa lengo hilo.

Kupitia ugatuaji wa udhibiti wa taka ngumu, Halmashauri ya Manispaa ya moshi imepunguza sana mzigo wa kazi makao makuu na imefanikiwa kujenga uwezo wa Kata, ambazo sasa hukusanya ada zaidi, na faini kutoka kwa wapokea huduma za taka ngumu wote kwa ufanisi na kutoa huduma za ukusanyaji taka kwa ufanisi. Kata zinaandaa taarifa zao za fedha na kila robo mwaka hukabidhi taarifa za fedha kwa Mkurugenzi zinazoelezea makusanyo, matumizi na mikutano sahihi ya Kata kuhusu usafi na ukusanyaji wa taka.

Wakazi wa Mji wa Moshi wamekuwa na mitizamo chanya kuhusu jitihada za usafi na utunzaji wa mazingira. Kwa kiasi kikubwa wanathamini usafi wa mazingira ya mji, upandaji miti, usafishaji wa mifereji ya maji na udhibiti wa wavunja sheria. Kila mkazi wa Manispaa ya Moshi amekuwa mwanamazingira. Kutokana na badiliko hili, ukusanyaji wa ada umekuwa fanisi. Utayari wa kulipa umefikia 95% katika eneo la kati la kibiashara na 70% katika kata za pembezoni.

Upandaji miti umekuwa jambo la kawaida katika Manispaa ya Moshi. Katika Kata na Mitaa yote watu wanashiriki kwa hiari kwenye upandaji wa miti pembezoni mwa barabara na maeneo ya wazi. Manispaa ya Moshi inafunikwa na rangi za kijani, nyekundu, zambarau na rangi nyingine za mimea hata katika eneo la kati la kibiashara. Upandaji miti na uboreshaji wa mazingira vimekuwa vipaombele visivyo na mjadala kwa Halmashauri na wakazi wake.



***Eneo la Shule ya Msingi Mwereni huwa kijani siku zote***

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji safi na Taka ya Moshi imefanikiwa kudhibiti magonjwa wa kuhara na matumbo kupitia utakatishaji wa maji kufikia viwango vinavyokubalika na Wakala wa Viwango Tanzania (TBS). Hili limepelekea kupungua kwa bajeti ya afya inayohusu magonjwa kama kuhara, kipindupindu na homa ya matumbo.

**Jedwali 2: Magonjwa ya Matumbo Mwaka 2010**

| | Chini ya miaka mitano | | Juu ya miaka mitano | |
|---|---|---|---|---|
| **Ugonjwa** | **Wagonjwa** | **Vifo** | **Wagonjwa** | **Vifo** |
| **Kipindupindu** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Kuhara** | 138 | 12 | 264 | 17 |
| **Homa ya Matumbo** | 148 | 4 | 253 | 18 |
| **Dysentery** | 22 | 0 | 41 | 0 |

**Chanzo: Manispaa ya Moshi**

**Jedwali 3: Magonjwa ya Matumbo Mwaka 2013**

| | Chini ya miaka mitano | | Juu ya miaka mitano | |
|---|---|---|---|---|
| **Ugonjwa** | **Wagonjwa** | **Vifo** | **Wagonjwa** | **Vifo** |
| **Kipindupindu** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Kuhara** | 126 | 3 | 214 | 11 |
| **Homa ya Matumbo** | 142 | 2 | 207 | 7 |
| **Dysentery** | 18 | 0 | 29 | 0 |

**Chanzo: Manispaa ya Moshi**

## 7.0 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA UENDELEVU

Ugatuaji wa ukusanyaji wa taka katika Manispaa ya Moshi ulikumbana na changamoto nyingi sana zilizohitaji hatua za haraka za kukabiliana nazo. Hizi zilijumuisha ongezeko la biashara ndogondogo na wafanya biashara ndogondogo (wamachinga) na mlundikano wao katika eneo la kati na la kibiashara la mji badala ya maeneo waliyotengewa, upungufu wa vifaa vya ukusanyaji taka na vifaa vya kushughulikia taka, mazuio kutoka serikali kuu ya kuajiri watumishi wapya wa kukusanya taka, upungufu wa bajeti ya shughuli za kudhibiti taka ngumu na mfumo chakavu wa maji taka mifereji ya maji inayopelekea mafuriko ya maji taka katika eneo la kati la mji. Changamoto hizi zimelazimu halmashauri kubuni mbinu za kujihakikishia uendelevu wa udhibiti wa taka ngumu uliogatuliwa zilizotajwa hapa chini;

(i) Ushirikishwaji madhubuti wa wadau mbalimbali (ikiwemo wamiliki wa biashara ndogondogo) katika kupanga masuala ya usafi na utunzaji wa mazingira.
(ii) Usimamizi mkali na wa dhati wa utekelezaji wa sheria ndogo za usafi mazingira.
(iii) Mpango wa safari za mafunzo katika miji mingine Afrika ianyofanya vizuri katika usafi na unadhifu.
(iv) Mpango wa kununua gari kubwa la kubeba Maghuba na magari manne makubwa ya kushindilia na kusaga taka.
(v) Uhamasishaji usiokoma kwa wakazi wa Manispaa ya Moshi kuhusu ushughulikiaji wa taka toka kwenye chanzo, yaani utenganishaji wa taka ngumu, usafishaji na uteketezaji.
(vi) Uboreshaji wa dampo ili liwe la kisasa pamoja na kujenga mtambo wa kuchakata gesi. Hili litatekelezwa kupitia hati ya makubaliano (MOU) na Jiji Dada wa Tuebingen huko Ujerumani.
(vii) Kuendeleza mahusiano na jiji Dada la Deray Beach (Marekani) katika mpango wa kuimarisha vikundi vya kijamii ambao hufadhiliwa ba Jiji hili.

## 8.0 SIRI ZA MAFANIKIO

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni ya pekee kwani Manispaa nyingi hapa Tanzania zimepambana sana kufanya miji yao misafi bila mfanikio. Kuna sababu nyingi sana zilizojificha za mafaniko haya. Hizi zimelezewa hapa chini.

*Ajenda ya Kudumu.* Udhibiti wa taka ngumu, usafi wa mji na utunzaji wa mazingira ni kipengele cha ajenda cha kudumu katika vikao vyote vya kisheria kama Baraza, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, Kamati za Maendeleo za Kata na Mikutano ya Mitaa. Ni kipaombele ambacho kinakubalika kwa madiwani na watumishi wote na hakuna misuguano kuhusu uhakikishaji wa usafi na unadhifu wa Manispaa.

*Ugatuaji thabiti wa huduma za taka ngumu.* Ugatuaji wa huduma hii kwenda kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata katika shughuli zote za uendeshaji, yaani, upangaji wa udhibiti wa taka ngumu, ukusanyaji wa ada, tozo na faini, usimamizi na ukarabati wa kila siku wa vifaa vya ukusanyaji na usimamizi wa watumishi umezitia motisha Kata kuweza kufanya kazi kwa juhudi katika kuhakikisha mji ni safi na umeleta ushindani kati ya Kata unaohusiana na usafi katika maeneo yao ya utawala. Zoezi hili pia limeibadilisha jamii na uhiari wa kulipia ukusanyaji wa taka umeongezeka sana. Makao makuu ya Halmashauri yamejikita zaidi katika kushauri na kujenga uwezo tu.

*Mji uliobuniwa na kupangwa vizuri.* Manispaa ya Moshi ni kati ya miji ambayo ina michoro na ramani za mji zilizokamilifu na zinazofuatwa tangu enzi za Moshi ya mkoloni. Barabara zote ni pana na wazi kiasi cha kutosha kuruhusu watu kupita na usafi.



*Kichochoro cha Del Chez kikiwa wazi, safi na kupitika*

Uboreshaji na ukarabati wa mara kwa mara wa barabara za manispaa. Siyo rahisi kuwa mji safi na nadhifu wakati barabara zina vumbi na matope. Halamashauri ya Manispaa ya Moshi hutumia fedha za za mfuko wa barabara na za ndani kuboresha na kukarabati barabara za lami na za changarawe zenye urefu wa Km 288.039. Barabara hizi ni bora, safi na hupitika mwaka mzima.



***Barabara ya mjini iliyo safi na wazi***

Ushiriki wa moja kwa moja wa taasisi mbalimbali katika usafishaji wa Mji. Halmashauri ya Manipaa ya Moshi ina makubaliano na taasisi nyingine ndani ya Manispaa kwa ajili ya kushiriki katika usafishaji wa mji. Taasisi hizi ni TANROADS, Gereza la Karanga, na Chuo cha Polisi Moshi. Taasisi hizi hushiriki katika ukataji nyasi, upandaji miti, usafishaji wa mifereji na ufagiaji wa barabara.

Kuendeleza urafiki na Majiji Dada. Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imedumisha mahusiano thabiti na majiji Dada ya Komaki (Japani), Halmstad (Sweden), Delaray Beach (Marekani) na Tuebingen (Ujerumani). Majiji haya hutoa msaada katika usafi wa mazingira, uhamasishaji wa jamii kuhusu usafi, utoaji wa mafunzo kwa watumishi nje ya nchi, usafishaji wa taka, usaidizi wa vifaa vya udhibiti wa taka na uzalishaji wa umeme kutokana na taka.

**Jedwali 3: Majiji Dada yaliyotembelewa na Misaada iliyopokelewa**

| Jiji | Mwaka | idadi | Kifaa Kilichopokelewa |
|---|---|---|---|
| Komaki (Japani) | 2008 | 6 | Lori (ISUZU FUSO) |
| Delray Beach (Marekani) | 2011 & 2013 | 6 | Maghuba 12 |
| Tuebingen (ujerumani) | 2011 & 2013 | 5 | Mtambo wa Gesi |

**Chanzo: Halmashauri ya Manispaa ya Moshi**




*Gari la kuzoa na kushindilia takataka lililotolewa msaada na Mji Dada wa Komaki (Japani)*

*Watu wa Moshi hutukuza Usafi.* Watu wanoishi katika Manispaa ya Moshi hupenda sana mazingira safi na kijani. Hii inapunguza upinzani kwa jitihada za halmashauri za kushirikisha watu katika udhibiti wa taka ngumu, upandaji miti na usafishaji wa mitaro ya maji.

*Matumizi thabiti ya vikundi vya hiari.* Vikundi hivi vya hiari vimeundwa na wajumbe kutoka mitaa ya Moshi ambapo taka hukusanywa. Vikundi hivi vinatambuliwa na vimeandikishwa katika Kata na Halmashauri kama wanamazingira na vinapewa vibali vya kufanya kazi ndani ya Kata na Mitaa yao kulingana na sheria ndogo na hukusanya ada, tozo na faini zilizoelekezwa. Vikundi vya hiari vya RAKAS na BORESHA hufanya kazi katika eneo la kati la manispaa, yaani kata za Bondeni, Mawenzi na Kiusa.

*Ushirikiano thabiti na Mpango wa Polisi Jamii.* Watumishi wa polisi jamii hushiriki katika kukamata wavunjaji wa sheria ndogo katika kuhakikisha mji wa Moshi ni safi na nadhifu. Jitihada hii pia inasaidia kudhibiti biashara ndogondogo katika eneo la kati la Manispaa.

*Matumizi ya Mabango Makubwa, Vibao na Vipaza Sauti.* Kwa wasafiri na wageni, Halmashauri imesimika mabango na vibao katika njia zote za kuingia mjini kuwaonya wageni kujiepusha na utupaji ovyo wa taka na tabia nyingine zinazo haribu mazingira. Pia stendi ya mabasi ya Moshi ina vipaza sauti ambavyo hutumika kutangaza maonyo na tahadhari dhidi ya utupaji ovyo wa taka na kufuata sheria ndogo za halmashauri.

*Mashindano ya Usafi ya Kata na Mitaa.* Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imetumia mkakati huu kuhakikisha kuwa Kata na Mitaa yote inajiingiza kikamilifu katika usafi na utunzaji wa mazingira kiushindani na ni mbinu ya kutoa zawadi na adhabu kwani zile kata zinazofanya vizuri zinapata zawadi wakati zile zisizofanya vizuri zinaonywa.

# HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

## UDHIBITI ENDELEVU WA TAKA NGUMU



*Uzoefu wa Halmashauri ya Jiji la Tanga*

**1.0 UTANGULIZI**

Udhibiti wa taka ngumu katika jiji la Tanga ni mfumo ambao una vipengele vya kisheria, kiutawala, kimasoko, kiteknolojia na kijamii, na unaweza tu kueleweka vema katika sura yake ya mageuzi ya kihistoria. Miaka mingi ya nyuma Jiji la Tanga lilikosa shughuli za umma zilizopangwa vizuri za usafi wa mitaa, utanatishaji wa mazingira, ukusanyaji wa taka, na uteketezaji wa taka hadi mwishoni mwa miaka ya 90. Milipuko ya magonjwa isiyokoma ililazimisha hatua kuchukuliwa za kuboresha afya ya jamii na mazingira. Jitihada nyingi za kuboresha afya ya jamii ziliwekwa katika kuimarisha huduma za kutibu magonjwa na huduma nyingine zinahusiana na tiba badala ya hudumu za kuzuia maradhi. Mpaka ilipofikia kipaumbele kinahamia katika udhibiti wa taka ngumu mwaka 1999, fedha hazikutosha halmashauri ya jiji kuweza kuwekeza katika udhibiti wa taka ngumu. Hivyo udhibiti wa taka ngumu ulianzishwa kama jukumu la jamii, lililoachwa katika vituo vya mitaani vya kukusanyia taka.

Halmashauri ya Jiji la Tanga ina wajibu wa kuhakikisha kuwa taka ngumu zinazozalishwa ndani ya eneo lake zinadhibitiwa kwa ubora kimazingira na kiuchumi ambapo afya na usalama wa jamii vinalindwa. Udhibiti wa taka ngumu umejikita zaidi katika hitaji la kulinda mazingira, kutunza na kurejesha raslimali za nishati na kulinda afya na usalama wa jamii. Hivyo, halmashauri ya Jiji inawajibika kwa umma inaoutumikia katika kupanga vyema na kutekeleza shughuli zitakawezesha kufikia sera ya Taifa na Malengo yaliyopo katika mipango ya udhibiti wa taka ngumu. Halmashauri ya jiji la Tanga inazingatia dira hii, inakubali jukumu lake, na ina nia ya kusonga mbele kiuwajibikaji. Dira ya Jiji la Tanga inasema *"Ustawi wa wakazi wa jiji ulioboreshwa na upatikanaji endelevu wa huduma za kijamii na kiuchumi katika misingi ya Utawala Bora"*.



***Ramani ya Kiutawala Jiji la Tanga***

Mwaka 1999, Halamshauri ya Jiji la Tanga ilianzisha mfumo ulioridhiwa wa kushirikisha Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), Vikundi vya Kijamii (CBOs) na Taasisi binafsi katika kutoa huduma za ukusanyaji wa taka ngumu katika Kata. Halmashauri ya Manispaa ya Tanga ya wakati huo ilitoa mikataba ya huduma za ukusanyaji wa taka ngumu kwa baadhi ya vikundi vya kijamii chini ya Mradi

wa Tanga Endelevu (STP) ambao ulifadhiliwa kwa kiasi na Benki ya Dunia kupitia Mpango wa USRP. Hata hivyo takwimu zilionyesha kuwa vikundi vingi vya kijamii havikuweza kuendelea kufanya kazi baada ya mradi wa STP kwisha. Hii ilitokana na mikataba dhaifu na usimamizi mbaya wa mikataba ambavyo vilichochewa zaidi na maandalizi duni ya mabadiliko kwa pande zote mbili za umma na binafsi.

Udhibiti wa taka ngumu ni jukumu la msingi na wajibu wa mamlaka za serikali za Mitaa (*Sheria ya Serikali za Mitaa "Za Mijini" kifungu Na 55g*). Sheria za Nchi na Sheria ndogo zinazosimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinataja vifungu maalumu kuhusu ukusanyaji, usafirishaji na uteketezaji wa taka. Sheria hizi zinampa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wajibu wa kutoa huduma. Sheria hizi zinaelezea masuala ya muhimu ya kitaalamu na kioganaizesheni kuhusu udhibiti wa taka ngumu katika maeneo ya Jamiii. Sheria zinaelezea ufagiaji wa barabara, ugawaji wa vifaa katika maeneo kadhaa vya kuhifadhi taka, na kusafirisha kwenda kwenye vituo vya kuteketeza taka kwa ujumla. Katika namna nyingine, sheria ndogo za Jiji zinaweka wazi majukumu yapi ni ya wananchi (kwa mfano, jukumu la kukamata wachafuzi wa mazingira katika mtaa). Zaidi ya hapo, sheria ndogo zinataja mifumo mahsusi ya ukusanyaji taka (kama ukusanyaji wa kaya kwa kaya), kuelekeza aina zinazofaa za kuhifadhi taka katika vituo mbalimbali, masuala muhimu ya usafirishaji wa taka, na zinataja vipengele muhimu vya uteketezaji wa taka na madampo salama. Kwa hiyo, Jiji la Tanga kwa sasa linaandaa mpango wa kutekeleza Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake na Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 na Kanuni zake.

**2.0 TATIZO**

Hali halisi ya Jamii ya Jiji la Tanga inahusiana sana na tabia zake za kiuchumi, kihistoria, kiutamaduni, kimazingira na mengineyo. Halmashauri ya Jiji iliainisha matatizo na changamoto nyingi mahsusi kuhusiana na mfumo wa zamani wa udhibiti wa taka; matatizo haya yalikuwa ukosefu wa maeneo na vifaa vinanyofaa kimazingira kwa ajili ya uteketezaji wa mwisho wa taka, upungufu mkubwa wa magari, mitambo na vifaa vya kazi vya kusafirisha taka ngumu, gharama za juu za uendeshaji na utengenezaji wa magari na mitambo zilizozidi uwezo wa bajeti ya Halmashauri na ukosefu wa shughuli za kati za utakatishaji wa taka.

Pia kulikuwa na mfumo duni wa uchambuaji taka pale zinapozalishwa iliyopelekea kuwepo kwa taka za majumbani za kila aina zikichanganyika na taka za madawa, na hata taka hatari sana za viwandani, zote zikihitajika kutupwa katika dampo moja lililokusudiwa kwa taka za kawaida. Taka zilizotupwa katika dampo hili hazikusambazwa wala kushindiliwa. Taka ziliachwa zikiwa wazi na kuharibu hali ya hewa ya asili. Dampo lilitengeneza mitiririko ya maji machafu na hivyo kuchafua hifadhi za jirani za maji safi, lilichafua hewa kwa kusambaza hewa chafu ya metheni, lilianzisha uchomaji moto usiodhibitika na kuleta madhara hatari ya kiafya na kimazingira kwa Jiji kiujumla, na kipekee kabisa, kwa watu waishio karibu na eneo la dampo.

Matatizo mengine yalijumuisha ukosefu wa ushiriki wa jamii katika uhifadhi wa taka pale zinapozalishwa, ambao ungewezesha ukusanyaji wa msingi katika kaya, tabia mbaya za wakazi ambao walizoea kumwaga taka barabarani, uongezekaji wa kasi wa uzalishaji wa taka kwa mwaka, uzito wa utakatishaji wa taka, milundikano ya taka katika vituo vya kukusanyia iliyoambatana na athari kwa mazingira na matumizi duni ya mbinu za kurejesha raslimali mazingira. Hakukuwa na hatua thabiti za kusimamia urejeshaji wa uwezo wa vifaa vya taka. Zaidi ya hapo raslimali za nishati na gesi zilikuwa zikiteketezwa katika dampo wakati ongezeko la taka lilikuwa likidhibitiwa kidhaifu sana katika vyanzo vyake.

## 3.0 MALENGO

Dhima ya jiji katika Udhibiti wa Taka Ngumu kupunguza taka, kuzuia uchafuzi wa mazingira, kukuza ufanisi na kuwa na miundombinu endelevu ya udhibiti wa taka ngumu, hivyo kulinda mazingira, afya ya jamii na usalama. Dhima inalenga uhifadhi wa nishati na raslimali. Lengo la msingi ni kulinda ardhi, hewa, maji, raslimali nyingine za Jiji na Afya ya Jamii kupitia mfumo jumuishi ambapo taka zitadhibitiwa kwa kutumia teknolojia mbalimbali. Halmashauri ina mbinu nyingi stahiki za kudhibiti taka ambazo ni muhimu kwa kufikia malengo ya udhibiti taka ngumu ulio endelevu na unaofaa; kwa kuwezesha na kushirikisha wadau wote wa maendeleo katika mchakato wa maendeleo ili kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa kutumia raslimali zilizopo.

Kuna malengo matano dhahiri katika dira ya uendelevu ambayo inatoa msingi kwa matokeo yanatohitajika kutoka katika shughuli za mpango wa udhibiti wa taka ngumu. Malengo haya ni kudhibiti taka ili kulinda mazingira na afya ya jamii, kuhifadhi raslimali, kudhibiti taka kwa kutumia njia mbalimbali kulingana na dhima ya jiji ya kuwezesha na kushishikisha wadau wote wa maendeleo katika mchakato wa maendeleo kwa kutumia raslimali zilizopo, kudhibiti taka kwa gharama nafuu na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kwa wananchi, biashara na walipa kodi.

Halmashauri ya Jiji la Tanga pia lilidhamiria kuwahimiza wajibu wa wazalishaji wa taka wa kudhibiti taka kwa mbinu ambazo zinakubalika kimazingira, kutenga raslimali na gharama za haki kwa watumiaji na kuhakikisha utekelezaji kamilifu wa mipango kwa matokeo mahususi na mikakati inayofaa katika kila ngazi ya udhibiti wa taka, pamoja na uchambuaji wa taka zinapozalishwa, upunguzaji wa sumu katika taka, urejeshaji wa raslimali, ufukiaji wa taka na mwisho, uteketezaji kabisa wa taka katika dampo.

## 4.0 MPANGO WA UTEKELEZAJI

### (a) Kuanzishwa kwa Msaragambo na Ushiriki wa Jamii

Kati ya mikakati mikuu iliyotekelezwa katika mpango muhimu wa maboresho ni Kampeni ya Usafi wa Jiji maarufu kama Msaragambo au “Siku ya Kalembo”. Wakati Makamu wa Rais alipotangaza kuhusu kuanza kwa Kampeni za Usafi kila mwezi (Jumamosi ya kwanza ya kila mwezi) Februari mwaka 2011, Mkuu wa Mkoa wa wakati huo, Brigedia Generali Mstaafu Kalembo alichukua mkakati huu na kuuwekea usimamizi mkali katika utekelezaji wake na kupelekea kuitwa Msaragambo na kutaniwa kama “Siku ya Kalembo”. Jitihada ya Msaragambo iliboreshwa na kuwa zoezi la kila Jumamosi toka Januari 2013 hadi Oktoba 2013 uliporudishwa Msaragambo wa mara moja kwa mwezi.

Kampeni ya Msaragambo huhusisha kila mtu katika Jamii na kila mtu katika Jiji anatakiwa kutii amri zifuatazo;

(i) Kushiriki katika tukio linaloandaliwa la usafi katika usafi wa pamoja katika mtaa au usafi wa kaya kutegemea na maamuzi ya Kata au Mtaa husika kwa siku hiyo.

(ii) Maduka yote na biashara nyingine zinatakiwa kufungwa kuanzia saa 3:30 asubuhi hadi saa 11: jioni, vinginevyo wasiotii hupigwa faini ya isiyozidi shs 50,000/= papo kwa papo.

(iii) Uongozi wa Kata na Mitaa ndio unaosimamia kampeni hii katika maeneo yao na kuchukua hatua zote dhidi ya wale wasiohudhuria.

(iv) Zaidi ya kutoa msaada kwa namna ya vifaa vya usafi na nguvukazi, Halamashauri ya jiji (kitengo cha udhibiti taka) kina timu ya ukaguzi inayotembea katika Jiji hasa katika maeneo kampeni na hutumia fomu maalumu ya ukaguzi ambapo maksi zinaingizwa na mwishoni mwa siku maksi hizi hulinganishwa na matokeo ya kata nyingine.

(v) Taarifa ya Msaragambo ya mwezi huandaliwa na kukabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Jiji, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa.

(vi) Kila mwezi, siku moja au mbili kabla ya siku ya Msaragambo, halmashauri ya jiji huandaa barua za kuwataarifu wadau wote kuhusu siku hiyo na kama kuna ujumbe mwingine wa kufikisha kwa umma. Barua hizi husainiwa na Mkurugenzi wa Jiji na kutumwa mapema kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Walezi wa Kata na Maafisa watendaji wa kata kuwajulisha kuhusu Msaragambo na ushiriki wao.


(vii) Halmashauri ya Jiji juandaa matangazo ya barabarani kuukumbusha Umma kuhusu Msaragambo ujao.

(viii) Wakati wa Msaragambo wakazi hufanya shughuli zote za usafi ambazo ni pamoja na ufagiaji wa barabara, usafishaji wa mitaro, usafishaji wa maeneo ya umma kama makaburi, hifadhi na bustani, usafishaji wa mazingira yanayozunguka kaya na majengo, ukusanyaji, usafirishaji na uteketezaji wa taka. Kuna fursa hutokea watu wakapatiwa mafunzo kuhusu maendeleo ya jamii zao. Pia hutokea katika baadhi ya kata michezo kufanyika baada ya tukio la msaragambo.

Mbinu ya Msaragambo inaweza kuigwa kitaifa kwa kuanzisha uwekezaji katika mitambo na vifaa taka. Hakika, hapatakuwa tena na milundikano ya taka isiyokusanywa katika Taifa. Msaragambo unatakiwa kuwa wa lazima kisheria na usiokwepeka ili watu wawajibike juu ya taka ngumu majumbani mwao, barabarani na katika sehemu zote za umma.

**(b) Kupitia na Kusimamia sheria ndogo za udhibiti wa taka**

Sheria ndogo ya Usafi wa mazingira ya Halmashauri ya Jiji la Tanga ya mwaka 2003 ndiyo sheria ya msingi kuhusu usafishaji wa mitaro na barabara, ukusanyaji wa taka na usafirishaji wake. Kulingana na kifungu cha 8(1) cha sheria hii ndogo ya Mwaka 2003 Halmashauri ina jukumu la kuhakikisha usafi wa jumla wa Jiji ambao unatakiwa kutekelezwa kwa kutumia raslimali za halmashauri au za mawakala; hii inajumuisha udhibiti kwa kukusanya taka za upili kwa kuziondoa katika vituo vya ukusanyaji/maghuba, na kuzisafirisha kwenda kwenye sehemu za mwisho za uteketezaji taka. Wakazi wanawajibika muda wote katika usafi wa maeneo yanayowazunguka na kutoa taka zao kulingana na mfumo rasmi au kuzipeleka katika vituo rasmi vya ukusanyaji ambapo kuna maghuba kama ilivyonyeshwa hapa chini.



Sera, sheria ndogo na sheria za nchi za udhibiti wa taka ngumu zilipitiwa kikamalifu ili kubaini kama zinaendana na teknolojia, idadi ya watu, ongezeko la shghuli za binadamu na kiwango cha utandawazi. Kati ya hizi ni sheria ndogo za jiji la Tanga za ukusanyaji taka na ukaguzi wa maeneo ya biashara za mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997, Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 1990, Sera ya Maendeleo endelevu ya viwanda ya mwaka 1996, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004) na kanuni zake, sheria ya afya ya Jamii ya mwaka 2004 na sheria nyingine nyingi.


**(c) Uimarishaji wa Ukusanyaji Taka wa Msingi**

Kwa ujumla ukusanyaji taka wa msingi ndilo eneo muhimu sana la huduma za udhibiti wa taka ngumu na katika Jiji la Tanga eneo hili limepewa kipaumbele cha kutosha, mfumo wa ukusanyaji upo katika maboresho ili kuingiza mifumo mizuri na fanisi zaidi ya kisasa. Halmashauiri ya Jiji hutoa huduma za ukusanyaji wa taka kwenye kingo za barabara na katika baadhi ya Kata huduma hii imebinafsishwa kwa sekta binafsi. Kata pia zilipewa mamlaka ya kutoa huduma za ukusanyaji taka na sheria ndogo za jiji. Wakazi pia wameelekezwa kutupa takataka zao katika vituo vya ukusanyaji vilivyowekwa na halmashauri ya jiji.

**(d) Kuimarisha Ukusanyaji Taka wa Upili na Usafishaji wa Barabara na Mitaro**

*Utengaji wa Raslimali*. Ingawa idadi ya wataalam wa udhibiti wa taka ngumu ni ndogo halmashauri hutenga vifaa na nguvukazi kwa ajili ya ukusanyaji taka wa upili. Pia ina magari ya kukusanyia taka na mitambo mingine muhimu. Kwa usafishaji wa barabara, mitaro na maeneo ya wazi halmashauri hutumia wasafishaji. Sifa ya pekee ya halmashauri ya jiji la Tanga ni kuwa wasafishaji hufanya kazi kwa wastani wa masaa saba kila siku katika siku nne.

*Mnyororo wa utawala na utoaji taarifa.* Mnyororo wa menejimenti una milekeo miwili inayopishana; yaani mnyororo wa utawala na mnyororo wa utoaji taarifa kama ulivyoonyeshwa hapa chini. Minyororo hii ikikamilika udhibiti wa taka ngumu hufanyika kwa uthabiti na ufanisi. Halmashauri ina mnyororo uliounganika vizuri wa utawala; na kwa mwelekeo mwingine, mnyororo wa utoaji taarifa unaendelea kuimarishwa kama inavyonyeswha hapa chini.




**(e) Uboreshaji wa Uteketezaji wa Mwisho wa Taka**

*Uwezo wa eneo la sasa la uteketezaji wa taka*. Mwang'ombe ndilo eneo pekee rasmi linalomilikiwa na Jiji. Taka zote ngumu zinazokusanywa kutoka vyanzo vyote hutupwa katika eneo la Mwang'ombe kwa kutupwa ovyo juu ya ardhi. Kwa sasa eneo hili la uteketezaji wa taka halijaendelezwa kuwa dampo safi kwa uteketezaji salama wa taka ngumu.




***Lori la kukusanyia taka likiwa katika dampo la Mwang'ombe***

*Utakatishaji wa taka ngumu.* Taka ngumu ambazo zinaweza kutakatishwa hutengwa kwa mikono na wakusanyaji wa taka na watu binafsi wanao okota takataka Jijini. Waokota taka hawa wakati mwingine hununua takataka zinazoweza kutakatishwa kutoka katika kaya na maeneo ya bishara, na katika masoko, maghuba ba madampo na kuzichambua kabla ya kuziuza. Vikundi vingi vya wakusanyaji hawa vipo katika vituo vya ukusanyaji wa taka na kika madampo. Hata hivyo taka hizi zinazoweza kusafishwa na kutumika tena hazichambuliwi vyema hivyo kuzifanya kuwa sehemu ya taka za dampo.

*Uhifadhi na Uchambuaji wa taka Majumbani.* Uhifadhi wa taka katika chanzo cha uzalishaji ni hatua muhimu sana kuelekea udhibiti sahihi wa taka ngumu. Kaya nyingi zimechukua jukumu hili hasa katika Kata zinazozunguka eneo la kati la Jiji ukiondoa Kata tano ambazo zinapata huduma ya ukusanyaji kwenye kingo za barabara ambazo ni Central, Ngamiani Kaskazini, Ngamiani Kati, Ngamiani Kusini na Majengo. Baadhi ya kaya, maduka, na biashara nyingine hutupa takataka zao bila uchambuzi hata kidogo. Halmashauri ya jiji imedhamiria kuanzisha mpango wa uchambuaji wa taka katika chanzo. Mpango huu utakuwa unafanya kazi vizuri kuanzia mwaka 2014/2015 baada ya kukamilisha tafiti kadhaa na miradi ya majaribio.

*Uchambuzi hafifu wa taka zinazoweza kusafishwa na kutumiwa tena*. Uchambuzi wa taka zinazoweza kusafishwa na kutumiwa tena kwenye chanzo bado haujaanza kutekelezwa kikamilifu na kaya, maduka na biashara mbalimbali. Takribani 15% mpaka 20% ya taka zote zinazweza kuchambuliwa kiurahisi katika vyanzo kwa ajili ya usafishaji kama zoezi hili lingeanza kufanywa kwa umakini. Hata hivyo, katika maeneo yote ya Jiji, watu hukusanya taka zote zitumikazo tena kama magazeti, chupa, madebe, vyuma chakavu na vitu vya plastiki na kuviuza tena. Sekta hii ina faida ndogo, na siyo rasmi lakini imeimarika sana. Wakusanyaji wengi wa taka hizi huzichukua kutoka kwenye vyanzo na kuzifikisha kwa wanunuzi ambao nao huzifikisha kwa wingi viwandani zinapotakatishwa na kutumika tena.

*Pia kuna wakusanya taka wengine wajulikanao kama waokotezaji*. Hawa hujitokeza kama maskini ambao huokota taka zinazoweza kutumika tena toka barabarani, kwenye maghuba na kwenye madampo; kuchambua baadhi ya taka na kuziuza kwa wanunuzi kwa malengo ya kupata kipato. Taka hizi zinazoweza kutumika tena huambatana na uchafu wa chakula, vinyesi na madawa. Bei za taka hizi ni ndogo ikilinganishwa na zile taka safi na kavu zinachukuliwa moja kwa moja kutoka

katika kaya na maduka. Pia kwa sababu waokotaji hawa ni maskini, wana uwezo mdogo sana wa kudai bei za juu toka kwa madalali.

**(f) Uanzishaji wa Mradi wa Ubinafsishaji**

Mpango wa ubinafsishaji wa udhibiti wa taka ngumu umekuwa ukiendelea tangu mwaka 1999 kama "Mradi wa Jiji wa kudhibiti taka katika Kata". Kupitia jitihada za jamii, vikundi vya kijamii vilichaguliwa na kupewa mikataba. Vikundi hivi hufanya kazi kama zinazofanywa na jiji katika maeneo waliyopangiwa kwa mkataba na hasa ukusanyaji wa msingi wa taka na tozo.

## 5.0 RASLIMALI ZILIZOTOMIKA

Kufikia malengo ya udhibiti wa taka ngumu katika Jiji la Tanga, halmashauri imetumia aina mbalimbali za raslimali. Raslimali watu ndio moja ya aina muhimu raslimali. Ukiacha watumishi katika idara wanaoshughulika na taka ngumu, Halmashauri hutumia raslimali watu zinazojumuisha watumishi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa, watumishi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya, wafanyabiashara, watumishi wa vyombo vya habari, watumishi wa taasisi za dini na jamii kwa ujumla. Pia Maafisa watendaji wa Kata pamoja na watumishi wa vikundi vya kijamii katika Kata zao ni sehemu muhimu ya raslimali watu wanaotumika katika udhibiti wa taka ngumu.

Mbili, Halmashauri ya Jiji la Tanga imekuwa na raslimali fedha nyingi za kutumia kudhibiti taka ngumu kwa miaka kadhaa. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2013/2014 halmashauri ilikadiria kutumia shs 426,850,000/=, (yaani shs 6,617.55/tani). Kiutendaji gharama za ukusanyaji na usafirishaji kwa kipimo kimoja ni gharama sana kuliko za uendeshaji wa dampo. Halmashauri ya Jiji pia ina vifaa vya taka kama inavyonyeshwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali 1: Vifaa vya udhibiti wa taka vilivyopo na Hali yao**

| Aina ya vifaa | Vifaa Vilivyopo | Hali ya vifaa |
|---|---|---|
| Malori ya kubeba Maghuba | 2 | 1 zima na 1 bovu |
| Maghuba | 20 | 9 yanafanya kazi kila siku |
| Wafagiaji | 1 | Amepumzishwa trekta bovu |
| Malori ya Kubinua Taka | 2 | Leo mazima, kesho mabovu |
| Malori ya kwenye Dampo | 4 | Mawili mazima, mabovu |
| Magari ya Ufuatiliaji | 3 | 2 mapya, 1 bovu |
| Matrekta | 3 | Yanafanya kazi |
| Matela | 5 | 2 mabove |
| Mapipa ya takataka katika maeneo ya Umma | 178 | Yapo kwa wingi |
| Mtambo wa Kushindilia | 1 | Unahitaji matengenezo mara nyingi |

**Chanzo: Jiji la Tanga**

## 6.0 MATOKEO YA JITIHADA YA MSARAGAMBO

*Kufikika kwa Maeneo ya Ukusanyaji Taka*. Vyanzo vingi vya taka vinafikika kupitia barabara na vichochoro kwa sababu vyote ni vipana na vinapitika. Maeneo mengi ya Jiji makazi yaliyopangwa na hivyo hakuna shida ya uchaguzi wa vifaa vya kukusanyia na kusafirishia taka.

*Uelewa na Mitizamo*. Kwa sasa jamii ina uelewa wa kutosha na mtazamo chanya kuhusu udhibiti wa taka ngumu. Hatua zote kuhusu udhibiti wa taka ngumu kuanzia utunzaji wa taka majumbani,

uchambuaji wa taka, utakatishaji wa taka, kasi ya ukusanyaji, utayari wa kulipia huduma na makubaliano kuhusu eneo la dampo na uteketezaji wa taka vimeboreshwa sana kutokana na uhamasishaji mkubwa wa umma na ushirikishwaji.

*Uwepo wa Vituo vya Ukusanyaji wa Taka.* Vituo vya kukusanyia taka na maghuba hupatikana karibu katika maeneo yote muhimu katika eneo la kati la kibishara la jiji. Picha zilizopo hapa chini zinasema ukweli huu.




***Maghuba katika vituo mbalimbali vya ukusanyaji wa taka***

*Matokeo Mengine*. Hamlashauri ya Jiji la Tanga imefanikiwa kuwa na muundo sahihi unaofanya kazi ya usafi wa mazingira, ugatuaji wa majukumu ya udhibiti wa taka kutoka halmashauri kwenda ngazi ya Mtaa pamoja na utunzaji mzuri wa bustani na mizunguko ya barabara kwa kuifanya ya kijani na ya kuvutia sana; vyote hivi vimepelekea kupungua sana kwa uchafuzi wa mazingira, Jiji kuwa safi na mwonekano wa kuvutia.



***Bustani na mzunguko wa barabara katika lango la jiji zinazotunzwa vizuri***

Halmashauri ya Jiji la Tanga sasa inajitapa kuwa imetokomeza kabisa mashimo ya taka wakati matumizi ya mapipa na mifuko ya uchafu imeimarika. Pia vikundi vya mitaa vyenye hamasa binafsi kushiriki kikamilifu katika ukusanyaji wa taka, utupaji wa taka na ukusanyaji wa ada vimeleta tofauti kubwa katika usafi wa Jiji.

Jitihada ya Msaragambo pamoja na mpango wa kudhibiti taka ngumu vimeleta uongozi wa kisiasa wenye nia thabiti ya usafi wa mazingira, mashindano na tuzo zinazotolewa kwa vikundi na kata kwa mwaka, ushirikiano unaofanya kazi na Jiji dada la Kemi huko Finland (hasa katika uchambuzi na utakatishaji wa taka), mfumo wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) unaofanya kazi katika utanatishaji wa Jiji na ongezeko la fursa za ajira zinazotokana na utunzaji wa bustani, ukusanyaji na uchambuzi wa taka.








## 7.0 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA UENDELEVU

Halmashauri ya Jiji la Tanga imefanikiwa sana kupitia jitihada ya Msaragambo na mpango wa udhibiti wa taka ngumu. Hata hivyo kuna changamoto nyingi zinatia wingu katika mafanikio haya. Hizi ni pamoja na uchakavu wa haraka wa vifaa vya taka kama magari na maghuba kwa sababu ya hali ya hewa yenye unyevu mwingi, uwekezaji mdogo wa Halmashauri kwenye mitambo ya taka uosababisha upungufu wa uwezo wa ukusanyaji wa taka, baadhi ya jamii bado zina uzito katika kuchangia na kushiriki katika jitihada ya Msaragambo na Vijana huona aibu kufanya kazi zinazohusianana na udhibiti wa taka.





***Maghuba yanayooza kutokana na hali ya hewa yenye unyevu mwingi***

Halmashauri ya Jiji la Tanga pia inakumbwa na miundombinu duni na uratibu dhaifu kati yake na taasisi nyingine za miundombinu kama TANESCO, TTCL na jitihada za Mipango Miji ambazo zingesaidia udhibiti wa taka ngumu. Pia sheria ndogo za sasa na viwango vya tozo vimepitwa na wakati lakini pia mchakato wa kupitia sheria na viwango hivi na kupata idhini ya kuvitumia inaweza kuchukua hadi miaka mine. Dampo pia bado linaendeshwa kidhaifu kutokana na upungufu wa watumishi, magari na teknolojia.




*Dampo linaloendeshwa kidhaifu*

Hata hivyo Jiji limeweka mikakati mingi yenye lengo la kufanya Jiji endelevu katika Usafi, Unadhifu na Uzuri. Mikakati hii imeelezewa hapa chini.

*Kuboresha uchambuaji na uhifadhi wa taka katika Vyanzo vya taka*. Halmashauri ya Jiji la Tanga ina nia ya kuhakikisha kuwa wakazi wote wana uelewa, elimu na motisha ya kutosha ya kuacha kutupa taka katika barabara ili kujenga tabia ya kuhifadhi taka katika vyanzo. Wakazi pia wataelimishwa kuhusu madhara ya taka kwa afya za binadamu na kwa mazingira na watafundishwa jinsi ya kuchambua taka hatari na ambukizi majumbani.

*Kuboresha Ukusanyaji Taka wa Msingi.* Ukusanyaji taka wa msingi uraboreshwa kwa kutenga magari sahihi na kutathmini hali ya makazi, hali ya barabara, na hali ya kijiografia na sura ya ardhi (topografia). Kwa namna hii ukusanyaji taka wa msingi utafanywa kwa magari madogo, yasiyoenda kasi na hayatakwenda safari ndefu, mfano ni mikokoteni, maguta na pikipiki na matairi matatu.

*Kasi ya Ukusanyaji taka.* Jiji la Tanga lina hali ya hewa ya joto na unyevu, taka zitokanazo na mimea na wanyama hurabika haraka na kutoa harufu zinavutia wadudu na vijidudu vya maradhi. Hivyo aina hizi za taka huhitaji kukusanywa kila siku. Katika maboresho haya ukusanyaji taka wa kaya kwa kaya, barabara kwa barabara, ufagiaji wa barabara, matumizi ya vikundi vya kijamii na kiraia na ukusanyaji binafsi wa nyumba kwa nyumba katika makazi yenye vipato vya juu vitahimizwa.

*Ufagiaji wa barabara.* Idara husika na udhibiti wa taka ngumu itaandaa ratiba ya usafishaji wa barabara inayoonyesha barabara zipi zinahitaji kusafishwa kila siku na zipi zinahitaji kusafishwa kwa vipindi maalumu, orodha ya barabara na mitaa hii, pamoja na urefu na upana wao, utaratibu wa usafi wa barabara hizi, taratibu za kazi ya usafi na ratiba ya kusafisha sehemu za umma zilizo wazi kila siku au kwa vipindi maalumu.

**Jedwali 2. Vifaa vya ufagiaji wa Barabara**

| Vifaa | Vigezo vya Utengenezaji |
|---|---|
| Ufagio | Muundo wa ugagio ni muhimu kwa ufanisi wa kazi na afya kazi ya mtumiaji |
| | Mipini mirefu ya duara inafaa zaidi. |
| Sahani na Masinia ya Chuma | Sahani na Masinia ya chuma husaidia usafirishaji wa taka za barabarani na kuziweka kwenye matoroli na maguta na hupunguza migusano kati ya mfagiaji na taka. |
| Matoroli na Maguta | Toroli la mikono hurahisisha shughuli za mfagiaji. |
| | Mapipa yanayogawanyika hurahisisha umwagaji taka katika maghuba kwa usafirishaji wa upili. |
| | Ujazo wa mapipa haya huzingatia uwezo wa kuyabeba kwa urahisi. |

| | |
|---|---|
| | Uwezo wa juu wa toroli la mikono ni kubeba taka za safari tatu za mkusanyaji. |
| | Toroli la mikono lazima liwe na matairi matatu na liwe na mishikio mirefu ili mtumiaji asilazimike kuinama wakati wa kulisukuma. |

Kuanzisha vutuo vya Upili vya uhifadhi na Ukusanyaji Taka. Taka zilizokusanywa kwa mbinu za msingi kutoka majumbani lazima zihifadhiwe mahali maalumu kusubiri usafiri kwa gharama nafuu kwa kuweka vituo vya uhifadhi. Walau maghuba manne kwa Kilometa moja ya mraba yanahitajika. Katika maeneo yenye mgandamizo kubwa wa watu, ghuba moja litawekwa kwa kila wakazi 5,000 mpaka 10,000, kutegemeana na ukubwa wa ghuba. Ghuba lenye ukubwa wa meta tatu za ujazo linabeba tani 1.25 mpaka tani 1.5 za taka, ambalo linatosha kwa wakazi 5,000 tu, na ghuba la ukubwa wa meta saba za ujazo linaweza kuhudumia watu kati ya 10,000 hadi 12,000.

*Uboreshaji wa Usafirishaji wa taka*. Magari yatatengwa na kugawanywa kulingana na gharama, uwezo wa kubeba, umri wa gari, kasi ya upakiaji, upakinaji wa vipuri, mwendokasi wa gari, utumiaji wa mafuta na gharama za matengezo.

*Ushiriki wa Sekta binafsi.* Ushiriki wa sekta binafsi ni mojawapo ya njia nyingine nzuri ya kuongeza utendaji, ambapo Halmashauri ya Jiji itabadilisha jukumu lake kutoka mtoa huduma na kuwa mwangalizi na mwezeshaji. Aina mbalimbali za ushirikiano na sekta binfsi zinatarajiwa, kama makubaliano na ubia wa namna mbalimbali. Maboresho kupitia ushiriki wa sekta binafsi yatategemea sana utashi wa kisiasa kuhusu mabadiliko, makubaliano na mikataba wazi, uwezo wa sekta ya umma kusimamia huduma, kufuatilia huduma, na kutekeleza vipengele vya makubaliano; uwezo wa fedha na kuaminiana kati ya pande mbili.

*Kuboresha Usimamizi wa Uteketezaji wa Taka*. Halmashauri ya Jiji la Tanga imetenga fedha kimsingi kwa ajili ya kuboresha eneo la uteketezaji taka la Mwang'ombe na kwa ajili ya baadhi ya shughuli za ujenzi. Eneo hili lina hekta 21.5 ambalo litaboreshwa kufikia ubora wa kuzuia taka kutapakaa wakati likisubiri kujengwa.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Juhudi za Halmashauri ya Jiji la Tanga kuwa na Jiji safi na nadhifu zimethibitika kuwa na mafanikio kutokana na sababu nyingi zilizojificha lakini zilizotumiwa vizuri. Sababu moja kubwa imekuwa ni mchakato mrefu na usiokoma wa maandalizi ya Jamii (ukusanyaji wa taarifa, elimu na matangazo) kwa zaidi ya miezi sita kabla ya jitihada ya Msaragambo. Kampeni za usafi wa siku ya Jumamosi (Msaragambo) zimekuwa jitihada zilizoleta hamasa kwa wakazi wote na wameweza kuiga na kuwa na tabia za kutunza mazingira yao na kuwa masafi. Pia imeleleta uwelewa wa uwajibikaji katika jamii. Msisitizo kuhusu ubora wa maisha umeleta msukumo kuelekea usafi wa mazingira ya Jiji.

Halmashauri ya Jiji la Tanga imeendelea kufanya kazi kwa ubia na sekta binafsi katika ngazi zote za kiutawala na katika sekta zote husika. Hii inaashiria mtazamo wa pamoja kuhusu usafi wa jiji na utunzaji wa mazingira. Halmashauri pia inatumia mabango katika maeneo ya Jiji yanayolenga kuongeza uelewa wa wakazi kuhusu matatizo yanayosababishwa na taka.


Ushiriki madhubuti na endelevu wa viongozi wa serikali katika kampeni za usafi (yaani Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, n.k) umewafanya wakazi kuwa waangalifu sana kuhusu takataka katika

mitaa yao. Jiji lililopangwa vizuri na hasa maeneo ya kati ya jiji pia kumechangia sana kufanikiwa kwa Msaragambo.

Siri pia zinajumuisha uwekezaji wa Jiji katika uanzishaji na utunzaji wa bustani na mizunguko ya barabara, utozaji faini mkali wa wahavunjaji wa sheria ndogo za mazingira na usimamizi na ufuatiliaji saidizi bora unaofanywa na idara ya usafi na mazingira.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA

**UTOAJI ENDELEVU WA CHAKULA CHA MCHANA KATIKA SHULE ZA MSINGI**




*Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni moja kati ya Halmashauri sita za Mkoa wa Shinyanga. Halmashauri ipo kusini mwa ziwa Viktoria. Halmashauri inapakana na Halmashauri za Kishapu na Manispaa ya Shinyanga kwa upande wa Mashariki, Geita na Kahama kwa upande Magharibi, Kwimba kwa upande wa kazkazini na Nzega kwa upande wa Kusini. Halmashauri ina eneo la $Km^2$ 42,121 na kiutawala imeganyika katika tarafa 3, kata 26, vijiji 117 na vitongoji 685.

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ina hali ya hewa ya tropiki yenye ukame na hupata mvua kidogo sana kwa mwaka. Wastani wa mvua kwa mwaka ni mm 450 – mm 990 na zinanyesha msimu wa miezi ya Oktoba – Mei kila mwaka. Kiasi hiki cha mvua kingetosha kwa kilimo kama mvua zingenyesha miezi yote na kwa uhakika. Lakini mvua katika Halmashauri ya shinyanga ni chache na za mtawanyika na hivyo kufanya shughulu za kilimo, hasa uzalishaji wa mazao kuwa mgumu. Kwa sababu hii Halmashauri inapambana sana kuwahamasisha wakulima kulima mazao ambayo yanavumilia ukame. Kutokana na ukosefu wa mvua za uhakika wakulima pia huwa na shida kubwa ya kupata majani na maji kwa ajili wanyama wanaowafuga kwa wingi.

Kulingana na sensa ya watu ya mwaka 2012, Halmashauri ina jumla ya wakazi 333,417 ambao 171,461 ni wanawake na 162,956 ni wanaume. Wakazi hawa wa Halmashauri ya Shinyanga wanaishi katika kaya 53,082 na kufanya idadi ya wakazi kwa $Km^2$ kuwa 79. Halmashauri ina shule za msingi 128, zote zikimilikiwa na Serikali. Kuna jumla ya wanafunzi wa shule za msingi 63,359 ambao kati yao 30,788 ni wanaume na 32,571 na wasichana walioandikishwa kwa darasa la kwanza hadi la saba.

**Mchoro 1: Ramani ya kuchora ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga**




## 2.0 TATIZO

Jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa ujumla ni ya Kilimo mchanganyiko ambapo kila familia inategemea uzalishaji wa mazao kwa kuishi na ufugaji wa ng'ombe na wanyama wengine. Kutokana na hali hii familia hazijali sana kuhusu watoto kwenda shule bali huwaruhusu zaidi katika kushiriki shughuli za kilimo na uchungaji wa ng'ombe. Kwa mfano mwaka 2009 mahudhurio katika shule za msingi yalikuwa 79% tu ya mahudhurio yote. Idadi ya walimu wa shule za msingi pia haikuwa ya kutoshaa.

**Jedwali 1: Mahitaji ya Walimu wa shule za Msingi**

| mahitaji | Waliopo | | | | | | | | | Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | shahada | | stashahada | | Cheti IIIA | | Jumla | | | |
| | M | K | M | K | M | K | M | K | JUMLA | |
| 1624 | 10 | 6 | 17 | 3 | 835 | 598 | 607 | 862 | 1469 | 155 |

**Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga**

Kama mwendelezo wa mahudhurio duni kiwango cha ufaulu wa mitihani ya darasa la saba pia ulikuwa chini sana. Sababu kubwa za kiwango cha chini cha ufaulu zimeegemea kwenye jamii yenyewe na mapungufu yake ya kiutamaduni. Jamii ya Halmashauri ya Shinyanga kwa kiasi kikubwa haithamini sana elimu ya kisasa ambayo inatolewa bure na Serikali kupitia mtandao wa shule za msingi. Wazazi kwa mfano hawawasaidii watoto kuhudhuria shule mara kwa mara. Watoto wanajisimamia wenyewe kuhusu masuala ya shule wakati mara nyingi wazazi huwataka watoto kushiriki katika kutunza ngo'ombe na kulima. Jamii hii pia ina tamaduni na imani zinazokandamiza ustawi wa mtoto wa kike. Watoto wa kike wakishafikisha umri wa balehe hutarajiwa kuolewa, na sio kuhudhuria shule. Wazazi pia wanatarajia kupata mali kupitia mahari ya motto wa kike ambayo hulipwa kwa ujumla kwa ng'ombe na mbuzi. Madhaifu haya ya kiutamaduni yalichangia sana katika madhurio duni na kiwango cha chini cha ufaulu kwa miaka mingi.

**Jedwali 2: kiwango cha Ufaulu miaka 4 (2009 – 2013)**

| Mwaka | Wanafunzi walioandikishwa | | | Ufaulu | | | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | K | Jumla | M | K | Jumla | |
| **2009** | 4143 | 4368 | 8511 | 1305 | 655 | 1960 | **23** |
| **2010** | 3494 | 3528 | 7022 | 1693 | 1135 | 2828 | **40.3** |
| **2011** | 4217 | 4861 | 9078 | 2086 | 1763 | 3849 | **43.3** |
| **2012** | **2904** | **3233** | **6137** | **2859** | **3178** | **6037** | **47.9** |

**Chanzo: Halmashauri ya Shinyanga**

Kama vile udhaifu wa kiutamaduni hautoshi kuharibu maisha ya shule ya watoto wa Halmashauri ya Shinyanga, ukame na mvua haba huleta dhahama kabisa kwa mototo wa shule na upungufu mkubwa wa chakula katika familia. Upungufu huu wa chakula hufanya watoto kupata mlo mmoja tu, hasa nyakati za jioni, yaani baada ya shule. Kwa maneno mengine watoto wa shule hawapati kifungua kinywa wala chakula cha mchana wanapohudhuria shule. Tatizo hili lilikuwa dhahiri kabisa kwa miaka na liliathiri sana uwezo wa kujifunza wa watoto, mahudhurio shuleni na ufaulu wa mitihani ya darasa la nne na la saba. Kwa kweli 79% ya mahudhurio shuleni ni mojawapo ya mahudhurio ya chini kabisa Tanzania.

**3.0 MALENGO YA MPANGO**

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ilitathmini hali ya utoaji wa Elimu ya Msingi katika Halmashauri na kuweka lengo dhahiri la kuondoa sababu za msingi za mahudhurio duni na ufaulu wa chuni katika mitihani ya Taifa. Halmashauri iliandaa mpango wa kutoa chakula cha mchana katika shule za msingi ili kuwatia motisha watoto kuhudhuria shule na kufurahia kuwepo shuleni. Mpango wa Utoaji wa Chakula cha Mchana ulitekelezwa chini ya ufadhili wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Mwanzoni Mpango huu ulianza na shule za Msingi 20 kati ya shule 128. Malengo ya moja kwa moja ya mpango huu yalikuwa

- Kuongeza mahudhurio ya wanafunzi ktoka 79% mawaka 2009 na kufikia 100% mwaka 2012

- Kuongeza kiwango cha ufaulu wa mithani ya darasa la saba kutoka 47.3% mwaka 2009 hadi 70% mwaka 2012
- Kutoa chakula kwa wanafunzi wote katika shule 128 ifikapo 2012

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Baada ya kuunda Mkakati wa Kutoa Chakula cha Mchana shuleni mwaka 2010 Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga iliendelea mbele kwa kuunda ushirikiano thabiti na WFP na kujikita katika hatua ambazo zimeelezewa hapa chini.

*Kutia saini hati ya makubaliano na WFP*. Hii ilikuwa muhimu ili kuhakikisha shughuli zote chini ya ufadhili wa WFP zinafanyika kwa voiwango vya Halmashauri na vya Serikali. Pia iliruhusu Halmashauri kutoa usaidizi mwingine kiufundi, kiutawala na watumishi.

*Utambuzi wa Shule za Msingi Zilizokuwa na Hali mbaya zaidi*. Halmashauri kwa pamoja na WFP walifanya utafiti wa msingi kutambua shule ambazo zipo kwenye jamii ambazo zinzkabiliwa sana na uhaba wa chakula katika kaya. Haya ni yale maeneo ambayo hukumbwa sana na ukame na mbua zisizotabirika na kupelekea mavuno duni sana kwa mazao yote ya biashara na chakula. Mchakato wa awali wa utambuzi uliorodhesha shule za msingi 20 ambazo zilihitaji sana kupatiwa chakula cha mchana. Hizi mara moja zilipatiwa vyakula kutoka WFP.

*Utoaji taarifa kwa kamati za Shule na Walimu*. Afisa Elimu wa Halmashauri alitoa taarifa ya lengo la halmashauri kutoa chakula cha mchana mashuleni kuptia ufadhili wa WFP kwa shule zote zilizotatajwa. Kamati za shule na Walimu waliridhia pendekezo hilo kwa kuandaa nafasi/stoo za kuhifadhi vyakula vitakavyogawiwa na kujenga majiko na Majengo ya kuweka majiko katika shule.

*Ugawaji wa Vyakula na WFP*. WFP waligawa mahindi, maharage, na mafuta ya kupikia kwa shule zilizotajwa. Vipimo vilivyotumika kugawa chakula ni 5gm mafuta ya kupikia, 30gm maharage, 120gm mahindi na 40gm unga wa uji kwa mwanafunzi mmoja. Hivyo idadi ya wanafunzi ndio iliamua kiasi cha vyakula vitakavyotolewa.

*Kufanya Uhamasishaji na kujenga uelewa katika Jamii*. Halmashauri iliendelea mbele na kufanya mikutano ya hadhara ya uhamsishaji kwa watu wazima na wazazi kuwashawishi kuhusu umuhimu wa elimu na jinsi ilivyo muhimu kwa watoto wao. Mpango huu pia ulijumuisha vipengele vya afya hasa kuwapa chakula cha mchana watoto wa shule ili wawe na afya bora na hivyo kujifunza kwa haraka. Katika shughuli hizi za uhamasishaji jamii pia zilihimizwa kujenga stoo, majiko, majengo ya kuhifadhi majiko shuleni ili kuhifadhi chakula kinachotolewa na WFP na katika baadhi ya shule chakula kinachochangwa na wazazi.

*Kubadilisha Mbinu za Kilimo*. Kutokana na ukame wa mara kwa mara na upungufu wa mvua zinazopelekea upungufu wa chakula katika kaya, Halmashauri iliamua kuziamuru Shule za msingi kulima mtama, ekari tatu kila shule. Mtama ni zao linalovumilia ukame na linaleta uhakika wa ongezeko la mavuno na chakula chenye afya. Shule zote zilitakiwa kufuata vipimo vya kilimo na upandaji vilivyotolewa na Halmashauri kupitia Afisa Kilimo wa Halmashauri na kutekelezwa na maofisa ugani. Halmashauri iligawa kilo 2 za mbegu za mtama kwa shule zote za msingi 128. Maofisa wote wa kilimo na ugani wa Halmashauri katika mpango huu walielekezwa kuanzisha mashamba darasa yam tama katika kila shule. Jamii pia iliombwa kubadilika kutoka kulima mahindi

na kuanza kupanda mtama ili kuleta uhakika wa chakula katika kaya na uhakika wa kutoa chakula cha mchana kwa watoto shuleni na nyumbani.

*Ukusanyaji wa Michango ya Jamii.* Jamii kupiti kamati za shule na walimu zilihamasishwa kuchangia nguvu kazi, mali na fedha katika ujenzi was too za vyakula ma majiko shuleni. Jamii pia ziliombwa na kukubali kuchangia fedha zitazotumika kununulia sukari, kusaga nafaka na kulipa wapishi mashuleni. Viwango vya uchangiaji vilipangwa kulingana na uwezo wa kaya katika maeneo husika. Hivyo kila shule ina kiwango chake kuanzia shs 200/= mpaka shs 1000/= kwa mwezi kwa mawanafunzi mmoja. Jamii pia inachangia kuni na maji kuwezesha upikaji wa chakula cha mchana mashuleni. Katika jijihada hii Halmashauri inawalipa wajenga majiko banifu kutoka TATEDO ambao hufanya mafunzo kwa wanavijiji kuhusu namna ya kujenga majiko ya udongo na saruji ambayo ni fanisi katika kutumia kuni.

**5.0 AINA NA KIASI CHA RASLIMALI ZILIZOTUMIKA**

Mikakati iliyotajwa hapo juu ilihitaji kiasi kikubwa cha raslimali ili kutekelezwa kwa ufasaha. Katika ngazi ya Halmashauri na katika jamii shughuli hizi zilihitaji fedha, nguvu kazi na raslimali nyingine zilizoelezewa hapa chini.

Raslimali Fedha. Halmashauri ilichangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa stoo, majiko na vifaa vingine. Fedha taslimu zilitumika kwa safari za ufuatiliaji. Jedwali 3 linaonyesha fedha zilizotumika. Halmashauri pia ilinunua na kugawa mabati, mbao na vyuma vnavyowekwa kwenye majiko banifu ya udongo na zege katika shule za msingi.

**Jedwali 3: Baadhi ya Raslimali Fedha Zilizotumika**

| s/n | Item of expenditure | Amount in Tsh |
|---|---|---|
| 1 | Construction of stores and stoves | 78,400,000 |
| 2 | Purchase and supply od millet seeds | 785,000 |
| 3 | Monitoring and supervision | 5,000,000 |
| | **Total** | |

**Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga**

Aina nyingine ya raslimali ilikuwa michango ya Jamii. Ukiacha fedha taslimu jamii zilichangia nguvukazi, ukusanyaji wa mawe, utengenezaji wa matofali na ujenzi wa stoo na majiko. Kwa upande wa Halmashauri, watumishi wa halmashauri walishiriki katika kufuatilia na kusimamia mpango mzima. Raslimali watu nyingine zilitoka WFP ( wafadhili wa mpango) na TATEDO (shirika lisilo la kiserikali linajihusisha na Nishati Vijijini.

Mwaka 2013/14 Halmashauri ilitumia fedha kununua na kugawa vyakula katika shule za msingi ambazo zilikuwa na upungufu mkubwa wa chakuala katika kaya zao. Kila shule iliyokuwa na hali hii ilipata magunia 17 ya mahindi. Hya yaliweza kusaidia kuwapa wanafunzi walau uji wakati wa chakula cha mchana.

Licha ya kutoa chakula, WFP pia ilizisaidia shule mbili pampu za maji ziitwazo "Money Maker". Lengo la pampu hizi ni kusaidia shule hizi ambazo zina bustani za mboga za zinazotumiwa na wanafunzi wakati wa chakula cha mchana kuweza kumwagilia bustani hizi na kupata mboga zaidi ili zitumiwe na wanafunzi au kuziuza na kupata fedha kwa ajili ya kupata fedha za kulipa wapishi na kununua sukari.

**6.0 MATOKEO YA MPANGO WA UTOAJI CHAKULA CHA MCHANA**

Mpango huu ulifikia malengo yake na kuna mifano mingi inayoonyesha kiwango cha mfanikio hayo. Vfungu vinavyofuata hapa chini vinaelezea mafanikio yaliyopatikana katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga katika mpango wake wa kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi zilizopo katika maeneo yanayoshambuliwa sana na ukame.

*Mitizamo chanya kuhusu Elimu*. Jamii za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga zimepata uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa usahihi wa elimu kwa watoto wao. Hii inaonekana katika utayari wao wa kuchangia chakula cha mchana kwa ajili ya wanafunzi na kushiriki katima shughuli za maendeleo ya shule. Wazazi pia wamekuwa na mitizamo chanya kwa walimu na kamati za shule na wanafanya kazi pamoja kuboresha ustawi wa shule na watoto wao. Mkurugenzi Mtendaji anaeleza.

*….hali ilikuwa mbaya sana nilipofika hapa… watoto walikuwa wanachelewa, au hawaji kabisa…. Ukiwaita wazazi wao, wanakuja na kusikiliza tu, lakini hawakuchukua hatua yoyote….kusaidia watoto kuhudhuria shule….baada ya mpango huu wa chakula na mikutano tuliyofanya….mambo yamebadilika kabisa….wazazi wanakuja hapa….wanafanya nasi kazi, hushiriki katika ujenzi was too na majiko uanyoyaona….na wana furaha kuona walimu hapa kijijini….hili ni badiliko kubwa….na mafanikio makubwa….*

*Ujenzi wa majengo shuleni.* Ujenzi was too za chakula, majiko banifu na majengo ya kusimika majiko hayo haujafanyika kwa msaada wa WFP tu, bali shule nyingine 15 zilikamilisha ujenzi wa majengo na majiko haya na yanatumika kuandaa chakula cha wanafunzi. Picha zilizopo hapa chini zinaonyesha stoo na majiko banifu kwa kutumia zege. Shule zote zilizopo kwenye ufadhili wa WFP pia zimekamilisha ujenzi wa majengo haya. Jamii zimekuwa zikishiriki kikamilifu katika shughuli hizi. Hivyo inatarajiwa kuwa jitihada hii itakuwa endelevu.



*Jiko la Zege lililopo Shule ya Msingi Nzagaruba*



*Stoo ya Vyakula*

*Utoaji wa chakula cha mchana katika Shule 60 za Msingi*. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga sasa inajigamba kuwa moja ya halmashauri ambazo zinatoa chakula cha mchana katika shule za msingi. Kati ya shule 128, shule za msingi 60 zinatoa uji asubuhi na chakula cha mchana, au chakula cha

mchana tu. Nafaka na maharage kwa ajili ya chakula cha mchana hutolewa na wazazi na kusaidiwa na halmashauri. Wazazi wanakubali kwa hiari kabisa kuchangia fedha na nguvukazi ili kuwezesha utoaji wa chakula katika shule za msingi na kufanya jitihada hii kuwa endelevu.

*Mashamba ya Kisasa ya Shule*. Shule za Msingi zimeiga mbinu mpya za kulima mazao na mboga mboga. Mazao haya ni pamoja na mtama, pamba, mihogo na karanga. Mazao haya ni mazuri kwa kuandaa uji na chakula cha mchana. Ziada ya mavuno huuzwa ili kupata fedha za kununulia sukari na kulipa wapishi. Mashamba katika shule za msingi yamefanikiwa sana kwa sababu maafisa kilimo na ugani wapo karibu sana na shule, hushirikiana vizuri na walimu na wanafunzi katika hatua zote za kilimo, yaani kulima, kupanda, kupalilia, kuweka mbolea na kuvuna.




***Mwalimu katika shamba la Shule ya Msingi Shingida na Kilimo cha matuta katika Shule za Msingi***

*Kuboreka kwa Ujumla kwa Afya za Wanafunzi.* Watoto wanopata chakula cha mchana shuleni katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa kweli wanaonekana tofauti walininganishwa na wanaobaki nyumbani au walio katika Shule ambazo hazitoi chakula mchana. Wako tofauti kabisa kwa kupendeza, uchangamfu, uwezo kiakili na nguvu za mwili. Wanashiriki darasani, michezoni na kwenye kilimo kwa uchangamfu. Uzoefu wa walimu unaonyesha kuwa hata matukio ya wanafunzi kuwa wagonjwa na kuhitaji kwenda kwenye huduma za afya yamepungua sana tangu kuanzishwa kwa utoaji wa chakula cha mchana shuleni. Wanafunzi wenye afya pia huwa hutulia na kuweka nguvu zao katika shughuli za kujifunza na wanakuwa na motisha wa kuendelea na maisha ya shule kuliko wale watoto wanaobaki majumbani na kujiunga na shughuli za kilimo na uchungani wa wanyama wa kufugwa.



***Wanafunzi wenye afya njema katika Shule ya Msingi Nzagaruba***



***Wanafunzi wenye afya njema wakiwa darasani***


*Kuongezeka kwa mahudhurio na kiwango cha ufaulu.* Lengo kuu la shughuli zote hizi chini ya mpango wa utoaji chakula cha mchana mashuleni ni kuondoa kabisa utoro, kuongeza mahudhurio shuleni na kuongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani ya taifa. Mpango huu wa Hamlashauri ya Wilaya ya Shinyanga umefanikiwa kufikia malengo hayo. Jedwali na mchoro uliopo hapa chini unaonyesha mabadiliko haya. Mafanikio haya yameunganika na matokeo yaliyoelezewa hapo juu, kuwa watoto wakipata chakula, afya njema inakuwa ni suala la uhakika, mahudhurio yanatiwa hamasa, kujifunza kunaongezeka na kufaulu mitihani ya taifa inakuwa shabaha inayofikiwa.

**Jedwali 4: Mahudhurio na Ufaulu**

| Mwaka | Mahudhurio % | Ufaulu % |
|---|---|---|
| 2009 | 79 | 23 |
| 2010 | 87 | 40.3 |
| 2011 | 91 | 43.5 |
| 2012 | 93.5 | 47.9 |

**Chanzo: Halmashauri ya Wilaya Shinyanga**

**Mchhoro 2: Mahudhurio na Ufaulu kwa mchoro**




**7.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI**

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imepata mafanikio makubwa katika kutoa chakula cha mchana katika shule za msingi ambazo zinashambuliwa sana na ukame, upungufu wa chakula na tamaduni mbaya za jamii; tamaduni zisizosaidia mtoto anayesoma. Utekelezaji hata hivyo ulikumbana na changamoto nyingi. Hizi zinajumuisha;

(i) Ushiriki wa Jamii ulikumbana na vikwazo vingi kwa sababu familia nyingi hazikuwa tayari kuchangia fedha na nguvukazi wakati wa ujenzi wa stoo na majiko mashuleni.

(ii) Kuendelea kwa uharibifu wa mazingira unaopelekea ukame zaidi na kupungua kwa mvua na hivyo hali mbaya zaidi katika mavuno na ukakika wa chakula.

(iii) Usugu wa baadhi ya familia kuiga mitazamo chanya. Pamoja na uhamasishaji kwa umma uliofanyika kuhusu umuhimu wa kuchangia chakula katika mashule, baadhi ya familia bado zinaamini kuwa uchangiaji wa chakula unawafaidisha walimu na siyo wanafunzi. Hivyo kuwa wazito katika kuchangia.

(iv) Ufugaji wa kuahamahama. Jamii za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga bado zinaishi maisha ya kuhamisha wanyama kwenda maeneo mengine yenye malisho na maji. Hii inahusisha uhamaji wa familia nzima kutoka kijiji kimoja kwenda vijiji, mabonde na misitu

ya mbali. Watoto wanaosoma shule huathiriwa sana na tabia hii kwani wanalazimika kuacha shule.

(v) Ndoa za utotoni. Hii inaathiri watoto wa kike walio shuleni kwani mara tu wanapoingia hatua za awali za balehe huolewa na wanaume wazima. Wazazi wanaridhika na mahari kuliko kuwaruhusu watoto wao wa kike kuendelea na maisha ya shule. Hii inachangia utoro na hivyo kuathiri kiwango cha mahudhurio katika shule za msingi ndani ya Halmashauri.

8.0 MIKAKATI YA KUPAMBANA NA CHANGAMOTO

Changamoto zilizotajwa hapo juu zilitaka kuathiri ufikiaji wa malengo ya mpango wa utoaji wa chakula cha mchana shuleni. Halmashauri hata hivyo haikuchoka kupambana na changamoto hizi na kushinda. Mikakati iliyotumika imeelezwa kwa kifupi hapa chini.

(i) Ujenzi shirikishi wa Uelewa. Halmashauri iliwashirikisha viongozi wa jamii za kila aina na watumishi wa halmashauri (walimu) kujadili na wanavijiji na kuwaelezea faida za mpango, njia za uchangiaji na ufuatiliaji wa matumizi ya vyakula vinavyopelekwa mashuleni. Katika mbinu hii familia zote zilishirikishwa bila kujali kama wana watoto katika shule husika.

(ii) Matumizi ya Sungusungu. Kwa ujumla katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wanaishi wasukuma. Wasukuma ni maarufu sana kwa kitengo chao cha vijana cha ulinzi na usalama maarufu kama Sungusungu. Sungusungu wanaheshimiwa sana na jamii kwani wanaleta usalama, amani na ulinzi kwa watu binafsi katika jamii, kaya zao na mali zao. Katika mpango huu sungusungu walimtumiwa kimkakati kabisa na Halmashauri kuifanya jamii ikubaliane na mpango. Sungusungu wamebaki na jukumu la kuzitembelea familia na kukusanya vyakula au fedha na kasha kuvikabidhi mashuleni.

(iii) Matumizi bora ya maafisa Ugani, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji na Wenyeviti wa Vijiji. Hawa walifanywa sehemu muhimu ya utekelezaji wa mpango huu na walipewa jukumu la kutumia aina zote za mikutano ya jamii kutangaza na kuelezea bila kuchoka umuhimu wa watoto kwenda shule na hitaji la watoto kupata mlo shuleni. Halmashauri imewawezesha maafisa hawa kwa kuwapatia vifaa vya usafiri (pikipiki na baiskeli) ili kurahisisha safari zao.



***Pikipiki zitakazokopeshwa kwa watumishi vijijini***

(iv) Matumizi bora ya Viongozi wa Kisiasa. Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Wabunge na Madiwani, wote walishirikishwa katika kutangaza mpango huu kupitia vikao vyao vya kisheria na ziara zao za kikazi kwa jamii.

Halmashauri pia imeweka mkakati wa kuhakikisha uendelevu wa mpango huu. Mkakati huu unahusisha kuanzishwa kwa Mfuko wa Elimu ambao utasaidia, pamoja na mambo mengine kutoa chakula katika shule za msingi na sekondari, kufanya Sungusungu kuwa taasisi ya kisasa katika mfumo wa polisi jamii ili itoe huduma za kisasa sa usalama na amani, uhamsidhaji wa jamii usiokoma na ujenzi wa uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa elimu katika maisha ya mtoto na kuwatia motisha vizuri watumishi wa halmashauri ili waweze kutekeleza vizuri mipango, miradi na programu za Halmashauri.

**9.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga si Halmashauri pekee Tanzania iliyojaribu kutoa chakula cha mchana katika shule za msingi. Halmashauri nyingine nyingi zimejaribu jitihada hii. Sio nyingi zilizofaulu. Mafanikio sahihi ya Halmashauri ya Shinyanga yametokana na utayari na kujitoa kwa wanasiasa kushiriki kikamilifu katika mpango, matumizi bora ya Maafisa Ugani na walimu kuutangaza na kuutetea mpango, ushirikiano thabiti na WFP, utulivu wa kisiasa katika Halmashauri, matumizi sahihi ya regesta ya wakulima kujua uzalishaji wao kwa mwaka na kiasi cha kuchangia na nia ya Mukurgenzi wa Halmashauri ya kuacha nyayo katika Halmashauri hii kwa Uongozi imara, usimamizi wenye matokeo na timu imara ya kazi.

# Sura ya Tano: Maendeleo ya Kiuchumi ya Jamii

Sura ya tano ina visa mkasa viwili vinavyohusiana na juhudi za jamii katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi kwa kutumia vuguvugu linalojulikana kama "**kijiji kimoja-zao moja**" au *OVOP* na dhana ya mnyororo wa ongezeko la thamani. Juhudi hizi zinazingatia nadharia ya kwamba maendeleo ya kiuchumi ya jamii asilia yataletwa na jamii yenyewe kwa kujitegemea na kutumia fursa walizo nazo. "Kijiji kimoja -zao moja" haina maana kwamba lazima liwe zao moja tu, bali ni kauli mbiu inayolenga jamii kuchagua bidhaa chache zile ambazo wana stadi na uzoefu nazo na zina uwezekano mkubwa wa kuwatoa katika umaskini kulingana hali ya udongo, mvua, na soko katika maeneo yao bila kulazimishwa na mtu au serikali. Katika vuguvugu hili, jamii huhamasishana ili kutambua fursa walizo nazo, kuzitumia, kuzalisha bidhaa zenye upekee wa aina yake, kuziongeza thamani, kuweka madaraja ya ubora wa bidhaa, kuzifungasha na kuzipa utambulisho maalum ili kulinda soko. Bidhaa hizi siyo lazima ziwe za kilimo au mifugo pekee, bali ni bidhaa na huduma zinazozalishwa eneo husika hata kama ni utalii wa vyakula, uchoraji, usukaji, utalii wa mandhari, chemichemi za maji moto, utalii wa nyumba za asili, kilimo cha mwani baharini, utamaduni na mila fulani za kipekee. Mfano, kwa upande wa kilimo wakulima wa Dodoma wanaweza kujikita kwenye kilimo cha zabibu kwani inastawi vizuri sana Dodoma; Wakulima wa Same wanaweza kujikita kwenye kilimo cha tangawizi, zinastawi vizuri huko, Wakulima wa Iramba wajikite kwenye kilimo cha alizeti na kadhalika kulinga na hali ya maeneo husika.

Uchaguzi wa bidha husika ni ridhaa ya watu wenyewe, Wawezeshaji wa ugani wanaweza kutumika kuwafungua watu macho waone fursa bila kuwalazimisha. Kazi ya Halmashauri katika vuguvugu hili ni kizitambua juhudi au bidhaa hizo, kuwatia moyo jamii, na kulea miradi michanga inayoanzishwa na jamii, na kuzitafutia soko bidhaa hizo.

Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ina kisa mkasa kinachohusu "**kijiji kimoja -zao moja**" au *OVOP* . Wao wamechagua kujikita katika zao la mhogo na kuamua kuliongezea thamani badala ya kuuza kama malighafi. Lengo lao ni kuongeza uzalishaji, kuongeza faida itokanayo na mhogo, na kuongeza kipato cha kaya. Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, zamani ikijulikana kama Mpanda, wao wamejikita katika uzalishaji wa zao la mpunga katika bonde la ziwa Rukwa. Waliamua kuanzisha kituo kikubwa cha kilimo cha Mwamapuli. Kituo hiki kina miradi kadhaa inayolenga kuboresha uzalishaji wa mpunga, kuukusanya, kuuhifadhi kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani, kukoboa, kupanga madaraja(1-4), kufungasha, kuweka utambulisho na kufanya matangazo ili kuuza. Wamejenga miundombinu ya soko la mazao mchanganyiko na kituo cha habari za masoko na bei za mazao ya kilimo.

Katika mfumo wa soko, mnyororo wa thamani ni dhana inayoainisha mlolongo wa jinsi ambavyo biashara au kiwanda fulani kinavyopokea malighafi kutoka eneo la uzalishaji, kuiongeza thamani, kuuza bidhaa ya mwisho kwa walaji pamoja na mrejesho katika kila ngazi. Myororo wa thamani ni mfululizo wa shughuli mbalimbali ambazo kikundi cha wakullima au mkulima mmoja mmoja, anazalisha zao au bidhaa fulani kwa kutumia pembejeo za aina fulani (mfano mpunga unaonukia) hadi kupeleka bidhaa iliyokamika na yenye viwango vinavyotakiwa na walaji sokoni. Mnyororo wa thamani unamrejesho, mfano walaji hupeleka mrejesho kuhusu ladha, ufungashaji unaotakiwa, rangi ya bidhaa, kiwango cha ubora au daraja, harufu ya bidhaa, jinsi ya kuzalisha kwa mbolea za

asili au za viwandani na kadhalika. Katika mnyororo wa thamani mrejesho huo ni lazima ufanyiwe kazi kuendana na mahitaji ya soko la sivyo hiyo biashara haitaweza kushindana sokoni. Kwa hiyo mnyororo wa thamani unahitaji ushirikiano wa karibu baina ya wote wanaohusishwa katika mlolongo huo wa kuongeza thamani na mrejesho wake wa kubadili mali ghafi kuwa bidhaa iliyokamilika, yenye uwezo wa kushindana katika soko huria. Tofauti na mfumo wa soko tuliozoa, mnyororo wa thamani hauanzii kiwandani au shambani, bali kwenye pembejeo za kuzalisha mali ghafi na unatiririka kama ifuatavyo:(i) mfumo wa usambazaji pembejeo (ii) kuzalisha mali ghafi na kuongeza thamani, (iii) mfumo wa usambazaji bidhaa iliyo tayari kuuzwa, (iv) uuzaji wa jumla na rejareja wa bidhaa husika na (v) shughuli za baada ya mauzo na mrejesho toka kwa walaji. Shughuli hizi zinasaidiwa na vijishughuli vingine mfano (vi) mfumo na kanuni za mauzo na manunuzi, (vii) mfumo wa utafiti na maendeleo, (viii) mfumo wa uendelezaji rasilimali watu wanaofanya kazi katika mnyororo wa thamani husika na (ix) miudombinu ya ushirikiano katika mnyororo husika.

Dhana ya mnyororo wa thamani ilielezwa kwa mara kwanza katika kitabu kilichoandkiwa na Porter, 1998. Katika maelezo yake Mwanadishi huyu anasema lengo kuu la mnyororo wa thamani ni kuzalisha na kupeleka sokoni kwa walaji **bidhaa yenye ubora na thamani ya hali ya juu inavyowezekana kwa gharama ya chini inavyowezekana ili kumudu ushindani katika soko huria**. Kwa kutumia mbinu hii, na kwa kuzingatia ubunifu, utafiti na kufanyia kazi mrejesho toka kwa walaji kila mara, mauzo yanaweza kuongezeka, mkulima atapata faida, maisha yake yatakuwa bora na mwishowe umaskini utapungua nchini na kufikia (maisha bora kwa kila mtu inawezekana).


Ikumbukwe katika ule mfumo wa mazoea wa soko, wakulima huzalisha bidhaa wanayowaza wao kwa namna wanayojua wao, kwa pembejeo na mbegu wanayoitaka wao na kisha "kuyasukumia sokoni" mazao yao kama mali ghafi. Kwa mtindo huu, mzalishaji yuko mbali sana na mlaji wa mwisho, hapati mrejesho toka kwa mlaji pia mkulima hana uamuzi kuhusu bei na aina ya pembejeo wanazotumia kwenye mashamba. Katika zama hizi za soko huria na ushindani ni lazima kubadilika kulekea mfumo wa mnyororo wa thamani. Katika mnyororo wa thamani, mzalishaji anahusishwa na mahitaji halisi ya walaji wa mwisho, hufanya kazi kwa karibu na wasambazaji wa pembejeo, wasindikaji au wachakataji ili kuzalisha bidhaa fulani ya kipekee yenye ubora anaoutaka mlaji wa mwisho. Vivyo hivyo, kufuatia mtiririko huu wa mrejesho wa taarifa na bidhaa walaji nao wanatambua na kuhusika na mahitaji ya wakulima katika uzalishaji wa bidhaa husika.

Katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, umuhimu wa mnyororo wa thamani unakuwa wa lazima kwa sababu ya mabadiliko katika mazingira ya uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mabadiliko ya tabia nchi, watu wengi kuhamia mijini na kuyakimbia mashamba na madhara yatokanayoo na mfumo wa soko huria uliopo duniani kwa sasa. Uzoefu wa soko huria hapa Tanzania unaonesha kwamba, walanguzi au wafanya biashara wa kati wana jukumu kubwa katika soko la bidhaa. Katika mazingira hayo ambayo mlanguzi ndiye mchakarikaji mkuu na lengo lake ni faida ya haraka, hakuna mfumo dhabiti wa kuongeza thamani ya mazao ya mkulima na wala hakuna utaratibu muafaka wa kusimamia ubora wa bidhaa za kilimo uendane na mahitaji ya soko, hapa ndipo tatizo lilipo. Hali hii hupelekea mkulima kupata hasara au faida ndogo kwa sababu bidhaa anayozalisha haina ubora wa kuweza kushindana na bidhaa zinatoka nje ya nchi. Hali hii inaelekea kuua soko la kahawa, pamba, korosho, sukari na hata soko la nafaka kama mchele.

Mabadiliko haya yanamkuma mkulima kwenye dimbwi la umaskini na mzunguko wa ufukara. Katika kukabiliana na hali hii, watetezi wa maendeleo ya wakulima wanapiga kelele na kutetea mfumo wa

soko unaomjumuisha mkulima maskini katika maendeleo. Hii ni pamoja na kubadili mfumo wa biashara kimataifa na hapo ndipo umuhimu kuzingatia mnyororo wa thamani. Mnyororo wa thamani unawataka wakulima waunganishe nguvu zao katika kuongeza thamani ya mazao yao na kujadili bei kwa pamoja badala ya kufanya kazi mmojammoja ili kujihakikishia uwezekano wa kubakia na sehemu katika soko.Ikumbukwe ukipoteza nafasi katika soko, kama ambavyo Tanzainia tumepoteza katika soko la pamba na kahawa, inakuwa vigumu mno kuipata nafasi hiyo kwa sababu ya ushindani.

Kabla ya kuingia kwenye soko huria ni lazima kufanya uchambuzi wa mnyororo wa thamani husika. Uchambuzi huu unasaidia kutambua na kuzielewa changamoto za ushindani. Pia husaidia kutambua mahusiano, utaratibu na uratibu unaotakiwa. Husaidia kujua ni jinsi gani wafanyabiashara walioko sokoni hufanya kazi na ni yupi mwenye nguvu ya soko na kuathiri mustakabali wa mnyororo wa thamani wa bidhaa husika, je ni mlanguzi, msafirishaji, msindikaji, muuzaji wa jumla au rejareja, anayeuza bidhaa nje? au je ni masoko yale makubwa?. Kutengeneza mnyororo wa thamani ni mbinu ya kutaka kupenya katika soko na ni njia yenye tija katika uzalishaji bidhaa bora inayorahisisha mtiririko wa bidhaa husika na kuhakikisha kwamba kila aliyeko katika mnyororo huo anpata faida. Mchoro huu hapa chini unaonyesha tofauti ya mfumo wa soko unaozingatia mnyororo wa thamani na ule mfumo wa soko wa mazoea kama ambavyo umeelezwa hapo juu.




**Mchoro namba 1: Mnyororo wa thamani ikilinganishwa na mfumo wa kawaida wa soko**
Chanzo: Imetafsiriwa kutoka World Report Fall 2006

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPANDA

## MNYORORO WA THAMANI KWA ZAO LA MPUNGA





*Uzoefu wa Kituo cha Kilimo cha Mwamapuli*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ni moja kati ya Halmashauri kongwe nchini na ilianzishwa mwaka 1947 wakati wa Mkoloni. Ilipofika mwaka 2007/2008 Halmashauri hii iligawanywa na kupata Halmashauri ya Mji- Mpanda. Kutokana na azma nzuri ya Serikali ya kuanzisha Mkoa wa Katavi. Mwaka 2011/2012 Halmashauri hii tena imegawanywa na kupata Halmashauri za Nsimbo na Mlele. Kituo cha Mwamapuli kilianzishwa kabla Mpanda haijawa Mkoa na ndiyo maana katika kisa mkasa hiki tutakuwa kunatumia Halmashauri ya Mpanda ya wakati huo kabla huijapanda hadhi na kuwa Mkoa wa Katavi.

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ina jumla ya Kilometa za Mraba 16,911, Tarafa 3 za Karema, Mwese na Kabungu, Kata 9 za Mishamo, Mpandandogo, Katumba, Mwese, Kabungu, Sibwesa, Kapalamsenga, Ikola na Karema, Vijiji 37 na Wakazi wapatao 179,136, hii ni kwa mujibu wa Sensa ya watu na Makazi ya Mwaka 2012. Shughuli kuu za wakazi wa Mpanda ni Kilimo cha mazao; upandaji wa tumbaku, Mahindi, Mpunga, Ufugaji wa nyuki, ufugaji wa mifugo, uchimbaji wa madini, Uvuvi na utalii. Kabla ya kuigawa Halmashauri ya wilaya ya Mpanda eneo lake lilikuwa ni jumla ya kilomita za mraba 47,528 (4,752,800ha). Ukubwa huu ni zaidi ya nchi za Rwanda na Burundi kwa pamoja au Mkoa wa Tanga na Kilimanjaro ikiwekwa pamoja. Eneo hili liligawanyika kwa shughuli mbalimbali kama ifuatavyo: Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 923,300; pori la akiba ni hekta 2,801,100; hekta 860,000 ni Mbuga za wanyama; maji ni hekta 168,400 na eneo linalobaki linatumika kwa ajili ya shughuli zingine kama ufugaji wa nyuki n.k. ngalia mchoro namba moja hapa chini.




**Mchoro 1: Matumizi ya ardhi Halmashauiri ya Wilaya ya Mpanda**

Baada ya kuanzisha mkoa wa Katavi, ukagawanywa katika Halmashauri tatu, yaani Halmashauri za Wilaya Mpanda, Mlele na Nsimbo. Halmashauri ya Nsimbo ina jumla ya Kilometa za Mraba 14,000, Tarafa 2 za Nsimbo na Ndurumo, Kata 11 za Ugalla, Litapunga, Nsimbo, Urwira, Kapalala, Magamba, Machimboni, Stalike, Itenka, Mtapenda na Kasokola, Vijiji 39 na wakazi wapatao 144,245.


Halmashauri ya Mlele ina jumla ya Kilometa za Mraba 14,000 Tarafa 3 za Inyonga, Mpimbwe na Mamba, Kata 13 za Ilunde, Ilela, Utende, Nsenkwa, Inyonga, Kibaoni, Usevya, Ikuba, Mbede, Majimoto, Mamba, Kasansa na Mwamapuli, Vijiji 43 na wakazi wapatao 138,323. Kituo cha Mwamapuli kinaangukia katika Halmashauri ya Mlele.

**Kituo cha Kilimo cha Mwamapuli**

Mradi wa kituo cha kilimo cha Mwamapuli yaani *Mwamapuli Agricultural Centre (MAC)* kwa sasa kiko katika eneo la utawala la Halmashauri ya Mlele na unatekelezwa katika kata ya Mwamapuli. Mwamapuli ni mojawapo ya kata 13 za Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na ni moja ya kata 8 za ukanda wa bonde la ziwa Rukwa wenye ardhi nzuri na yenye rutuba ambayo hustawisha mazao mbalimbali kama vile mahindi, mpunga, alizeti, ufuta, karanga, viazi vitamu na aina mbalimbali za mboga. Ukanda huu una wakazi wapatao 170,484 ambao shughuli yao kuu ya kiuchumi ni kilimo na hasa kilimo cha zao la mpunga ambao huzalishwa kwa kiwango kikubwa kati ya tani 4 hadi 8 kwa hekta. Karibu asilimia 60 ya mpunga wa Mkoa wa Katavi hutoka katika ukanda huu.

**2.0 TATIZO**

Pamoja na mafanikio ya uzalishaji mkubwa wa zao la Mpunga na mazao mengine yaliyopatikana (ona mchoro namba 2) bado wananchi hawakuwa na soko la uhakika kwa ajili ya kuuza mazao yao. Wachuuzi, walanguzi na wafanyabiashara wa kati walifika hadi mashambani na kupanga wenyewe bei za kununulia mazao ya wakulima. Wakulima walikuwa hawana umoja wala uwezo wa kutetea bei za mazao yao hivyo walipewa bei ndogo mno isiyokidhi hata gharama za uzalisha.




**Mchoro namba 2: Uzalishaji wa mpunga katika misimu minne ikilinganisha tarafa za Mpimbwe (rangi nyekundu) na Halmashauri nzima ya Mlele (rangi ya bluu bahari)**

Matatizo mengine ni pamoja na:- Fursa za kilimo zilizopo bonde la Ziwa Rukwa kutotumika kikamilifu, bei ndogo kwa mazao makuu kama vile mpunga, ufuta, alizeti na mahindi, ukosefu wa mitambo ya kuchakata mazao , kupanga madaraja na kufungasha zao la mpunga; kuwepo kwa mfumo holela wa masoko ya mazao ya kilimo na kilimo duni kisichozingatia ubora wa bidhaa na mbinu za kisasa za uzalishaji na uchakataji mazao.

## 3.0 MALENGO

Dira ya jamii ya Mwamapuli ni kufikia kilimo cha kiwango kikubwa, mradi wa uzalishaji mkubwa (ili kupata thamani ya hela inayowekezwa kwenye kilimo) na kuzitumia vilivyo fursa zilizopo katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Mlele. Kwa mantiki hiyo Halmashauri ilianzisha kituo cha kilimo cha Mwamapuli, ili kuratibu uanzishwaji wa mnyororo wa thamani kwa zao la mpunga. Malengo mahsusi ya kituo hiki ni: (i) Kutoa mafunzo yanayolenga kuboresha uzaishaji wa mazao ya wakulima na wafugaji. (ii) Kuongeza uzalishaji kwa kila hekta moja kama inavyooneshwa kwenye jedwali namba moja na mbili. (iii) Kuboresha mfumo wa upashanaji habari za masoko na bei za mazao yaani *market information system (MIS)* kwa bidhaa za kilimo. (iv) Kuanzisha mfumo wa "stakabadhi ghalani" ili kuongeza pato la mkulima ikilinganishwa na pato la wakulima wanaouza mali ghafi moja kwa moja kwenye soko huria mara baada ya kuvuna, rejea jedwali namba tatu. (v) Kuhamasisha ujenzi wa nyumba bora, uhifadhi wa mazingira na matumizi ya nishati mbadala (pumba za mpunga) kwa ajili ya kuchomea matofali. (vi) Kuanzisha kiwanda cha kutengeneza *chip bodi* kwa kutumia pumba za mpunga, ili chipbodi hizo zitumike kwenye programu ya ujenzi wa nyumba za kisasa. (vii) Kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa njia ya "umwagiliaji-kilimo cha uhakika" katika hekta 13,650 zilizoko kwenye mradi. (viii) Kupunguza gharama za usafirishaji wa mali ghafi toka shambani au sehemu ya uzalishaji kwenda eneo la kuchakatia hadi kufika sokoni. (ix) Kuhifadhi mazao katika mfumo wa "stakabadhi ghalani" na (x) Kuongeza thamani ya mazao kwa kuchakata bidhaa za kilimo kama inavyooneshwa katika jedwali namba tatu.

**Jedwali Namba 1: Uzalishaji duni wa huko nyuma na mategemeo ya baadaye ya ongezeko la uzalishaji kwa mazao makuu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele**

| zao | Uzalishaji wa wastani wa siku za nyuma tani/hekta | Matarajio tani/hekta |
|---|---|---|
| **Mahindi** | 2.4 – 4 | 4.5-5.6 |
| **Mpunga** | 3.0 – 4.5 | 5.6-6.6 |
| **Ufuta** | o.5-0.8 | 1-1.25 |
| **Alizeti** | 0.4– 0.6 | 0.8-1.0 |

**Jedwali Namba 2: Tofauti ya bei za mazao makuu katika mfumo wa stakabadhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele**

| Zao | Bei za wastani wakati wa mavuno (Tsh)/gunia la debe 6 | Bei za wastani katikati ya msimu (Tsh)/gunia la debe 6 | Tofauti ya bei kwa vipindi hivi viwli vifupi (Tsh)/gunia la debe 6 |
|---|---|---|---|
| **Mahindi** | 24,000 | 42,000 | 18,000 |
| **Mpunga** | 30,000 | 65,000 | 35,000 |
| **Ufuta** | 90,000 | 130,000 | 40,000 |
| **Alizeti** | 25,000 | 40,000 | 15,000 |

**Jedwali Namba 3: Tofauti ya bei baada ya kuongeza thamani kwa mazao makuu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele**

| Zao | Bei wakati wa mavuno (Tsh)/gunia la debe 6 | Bei za wastani katika ya msimu (Tsh)/gunia la debe 6 | Bei za watani baada ya kuongeza thamani (Tsh)/gunia la debe 6 | Tofauti ya bei baada ya kuongeza thamani (Tsh)/gunia la debe 6 |
|---|---|---|---|---|
| **Mahindi** | 24,000 | 42,000 | 60,000 | 36,000 |
| **Mpunga** | 30,000 | 65,000 | 78,000 | 48,000 |
| **Ufuta** | 90,000 | 130,000 | 147,600 | 57,600 |
| **Alizeti** | 25,000 | 40,000 | 57,600 | 32,600 |

## 4.0 Mikakati ya Utekelezaji

Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi na kupitia mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) waliibua mradi wa kituo cha kilimo cha Mwamapuli kwa kuanza na kujenga soko la mazao, kituo cha habari za soko la mazao ya kilimo na bei, mashine ya kukoboa mpunga na kupanga madaraja ili kuongeza ubora na thamani ya mazao yanayolimwa na wananchi (Mnyororo wa thamani mazao ya kilimo). Hatua za utekelezaji zilikuwa kama ifuatavyo: Kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa wakulima, kufanya ziara za mafunzo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga kwa lengo la kupata uzoefu wa uzalishaji, uchakataji, uendeshaji wa masoko na teknolojia husika; kuimarisha vyama vya Msingi vya wakulima vya Mawamapuli na Majimoto SACCOs, kujenga soko la mazao lenye uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 200, kujenga ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 200 za mpunga, Kuanzisha kituo cha habari za soko la mazao ya kilimo na bei, kuunda kamati ya uendeshaji wa mtambo wa kukoboa mpunga na kusimamia shughuli za soko la mazao, kununua mtambo wenye uwezo mkubwa wa kuchakata na kupanga madaraja ya mpunga kiasi cha tani 30 - 50 kwa siku na kujenga mfumo wa uvunaji maji ya mvua wenye uwezo wa kuhifadhi lita 200,000 kwa wakati mmoja.

Mikakati hiyo ilifuatiwa na ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 200 za mpunga. Baadaye jamii kwa ushirikiano na Halmashauri walianzisha kituo cha habari za masoko, (mazao na bei) au kituo cha rasilimali. Kwa vile shughuli hizi zilikuwa nyingi na tofauti tofauti, Halmashauri iliunda kamati maalum ya kusismamia mradi wa mtambo wa kukoboa mpunga na kupanga madaraja pamoja pamoja na jingo la soko la mazao. Kamati hii ya pamoja Halmashauri na jamii ndiyo iliyosimamia manunuzi ya mtambo na kazi ya kuusimika. Kwa vile Mwamapuli hakuna mfumo wa maji ya bomba, kamati iliamua kutengeneza mfumo wa kuvuna maji ya mvua na kujenga tenki lenye uwezo wa kuhifadhi lita 200,000.

## 5.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Gharama zilizotumika kwenye kituo cha kilimo cha Mwamapuli zimeainishwa kwenye jedwali namba 4. Halmashauri na jamii wote kwa pamoja walishirikiana katika gharama za kuanzisha kituo, hili ni jambo la kujifunza katika kituo hiki.

**Jedwali Namba 4: Gharama za kuanzisha Kituo cha Kilimo cha Mwamapuli**

| Mradi | Kiasi na chanzo | | Ujenzi wa miundombinu |
|---|---|---|---|
| | Toka Halmashauri | Toka kwa Jamii | |
| **Soko la mazao** | 60,000,000.00 | 12,000,000.00 | Hili ni jengo la kisasa la kuuzia mazao mchanganyiko ya kilimo. Jengo hili litasadia katika kudhibiti ukusanyaji wa ushuru wa mazao kwani ukwepaji kodi hauna faida kwa mkulima; Soko hili pia linatengeneza fursa za ajira kwa wenyeji. |
| **Ghala** | 58,400,000.00 | 11,600,000.00 | Kukodisha ghala kwa ajili ya mtambo wa kukoboa mpunga |
| **Mtambo wa kupura mpunga** | 98,785,500.00 | 00.00 | Kufunga mtambo wa kukoboa mpunga wenye uwezo wa tani 30 – 50 kwa siku. |
| **Kituo cha habari za masoko na bei za mazao kilimo** | 99,400,000.00 | 00.00 | Kituo cha habari za masoko ya kilimo na bei za mazao hutoa mafunzo ya ujasiriamali, teknolojia rahisi na muafaka za kilimo, ushirika na uvuvi kwa jamii zinazokizunguka kituo. Hutoa habari kuipitia tovuti, redio, runinga na vijitabu vya mkononi. Kinaunganisha wakulima wa Mwamapuli na sehemu nyingine za nchi yetu. |
| **Mashine ya kufua umeme (jenereta)** | 86,952,700.00 | 00.00 | Jenereta hutoa umeme kwa ajili ya kuendesha mtambo wa kukoboa mpunga, kwani Mwamapuli hakijaunganishwa kwenye umeme wa msongo wa taifa. |
| **Trekta na tela lake** | 48,400,000.00 | 10,000,000.00 | Trekta na tela husaidia wakulima kuongeza uzalishaji kwa kukodishwa ili kulima mashamba makubwa na kusafirisha mazao toka shambani hadi sokoni. |

## 6.0 MATOKEO

Matokeo ya mradi huu yameoneshwa kwenye picha hapa chini. Tayari kuna miundombinu na inatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa. Kuna jengo kubwa linalotumika kama soko, kuna kituo cha habari za masoko na kimewekewa vifaa na samani zinazotakiwa, mtambo wa kukoboa mpunga unafanya kazi, maji yanapatikana kupitia tenki la kuvuna maji ya mvua, mashine za shambani kama trekta na tela vinatumika kuongeza uzalishaji.



Kituo cha taarifa za masoko na bei



Jingo la soko kwa mazao mchanganyiko

















Wananchi wanakoboa mpunga ndani ya eneo la mradi na kuuza katika maeneo mbalimbali. Wananchi wameondokana na adha ya kusafirisha mpunga kwa ajili ya kukoboa. Taasisi za kifedha mfano Benki ya CRDB wana imani kubwa ya kuweza kuwakopesha wakulima kupitia SACCOS zao. Kuna mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji.

## 7.0 CHANGAMOTO

Kituo cha kinakutana na ushindani mkubwa kutokana na bei za chini kwa mchele unaoingizwa nchini toka nje mfano Thailand, licha ya kwamba mchele huo una ubora wa chini kuliko huu wa ndani. Mfano bei ya gunia la mpunga wa ndani ilikuwa Tsh 30,000 mwezi Disemba 2013 ukilinganisha na Tsh 50,000 mwaka 2012. Katika kupingana na hali hii, wakulima walio wengi bado wamehifadhi mzigo mkubwa wa mpunga ndani wakingoja bei ziwe nzuri angalao zifidie gharama za

uzalishaji. Hata hivyo mazingira unakohifadhiwa mpunga si mazuri na yanapelekea upotevu mkubwa wa mazao baada ya kuvunwa unyevu, wanyama waharifu mazao ghalani.

Gharama za kukoboa na kupanga madaraja bado ziko juu mafano gunia moja la debe sita ni Tsh.5000 kutokana na mtambo kutumia umeme wa jenerata kwani hawajaunganishwa na msongo mkubwa wa taifa wa umeme. Kama zilivyo sehemu nyingi za vijijini hapa nchini, hali ya miundo mbinu hasa barabara ni duni sana.

Ghala lililopo kwa sasa halina uwezo wa kuhifadhi mpunga ulio mikononi mwa wakulima. Kutokana na sababu za urasimu bado mfumo wa stakabadhi ghalani ulikuwa haujaanza wakati kitabu hiki kinachapishwa. Hata hivyo jamii ya Mwamapuli haina uzoefu wa jinsi mfumo wa stakabadhi ghalani unavyofanya kazi, na hivyo wanahitaji muda wa kujiandaa kikamilifu ili yasitokee mambo yasiyotarajiwa kama ilivyotokea kwenye soko la korosho. Japokuwa kuna fursa za soko katika nchi jirani za DRC -Congo, Burundi na Zambia. Bado Maafisa Biashara wetu hawajaweza kuchangamkia na kwenda kutafuta mahitaji ya majirani na kufanya miamala ya biashara za huko nje na hata hapa ndani ya nchi.

**8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili juhudi hizi ambazo zimeanzishwa ziweze kuwa endelevu, Halmashauri ya Wilaya itaendelea kutoa mafunzo kwa wananchi ili waweze kuhifadhi mpunga katika ghala kwa njia muafaka huku wakisubiri bei zipande angalao wapate faida. Kuongeza juhudi na kuimarisha SACCOs za wakulima za Mwamapuli na ile ya Majimoto. Watendaji na wanasiasa kuhamasisha na kushawishi taasisi za fedha za kibenki na ambazo siyo za kibenki kukopesha SACCOs za jamii ili wakulima wapate mitaji ya kununulia pembejeo. Kuhakikisha kwamba bei ya kukobolea mpunga inapungua kutoka Tsh.5, 000 ilivyo sasa hadi kufikia Tsh.4, 000 kwa gunia. Kuendelea na mpango wa kujenga ghala kubwa jipya lenye uwezo wa kuhifadhi tani 500,000 ili wakulima na wafanyabiasharai waweze kupata nafasi ya kutunza mpunga wao. Pia viongozi wanawavishawishi vijiji vya jirani wajenge maghala ili kupunguza msongamano. Kuhakikisha jengo soko linaanza kutumika ipasavyo.

Kuboresha miundo mbinu hasa kwa kupanua barabara za vijijini ziweze kupitika wakati wote, mfano barabara ya kutoka Mbede hadi Mwamapuli. Kuboresha usimamizi wa mradi , kutafuta bei nzuri ya mchele ndani na nje ya nchi, kuendelea kuishirikisha jamii juu ya mradi huu ili waweze kuona kwamba ni wa kwao. Kituo cha habari za kilimo na mifugo kilichojengwa katika eneo hili kitawezesha upatikanaji wa habari sahihi za masoko, bei na ubora unaotakiwa. Miundombinu ya kudumu kama maghala, soko, kituo cha habari na mashine ya kukoboa Mpunga vitakifanya kituo hiki kiwe endelevu. Kituo hiki kufanyika kuwa ndio kitovu cha kutoa elimu ya kilimo kwa vitendo hususan kwa wakulima ugani. Kujengwa kwa maghala katika kata jirani ambayo ni muhimu kwa ajili ya uendelevu wa mradi. Kazi zingine zinazotarajiwa kufanyika hapa ni ujenzi wa maghala makubwa mawili ya kuhifadhia mazao ambapo mfumo wa stakabadhi mazao ghalani unaweza ukatumika pamoja na nyumba za watumishi, kununua samani na vifaa au zana mbalimbali zinazohitajika kwa kituo cha habari kwa mujibu wa mwongozo.

**9.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Ubunifu wa watumishi wa Halmashauri wakiongozwa na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji Eng. Emmanuel Kalobelo ambaye kwa sasa ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi. Miradi mikubwa ya

kiuchumi kama hii inahitaji uratibu wa ngazi ya juu zaidi kama vile Mkoa badala ya Halmashauri moja peke yake kujaribu kufanya kila kitu.

Utayari wa wakulima wa Mwamapuli katika kushiriki kutambua, kuainisha vipaombele na utekelezaji wa mikakati iliyoandaliwa kwa pamoja na Halmashauri. Mshikamano na ushirikiano baina ya watendaji wa Halmashauri na viongozi wa kisiasa. Uwepo wa stadi stahiki za ushawishi na utetezi za timu ya menejimenti ya Halmshauri (CMT) kwa Kamati ya Uchumi na Baraza la Madiwani kuthubutu kuwekeza katika kituo cha kilimo cha Mwamapuli. Jamii ya Mwamapuli ni mchanganyiko wa makabila, kwa mfano kuna Wasukuma wengi na Wasukuma wanajulikana kwa jinsi walivyo na juhudi ya kazi mashambani. Uwepo wao hapo ni kichocheo kikubwa kwa wananchi wenyeji kujituma.

Ushirikiano na maelewano kati ya wanasiasa na watendaji ilikuwa kitu muhimu sana. Huu ni mradi unaowapa sifa nyingi na kura wanasiasa wanaotoka maeneo haya. Ikumbukwe pia kwamba Waziri Mkuu wa wakati huu, Mheshimiwa Mizengo Pinda anatoka kijiji cha jirani cha Kibaoni, na siyo mbali na Mwamapuli. Kutokana uwepo wake hapa karibu wahusika wote wa mradi huu wanalazimika au wana msukumo wa ziada kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa.

Mradi wa ukubwa huu unahitaji stadi za ushawishi na utetezi ambazo timu ya menejimenti ya Halmashauri (CMT) ilizitumia ili kuweza kuwashawishi Madiwani kukubali kuingia katika mradi mkubwa kama huu unaohitaji tahadhari. Mwisho ikumbumbukwe kwamba mpunga ni zao la chakula kinachopendwa na wengi, pia mpunga ni zao la biashara. Mpunga unaweza kuhifadhika kwa muda mrefu bila kuharibika. Kwa kuwa mpunga unauzika na kuleta fedha kwa mkulima, basi hicho nacho ni kichocheo kwa watu kushiriki ili kupata faida za kiuchumi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA

## UZALISHAJI WA MHOGO NA MNYORORO WA ONGEZEKO LA THAMANI



*Mimea ya mhogo*




*Unga wa mhogo umefungashwa vizuri*

***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga***

## 1.0 UTANGULIZI

Wilaya ya Mkuranga ni miongozi mwa wilaya sita za mkoa wa Pwani. Wilaya zingine ni pamoja na Mafia, Kisarawe, Rufiji, Bagamoyo, na Kibaha. Wilaya hii inapatikana upande wa Mashariki mwa mkoa, kilomita 50 Kusini mwa jiji la Dar Es salaam. Kwa upande wa Mashariki wilaya hii inapakana na baharia ya Hindi, Kusini ni Wilaya ya Rufiji na Wilaya Kisarawe iko Kusini-Magharibi. Wilaya hii ilanzishwa tarehe 1 Julai, 1995 wakati Wilaya ya Kisarawe ilipogawanywa na kuwa wilaya mbili.

Ukubwa wa wilaya ni kilomita za mraba 2,432, kati ya hizi 1934 $km^2$ zinafaaa kwa shughuli za kilimo. Kiasi cha 51 $km^2$ ni misitu ya hifadhi ukiwemo ule wa Vikindu wenye ukubwa wa 15.99 $km^2$ na msitu wa mikoko pembeni mwa bahari una ukubwa wa 34 $km^2$. Kulingana na sense ya watu na makazi ya mwaka 2012, wilaya ilikuwa na watu wapatao 222,921 kati ya hao 108,024 ni wanawake na 114,897 ni wanaume. Ongezeko la watu ni 3.5% kwa mwaka. Kulingana na ongezeko hili la watu kwa mwaka, wakati wa uhakiki wa kisa mkasa hiki, wilaya ya Mkuranga ilikuwa na watu 246,369, yaani wanaume 118,257 (48%) na wanawake 128,112 (52%). Ujazo wa watu kwa aeneo ni watu 101 kwa kila kilomita ya mraba, wastani wa ukubwa wa kaya ni watu 4.3. Kiutawala wilaya hii imegawanyika katika tarafa nne, kata 18, vijiji 121, vitongoji 460 kama ilivyo kwenye jedwali namba moja.

**Jedwali namba 1: Vitengo vya utawala kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga**

| Tarafa | Kati | Vijiji | Vitongoji |
|---|---|---|---|
| Kisiju | 5 | 37 | 135 |
| Mkamba | 6 | 43 | 146 |
| Mkuranga | 5 | 31 | 144 |
| Shungubweni | 2 | 10 | 35 |
| **Jumla** | **18** | **121** | **460** |

***Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi, 2012***

Zaidi ya 85% ya wakazi wa wilaya ya Mkuranga hutegemea kilimo kwa ajili ya maisha yao. Mhogo ndilo zao kuu la chakula na pia ni zao la biashara ambalo hushamiri vizuri mmno kwenye kila kijiji ndani ya wilaya hii. Kutokana na umuhimu wa zao la mhogo kwa jamii ya Mkuranga, taasisi za utafiti na mashirika ya misaada ziliendesha utafiti shirikishi jamii ili kuchambua changamoto za kiuchumi na kijamii zinazokabili zao hili. Matokeo ya utafiti huu yalibaini changamoto kadhaa katika eneo la uzalishaji, usimamizi, na matumizi ya mhogo wenyewe. Kwenye eneo la uzalishaji, changamoto kuu ni matumizi ya mbegu za kienyeji ambazo hazina uwezo wa kuzaa sana kutokana na vinasaba duni vya uzalishaji, hii hupelekea jamii kutoweza kuzalisha kiasi kikubwa cha mhogo unaotakiwa na soko.

## 2.0 TATIZO

Licha ya ukweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga District inazo fursa za kupanua kilimo cha mhogo na kupanua soko lake, zao la mhogo linakabiliwa na changamoto kadhaa. Changamoto hizi ambazo hutegemeana moja kwa nyingine zimeelezwa hapa chini.



***Majani Ya Mhogo yameathiriwa na ugonjwa wa Batobato (Cassava Mosaic Disease)***

***Matumizi ya teknolojia duni:*** Kama ilivyo sehemu nyingi nchini, bado jembe la mkono na mapanga au nyengo ndio vifaa vikuu katika kilimo na vinatumiwa na zaidi ya 90% ya wakulima. Elimu duni na umaskini miongoni mwa wakulima ni vikwazo vikubwa katika kupokea na kutumia teknolojia ya kisasa ya kilimo. Kuna upungufu mkubwa wa huduma za ugani kwa wakulima, hasa katika ngazi ya kijiji na hivyo kufanya wakulima washindwe kufikia teknolojia za kisasa. Picha hiyo hapo juu ni mimea ya mhogo ikiwa imeshambuliwa na ugonjwa wa batobato maarufu kama *Cassava Mosaic Disease(CMD)*. Mbegu nyingi za kienyeji zinaathiriwa na wadudu pamoja magonjwa mbalimbali.

***Kulima eneo dogo na mavuno kidogo:*** Uzalishalishaji wa mhogo hufanyika katika vipande vidogo vya ardhi na asilimia kubwa ya vishamba hivi (80%) ni chini ya eka mbili, na wakulima zaidi ya 90% hawapandi kwa nafasi iliyoshauriwa kitaalam. Miche inayopandwa na wakulima walio wengi huchaguliwa kienyeji kutokana na kutokuwepo kwa mashamba ya mbegu katika sehemu nyingi za wilaya. Zaidi ya 10 -20% ya mazao ya mhogo hupotelea shambani kabla au wakati wa mavuno kutokana na wanyama waharibifu, wadudu, magonjwa, zana duni zinazotumika wakati wa kuvuna.

***Uhaba wa nguvu kazi katika kilimo:*** Kutokana na mavuno kidogo na kipato kidogo, wanawake na wazee ndio hujishilisha zaidi na kilimo katika wilaya hii ya mwambao, huku makundi makubwa ya vijana wenye nguvu wamekimbilia kwenye biashara ndogondogo za uchuuzi kwenye jiji la kibiashara la Dar es salaam.

***Ukosefu wa teknolojia ya kisasa ya kuchakata mazao ya kilimo:*** Uwezo wa wakulima ni mdogo wa kununua teknolojia ya kisasa na miundombinu stahili kwa ajili kuchakata na kuongeza thamani ya mhogo. Hali hii husababisha asilimia 90 ya mhogo kuuzwa kama ulivyo bila kuongezwa thamani. Kukosekana kwa mbinu mbadala wa kuhifadhi mhogo ni moja ya sababu ya bei ndogo wanayopewa wakulima. Mhogo baada ya kuvunwa huharibika na kubadilika rangi kama hautachakatwa mapema na hivyo kupoteza thamani.

***Ubora duni wa mhogo uliochakatwa:*** uzalishaji wa mhogo usio na ubora unaotakiwa na soko na usioweza kuhimili ushindani wa soko ni matokeo ya kutumia zana duni na mazingira yasiyo salama kwa afya ya binadamu. Zaidi ya yote kiasi kinachozalishwa ni kidogo mno ukilinganisha na mahitaji ya soko.

***Mfumo wa Soko Usioridhisha:*** Kukosekana kwa taarifa za masoko (mahitaji ya soko, muda bidhaa inapotakiwa, mahali inapotakiwa, aina ya bidhaa na hali ambayo inatakiwa na soko ; kukosekana kwa uelewa kuhusu matumizi ya bidhaa za mhogo katika viwanda kunawapa mwanya walanguzi ambao huunganisha wakulima na wafanya biashara ambao hununua mazao ghafi toka shambani kwa bei ya chini sana. Hali hii huwanyima wakulima hadi 70% ya bei waliyostahili na hivyo zao la mhogo humnufaisha mlanguzi kuliko mkulima.

***Kukosekana kwa Chombo Imara cha Kuwaunganisha Wakulima wa Mihogo:*** Kilimo na biasahara ya mihogo vilikuwa vikifanyika katika mazingira ambayo kila mkulima anajifanyia atakavyo na kupatana bei akiwa pekee dhidi ya walanguzi wadanyifu wasio na huruma. Hali hii ni jambo ambalo huwafanya wakulima wapewe bei za chini sana kwa mazao ya mhogo na bidhaa zitokanazo na mhogo kwani hawana sauti wala uwezo wa kubishana bei na hawa habari mabadiliko ya bei katika soko.

***Kukosekana kwa taasisi za fedha za kuwakopesha wakulima vijijini:*** Kilimo kwa ujumla kinakosa mitaji kutokana na uchache wa vyombo vya fedha vyenye mitaji ya kutosha kukopesha na vilivyo tayari kutoa mikopo kwa ajili ya maendeleo ya kilimo. Pia kuna hofu ya kuwakopesha wakulima wadogo ambao wanazalisha katika mazingira yenye hatari na hofu nyingi ambazo huwafanya washindwe kurejesha mikopo.

***Kukosekana au uduni wa dhamana kwa ajili ya kuwezesha kukopa mitaji:*** Wakulima walio wengi hawana dhanama zinazokubalika kisheria ili kuwawezesha kupata mikopo. Hii ndio changamoto kubwa kabisa katika kupata mikopo ya kuwekeza katika kilimo. Sekta ya kilimo imeendelea kubaki nyuma kwa kukosa uwekezaji na mitaji ambayo ni muhimu sana katika maendeleo vijijini.

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ilikuwa ni kuwezesha uanzishwaji wa mnyororo wa thamani katika zao la mhogo kwa kutatua changamoto kubwa za uzalishaji; uchakataji na uuzaji kwa jili ya kuboresha maisha ya mkulima kwa kuongeza kipato na kuongeza usalama wa chakula ngazi ya kaya zilizo ndani ya wilaya nzima. Malengo mahsusi yalikuwa (i) kuendeleza zao la mhogo ambalo lina faida linganifu hususan katika hali ya hewa na udongo unaofaa kwa kilimo hicho (ii) kuongeza thamani na (iii) kuanzisha vituo vya mauzo na kuweka mfumo wa kupashana habari za masoko na bei za mazao ya kilimo.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

**Ushirikiano baina ya Wadau walioko kwenye Halmashauri na Jamii yenyewe:** Katika kuwawezesha wakulima wapate mbegu bora zenye viwango, Halmashauri iliwakaribisha wadau wa maendeleo ya kilimo kushiriki katika kutatua kero zilizokuwepo ili kuwanusuru wakulima wa mhogo. Kuanzia mwaka 2008 Halmashauri ya Mkuranga ilianza kutekeleza mradi wa kuweka mnyororo wa thamani kwa zao la mhogo kwa ushirikiano na wadau wa maendeleo ya kilimo.

Halmashauri ilianza kutatua kero ya uzalishaji, uchakataji na masoko kupitia miradi miwili iliyojulikana kama (i) Uzalishaji wa Mbegu bora za Mhogo kwa Wingi" na (ii) "Mnyororo wa Thamani kwa Zao la Mhogo". Katika mradi wa kwanza, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) walikubali kufadhili uanzishwaji wa mashamba matano ya kuzalisha na kuzidisha mbegu yenye ukubwa wa eka 10 (hekta 4) kila moja katika vijiji vitano tofauti ndani ya Halmashauri. Katika mradi wa pili, Shirika la *Verseilanden* kwa kifupi (VECO) ofisi ya Tanzania,

shirika la MUVI ambalo hufanya kazi zake chini ya Shirika la maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) wakishirikiana na Mamlaka ya Chakula and Lishe (TFDA) walitoa usaidizi uliowezesha kuanzisha mnyororo wa thamni kwa zao la mhogo kwa kununua vifaa na mitambo inayohitajika. Shirika lingine la "Kuongeza Thamani kwa zao la Mhogo Afrika" maarufu kama *Adding Value for Africa (CAVA)* waliwezesha uanzishwaji wa mnyororo wa thamani ili kuzalisha unga wa mhogo mweupe wenye ubora wa hali ya juu ndani ya wilaya ya Mkuranga.

**Mchango wa Taasisi mbalimbali:** Taasisi za Utafiti, hususan; Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni, Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Mizizi-Kibaha, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kwa fedha za ufadhili kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Mazao ya Ukanda wa Joto wa Tropiki yaani *International Institute of Tropical Agriculture (IITA)* waliendesha utafiti kuhusu magonjwa ya mhogo na matumizi ya mbegu za kisasa. Utaalam na mapendekezo ya tafiti hizi yalikuwa muhimu sana katika kuboresha mfumo wa kilimo cha mhogo.

**Mchango wa Halmashauri ya Wilaya:** Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ina mchango mkubwa sana katika kuunda vikundi na kuviimarisha, kujenga stadi, uelewa na maarifa ya vikundi vilivyohusika katika uzalishaji mhogo na kuongeza thamani ya zao la mhogo. Halmashauri iliwezesha katika kupanua kilimo na uzalishaji wa zao la mhogo pamoja ongezeko la mazao ya mhogo mbichi kwa kila eka moja. Halmashauri iliratibu majukumu ya wadau wote katika kila ngazi ya ongezeko la thamani, kwa njia hii wakulima walipanua mashamba ya mhogo kutoka eka mbili kwa mkulima ya awali na pia ongezeko la mazao kwa eka.

**Kuhamasisha Jamii na Kuendesha Mafunzo.** Maafisa ugani waliendesha mafunzo ya ujasiriamali, mnyororo wa thamani na kufanya mikutano ya kuhamasisha vikundi vya wakulima na wakulima wa mfano au wawezeshaji ngazi ya jamii; lengo likiwa ni kuanzisha mradi wa mashamba ya kuzalisha na kuzidisha mbegu ili kujihakikishia upatikanaji wa mbegu au miche bora ya zao la mhogo. Wakulima walitakiwa kutafuta na kuliandaa shamba la mbegu huku Halmashauri ikitoa usadizi-elekezi kwenye masuala ya kitaalam na matunzo.

**Kufunga Mitambo ya Kisasa ya Kuchakata Mhogo:** Ili kwezesha wakulima kutumia zana za kisasa zenye tija, wakulima walifundishwa kuhusu stadi na mbinu za kuweka vifaa vya kisasa vitakavyowawezesha kuendesha biashara ya bidhaa mbalimbali za mhogo kwa kutumia mashine zao wenyewe. Hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kulea miradi midogo ya vikundi vya wakulima.

**Ongezeko la thamani:** Vikundi vya wakulima vilifanya ziara za mafunzo ndani na nje ya wilaya ili kupanua uwezo wa wakulima kuhusu stadi za kuchakata mhogo na kutengeneza bidhaa mbalimbali za mhogo. Ziara hizi zilifanyika kwenye Taasisi ya Utafiti Kibaha kujifunza mapishi ya vyakula mbalimbali kutokana na unga wa mhogo. Matumizi mengine ya mhogo ni pamoja na kutengeneza sabuni za kupiga deki sakafuni na gundi, ona picha hapa chini.

**Mchango wa Wadau wa Maendeleo:** Wadau wa maendeleo wana mchango mkubwa wa fedha zilizotumika katika kutekeleza mchakato mzima, ufuatiliaji na tathmini. Wadau waliwezesha kujenga uwezo wa kuchakata mhogo na kuongeza thamani. Lengo lilikuwa kuhakikisha kunajengeka uwezo na mbinu na stadi za kuchakatia au kuongeza thamani kulingana na mahitaji ya soko na bidhaa zinazotokana mhogo.

Mdau wa muhimu alikuwa ni Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) ambaye alihamasisha wakulima, hamasa ya MVIWATA ndiyo iliyopelekea wakulima kujipanga wenyewe kwenye vikundi vya kibiashara na uzalishaji mali kwa ridhaa yao na kulingana na mahitaji yao. Matokeo ya hamasa yao ni kuundwa kwa vikundi sita vya kibiashara kwa lengo la kuanzisha vituo vyao vidogo vya kuchakata mhogo.



***Kuongeza thamani na bidhaa mbalimbali zitokanazo na zao la mhogo***

MVIWATA iliviwezesha vikundi vya wakulima wa mhogo kuanzisha mahusiano ya kibiashara na wadau wengine walio katika ngazi mbalimbali za mnyororo wa thamani kwa zao la mhogo na pia walitoa usaidizi katika ngazi ya kijiji ambako ndiko mhogo ulikuwa unafanyiwa uchakataji wa mwanzo kabisa. Mdau mwingine wa muhimu ni VECO ambaye alijenga uwezo wa Asasi ya Wakulima wa Mhogo au muungano wa vikundi vya kuchakata mhogo ngazi ya wilaya yaani *Cassava Farmers' Organisation*(CFO) yenye uhalali na mamlaka ya kisheria. Jukumu la CFO ni kutafuta soko la mhogo na bidhaa zake, kukusanya na kuhifadhi mhogo na bidhaa zake na kuongeza thamani kwa niaba ya wanachama wake.

**Soko la Pamoja la mhogo na Bidhaa za Mhogo.** Katika kukabiliana na changamoto za soko, Halmashauri na wadau wengine waliweka juhudi, msisitizo na mkazo katika kuimarisha uwezo wa asasi ya wakulima ili wakulima wawe na sauti au kauli moja na nguvu ya kubishana na kushawishi bei halali kwa mhogo na bidhaa zitokanazo na mhogo. Ni kwa mantiki hii Halmashauri, VECO ofisi ya Tanzania na MVIWATA walikuwa wanawezesha wakulima kuunda Asasi ya Wakulima wa Mhogo (CFO) kwenye kila kijiji baada ya kuwezeshwa. Kikundi kimoja cha wakulima walituma wajumbe kwenda kutafuta fursa za soko, kutembelea na kufanya mahojiano na wadau wa masoko, maduka makubwa ya mhogo na bidhaa za mhogo zilizoko jijini Dar es Salaam.

## 5.0 MATOKEO

Katika Halmashauri ya Mkuranga kuna matokeo kadhaa ya kutia moyo na yanayofaa kuigwa na wakulima wa maeneo mengine yanayolima mhogo**.** Lakini hata hivyo wakulima wa mazao mengine wana jambo la kujifunza kutoka kisa mkasa hiki hasa katika suala zima la mnyororo wa thamani.

**5.1 Kupokea na Kutumia Mbinu za Kisasa za Uzalishaji mhogo:** Kutokana juhudi za wadau mbalimbali zilizoelezwa hapo juu, kuna maendeleo mazuri. Juhudi hizi zinajumuisha programu ya maendeleo ya kilimo (DADPs). Wakulima sasa wameanza kutumia mbinu za kisasa za kilimo ambazo ni kuondoa visiki mashambani, kulima kwa kuchimbua chini ili

mizizi iweze kupenya na mhogo upanuke; uchaguzi wa mbegu bora, kupanda kwa nafasi ili kupata idadi kubwa ya miche inayoshauriwa kwa eneo yaani (mimea 4,000 kwa eka). Kutokana na kupokea na kutumia mbinu za kisasa maeneo ya uzalishaji na uzallishaji kwa eneo vimeongezeka. Maeneo yameongezeka kutoka eka 0.5-1 kwa mkulima hadi eka 2 kwa mkulima huku uzalishaji ukiongezeka maradufu kwa wastani wa tani 4 kwa eka kwa sasa ikilinganishwa na tani 2 kabla ya juhudi hizi.

**5.2 Mashamba ya kuzalisha na kuongeza mbegu yameanzishwa:** Eneo lingine ambalo Halmashauri imepata mafanikio makubwa ni kuanzishwa kwa mashamba matano ya mbegu yenye hekta nne kila moja katika vijiji vya Njopeka, Misasa Hoyoyo, Kiwambo na Nyamato. Kwa ujumla ni hekta 20 zimeanzishwa kwa ufadhili wa FAO na VECO- ofisi ya Tanzania. Wadau wengine ni Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Mizizi-Kibaha, Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha mazao ya Ukanda wa Joto wa Tropiki yaani *International Institute of Tropical Agriculture (IITA)*. Wataalamu toka mashirika haya walishirikiana na wakulima bega kwa bega katika kuzalisha mbegu safi na za kisasa. Taasisi ya uhakiki wa mbegu nchini yaani *Tanzania Official Seed Certification Institute (TOSCI)* walisimamia zoezi zima la uzalishaji ili kuhakikisha kwamba zinakidhi viwango vinavyotakiwa.




***Mashamba ya uzalishaji mbegu za mihogo***

**5.3 Ujenzi wa Vituo vya kuchakata mhogo.** Vituo sita vya kuchakata mhogo vimeanzishwa na vinamilikiwa na wakulima wenyewe. Picha hizi hapa chini zinaonesha baadhi ya vituo hivyo.




***Vituo vya kuchakata mhogo***

Wakulima siyo tu kwamba walifundishwa jinsi ya kutumia mashine za kuchakata mohogo, bali walipewa misaada ya mashine zenyewe. Programu ya DADPs, VECO – ofisi ya Tanzania, Asasi ya

Wanawake Wasomi fani za kilimo (TAWLAE) na Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) walitoa misaada ya mashine za kutengeneza chips za mhogo na mashine za kucharanga yaani *Cassava chippers na graters*, kwa vituo husika. Kwa vile misaada hii ililenga hitaji halisi la wakulima, iliwatia sana wakulima moyo wa kupokea na kutumia teknolojia za kisasa za kuongeza thamani ya zao la mhogo kama ilivyo kwenye jedwali namba mbili hapa chini.

**Jedwali 2: Mgawanyo wa vifaa vya kuchakata mhogo kwa vijiji vya Mkuranga na mtoaji**

| Mtoaji: DADPs | | | VECO | | | | | TAWLAE | | | SUA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vijiji | CH | GR | **Vijiji** | CH | GR | MM | DR | **Vijiji** | CH | GR | **Vijiji** | CH | GR |
| Kitomondo | 1 | | Misasa | 1 | | 1 | 1 | Sotele | 1 | | Tipo | 1 | |
| Njianne | 1 | | Mamdimpera | 1 | | | 1 | Mwanambaya | 1 | | Kilamba | 1 | |
| Magawa | 1 | | Mamdikongo | 1 | | | | Dundani | 1 | 1 | Nyanduturu | 1 | |
| Lukanga | 1 | | Lupondo | 1 | | 1 | 1 | | | | | | |
| Njopeka | 1 | | Kizapala | 1 | 1 | 1 | 1 | | | | | | |
| Mkerezange | 1 | | Tungi | 1 | | | 1 | | | | | | |
| Sotele | 1 | | Sotele | | | | 1 | | | | | | |
| Kolagwa | 1 | | | | | | | | | | | | |
| Misasa | 1 | | | | | | | | | | | | |
| Mkuranga | 2 | | | | | | | | | | | | |

**Ufunguo**: CH ni Chipper, GR ni Grater, MM: ni Mashine ya kusaga , DR ni kifaa cha kuanika (Seti moja ni vifaa 35 )

**5.4 Kuanzishwa kwa Asasi Imara za Kibiashara za Wakulima:** Wakati kitabu hiki kinapelekwa kuchapwa, vikundi vinne viliashaanzisha biashara ya mhogo na bidhaa za mhogo ndani ya wilaya. Kutokana na uimara wa vikundi hivi, wakulima waliweza kuongeza bei ya unga wa mhogo toka Tsh 300 hadi Tshs 1000 kwa kilo moja.

***5.5 Ubora wa bidhaa za mhogo na ufungashaji vimeongezeka:*** Kama unavyoona hapa juu, ongezeko la bei linatokana na kuongeza kwa ubora wa unga wa mhogo na bidhaa zitokanazo na unga huo na jinsi zinavyofungashwa kwa ustadi mkubwa na kupewa utambulisho, ushahidi uko kwenye picha hapa chini. Wakulima wa Mkuranga sasa wana utambulisho au "nembo"kwa ajili bidhaa zao maarufu kama (Brand) ambayo ni muhimu sana katika kutambulisha bidhaa sokoni. Nembo hii huonekana kwenye vibandiko kwenye vifungashio. Baadhi ya vifungashio vimeoneshwa kwenye picha hapa chini.




***Vifungashio vilivyoboreshwa vikionesha nembo ya bidhaa za mhogo wa Mkuranga***

**5.0 CHANGAMOTO**

Baadhi ya changamoto za kuanzisha mnyororo wa thamani wa zao la mhogo ni pamoja na:- Uhaba wa vyombo vya usafiri. Halmashauri in upungufu mkubwa wa vyombo vya usafiri hasa pikipiki 121 kwa ajili ya Maafisa ugani katika Halmashauri nzima. Halmashauri ni kubwa na hali ya nchi ni miinuko na mabonde na kwa hiyo panahitajika usafiri wa chombo kinachoweza kupenya sehemu ngumu ili kufikia jamii ziliko. Kuna upungufu mkubwa wa maafisa ugani (50) wanaohitajika ili kuwawezesha vikundi vya wakulima waweze kuchakata mhogo. Kwa sasa maafisa ugani huajiriwa na sekretarieti ya ajira na vibali vya ajira hutolewa na Idara Kuu Utumishi na hawajakubali Mkuranga wajaze mapengo yaliyopo.

Bado bei anazopewa mkulima ni za chini, na bei zinabadilika mara kwa mara jambo ambalo humfanya mkulima akate tamaa ya uzalishaji. Wakulima hufanya maamuzi ya uzalishaji kutokana na bei za mwaka au msimu uliotangulia. Kwa hiyo kama bei za msimu uliopita zikuwa nzuri wakulima huongeza mazao na msimu unaofuata mazao hufurika sokoni na bei kushuka. Vivyo hivyo msimu unaofuata wengi hawatalima na bei huenda zikapanda. Wadudu na magonjwa nayo ni changamoto inayofanya mipango isiende kama ilivyokusudiwa. Kuna mashambulizi makubwa ya magonjwa hasa ugonjwa wa batobato yaani *Cassava Mosaic Virus (CMD)* na ugonjwa wa michirizi ya kahawia yaani *Cassava Brown Streak Disease (CBSD*).

**Kasi ndogo ya kuundwa kwa hiari vikundi ya uzalishaji kibiashara**: Wakulima wengi bado wanashindwa kulipa mchango wa asilimia 20 ya gharama ya uzalishaji ambayo ni kigezo muhimu cha uendelevu na umiliki wa mchakato kwa wakulima wenyewe. Kigezo hiki ni kikwazo kwa wakulima wengi hasa kwa sababu ni kigeni kwao lakini matarajio ni kwamba wanavyoendelea wakulima wengi wataona umuhimu na kuwa tayari kuchanga na kujiunga kwenye vikundi. Ikumbukwe wakulima walio wengi hapa mwanzoni hawana ujasiri na wala hawamwamini mtu. Hii inatokana na historia mbaya iliyoachwa na vyama vya ushirika vilivyokufa na madeni makubwa ya wakulima. Baadhi ya waliokuwa wanaushirika wako hai bado na wanayo kumbukumbu mbaya ya chama cha Ushirika cha Mkoa wa Pwani. Kundi la vijana limeachwa nje, hawataki kujishughulisha na kilimo cha mhogo ambacho wanadai hakilipi, badala yake wamekimbilia Dar es Salaam na vitongoji vyake wakifanya shughuli za uchuuzi.

**Kucheleweshwa kwa fedha za ruzuku za miradi ya maendenleo toka serikkali kuu**: Hela za miradi ya maendeleo ya kilimo hufika huku msimu wa kilimo ukiwa unafikia ukingoni. Hali hii huathiri sana ubora wa shughuli na bidhaa zilizokusudiwa. Jambo lingine ni kwamba wakulima hawako wepesi katika kutii, kukubaliana na kufanya kulingana na ubora wa bidhaa unaotakiwa sokoni. Hii ni kasoro kubwa kwani katika soko huria, ubora wa bidhaa ni muhimu sana ndio unayoamua mzalishaji fulani abakie au aondoke kwenye mnyororo wa thamani. Kikwazo kingine ni uchache wa mazao au udogo wa mzigo na bidhaa zinazozalishwa na mhogo ambazo hazikidhi mahitaji makubwa ya soko. Hatimaye bado vikundi vinavyojishughulisha na uchakataji wa mhogo havijapata uhakiki na idhini toka Mamlaka ya Vyakula na Madawa (TFDA). Hii ni muhimu katika kumhakikishia mlaji usalama wa chakula toka kwa vikundi hivi.

**Uwezo mdogo wa wakulima wa kushawi bei kutoka na uzalishaji mdogo:** wakulima hawana uzoefu wa kukabili changamoto za soko la pamoja. Kwa upande wa wafanya biashara gharama za usafirishaji ni kubwa kwani mzigo unaopatikana kwa wakati mmoja ni mdogo kuliko uwezo wa vyombo vya usafiri vinavyohusika. Kukosekana kwa uaminifu au kuaminiana: Kuna mahusiano yasiyo ya kuamiania baina ya wanaohusika katika soko yaani kwenye mnyororo wa ongezeko la thamani kwa zao la mhogo.

## 7.0 UENDELEVU

Katika kukabiliana na changamoto hizo hapo juu Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga iliamua:- Kuhamasisha kilimo kinacholenga kuzalisha kwa wingi katika eneo dogo badala ya maeneo makubwa mazao kidogo. Hii inalenga kuongeza uwezo wa kuzalisha mzigo mkubwa wa bidhaa za mhogo kwa kutumia teknolojia muafaka. Kuna juhudi za kuhamasisha uanzishwaji wa kituo cha kudhibiti ubora wa mazao ya mhogo ili kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa ni bora kwa viwango vinavyokubalika na zinauzika.

**Kujifunza kwa wengine waliofanikwa humu nchini**: Halmashauri imekua ikiandaa ziara za mafunzo za kubadilishana baina ya vikundi vya wakulima, siku za maonesho ya kilimo, na ziara za mafunzo zikijumuisha maafisa ugani na wakulima kwa lengo la kubadilishana uzoefu na wakulima wa maeneo mengine waliofanikiwa. Halmashauri imeingiza mbegu zinazovumilia magonjwa na wadudu kutoka ndani na nje ya nchi.

Ili kijihakikishia mnyororo wa thamani unakuwa endelevu kituo kikubwa cha kuuzia bidhaa za mhogo kitajengwa eneo la kijiji cha Vikindu. Kuna juhudi za kukaribisha wadau wengine mfano shirika la MUVI wameonesha nia ya kuwezesha mnyororo wa thamani na uuzaji wa mazao ya mhogo ili kuwatia vijana katika kilimo na kutengeneza kipato kutokana na zao la mhogo. Kuna juhudi endelevu za kuimarisha vikundi vya wakulima ili waweze kujitawala na kujipanga wenyewe. Pia kuna juhudi za kendelea kuwahimiza wakulima watumie mbinu za kisasa katika uzalishaji ili kuongeza wingi wa mazao, ubora na thamani, kutengeneza mitandao ya kitaasisi ili kunasa fursa za masoko na mitaji ya kilimo kutoka vyombo vya fedha.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

**Ushirikiano wa wadau.** Ushirikiao wa wadau ni jambo muhimu katika kuanzisha mnyororo wa thamani kwa zao lolote. Kama ilivyooneshwa hapa juu katika Halmashauri ya Mkuranga kuna juhudi za pamoja za wadau mbalimbali mfano FAO, MVIWATA, MUVI, VECO, Taasisi za utafiti za Mikocheni, Kibaha TOSCI na (SUA). Wengine ni IITA, CAVA, SIDO, TFNC na TFDA katika kuthibiti ubora. Ule ushirikiano wao ndio jambo la msingi zaidi katika mnyororo wa thamani kuliko juhudi ya mdau mmoja mmoja.

**Eneo la kijiografia la wilaya limekaa kimkakati.** Halmashauri ya Mkuranga imekaa kimkakati katika kufikia soko kubwa la pembejeo na bidhaa la Dar es Salaam. Pia wasafiri wanaopita barabara kuu ya Dar es Salaam hadi Mtwara hupitia Mkuranga na husimama kununua bidhaa kwenye masoko yaliyo pembeni mwa barabara kuu. Masoko haya ni fursa nzuri ya kuuza mhogo na bidhaa za mhogo.

**Uwezeshaji makini.** Uwezeshaji uliofanywa na wagani na wadau wengine ulikuwa jambo muhimu sana. Katika uwezeshwaji, wakulima walihitaji kuunganishwa na taasisi zinatoa tekinolojia ya kisasa ya kuchakata mhogo, soko la bidhaa za mhogo, pembejeo, tasisi za mafunzo na utafiti. Kwa hiyo uwezeshwaji ulofanywa na wawezeshaji mahiri na waliodhamiria wa ugani toka Halmashauri ulikuwa jambo la msingi mno. Kwa mantiki hiyo kwa vile idadi ya wagani haitoshi, Halmashauri imewapanga maafisa ugani kimkakati katika ngazi ya Kata na vijiji kulingana na wingi wa shughuli za uzalishaji zilizopo kwenye eneo husika. Wagani na vikundi vya wakulima wote kwa pamoja

wanapata mafunzo yanayolenga kuongeza uwezo wao kupitia ufadhili wa wadau wa maendeleo. Kwa vile uwezeshaji ni mzuri baadhi ya washiriki wa vikundi vya wakulima wana uwezo sasa wa kwenda kusaka masoko wenyewe katika jijiji la Dar es Salaam.

**Uongozi shupavu wa Halmashauri na Sekretairieti ya Mkoa.** Kisa mkasa cha Mkuranga, kinabebwa sana na uongozi wenye dira. Ikumbukwe kwenye miradi mikubwa ya uchumi wa eneo hutegemea ushirikiano na maono ya viongozi wa Halmashauri na Mkoa. Ngazi hizi mbili wanahitaji kuungwa mkono na wanasiasa walio katika eneo husika. Kwa Mkuranga Mkurugenzi wa Halmashauri alikuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha uanzishwaji wa mnyororo wa thamani. Yeye binafsi alikuwa na shamba la kwake la mbegu la mfano, ambako wakulima walienda kujifunza na kupata miche ya kisasa. Mkurugenzi alipata ushirikiano mzuri toka ngazi ya Mkoa, mfano Mkuu wa Mkoa aliwanunulia mashine ya kuparaza mhogo (grater) kikundi kimoja katika kitongoji cha Mpera, kijiji cha Hoyoyo kutokana na bidii waliyoonesha kwa kuanzisha na kusismamia vizuri na kwa makini shamba la mbegu la hekta 4. Ili kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi ni wajibu wa ngazi ya Sekretarieti za Mikoa(RS) kuwajengea uwezo na kutoa usimamizi elekezi kwa ngazi za serikali za mitaa zilizo chini yao. Ushirikiano wa wadau ngazi ya Halmashauri na idara zake mfano Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya, wa kata na wale vijiji walikua mstari wa mbele kutatua kero za wakulima.

# Marejeo

*Abiona, A. I. and Bello, W. N. (2013). Grassroots Participation in Decision-Making Process and Development Programmes as Correlate of Sustainability of Community Development Programmes in Nigeria, Journal of Sustainable Development; Vol. 6 (3):47-57. Canadian Centre of Science and Education, [www.ccsenet.org/jsd] site visited on 19 /03/ 2013.*

Chibehe, M.M. (2004). Factors Affecting Sustainability of Farmer Groups: the case of Twikinde Malimbichi Cooperative Society. MA Dissertation, SUA, Unpublished, 90pp.

Helene Bie Lielleor and Ulrik Lund-Sorensen (2013). FARMERS' CHOICE Evaluating an approach to agricultural technology and adoption in Tanzania, Rockwool Foundation research Unit, PRACTICAL ACTION Publishing, pp. 154.

Howlett. D and J. Nagu. (1997). *Agricultural Project Planning in Tanzania, A handbook on cycles and sequences, participation, identification, planning and design, economic and financial analysis, and environmental assessment of agricultural projects.* ISBN 1898828261. pp 89.

Kusago, Takayoshi. (2008). *Sustainable Livelihood and Happy Generation in Minamata-City Japan*: A Model for Endogenous Community Development.

Makonda, K.S.C. (2003). Partnership and sustainability of water supply systems in Bukombe District, Tanzania. *MA Dissertation*, Sokoine University of Agriculture, Morogoro, Tanzania. Unpublished. pp.154

Mwanga, J.N. (2011). Empowerment of Local Society in Tanzania–the Nucleus for Development-With Experience from Indonesia and Japan, *Rare Series Policy Paper*, Local Government Training Institute, Dodoma Tanzania. 100 pp.

Ohama, Y. (2002). Basic Framework and viewpoints of Participatory Local Social Development (PLSD) and construction of its evaluation framework.

Porter, M. E. (1998). *Competitive Advantage: Creating and Sustaining Superior Performance*, 397 pp, Amazon.

Pretty, J.N. (1995). Participatory learning for sustainable agriculture. *World Development* 23(8): 1247-1263.

Scoones, I. and John Thompson (1994). *BEYOND FARMER FIRST: Rural people's knowledge, agricultural research and extension practice*. Intermediate Technology Publications LTD, London, UK, pp.301.

Sharma, P.N. and Ohama, Y. (2007*). Participatory Local Social Development-An Emerging Discipline*, Bharat Book Centre Publishers & Distributors, Lucknow India. pp. 467.

Shikuku, O.M. (2012). Community related Variables influencing sustainability of water projects in Nyando District a case. *MA Dissertation*, University of Nairobi, Digital Repository

URT, (2010). Public private partnership (PPP) *Act*, no 18 of 2010, pp 21

URT (2011). Millennium Development Goals, Tanzania country report. Ministry of Finance and Economic Affairs, Dar es Salaam – Tanzania.

Zadeh, B.S. and Nobaya, A. (2010). Participation and Community Development. *Current Research Journal of Social Sciences* 2(1): 13-14, 2010. [http://maxwellsci.com/print/crjss/v2-13-14.pdf] site visited on 22/07/2014.